

**UCHANGANUZI WA UPOLE KATIKA MAZUNGUMZO YA VIPINDI VYA
SOBETAB KAPCHI KATIKA IDHAA YA *KASS FM***

NA

MUGE TECLA C. NGISIREI

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI, KATIKA IDARA YA
KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

CHUO KIKUU CHA MOI

2018

IKIRARI

IKIRARI YA MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya utafiti katika Chuo Kikuu kingine. Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku kunakili au kutolesha sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi.....Tarehe.....

Muge Tecla C. Ngisirei

SASS/DPHIL/KIS/05/14

IKIRARI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini na ridhaa yetu kama washauri na wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi.....Tarehe.....

Dkt. Mosol Mark Kandagor

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi.....Tarehe.....

Dkt. Opijah Allan Lennox,

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi.

TABARUKU

Kwako ewe mume wangu mpendwa,

kwa kunitia nguvu na kunipa msaada wa aina yoyote niliohitaji.

Hakika ulinishauri kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto za maisha.

Kwenu nyie wanangu; Jeruto, Kiplimo na Jemutai, kwa kunielewa muda wote

nilipojitenga nanyi kwa ajili ya kushughulikia kazi hii. Naam,

nawapokezeni mwanga huu wa elimu,

ambao ni hazina kuu katika maisha

ya sasa, mnapojiandaa kwa

maisha ya mbingu

mpya.

SHUKURANI

Kwa Jalali. Kwa kunipa uwezo wa kutekeleza mahitaji ya kazi hii. Kama si Mungu aliyekuwa nami, nisingefika hapa. Kama si Mungu aliyekuwa pamoja nami maji yangenigharikisha... kwa hivyo msaada wangu u katika jina la Bwana, aliyeziumba mbingu na nchi... **Zaburi 24:1, 6. Asante Yahweh.**

Shukrani za dhati kwenu nyie wasimamizi wangu Dkt. M. M. Kandagor na Dkt. A. L. Opijah ambao mlijitolea kwa moyo wote kunishauri na kunielekeza ili kuhakikisha ufanisi wa kazi hii. Bila ninyi nisingekuwa hapa. Mlinibidiisha kila wakati, na hiyo ilinitia hamu ya kujikaza, naam, matunda yameiva sasa. Awatuze Mola ajuavyo jamani!

Ninatambua juhudi zako Dkt. M. N. Wafula mwanzoni mwa kazi hii. Maoni yako yalinitia hamu ya kufanya kazi hii kwa bidii. Nilipolegea, hukuchoka kuniulizia kila wakati hatua niliyopiga. Mungu aibariki aila yako kwa ajili ya moyo wako mwema.

Dadangu H. K. Ibala, licha ya kazi yako kama hii, kwangu umekuwa msaada. Tulitiana nguvu pamoja na kujipa moyo, moyo wa kuendelea licha ya shughuli nyingi za hapa na hapa, matunda tutayavuna hakika. Maoni yako yalinipa nafuu wakati wa msongo.

Wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, heko kwa ushirikiano wenu. Wote walionifunza kama vile Prof. Simatei, Prof. Kahiga, Dkt. Obuchi, Dkt. Kandagor na Dkt. Makoti. Mihadhara yenu ilinifungulia njia na kunishawishi kufanya uteuzi wa mada hii. Maelekezo yenu wakati wa mawasilisho katika hatua zote mbili yalinijenga. Baraka tele tele.

Sitamsahau naibu wa mkuu wa kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii Prof. Maria Wahome. Kwangu ni dada kamili. Kila tulipokutana angenishawishi nimalize kazi hii kwa kunijaza utamu wa kuwa na Shahada ya Uzamifu. Kwa kweli mkono wa Maulana umneemeshe.

Kwenu wazamifu wenzangu, Joseph Mulalu, Barnabas Abuga, Ann Kyamba, Sophia Jeptoo, Hellen Barno, Sylvester Kimkung na Ramadhan Thomas Kadallah. Ushindi wa mmoja ni wetu sote. Mbele daima, nyuma kamwe. Neema ya Bwana na ukarimu wake ujalize mioyo yetu.

Kituo cha utangazaji cha idhaa ya *KASS FM* na watangazaji husika. Kwanza ni mwasilishaji mkuu Edward Rotich, na mwelekezi wa vipindi vya *Sobetab Kapchi* Winny Jepkorir. Mmekuwa msaada wa pekee kwangu. Hamkuchoka nilipowapigia simu kila nilipohitaji kujua kitu. Ndugu Rotich ulinivumilia nilipokutembelea ofisini na kuhitaji data fulani kutoka kwako. Nitawakumbuka siku zote na zaidi, Jalali atawakumbuka daima.

Mwisho ni kwa familia yangu. Shukrani za dhati kwa mume wangu ndugu Julius Muge pamoja na watoto wetu Abby Jeruto, Joel Kiplimo na Ruth Jemutai. Miaka mitatu niliadimika lakini mlinivumilia. Mlikuwa ngome na msaada katika safari yangu ya kukamilisha shahada hii. Matunda tutakula pamoja.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kushughulikia umuhimu wa upole katika mazungumzo kwa kuchanganua mikakati ya upole inayotumika katika vipindi vya *Sobetab Kapchi* (Maisha ya Jamii) kwenye idhaa ya *KASS FM*. Ili kutekeleza jukumu hilo, utafiti uliongozwa na madhumuni yafuatayo: kuchanganua mikakati ya upole inayotumika kuwasilisha vipindi vya *Sobetab Kapchi (SK)* katika idhaa ya *KASS FM*, kuhakiki athari za uzingatiaji na ukiukaji wa kanuni za upole kwenye vipindi vya *SK*, kutathmini hali zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole katika vipindi husika vya *SK* na kupambanua na kujadili changamoto zinazosawiriwa na wahusika wa mazungumzo ya *SK* wakati wa utekelezaji wa kanuni za upole. Aidha, utafiti uliongozwa na maswali manne. Kwanza, je, ni mikakati gani ya upole inatumika kuendeleza mazungumzo ya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*? Pili, uzingatiaji au ukiukaji wa mikakati ya upole una athari gani kwa mazungumzo ya vipindi vya *SK*? Tatu, Ni hali zipi zinaathiri uteuzi wa mikakati ya upole katika mazungumzo ya vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*? Mwisho, wahusika wa mazungumzo ya *SK* wanasawiri changamoto zipi wakati wa kutekeleza mikakati ya upole? Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Upole, hasa mhimili wa ‘kuokoa uso’, kama ilivyopendekezwa na Brown na Levinson. Kulingana na waasisi wa nadharia hii, uso ni thamani ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na atakavyo kuchukuliwa na wengine. Unarejelea kile ambacho mtu anatamani katika mawasiliano yoyote. Nadharia ya Upole inaeleza kuwa mtu ana aina mbili za uso; uso chanya na uso hasi. Aidha, nadharia hii inasisitiza kuwa mawasiliano yoyote hufanikiwa iwapo washiriki wa mazungumzo wanazingatia kanuni za upole kwa makusudi ya kuokoa nyuso zao na za wenzao. Isitoshe, kila mshiriki wa mazungumzo anatakiwa kuhisi kukubalika na kupewa uhuru wa kutoingiliwa. Sampuli ya utafiti iliteuliwa kimakusudi kuambatana na nadharia ya utafiti, malengo na maswali ya utafiti pamoja na upeo wa utafiti kwa kuangazia masuala mahsusi ya kipindi hiki kulingana na utamaduni wa jamii ya Kikalenjin. ‘Pasta’ Edward Rotich na mwelekezi wa vipindi Winny Jepkorir (‘Koriryo’), ni wahusika wakuu na pamoja nao ni mashabiki waliochangia katika vipindi husika. Vipindi vya *SK* vilisikilizwa kwa makini kabla ya kunaswa. Kinasa sauti kilitumika kukusanya data kwa kurekodi vipindi vinane vya *SK*. Mwisho, hoja zinazohusiana na upole zilinakiliwa na kuwekwa kwenye makundi manne ya mikakati ya upole ili kuchanganuliwa. Makundi hayo ni ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi na mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Uchanganuzi wa data ulifanywa kimaelezo kwa kutumia mazungumzo ya washiriki kama mifano halisi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wahusika wa mazungumzo ya *SK* hutumia mikakati anuwai ya upole kuwasiliana ili kudumisha mahusiano kati yao. Pia, wahusika hao hukumbana na changamoto nyingi wanapotekeleza mikakati ya upole wakati wa mazungumzo. Kutokana na matokeo hayo, utafiti huu ni matini muhimu katika uwanja wa mawasiliano kwenye vyombo vya habari hasa vya redio. Utafiti huu ni mchango mkubwa kwa taaluma ya isimu, hasa kwa wale walimu na wanafunzi wa uamali na isimu-jamii, wanaotafitia suala la upole katika mazungumzo kwenye vyombo vya habari katika lugha yoyote ya Kiafrika, hasa lahaja za Kikalenjin. Pendekezo la jumla ni kuwa watafiti wajitokeze kushughulikia masuala ya upole katika nyanja za fasihi na tafsiri.

ABSTRACT

The study aimed at analyzing politeness strategies that are employed in airing *Sobetab Kapchi* (Family Life), a radio program of *KASS FM*. It sought to establish ways in which politeness strategies were evident in the program and how they are used to strengthen and maintain good relationships among the participants of *Sobetab Kapchi* (*SK*) radio program. Specifically, the study sought to: one, analyze politeness strategies that are employed by speakers and listeners of *SK* radio program. Two, critique the effects of observing or infringing politeness strategies in *SK*. Third, evaluate circumstances that influence the choice of politeness strategy. Fourth, identify and discuss challenges that face the participants of *SK* radio program when adhering to politeness rules. The study was guided by the following research questions: Which politeness strategies are employed by participants of *SK* radio program of *KASS FM*? What are the effects of employing or breaking politeness rules during *SK* radio program conversation? Under what circumstances do conversationalists of *SK* choose to use a politeness strategy over another? Finally, what are the challenges facing participants of *SK* radio program when employing politeness rules? This study was guided by Politeness Theory, especially ‘face saving’ tenet as proposed by Brown and Levinson. According to this theory, face is a positive social value that individuals have in respect to what others take them for. It is a feeling that one wishes to have in every communication. Politeness Theory claims that during communication, every other person has either one of the two types of faces, i.e. a positive and a negative face. It maintains that for a successful communication in every social interaction, each participant should employ politeness strategies in order to ‘save their faces’. Moreover, participants of any dialogue should feel affirmed and protected from intrusion against their will. Data was purposively sampled in regard to the research theory, objectives, research questions and the scope of the study and in consideration of basic issues chosen in the program according to Kalenjin speakers. *SK* program was purposively selected from many other programs due to its openness in relaying themes on family issues. ‘Pastor’ Edward Rotich, the main presenter and Winny Jepkorir (‘Koriryo’) are the main participants of the program. With them are fans of the program who contribute during presentations. To collect data, the program was keenly listened to. A tape recorder was used to record eight sessions of *SK* program. Finally, data regarding politeness was decoded and classified into the following four groups: On-record politeness strategies, positive politeness strategies, negative politeness strategies and off-record politeness strategies. Data was analyzed descriptively using conversations of participants as major examples. From the analysis, it was evident that participants of *SK* radio program employ several politeness strategies to enable them maintain good relationships. Secondly, the participants of the *SK* encounter many challenges when employing politeness rules during the program. This study will be a valuable resource to teachers and students of pragmatics and sociolinguistics who wish to study politeness strategies in media programs aired in African languages more so, in Kalenjin dialects. The general recommendation of the study is that more researchers should study on politeness strategies employed in other fields like literature and translation.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKURANI.....	iv
IKISIRI	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO	viii
UFAFANUZI WA ISTILAHU	xiii
TAFSIRI YA MSAMIATI	xvi
MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO	xvii
SURA YA KWANZA	1
MISINGI YA UTAFITI	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti	1
1.1.1 Mazungumzo kwenye Vipindi vya Redio	3
1.1.2 Maisha na Tajriba ya Mwasilishaji Mkuu.....	6
1.1.3 Dhana ya Lugha	9
1.1.4 Kanuni za Mazungumzo.....	10
1.1.4.1 Kupokezana Zamu	10
1.1.4.2 Usikivu na Umakinifu	11
1.1.4.3 Kuzungumza kwa Sauti	12
1.1.5 Upole katika Utamaduni wa Kikalenjini	13
1.2 Suala la Utafiti	15
1.3 Malengo ya Utafiti	17
1.4 Maswali ya Utafiti.....	17
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	17
1.6 Umuhimu wa Utafiti	19
1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	20
1.8 Mbinu za Utafiti	21
1.8.1 Utangulizi	21
1.8.2 Eneo la Utafiti	21
1.8.3 Utafiti Mwigo.....	23
1.8.4 Uteuzi wa Sampuli	24

1.8.5 Vifaa vya Kukusanya Data.....	26
1.8.6 Ukusanyaji wa Data	27
1.8.7 Unukuzi wa Data.....	28
1.8.8 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data.....	28
1.9 Hitimisho.....	28
SURA YA PILI.....	30
MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA.....	30
2.0 Utangulizi.....	30
2.1 Dhana ya Upole.....	30
2.2 Mazungumzo kwenye Vyombo vya Habari	32
2.3 Tafiti Zinazohusiana na Mada ya Utafiti	34
2.4 Msingi wa Nadharia.....	39
2.4.1 Upole Kulingana na Lakoff (1973)	39
2.4.2 Upole kulingana na Leech (1983)	40
2.4.2.1 Upole kama Kaida ya Mkakati	41
2.4.2.2 Upole kama Kaida ya Ukarimu	41
2.4.2.3 Upole kama Kaida ya Kumsifu Msikilizaji	42
2.4.2.4 Upole kama Kaida ya Kujitweza	42
2.4.2.5 Upole kama Kaida ya Makubaliano	43
2.4.2.6 Upole kama Kaida ya Kumwonea Huruma Msikilizaji.....	43
2.4.3 Upole Kulingana na Fraser (1990)	44
2.4.3.1 Upole kama Kaida ya Kijamii	44
2.4.3.2 Upole kama Mkakati wa Mazungumzo	44
2.4.3.2.1 Kanuni Ushirika	45
2.4.3.3 Upole kama Mkataba wa Mazungumzo	49
2.4.4 Upole Kulinganana na Brown na Levinson (1978, 1987).....	49
2.4.4.1 Upole kama Mkakati wa Kuokoa Uso.....	49
2.4.4.2 Vitendo Vinavyotishia Uso	51
2.4.4.3 Kukabiliana na Vitendo Vinavyotishia Uso	52
2.4.4.3.1 Kuwa Kwenye Rekodi	52
2.4.4.3.2 Mkakati wa Upole Chanya.....	54
2.4.4.3.3 Mkakati wa Upole Hasi	56
2.4.4.3.4 Mkakati Nje ya Rekodi	60
2.4.4.3.5 Mkakati wa Kutosema Ujumbe Unaotishia uso.....	63

2.5 Hitimisho.....	65
SURA YA TATU.....	67
MIKAKATI YA UPOLE KATIKA VIPINDI VYA SOBETAB KAPCHI	67
3.0 Utangulizi.....	67
3.1 Upole Chanya Katika Vipindi vya <i>SK</i>	67
3.1.1 Kuepuka Kutokubaliana.....	68
3.1.2 Kutumia Utambulisho wa Usonde Jamii.....	71
3.1.3 Kuchopeka na Kurefusha Irabu [i] Mwishoni mwa Vitenzi amrifu.....	73
3.1.4 Kumtambua Msikilizaji.....	75
3.1.5 Kutumia Ucheshi.....	77
3.1.6 Kutafuta Makubaliano.....	78
3.1.7 Kuwa Mrajua.....	81
3.1.8 Kujitambulisha na Kundi Moja na Msemezwa.....	83
3.1.9 Kumchenga Msikilizaji	85
3.1.10 Kudai Hali ya Kutendeanana	88
3.1.11 Matumizi ya Chuku.....	89
3.1.12 Kumwelewa Msikilizaji	92
3.1.13 Kutoa Ahadi kwa Msikilizaji	94
3.1.14 Kutanguliza Mawali kabla ya Kutoa Sababu ya Kitendo	95
3.1.15 Kuzidisha Kauli Zinazomshawishi Msikilizaji Kukubaliana na Msemaji	98
3.2 Upole Hasi Katika Vipindi vya <i>SK</i>	99
3.2.1 Kuwa Bila Rajua	100
3.2.2 Matumizi ya Kauli za Jumla.....	103
3.2.3 Matumizi ya Vitangulizi.....	105
3.2.4 Kuuliza Maswali	108
3.2.5 Kutokuwa Bayana	110
3.2.6 Kutaja Kitendo cha Kutisha Uso kama Kanuni ya Ujumla.....	112
3.2.7 Kupunguza Ulazimishaji wa Kauli	115
3.2.8 Kudhihirisha Staha/Heshima Baina ya Msemaji na Msikilizaji.....	117
3.3 Mkakati Ndani ya Rekodi	119
3.3.1 Wakati Washiriki wa Mazungumzo Wanahusiana kwa Karibu.....	120
3.3.2 Katika Mazingira ya Dharura.....	122
3.3.3 Wakati Msemaji na Msikilizaji Wanatofautiana Kimamlaka	123
3.4 Mkakati Nje ya Rekodi	125

3.4.1 Kutumia Maelezo Pungufu.....	125
3.4.2 Matumizi ya Vidokezo	126
3.4.3 Kutumia Maswali ya Balagha	127
3.4.4 Udondoshaji wa Kauli.....	130
3.3.5 Matumizi ya Kejeli yenye Ucheshi	132
3.5 Hitimisho.....	133
SURA YA NNE	134
ATHARI ZA UZINGATIAJI NA UKIUKAJI WA MIKAKATI YA UPOLE	
KATIKA VIPINDI VYA <i>SOBETAB KAPCHI</i>	134
4.0 Utangulizi.....	134
4.1 Athari za Uzingatiaji wa Mikakati ya upole	135
4.1.1 Kukuza Heshima Baina ya Wahusika wa Mazungumzo	135
4.1.1.1 Matumizi ya Misemo.....	136
4.1.1.2 Matumizi ya Methali	139
4.1.1.3 Matumizi ya Ubadilishaji Msimbo	143
4.1.1.4 Kuzungumza kwa Zamu	145
4.1.1.5 Matumizi ya Sifa za Kiarudhi.....	148
4.1.1.6 Udondoshaji wa Maneno/kauli	151
4.1.2 Kufurahisha na Kuwavutia Mashabiki	154
4.2 Athari za Ukiukaji wa Mikakati ya Upole katika Mazungumzo ya <i>SK</i>	158
4.2.1 Matumizi ya Lugha Mwiko.....	160
4.2.2 Kukatizana Zamu	163
4.2.3 Matumizi ya Kauli Zinazolenga Kundi Maalum.....	166
4.2.4 Kuzungumzia Mada Zinazotishia Uso wa Hadhira.....	169
4.3 Hitimisho.....	171
SURA YA TANO	173
HALI ZINAZOATHIRI UTEUZI WA MIKAKATI YA UPOLE NA	
CHANGAMOTO ZA MIKAKATI HIYO KATIKA VIPINDI VYA <i>SOBETAB</i>	
<i>KAPCHI</i>	173
5.0 Utangulizi.....	173
5.1 Hali Zinazoathiri Uteuzi wa Mkakati wa Upole	174
5.1.1 Faida za Mkakati	175
5.1.1.1 Faida za Mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi	175
5.1.1.2 Faida za Mkakati wa Upole Chanya.....	178

5.1.1.3 Faida za Mkakati wa Upole Hasi.....	180
5.1.1.4 Faida za Mkakati wa Kuwa Nje ya Rekodi	184
5.1.1.5 Faida za Mkakati wa Kutosema Kabisa Jambo la Kutishia Uso	187
5.1.2 Sababu za Kijamii	189
5.1.2.1 Tofauti za Kiumri Kati ya Wahusika wa Mazungumzo	189
5.1.2.2 Tofauti za Kijinsia kati ya Msemaji na Msemezwa	191
5.1.2.3 Uwezo wa Kitabaka/Kihadhi kati ya Msemaji na Msikilizaji	194
5.1.2.4 Muktadha wa Mazungumzo	197
5.1.2.5 Mada ya Mazungumzo	200
5.2 Changamoto za Matumizi ya Mikakati ya Upole	202
5.2.1 Changamoto za Mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi	203
5.2.2 Changamoto za Mkakati waUpole Chanya.....	204
5.2.3 Changamoto za Mkakati Hasi wa Upole.....	205
5.2.4 Changamoto za Mkakati wa Kuwa Nje ya Rekodi	206
5.2.5 Changamoto za Mkakati wa Kutosema Kabisa Kitendo cha Kutishia Uso ..	211
5.3 Hitimisho.....	211
SURA YA SITA.....	213
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	213
6.0 Utangulizi.....	213
6.1 Muhtasari wa Tasnifu	213
6.2 Matokeo ya Utafiti	220
6.3 Mchango wa Utafiti	222
6.4 Hitimisho.....	223
6.5 Mapendekezo Kuhusu Tافiti Zijazo.....	224
MAREJELEO	226
VIAMBATISHO.....	236
Kiambatisho I: Baadhi ya Data ya Kikalenjin Iliyochanganuliwa.....	236
Kambatisho II: Tafsiri (Kwa Kiswahili) ya Baadhi ya Data Iliyochanganuliwa ...	240
Kiambatanisho III: Idhini ya Utafiti Kutoka kwa Mtayarishi wa <i>SK</i>	244
Kiambatanisho IV: Idhini ya Utafiti Kutoka <i>KASS MEDIA</i>	245
Kiambatanisho V: Idhini ya Utafiti Kutoka <i>NACOSTI</i>	246

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Upole** Ni dhihirisho la nia ya msemaji la kutaka kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji wakati wa mazungumzo.
- Mikakati ya upole** Mbinu zinazotumiwa na wazungumzaji kukinga mkwaruzano baina yao na kuhakikisha kuwa wanajaliana kihisia. Ni kanuni zinazobuniwa na kutumiwa na wahusika wa mazungumzo ya *SK*, hasa msemaji, wakati amelazimika kutaja kitendo kinachotishia uso ili kuhakikisha kuwa anatunza uso wa msemazwa.
- Uso** Neno hili limetumiwa kuashiria kile ambacho mtu anatamani katika mawasiliano yoyote.
- Uso chanya** Haja ya kila mhusika wa mazungumzo kutaka kukubalika na wengine. Ni haja ya kutaka kupendwa, kutamaniwa na kukubalika kwa hoja anazotoa mtu wakati wa mazungumzo.
- Uso hasi** Umetumika kwa maana ya nia ya msikilizaji ya kutaka kujiwekea mipaka na uhuru wa kutoingiliwa na msemaji bila idhini yake.
- Kitendo kinachotishia uso**
- Ni lugha/usemi unaoibua hisia za aibu au kuonekana kumlazimisha msemaji au msikilizaji kutekeleza kitu kinyume na matakwa yake. Ni kufanya/kusema kinyume na mahitaji au matarajio ya wengine.

Matendo yanayotishia uso hasi

Ni mazungumzo ambayo hufanywa bila kujali hisia za wahusika wa mazungumzo. Ni mazungumzo yanayozuia uhuru wa kuchagua na hivyo kumlazimu msemaji au msikilizaji kukubali kupoteza uhuru huo kwa kutekeleza jambo asilotaka.

Matendo yanayotishia uso chanya

Ni lugha inayobagua na kuonyesha mipaka ya mahusiano au kihadhi kati ya wahusika wa mazungumzo ya *SK*. Uso chanya hutishiwa wakati mhusika mmoja wa mazungumzo hajali hisia au hataki mahitaji ya mwenzake.

Mwasilishaji mkuu

Ni ‘Pasta’ Edward Rotich ambaye ni galacha wa masuala ya ndoa na hutoa mashauri kwa wanandoa kwa kutoa suluhu ya mambo ambayo yanachangia ulegevu wa ndoa nyingi katika jamii husika ya Wakalenjin.

Mwelekezi wa vipindi

Huyu ni Winny Jepkorir (‘Koriryo’) ambaye ni mtangazaji wa *KASS FM* na ambaye ni mwelekezi wa vipindi vya *SK*. Yeye hushirikiana na mwasilishaji wa Vipindi kwa kumchochea ili kuhakikisha kuwa mashabiki hufurahia na kuchangia mada za vipindi husika.

- Mashabiki** Hawa ni wasikilizaji wanaosikiliza na kuchangia vipindi vya *SK* kwa kutuma jumbe zao kupitia simu za rununu. Ni wazazi wa umri mbalimbali ambao hufanya vipindi kuvutia kwa kuuliza maswali ili kuhakikisha mwendelezo wa vipindi.
- Vipindi** Ni mada zote nane za *Sobetab Kapchi* zilizohusishwa katika uchanganuzi. Inatumiwa kurejelea kipindi chote cha *Sobetab Kapchi* kinachowasilishwa na pasta Rotich kila siku ya Jumatano, saa nne hadi saa sita usiku..
- Kipindi** Neno hili limetumiwa kuashiria mada mojawapo ya vipindi vinane vya *Sobetab Kapchi*. Ni mjadala wa siku moja wenye mada moja na inayozungumziwa kwa siku moja.
- A, B, C, D, E, F, G ...** Herufi hizi zinatumiwa kama majina ya mashabiki ambao majina yao yamebanwa kwa minajili ya kuepuka kutaja majina kamili ya mashabiki.

TAFSIRI YA MSAMIATI

Kiswahili		Kiingereza
Kaida ya kiasi	-	Maxim of quantity
Kaida ya namna	-	Maxim of manner
Kaida ya ubora	-	Maxim of quality
Kaida ya uhusiano	-	Maxim of relevance
Kanuni Ushirika	-	Cooperative principle
Kuwa bila urajua	-	To be pessimistic
Kuwa mrajua	-	To be optimistic
Mbinu ya kiustahimilifu	-	Qualitative method
Mhimili	-	Tenet
Mikakati ya upole	-	Politeness strategies
Mkakati wa kuwa kwenye rekodi	-	Bald on-record politeness strategy
Mkakati wa kuwa nje ya rekodi	-	Off-record politeness strategy
Nadharia ya Upole	-	Politeness Theory
Upole chanya	-	Positive politeness
Upole hasi	-	Negative politeness
Vitendo vinavyotishia uso	-	Face threatening acts
<i>Sobetab Kapchi</i> (Maisha ya Jamii)	-	Family Life

MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO

<i>FM</i>	-	<i>Frequency Modulation</i>
Kik.	-	Kikalenjin
Kis.	-	Kiswahili
Kur	-	Kurasa
Mhar.	-	Mhariri
<i>SK</i>	-	<i>Sobetab Kapchi</i>
TUKI	-	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Uk	-	Ukurasa
Wahr.	-	Wahariri

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii imeweka misingi ya taratibu zilizoongoza utafiti huu. Katika sehemu hii, tumebainisha usuli wa suala la utafiti ambapo diskosi kuhusu upole katika vipindi vya *Sobetab Kapchi (SK)* kwenye idhaa ya *KASS FM* imehakikiwa. Pia, sura hii inafafanua suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Aidha, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti umeelezwa kwa kina. Mwisho, mbinu zilizotumika kufanikisha utafiti zimefafanuliwa kwa utendeti.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Lugha ni zana inayotumika kukuza uhusiano baina ya watu. Wakati wa kuwasiliana, watu huchagua mbinu zinazowawezesha kupatana. Washiriki wa mazungumzo hutumia mbinu zinazohakikisha kuwa mawasiliano yanafanyika bila mkwaruzano. Jamii ina kaida mbalimbali ambazo hutumika wakati wa mazungumzo. Ili kuwe na mlahaka mzuri kati ya wanajamii, wahusika katika mazungumzo yoyote yale hufuata kanuni za mazungumzo katika jamii husika. Jamii huanzisha na kudumisha mahusiano mema baina ya watu kupitia mitagusano ya kila siku. Uhusiano huo unalenga kuteka makini ya msikilizaji na kuufanya ujumbe unaopitishwa kuwa muhimu kwake (Sperber & Wilson, 2004).

Mahusiano hayo hudumishwa wakati wanajamii wanazingatia mikakati mbalimbali ya upole katika mazungumzo yao. Mikakati hiyo ni ya upole na ina kanuni kadhaa kuhusu namna ya kuwasiliana. Mikakati ya upole ni mbinu wanazobuni wahusika wa mazungumzo ili kujaliana na kuhakikisha kuwa mazungumzo yao yanafana. Kuwa

mpole hakumhitaji mtu kujua lugha tu bali pia kuelewa kaida na tamaduni zinazothaminiwa na jamii husika.

Mikakati ya upole huzingatiwa ili 'kuokoa nyuso' za wahusika wa mazungumzo. Maelezo hayo yanaashiria upole kama hali ya kuonyesha heshima kwa washiriki wengine katika mazungumzo. Ili kudumisha upole, wanajamii-lugha huzingatia kaida fulani za lugha husika. Kama asemavyo Goffman (1967), upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kwa kuzingatia au kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo. Kwa ujumla, kuwa mpole ni kujali hisia za wengine kwa kuhakikisha kuwa wanastareheka.

Matumizi ya maneno au matendo ya upole huashiria taratibu, adabu na heshima katika lugha husika. Akishadidia wazo hili, Qanbar (2011) anasema kuwa urazini humwezesha mtu kuendeleza haiba chanya. Haiba hii humwezesha mwanajamii kuwa na mazoea ya kudumisha tabia zenye kuvutia heshima, unadhifu na uongofu. Wazungumzaji wanapozingatia nidhamu katika mawasiliano, huonekana kuwa na utaratibu mzuri wa kutekeleza shughuli zao. Wanajamii wanaofanya kinachokubalika na kupendeza mbele ya wenzao huchukuliwa kuwa watu wenye adabu na staha. Mwanadamu atangamanapo na wenzake, huzingatia viwango vya kimsingi kitabia, vinavyomwezesha atende matendo yanayokubalika. Viwango hivyo vya kimsingi humwezesha kuzingatia kaida maalum kulingana na jamii-lugha husika.

Kwa mujibu wa Leech (1983), upole ni kama maumbo yanayothibitisha na kudumisha uhusiano wa kirafiki. Ni uwezo wa washiriki katika mtagusano wa kijamii kujihusisha na mazingira yanayowiana na matakwa ya jamii. Mathalan, watu wanapoongea hutumia maneno ambayo hukuza uhusiano unaoweza kuwa ama mwema au mbaya. Mtu mpole husema na kufanya mambo bila kuwaudhi wengine. Katika kikosi cha

askari kwa mfano, tunaona mahusiano ya kimamlaka askari wakiwa kazini. Yule wa cheo cha juu azungumzapo, askari wa cheo cha chini hujibu “Yes sir” (ndio afande). “Yes sir” (ndio afande) huchukuliwa kama usemi wenye upole na heshima.

1.1.1 Mazungumzo kwenye Vipindi vya Redio

Utanzu wa mazungumzo kwenye vyombo vya habari hujadili mada nyingi zinazovutia na kwamba uchanganuzi wa upole ni moja tu ya mada hizo (Petrickova, 2012). Kuna sababu nyingi ambazo kwazo utanzu wa mazungumzo katika vyombo vya habari unafaa kuchanganuliwa katika mtazamo wa upole. Mazungumzo kwenye vyombo vya habari huashiria muundo wa mazungumzo ambao hutawaliwa na kanuni nyingi za mazungumzo rasmi. Vilevile, kulingana na Petrickova (2012), uhusiano tata baina ya makundi yanayoshiriki mazungumzo hayo huashiria umuhimu wa uteuzi makinifu wa mikakati ya upole katika mazungumzo yoyote.

Vipindi vya redio ni njia mojawapo ya kufahamisha umma kuhusu masuala tofauti ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Vipindi hivi huwa ama vimerekodiwa awali kabla ya kupeperushwa hewani au hupeperushwa hewani moja kwa moja wakati wa mazungumzo/mahojiano. Washika dau huwaalika wataalamu mbalimbali walio na tajriba kuhusiana na mada tofautitofauti, ili kuwahusisha katika mijadala ya kuwafahamisha wanajamii kuhusu matatizo yanayowakumba na vilevile namna ya kukabiliana na matatizo hayo.

Nchini Kenya, kuna vituo vya redio vinavyopeperusha vipindi kupitia lugha rasmi; Kiswahili na Kiingereza. Baadhi ya vituo hivi ni *Citizen*, *Kiss FM*, Redio Maisha, *KBC* na *BBC*. Kuna vituo vinavyorusha matangazo kwa lugha za mama. Vituo hivyo ni pamoja na *Musi FM* (Kikamba), *Kass FM* (Kikalenjin), *Inooro FM* (Kikikuyu), *Chamgei FM* (Kikalenjin), *Ramogi FM* (Kiluo), *Kitwek FM* (Kikalenjin), *Sulwe FM*

(Kiluhya), *Ingo FM* (Kiluhya) na *Emoo FM* (Kikalenjin) miongoni mwa vituo vingine. Vituo hivi hupeperusha vipindi mbalimbali vya mazungumzo kupitia kuwahoji viongozi katika taaluma mbalimbali pamoja na wasanii na wataalamu katika nyanja mbalimbali.

KASS FM ni kituo cha kibinafsi nchini Kenya. *Kass* ni neno linalotumiwa na lahaja za Kikalenjin kwa maana ya ‘sikia’ na kwa hivyo hutumiwa katika idhaa hii kurejelea kituo kinachosikizwa na wasemaji wa Kikalenjin. Ogechi (2002) anafafanua lahaja kama tawi au mgawanyiko wa lugha kutokana na sababu za kijiografia au kijamii. Anaendeleza kuwa sababu hizo hazizuii au kutatiza mawasiliano kati ya watumiaji wa lugha husika. Kulingana na tovuti ya www.kassfm.co.ke, vipindi vya redio ya *KASS FM* husikilizwa na zaidi ya asilimia 92 ya Wakalenjin wanaoishi nchini Kenya kando na wasikilizaji Wakalenjin wanaoishi nchi jirani kama vile Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini. Isitoshe, baadhi ya Wakalenjin wanaoishi ughaibuni husikiliza kituo hiki na mara nyingi huchangia katika mada husika.

KASS FM ilianzinshwa mnamo mwaka wa 2005 kutokana na kuongezeka kwa hitaji la kuwepo vituo vinavyofanya matangazo kwa lugha za kiasili. Kwanza, kituo cha *KASS FM* kilianza kwa kurusha matangazo yake kufikia sehemu za Nairobi na vitongoji vyake. Baada ya muda mfupi, matangazo hayo yalipanuliwa na kufikia wasemaji wa Kikalenjin katika sehemu iliyokuwa mkoa wa Bonde la Ufa. Kwa sasa, matangazo ya *KASS FM* huwafikia karibu watu wote nchini Kenya (Kass Media, 2011). Hata hivyo, jamii kubwa inayosikiliza kituo hiki ni ya lahaja za Kikalenjin.

Huntingford (1953) anatoa orodha ya lahaja kumi na nne za Kikalenjin: Kinandi, Kitugen, Kikipsigis, Kikeiyo, Kimarakwet, Kipokot, Kiendo, Kiterik, Kikony, Kisapei, Kipok, Kisabaot, Kipsurai na Kimbai. Kutokana na sensa ya 2009,

Wakalenjin ni zaidi ya milioni tano na hivyo huwakilisha sehemu kubwa ya Wakenya. Licha ya kuwa na lahaja hizo zote, mara nyingi idhaa ya *KASS FM* hutumia lahaja ya Kinandi kuwasilisha vipindi vyake. Hii ina maana kuwa data nyingi katika *SK* ni za Kinandi.

Kwa mujibu wa Boen (2014), Kinandi kilikuwa lahaja ya kwanza kati ya lahaja zote za Kikalenjin kuwekwa katika maandishi na baadaye kufuatwa na Kikipsigis. Kinandi na Kikipsigis hukaribiana sana kimaandishi na pia kileksia. Wamishenari walipokuja nchini Kenya, walihitaji tafsiri za vitabu vya nyimbo za Kikristo, Bibilia na vitabu vya maombi katika lugha za Waafrika. Vitabu hivyo vilitafsiriwa katika Kinandi ili kuwafaidi Wakalenjin wote. Hii ndiyo sababu kuu inayofanya Kinandi kuchukuliwa kama lahaja ya wastani kwa Wakalenjin wote. Hata hivyo, kuna baadhi ya wasomi kama vile Koske (2006), ambao wanapinga dai hilo na kutetea kuwa Kikipsigis ndiyo lahaja inayoeleweka kwa Wakalenjin wote. Utafiti huu unakubaliana na madai yote mawili lakini tumechagua kutumia Kinandi kwa sababu kwanza, vipindi vya *SK* huwasilishwa kwa lahaja ya Kinandi, pili, mtafiti ni Mnandi na anakifahamu sana Kinandi. Tatu ni kwamba, mwasilishaji mkuu wa vipindi hivi ni Mnandi.

Kituo cha redio cha *KASS FM* kina vipindi anuwai kama vile: *Kwondo ne Ng'om* (Mke Mwenye Hekima), *Len Nee Emet?* (Kuna nini Nchini?), *Teeb si Inai* (Uliza Ujibiwe), *Twoliot* (Mambo ya Ngono), *Kass Taibwotii* (Sikia! Bado Wakumbuka), *Heshimu ukuta*, *Tigitiotab Bambaniat* (Chanzo cha Mapenzi) na kipindi kimojawapo maarufu ni *Sobetab Kapchi (SK)* (Maisha ya Jamii).

Kwa mujibu wa www.kassfm.co.ke, vipindi vya *SK* vina mashabiki wengi kutokana na mada zake ambazo huwajua wasikilizaji mengi kuhusiana na masuala ya kijamii hasa katika asasi ya ndoa. Vipindi hivi huangazia masuala kama vile: sababu za

kuvunjika kwa ndoa, ‘mpango wa kando’, wakati wa kupeana talaka, mahusiano katika ndoa, ubakaji wa wanawake, usafi, mahusiano na mashemeji na jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo.

Vipindi vya *SK* ni maarufu kutokana na sababu kuwa wasikilizaji hupewa fursa ya kuchangia kwa kuuliza maswali au kutoa maoni yao. Kupitia kwa vipindi hivi, wasemaji wa Kikalenjin hupata sio tu ufahamu kuhusu masuala tofauti katika jamii bali hata burudani. Aidha, mwasilishaji mkuu wa vipindi pamoja na mwelekezi wa vipindi wana namna ya kipekee ya kuwasiliana na wasikilizaji wao ili wapate kuelewana.

1.1.2 Maisha na Tajriba ya Mwasilishaji Mkuu

Katika mazungumzo ya vipindi vya *SK*, mwasilishaji mkuu ni Edward Rotich. Rotich alizaliwa siku ya Jumapili tarehe 12/03/1967 nchini Uganda. Babake alikuwa mwana wa pekee kwa wazazi wake na hivyo hakushughulikia utafutaji wa mali kwa sababu aliirithi kutoka kwa wazazi wake. Kufikia mwaka wa 1976, wazazi wa Rotich walihamia Kenya na Rotich akaanza masomo yake ya darasa la kwanza mwaka wa 1977. Akiwa darasa la tatu, wazazi wake walitengana kwa sababu ya mateso ya babake kwa mamake. Hayo yalitokea kwa sababu baba hakuzoea kutafuta mali ili kukidhi mahitaji ya jamii yake.

Kutengana kwa wazazi kulimlazimisha Rotich akimbilie kwa mjomba, kisha kwa shangazi na mwisho kwa nyanya aliyemzaa baba. Rotich alishuhudia na kupitia changamoto nyingi kutokana na maisha ya kuishi kwa watu wasiokuwa wazazi wake. Alizoea maisha ya vita kila wakati jamaa hao walipokosana na kupigana. Aidha, aliteswa na jamaa hao kwa kulazimishwa kufanya kazi ngumu akiwa na umri mdogo sana. Aliona jinsi wasichana wa watu walivyoolewa kwa jamii hizo na kuchapwa na

waume zao kila walipojaribu kujitetea. Katika mwaka wa 1980, wazazi wa Rotich walirudi kuishi pamoja na Rotich akarudishwa nyumbani. Kutowajibika kwa babake hakukukoma. Baba huyo aliendelea kumtesa mamake hadi watoto wakazoea maisha kama hayo na ikawa kawaida kwao kutoroka nyumbani baba afikapo.

Tajriba hii ngumu ilimpa Rotich hamu ya kutaka kuwanasua wanajamii kutoka kwa mtego wa shetani wa kutaka kutenganisha jamii. Rotich aliendelea na masomo yake na baada ya muda mrefu wa shida na majuto, alikamilisha kidato cha nne akiwa na miaka 26. Kwa sababu alikuwa kifungua mimba, Rotich alilazimika kuwashughulikia nduguze kwanza kabla ya kuo. Mwaka wa 1992 ulikuwa baraka kwa Rotich kwa sababu alipata jiko na maisha yake yakabadilika kutoka yale ya jamii yenye vita kila wakati na kuwa ya furaha. Shida alizopitia Bw. Rotich wakati akiishi na jamaa wa wazazi wake zilimpa motisha ya kutaka kubadilisha hali ya jamii yake. Kuanzia hapo, Rotich alijizatiti kuhakikisha kuwa mkewe na watoto walipata mapenzi, mahitaji na malezi bora.

Rotich aliamua kukita mawazo yake katika maisha ya jamii hasa yale yanayohusu ndoa. Alichukua mkondo wa kutoa mawaidha na kuwashauri wanandoa kuhusiana na masuala nyeti kama vile malezi, uke wenza, talaka na mapenzi. Jambo hilo lilimuelekeza kusomea kozi zinazohusiana na maisha ya jamii. Alianza masomo hayo na akapata stahahada 3 katika masuala yanayohusiana na ndoa. Stahahada ya kwanza ni katika ushauri kwa mambo ya ndoa (Family Counseling). Ya pili ni katika haki za binadamu na hasa kwa kujikita katika haki za wanawake na watoto (Children's and Women's Rights). Ya mwisho ni katika mambo ya kijinsia (Gender and Civic Education).

Masomo hayo yalimpa Rotich fursa ya kutangamana na wanandoa wengi katika eneo la Uasin Gishu. Siku zilipoendelea kupita, umaarufu wake ulifikia vyombo vingi vya habari na ndipo akaalikwa kufanya matangazo yake katika idhaa ya *KASS FM*. Alianza kufanya kazi katika kituo hicho cha radio siku ya Ijumaa, tarehe 04/05/2007. Kwa muda mrefu, Rotich amekuwa akitoa ushauri kanisani, kwenye mikutano ya wanawake, katika mikusanyiko ya wazee na pia katika makambi ya vijana kuhusiana na masuala ya ndoa. Umaarufu wa kazi yake ulipoenea zaida, alipata mialiko mingi mpaka akaamua kufungua ofisi mjini Eldoret aliyoiita “Kliniki ya Ndoa” ili kuwahudumia wateja waliomhitaji kwa siri. Uzoefu huu wa kushauri, kuonya na kutoa mwelekeo ndio msingi wa lakabu ya jina ‘Pasta’. Kwa kweli Rotich si kasisi wa dhehebu lolote lakini kazi anayoifanya na namna anaifanya imempa sifa nyingi mno za ukasisi.

Pamoja na ‘Pasta’ Rotich, kuna mwelekezi wa vipindi Winny Jepkorir. Katika jamii ya Wakalenjin, watu hupewa majina kulingana na wakati wa kuzaliwa. Jina ‘Jepkorir’ lina maana ya kuzaliwa asubuhi na mapema kabla ya jua kuchomoza. Baada ya kuzoeana na kutaniana na mashabiki wake, Winny amepewa lakabu ‘Koriryo’ ambalo linatokana na ufupishaji wa jina Jepkorir. Jepkorir ni jina la mwana wa Kike aliyezaliwa asubuhi sana kabla ya kuchomoza jua. Mara nyingi utamsikia ‘Koriryo’ akisema kiutani kuwa siku zake zote zina heri kwa sababu alizaliwa asubuhi wakati mamake alikuwa akianza siku mpya.

Rotich na Jepkorir wanatumia lugha inayovutia kuwasiliana na wasikilizaji wao ambao ni mashabiki wa vipindi vya *SK*. Lugha hiyo yenye mnato inawafanya kuwa na mashabiki wengi. Ni bayana kuwa, lazima kuna mikakati fulani ambayo waendeshaji wa vipindi hivi huzingatia ili kuimarisha mawasiliano na wateja wao. Vinginevyo, vipindi vyao vingekatika baada ya muda au kukosa mchango wa wasikilizaji.

1.1.3 Dhana ya Lugha

Azma yetu kuu ni kubainisha na kujadili mikakati ya upole inayotumika katika vipindi vya *SK*. Mikakati hii huwasilishwa kwa njia ya mazungumzo na mazungumzo hayo ni lugha. Hivyo basi, mjadala kuhusu mikakati ya mazungumzo hautakamilika bila kufafanuliwa kwa dhana ya lugha.

Wataalamu wengi wamefafanua dhana ya lugha kwa njia tofautitofauti. Kandagor (2014) anahoji kuwa lugha ina tafsiri nyingi na hivyo si rahisi kupata ufafanuzi wa moja kwa moja. Hoja hii inaungwa mkono na Habwe (2004) ambaye anasema kuwa lugha si rahisi kutolewa ufafanuzi bali hutumika kila siku na wanajamii-lugha kama mfanyiko wa kawaida. Maelezo hayo yanaonyesha kuwa lugha inaweza kufafanuliwa kwa njia nyingi mno. Hata hivyo,fafanuzi hizi zote zinaelekea kutoa wazo moja la kuashiria kuwa lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano.

Algeo na Pyles (2004) wanatoa maelezo ya lugha kama mfumo wa sauti zinazobuniwa na wanadamu kwa minajili ya kuwasiliana kupitia kwa mazungumzo. Maoni ya wataalamu hao ni muhimu kutokana na msingi kuwa sauti ni kipengele kidogo kabisa katika vipashio vya lugha. Maoni hayo yanaashiria kuwa lugha huundwa na wasemaji wake. Maoni ya Ogechi (2002) yanaafikiana na ya Obuchi na Mukhwana (2010) katika ufafanuzi wa dhana ya lugha. Wataalamu hao wanashadidia kuwa lugha ni kama zana inayowawezesha wanadamu kutangamana na kufanikisha shughuli zao za kila siku. Ndiposa kwa maoni yao tunajifahamisha kuwa lugha ipo kwa manufaa ya mwanadamu ili kukidhi haja zake za mawasiliano.

Maoni kama hayo yametolewa pia na wataalamu wengine kama vile Adeniyi na wenzake (2006), Alexander (2007), Kembo-Sure (2009), Casale na Posel (2010), Kandagor (2011, 2012), Mutiga (2014), Mukhwana (2014). Kutokana na maelezo

yao, tunaweza kujumlisha ufafanuzi wa lugha kama chombo kinachotumiwa na mwanadamu kuwasilisha ujumbe kwa mwenzake. Kupitia kwao, tunapata kuwa dhima kuu ya lugha ni kuwasiliana. Hii ina maana kuwa binadamu ndiye kiumbe cha pekee aliye na uwezo wa kutumia lugha ya mazungumzo kupitisha ujumbe.

Hata hivyo, wataalamu hao wameonyesha tu maana na matumizi ya lugha kwa ujumla. Utafiti wetu unafafanua namna lugha hutumika ili kukidhi mahitaji ya wahusika katika mazungumzo. Aidha, tumebainisha kanuni anuwai ambazo huelekeza matumizi ya lugha katika mazungumzo yoyote yale ili kuleta maafikiano katika hali inayokubalika kwa washiriki wa mazungumzo husika.

1.1.4 Kanuni za Mazungumzo

Kila jamii-lugha huwa na kanuni maalum ambazo hutawala mazungumzo yoyote yale. Kanuni hizo huwezesha mawasiliano na maelewano baina ya wazungumzaji na pia kuboresha mahusiano baina yao. Kanuni mbalimbali kama vile kuzungumza kwa sauti, kupokezana zamu na vilevile kuwa makini hutawala mazungumzo yoyote. Brown na Levinson (1978, 1987), wanaeleza kuwa mazungumzo yoyote yale huwa tishio kwa nyuso za wahusika, na mazungumzo katika vipindi vya *SK* hayaepuki ukweli huu.

1.1.4.1 Kupokezana Zamu

Kwa kuwa mazungumzo ni kupokezana hisia za moyoni, maoni au dhana, kila mshiriki wa mazungumzo anastahiki kupewa wakati maalum wa kutoa hisia hizo. Upokezanaji wa zamu basi ni mbinu inayotumiwa kuhakikisha kwamba washiriki wa mazungumzo hupeana muda nyakati za kuzungumza. Upokezanaji huu wa zamu ni mbinu wanayoitumia wazungumzaji kupokezana na kuendeleza mazungumzo yao. Ni

kubadilishana majukumu ya uzungumzaji kati ya msemaji na msemazwa. Kanuni ya ubadilishanaji zamu inahakikisha kuwa mja mmoja anazungumza kwa wakati mmoja.

Ubadilishanaji zamu ni njia ya kuwapa haki washiriki wa mazungumzo kwa sababu mmoja anapozungumza, wengine humsikiliza (Sacks na wenzake, 1974 na Dubois na wenzake, 1996). Kwa mujibu wa Jan (2013), mzungumzaji anamkabidhi mwenzake zamu ya kuzungumza kwa kunyamaza, kumteua kati ya wengine au hata msikilizaji kujitokeza mwenyewe. Katika mazungumzo yasiyo ya ana kwa ana, waelekezi wa mazungumzo pamoja na mwasilishaji mkuu wa vipindi hubadilishana zamu labda kwa kupewa fursa au kwa kuingilia kati ya usemi wa mwingine.

Yang (2007) anadokeza kuwa watu hukabiliwa na tatizo la kuzungumza na kusikiliza kwa wakati mmoja. Hali kama hii ndiyo husababisha makubaliano ya wakati wa kuzungumza kiutaratibu kwa njia ya kubadilishana zamu. Crystal (1995) naye anasisitiza kuwa mojawapo ya sifa za mazungumzo ni kubadilishana zamu na kukatizana usemi.

Wakati mwingine, msikilizaji anaweza kukerwa na jambo fulani na kujipata akikatiza zamu ya msemaji. Pia, msikilizaji akiwa na ongezeo la kusisitiza au kuunga mkono wazo la msemaji, anaweza kukatiza usemi wa msemaji. Hali hii ilijitokeza mara nyingi kati ya Rotich na Jepkorir. Kwa mfano, Winny anapokerwa na jambo fulani au kuona kuwa kuna unyanyasaji wa jinsia ya kike katika usemi wa Rotich, anamkatiza Rotich kwa kutumia maneno kama vile, *Acha akinye 'Pasta'...*, (Si hivyo 'Pasta'...), *Heiii, 'Pasta'!* (Heiii 'Pasta'!) kati ya mengine mengi.

1.1.4.2 Usikivu na Umakinifu

Usikivu na umakinifu ni kanuni inayosisitiza kwamba, ili kuwe na mawasiliano katika mazungumzo yoyote, ni muhimu kwa wasikilizaji kuwa makini. Fishman (1980)

anasema kuwa wazungumzaji wa kike huwa makini katika kusikiliza kuliko wale wa kiume. Wazo hilo linadhihirika katika mazungumzo ya redioni kwani wanaume hukereka haraka na kuzungumza kila wakati bila kuwasikiza wenzao.

Kanuni ya usikivu na umakinifu hukiukwa mara nyingi wanapozungumza waja. Ukiukaji huu unadhihirika kila ambapo msemaji anataka kudokeza jambo ambalo msikilizaji labda hakubaliani nalo au anataka kulishadidia. Usikivu na umakinifu unahitajika kutekelezwa ili wahusika wote wa mazungumzo wapate kuridhika na kuhisi kuwa maoni yao yanakubalika kwa wenzao. Kanuni hii ya usikivu na umakinifu inapozingatiwa hudhihirisha na kudumisha heshima baina ya wazungumzaji. Wasikilizaji wanafaa kuwa wasikivu tena kwa umakinifu ili kupata ujumbe wa msemaji. Kadhalika, msikilizaji akiwa makini, msemaji hupata ari ya kutaka kuendelea kuzungumza. Ni kanuni ya lugha ambayo ikipuuzwa na wasikilizaji, husababisha kuvunjika kwa mawasiliano.

1.1.4.3 Kuzungumza kwa Sauti

Katika mazungumzo yoyote, msemaji anapaswa kusema kwa sauti ambayo wasikilizaji hawatakuwa na tatizo la kupata ujumbe wake. Mbinu hii hurahisisha mawasiliano na pia kufupisha muda wa mawasiliano. Vilevile, sauti inayosikika huchangia umakinifu wa wasikilizaji kwa sababu msemaji ananasa mawazo yao. Kanuni hii huongoza sana mazungumzo yasiyo ya ana kwa ana kwa sababu washiriki wanaopiga simu hawapati nafasi ya kuona ishara za wenzao, ambazo zingewasaidia kukisia maana ya usemi.

Kuzungumza kwa sauti inayosikika huwa na faida kwa msemaji kwa sababu sauti hiyo ina uwezo wa kudhibiti hadhira. Msemaji asemapo chochote kwa sauti, ukakamavu wake unadhihirika na kuchukuliwa kuwa ana uhahika wa kile

anachosema. Iwapo sauti yake itakuwa ya chini, mawazo ya hadhira yatachukuliwa na mambo mengine yaliyo katika mazingara. Pia, msikilizaji huchoka na kujipata katika ulimwengu wa shughuli tofauti. Kanuni ya kuzungumza kwa sauti huwezesha upatanifu kati ya wasemaji na wasikilizaji.

1.1.5 Upole katika Utamaduni wa Kikalenjin

Wakalenjin huchukulia upole kama kuenenda kulingana na matakwa ya jamii. Mwanajamii huonekana mpole iwapo anafanya kinachokubalika machoni pa wenzake. Mtu atamkapo jambo lililopendeza, watu hufunika nyuso zao kwa sababu jambo lililosemwa ni la kuaibisha. Kutokana na tajriba ya mtafiti, kama mmoja wa Wakalenjin, kuficha uso hutokana na uwezekano kuwa neno mwiko limesemwa visivyofaa au limesemwa miongoni mwa vikundi vinavyotofautiana kiumri. Kule kufunikwa kwa uso kunamaanisha kuwa msemewa ameona haya kwa sababu kilichosemwa ni kinyume na matarajio yake.

Dhana ya uso ni muhimu sana katika utamaduni wa Wakalenjin. Wao huzingatia na kujali sana jinsi wanajamii wengine wanawachukulia. Dhana *keuny togoch* (kuficha uso) hutumika kurejelea hali ambayo watu hujipata baada ya kufanya, kusema au kufanyiwa kile ambacho ni kinyume na matarajio yao. Kwa mfano, mtu huogopa kumkemea mwenzake hadharani kwa sababu jamii ya Wakalenjin huchukulia kukemea huko kama ukosefu wa adabu. Mtu anayependa kusema mambo ovyo bila kujali hisia za wengine mara nyingi hupewa lakabu *Kip/Chepyaach ng'ala* (mwenye maneno machafu).

Wakalenjin hupenda ustaarabu. Kwao, kustaarabika ni kutomkasirisha au kutomfanya mwingine ahisi vibaya. Kwao, mja aliyestaarabika huchukuliwa kuwa mpole. Kama jamii zingine za Kiafrika, Wakalenjin huzingatia mikakati fulani katika mazungumzo

ili kuokoa nyuso za wahusika katika mazungumzo. Baadhi ya mikakati hiyo ni: kusema neno kimzunguko, kutumia tasfida, kutosema kabisa jambo linalotishia uso, na maswali ya balagha. Katika mbinu ya maswali ya balagha, mzungumzaji anaweza kusema: *Tos ng'o ne mengen magutikab manong'otionyi?* (Ni nani asiyejua mahitaji ya mumewe?). Maswali kama hayo hutumika wakati mzungumzaji anataka kupasha ujumbe fulani pasi na kutishia uso wa msikilizaji. Usemi huu unaonekana wa kijumla na kwa hivyo kuonekana kutomlenga mtu binafsi.

Katika matumizi ya tasfida, maneno ya heshima hutumika badala ya maneno halisi ili kudhihirisha heshima. Kwa mfano: *Kokolal ma kap Chepkwony* (Familia ya Chepkwony wamepata mtoto). Dhana *kokolal ma* inaonekana ya upole kuliko kutumia neno *kokosich* (wamezaa) ambalo linaonekana kutishia uso wa msemazwa. Kama wasemavyo Allan na Burrige (2006), kuna maneno ambayo kila jamii huyachukulia kuwa mwiko kuyataja hadharani.

Jamii ya Wakalenjin ina maneno mengi ambayo yakitajwa hadharani, hutishia nyuso za washiriki wa mazungumzo. Wao hulazimika kutumia maneno mbadala ya yale halisi ili kudumisha heshima baina yao. Nia kuu ya kutumia tasfida ni kupunguza makali ya usemi unaotarajiwa kusemwa. Vipindi vya *SK* vinatumia tasfida kwa wingi kwa sababu makundi yanayoshiriki mazungumzo ni ya wazazi wachanga, wa umri wa makamo baina ya wakongwe.

Mazungumzo katika vipindi hivi vya *SK* huhitaji upole kwa sababu hujadili masuala muhimu ambayo mara nyingi huhitaji umakinifu wa wahusika katika mazungumzo. Hivyo basi ili kukabiliana na tishio kwa nyuso za wahusika katika mazungumzo mbalimbali, wazungumzaji huhitajika kutumia mbinu mbalimbali za upole ili kuhifadhi nyuso zao na za wasikilizaji wao. Mifano mingine ya mbinu hizo ni:

kuchopeka na kurefusha irabu ‘i’ mwishoni mwa vitenzi vya Kikalenjin, unominishaji wa vitenzi, matumizi ya semi na sitiari miongoni mwa mbinu nyinginezo. Tazama mifano ifuatayo katika uchopekaji na urefushaji wa irabu “i” mwishoni mwa vitenzi amrifu vya Kikalenjin:

Kitenzi *ibwo* (niletee) + {i} → *ibwoii* (*ibwoi:*)

Kitenzi *kono* (nipe)+ {i} → *konoii* (*kono:*)

Uongezaji na urefushaji wa irabu ‘i’ mwishoni mwa kitenzi humpa msikilizaji hisia tofauti na za awali kabla ya kuongezwa na kurefushwa kwa irabu ‘i’. Vitenzi hivi hubadilika kutoka hali ya kuamrisha na kuwa vya kurai. Hata hivyo, mchakato huo haubadilishi maana za vitenzi hivyo.

1.2 Suala la Utafiti

Kila jamii kote ulimwenguni ina kaida zake maalum ambazo hudhibiti shughuli mbalimbali katika mawasiliano. Katika mkabala huo, mawasiliano huongozwa na kaida na mikakati mahsusi kutegemea muktadha husika. Mikakati hiyo ni ya upole na ambayo inadhihirika kupitia lugha ya maridhiano kati ya wahusika wa mazungumzo. Upole ni udhihirikaji wa heshima na adabu kupitia usemi wa wazungumzaji. Watu huzingatia upole ili kukidhi mahitaji au hisia za wengine na kudumisha heshima miongoni mwa wazungumzaji.

Mazungumzo katika vipindi vya redio hupaswa kuwa ya upole ili washiriki wa mazungumzo hayo wapate nafasi ya kujieleza na kupitisha ujumbe unaotarajiwa bila kuwakwaza wengine. Uzingatiaji huo wa kanuni za upole ni muhimu kwa sababu kutakuwa na mwendelezo mzuri wa vipindi bila ukatikaji. Vipindi vya *SK* vinaangazia masuala muhimu ya kijamii kama vile ngono, mapenzi, elimu katika

jamii, siasa na ndoa, wakwe, ukosefu wa uaminifu katika ndoa na hata malezi. Masuala hayo yanahitaji kuzungumziwa kwa makini ili washiriki wasikereke.

Kadhalika, vipindi vya *SK* huwasilishwa kwa njia iliyo wazi, yaani hutaja mambo yalivyo katika asasi ya ndoa na pia kuwapa wasikilizaji fursa ya kuuliza maswali na kutoa maoni yao bila kuficha lolote. Hali hizi zilitutia hamu ya kutaka kubainisha iwapo vipindi hivi hujali mahitaji ya uso au la. Utafiti huu basi, ni uchunguzi wa nafasi ya mikakati ya upole katika kufanikisha mazungumzo kati ya wahusika wa vipindi maarufu vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu upole na umuhimu wake katika kudumisha mahusiano baina ya msikilizaji na mzungumzaji wakati wa mazungumzo. Hii ina maana kuwa, tafiti nyingi ambazo zimefanywa zimejikita katika tamaduni za kimagharibi. Pia, kuna tafiti chache kuhusu upole ambazo zimefanywa katika lugha za Kiafrika hasa Kiswahili. Tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa Kariithi (2010), Walubengo (2010), Mwari (2013) na Opindi (2014). Baada ya kupitia kazi hizo mbalimbali, imebainika kwamba suala la upole halijachunguzwa kwa kina katika muktadha wa mazungumzo ya redio hasa katika lugha ya Kikalenjin. Ili kubainisha umuhimu wa matumizi ya upole katika kufanikisha mazungumzo na kujaribu ubia wa mikakati ya upole, tafiti kuhusu upole zinafaa kufanywa katika lugha-mama.

Ni kutokana na kuwepo kwa pengo hilo, ndipo kazi hii inachunguza mikakati ya upole katika muktadha wa mazungumzo ya redioni na katika lugha ya Kikalenjin, ambapo utafiti huu unapata msingi wake. Utafiti huu, ulichanganua kaida maalum za upole zinazobainika katika vipindi hivyo vya *SK* kwa kupima utendakazi wa mikakati anuwai ya upole katika kufanikisha mawasiliano.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kuchanganua mikakati ya upole inayotumika kuwasilisha vipindi vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*
2. Kuhakiki athari za uzingatiaji na ukiukaji wa kaida za upole kwenye vipindi vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*
3. Kutathmini hali zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole katika vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*.
4. Kupambanua na kujadili changamoto zinazosawiriwa na wahusika wa mazungumzo ya *SK* wakati wa utekelezaji wa kanuni za upole.

1.4 Maswali ya Utafiti

1. Je, ni mikakati gani ya upole ambayo hutumika kuendeleza mazungumzo ya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*?
2. Uzingatiaji na ukiukaji wa kaida za upole una athari gani kwa mawasiliano ya vipindi vya *SK* katika *KASS FM*?
3. Ni hali zipi zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole katika mazungumzo ya vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*?
4. Je, wahusika wa mazungumzo ya *SK* wanasawiri changamoto zozote wakati wa kutekeleza mikakati ya upole?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Uchunguzi huu unafungua ukurasa wa utafiti katika vipindi vya redio nchini Kenya. Kufikia sasa, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu mikakati ya upole katika vipindi vya redio au vya runinga vinavyopeperushwa katika Kikalenjini. Kwa hivyo, kazi hii

itakuwa kama msingi wa tafiti zijazo kuhusiana na suala la upole katika vipindi vya redio katika lugha ya Kikalenjin. Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusiana na upole zilijikita katika mazungumzo kwenye vipindi vya runinga. Tafiti hizo ni kama vile za Yan (2010), Petrickova (2012), Putri (2013) na Machira (2015).

Hata hivyo, vipindi vya runinga huwapa wahusika nafasi ya kutazama na kusikiliza. Katika kutazama, wahusika huweza kutumia viziada lugha na hivyo kuchangia udokezaji na ufasirikaji wa maana katika lugha. Kwa upande mwingine, hadhira ya redio hutegemea tu sauti za wazungumzaji. Mawasiliano yanayotegemea tu sauti za wahusika huhitaji umakinifu na uwazi hasa katika mjadala unaohusu masuala nyeti kama vile ya ndoa, ili kudumisha uhusiano mzuri wa wahusika.

Kujadili masuala ya ndoa kwa uwazi ni mojawapo ya mbinu zinazotumiwa kuimarisha asasi ya ndoa. Hii itawezekana tu iwapo masuala hayo yatawekwa wazi, lakini kwa kuzingatia upole, wakati wa mazungumzo. Kwa kuwa ni mwiko katika jamii za Kiafrika kuzungumzia masuala ya ndoa mbele ya wazazi, vijana na watoto, kipindi hiki huwasilishwa usiku kwa ajili ya wazazi, wakati makundi ya watoto na vijana yamefumukana. Jambo hili linafaa kuzingatiwa kwa sababu uhusiano ni kitovu cha maisha ya wanajamii. Ili kudumisha uhusiano huo, wahusika huhitajika kuwasiliana kwa heshima.

Mazungumzo yasiyo ya ana kwa ana yana nafasi nzuri ya kuwasilisha hoja kwa njia huru. Vipindi vya redio humpa msikilizaji fursa ya kusikiliza tu. Bila kuogopa, wasikilizaji wanaweza kuchangia mazungumzo bila kukwepa lolote kwa sababu hawaonekani kwa watazamaji wengine. Wasikilizaji wanaweza kutoa maoni yao kwa kusimba au kutotaja majina yao, na hivyo kutoa hoja zao bila kuogopa. Hata hivyo, heshima baina yao ni muhimu.

Aidha, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu dhana ya upole katika vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*. Utafiti huu utaangazia kwa mara ya kwanza mikakati ya upole inayozingatiwa na wazungumzaji na athari yake katika ufanisi wa vipindi husika. Kadhalika, wakati wa uwasilishaji wa vipindi ni mtulivu, kwa hivyo mtafiti hakuzuiliwa na kelele za watoto au wale walio na pilkapilka za wakati wa mchana. Mwasilishaji mkuu katika vipindi vya *SK*, Rotich, ni mshauri katika masuala nyeti ya kijamii hasa katika asasi ya ndoa. Yeye huangazia changamoto kama vile ulevi, mahusiano na mashemeji, tabia zinazokera katika ndoa, wakati mwafaka wa kutalikiana vilevile namna ya kukabiliana na changamoto hizo miongoni mwa masuala mengine. Vipindi hivi hupeperushwa hewani kila Jumatano saa nne na robo hadi saa sita usiku.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu katika taaluma ya lugha hasa isimu-jamii na uamali kwa sababu walimu na wanafunzi wa isimu watapata msingi wa tafiti kuhusiana na mikakati ya upole katika mazungumzo ya redio. Kadhalika, jamii ya Kikalenjin itazingatia mahitaji ya matumizi ya lugha ili kukuza uhusiano mzuri kati ya wanajamii. Aidha, jamii-lugha na idhaa ya *KASS FM* zitafaidika kupitia kwa uelewa wa mikakati ya upole katika mazungumzo yoyote yale ili kuwezesha mwendelezo mzuri wa mawasiliano. Kando na hayo, mada za vipindi hivi pia zitawaelimisha wanajamii-lugha jinsi ya kukabiliana na matatizo ya upuuzaji wa mikakati ya upole katika mazungunzo. Mwisho, idhaa ya *KASS FM* itanufaika kupitia kwa utafiti huu ambao utawajaza waelekezi na wasimamizi wa vipindi vya redio umuhimu wa kujali mahitaji ya uso wanapokuwa na mijadala na hadhira yoyote.

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ni mwingiliano wa taaluma za uamali na isimu-jamii katika kujadili mikakati ya upole kwenye vipindi vinane (8) tu vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*. Imekuwa kawaida kwa watu kuweka mipaka kati ya uamali na isimu-jamii lakini mtazamo wetu ni kuwa taaluma hizi huingiliana pale ambapo jamii hutumia lugha kimuktadha ili kuwe na maana katika mawasiliano.

Ujumuishaji wa taaluma hizi mbili unatokana na ukweli kuwa isimu-jamii ni uchunguzi wa matumizi ya lugha katika jamii na uamali ni uchunguzi wa maana katika lugha kwa kuzingatia muktadha. Hii inamaanisha kuwa lugha hupata maana inapohusishwa na kikundi fulani cha watu na katika muktadha maalum. Hapa ndipo tunapata mwingiliano mkubwa kati ya isimu-jamii na uamali. Tunapochunguza maana ya usemi, tunahusisha jamii mahususi. Hii ni kwa sababu kila jamii ina matumizi maalum ya lugha kulingana na kaida za jamii husika. Tumeangazia namna dhana ya upole inadhihirika katika mazungumzo. Aidha, tulitumia tu data kutoka vipindi vinane vya *SK*. Kipindi kimoja cha kila juma huchukua masaa mawili na hivyo tulirekodi data ya masaa kumi na sita ndani ya majuma manane. Tulitumia data ya mwasilishaji mkuu, mwelekezi na wasikilizaji wanaotoa mchango wao kwa njia ya utumaji ujumbe.

Katika upeo wa kinadharia, utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1978, 1987). Kwa kutumia mhimili wa mkakati wa kuokoa uso, tulitathmini ufaafu wa Nadharia ya Upole katika uchanganuzi wa mikakati ya upole kwenye vipindi vya *SK*. Mhimili huo wa uso umetuelekeza kuchanganua data za wahusika wa mazungumzo ili kufafanua mbinu anuwai za mikakati ya upole na changamoto za mbinu hizo.

1.8 Mbinu za Utafiti

1.8.1 Utangulizi


Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani. Utafiti ulitumia mbinu ya uchunguzi kistahilifu kwa sababu data iliyokusanywa ni matamshi ya wahusika katika vipindi teule na kwamba sehemu kubwa ya utafiti ni maelezo ya mbinu zilizotumika kufanikisha kipindi cha *SK*. Aidha, kwa kuwa utafiti ni wa kistahilifu, mchakato wa uchunguzi ulikuwa wa kiduara kwamba, baada ya kumaliza hatua moja, kulikuwa na uwezekano wa kurudi katika hatua zilizotangulia ili kubadilisha vipengele vingine kwa minajili ya kuboresha kazi. Sehemu hii inaangazia namna sampuli iliteuliwa na njia zilizotumiwa kukusanya na kuchanganua data. Mtafiti alinasa vipindi vya *SK* ili kupata data za kimsingi alizotumia katika uchanganuzi.

1.8.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika idhaa ya *KASS FM* ambayo ni moja kati ya stesheni za radio zinazorusha matangazo kupitia lugha za kiasili nchini Kenya. Stesheni hii hutumia lugha ya Kikalenjin kuwasilisha habari zake. Inakadiriwa kuwa, stesheni hii huwafikia takriban watu milioni 4.5 kila siku (Ronoh, 2013). Matangazo ya *KASS FM* husambazwa na kufikia sehemu zifuatazo; Nairobi na mazingira yake ambazo ni pamoja na Machakos, Thika, Kiambu na Limuru. Sehemu nyingine ni ile iliyokuwa mkoa wa Bonde la Ufa na mazingira yake kama vile Nakuru, Eldoret, Kitale, Baringo, Kapenguria, Timboroa, Gilgil, Naivasha, Bomet, Litein na Kericho. Katika upande wa Pwani, *KASS FM* hufikia sehemu za Mombasa, Malindi, Mtwapa, Changamwe, Ukunda na Kilifi. Sehemu za Magharibi na Nyanza, kituo hiki kinawafikia wasikilizaji wa Kakamega, Kisumu na Kisii. Pamoja na sehemu hizo ni sehemu za

ughaibuni ambazo hutumia mitandao ya kijamii kupata matangazo katika lugha husika (Kass Media, 2011).

Ramani Inayoonyesha Sehemu Zinazofikiwa na Kass Redio



Asili: Kass Media

Ramani hiyo inaonyesha sehemu zinazofikiwa na matangazo ya *KASS FM*. Sehemu hizo zimetokana vituo vinavyoteua kupeperusha kufikia mahali fulani ambapo ni teule kulingana na mahitaji ya wakaazi.

1.8.3 Utafiti Mwigo

Awali, kabla ya utafiti mkuu, tulifanya utafiti mwigo ili kupata habari za kiusuli. Dhima ya utafiti mwigo ilikuwa kubaini ufaafu wa kifaa cha utafiti tulichokusudia kutumia. Fraenkel na Wallen (2000) wanahoji kuwa utafiti mwigo ni jaribio dogo linalofanywa ili kupima kifaa cha utafiti na kujua iwapo kitazalisha data inayofaa na kutosha mchakato wote wa uchanganuzi. Kifaa hicho kinapaswa kutegemewa. Utegemevu wa kitu ni hali ya kiuwezo wa kitu hicho kupima kile kinachochunguzwa ili kutoa matokeo yaliyo sahihi (Babbie, 1992). Cozby (2001) anasema kuwa iwapo kifaa hicho hakijapangwa ipasavyo, utafiti mwigo utatoa mwanga wa jinsi ya kuirekebisha kabla ya kutumiwa kwenye utafiti mkuu. Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa hata kifaa kipangwe kwa uangalifu, hakiwezi kuzaa data ambayo usahihi wake ni asilimia mia moja (Murray, 2003).

Ili kuendesha utafiti mwigo mtafiti alinasa vipindi viwili vya *SK* na kutumia data hizo kama jaribio la utafiti mkuu. Nia ya mtafiti hasa ilikuwa kujaribu iwapo utafiti unaonuiwa kufanywa ungefanikiwa kupitia mtindo wa uchanganuzi ulioteuliwa na idadi ya vipindi vilivyokusudiwa kunaswa. Pia, utafiti mwigo ulimsaidia mtafiti kukisia muda ambao ungetumiwa katika ukusanyaji wa data alizohitaji. Wakati huo pia, mtafiti aliweza kubainisha mbinu faafu za ukusanyaji data.

Utafiti mwigo ulimpa mtafiti nafasi ya kutagusana na baadhi ya mashabiki ili kupata maarifa kuhusiana na jinsi wanachangia mada tofautitofauti katia vipindi vya *SK*. Aidha, mtafiti alipata fursa ya kuwasiliana na mwasilishaji mkuu ambaye ni 'Pasta' Rotich ili kupata idhini ya kutafitia mazungumzo katika vipindi husika vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*. Kukutana na Bw. Rotich kuliwezekana kwa urahisi kwa sababu anaishi katika Kaunti ya Uasin Gishu. Rotich ana ofisi yake inayoitwa

Kokwatai kwenye orofa ya pili katika jengo la *Kaplimo House* mjini Eldoret. Yeye hutoa huduma yake ya ushauri kwa wateja wake siku tano za juma kwa kuwaelekeza juu ya mambo yanayohusiana na asasi ya ndoa. Yeye husafiri kwenda Nairobi siku ya Jumatano ya kila juma kwa minajili ya kuwasilisha vipindi vyake saa nne hadi saa sita usiku.

Kwa kutumia kinasa sauti kama kifaa kikuu, jaribio hili lilikusanya jumla ya matamshi kumi na saba kutoka kwa vipindi viwili. Data hiyo ilichanganuliwa na kumwelekeza mtafiti kuwa alihitaji kunasa kati ya vipindi sita na nane ili kupata data ambayo ingewezesha ufanisi wa utafiti. Matokeo hayo yalimwezesha kukadiria idadi ya data anayohitaji na idadi ya vipindi vitakavyozalisha data hiyo.

1.8.4 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya utafiti ilituliwa kimakusudi. Hii ni kwa kuambatana na malengo ya utafiti, upeo na vipengele vilivyotumika katika uchanganuzi. Kwa mujibu wa Kothari (2004), uteuzi wa elementi moja kati ya mkusanyiko wa elementi nyingi hutokana na sababu kuwa kila kipengele katika mkusanyiko kina nafasi sawa ya kuteuliwa. Hivyo basi uteuzi ulifanyika bila mpangilio kwa sababu kipengele kimoja kina uwezo wa kuwakilisha mkusanyiko wote. Usampulishaji huo wa kimakusudi ulitekelezwa kwa hatua tano. Kwanza, usampuli wa kimakusudi ulitumika kuteua kituo cha redio chenye kutumia lugha ya Kikalenjin miongoni mwa vituo vingi vya redio nchini Kenya vinavyotumia lugha kama vile ya Kiswahili, Kimombo na vyenye kutumia lugha za kiasili. Vituo vingi kwa mfano KBC, Sulwe FM, Inooro FM, Redio Citizen, Redio Maisha miongoni mwa vituo vingine vingi havikuzingatiwa.

Hatua ya pili ilikuwa ya kuteua kituo chenyewe cha idhaa ya *KASS FM* miongoni mwa vituo vingine vya redio vinavyotumia lugha ya Kikalenjin kupeperusha

matangazo yake kama vile *Chamgei FM*, *Kitwek FM* na *Emoo FM*. Uteuzi huu wa kimakusudi uliambatana na malengo yetu ya utafiti kwa kuzingatia mada za kituo na namna ya uwasilishaji wa mada hizo. Uteuzi huu wa kimakusudi ulifanyika kwa misingi ya idadi ya mashabiki wakati wa uwasilishaji na ufaafu wa vipindi katika kituo cha redio kwa wasemaji wa lugha husika.

Tatu, uteuzi wa kimakusudi ulitumika kuteua kipindi cha *SK* kati ya vipindi anuwai vya kituo hicho cha *KASS FM*. Pamoja na kipindi cha *SK*, idhaa ya *KASS FM* ina vipindi vingine kama vile *Kwondo ne Ng'om* (mke mwenye hekima), *Len Nee Emet?* (Kuna nini Nchini?), *Teeb si Inai* (Uliza Ujibiwe), *Twoliot* (Mambo ya Ngoni), *Heshimu ukuta* (Heshimu Ukuta) *Tigitiotab Bambaniat* (Chanzo cha Mapenzi). Kipindi cha *SK* kiliteuliwa kwa sababu ya mada zake ambazo zinanata mawazo ya wasikilizaji na kuwapa hamu ya kutaka kuchangia au kusikiliza kipindi kitakachofuata wakati ujao. Sababu nyingine ya uteuzi ni kuwa mwasilishaji mkuu wa vipindi vya *SK* ana umahiri katika kazi ya kutoa ushauri kuhusiana na maswala ya ndoa.

Rotich amekomaa katika uwanja huu na hilo linathibitishwa na kazi anazofanya ofisini mwake iliyoko mjini Eldoret. Amejizatiti katika kuwashughulikia wasikilizaji ambao labda hawapendi kutaja mambo yao hadharani. Rotich hutoa nambari yake ya simu kwa yeyote anayetaka kuzungumza naye ana kwa ana ili wawasiliane kuhusu namna ya kukutana ofisini mwake. Aidha, mwasilishaji huyu mkuu anafanya matangazo yake na Winny ambaye ni mcheshi na huelekeza vipindi kwa namna inayowapendeza mashabiki wa *SK*. Licha ya umri wake mdogo, Winny ana uwezo wa kuwaunganisha mashabiki ambao ni wa umri tofautitofauti. Anafanya hivyo kwa kutumia lugha ya heshima baina yake na mashabiki hao ambao humpongeza kuwa anasema mambo ambayo yanapiku umri wake. Lugha yake inadhihirisha ukomavu.

Hatua ya nne katika uteuzi wa sampuli ni wa idadi ya vipindi vya kunaswa na kusikizwa. Tuliteua vipindi vinane vya *SK*, kila kipindi kikirushwa kwa masaa mawili kila juma na hivyo tulikuwa na jumla ya masaa kumi na sita ya kusikiliza na kurekodi data. Vipindi vyote vinane viliteuliwa kimakusudi kwa sababu ya mada zilizohusishwa navyo. Mtafiti alipokuwa akisikiliza na kunasa vipindi anuwai vya *SK*, alifanya uamuzi wa kutumia data ya vipindi vinane kutokana na sababu kuwa zingeweza kutosheleza mahitaji ya uchanganuzi kwa kuzingatia upeo wa utafiti.

Uteuzi wa kimakusudi katika hatua ya mwisho ulikuwa wa kusampuli mashabiki wachache kati ya mashabiki wengi waliochangia vipindi husika. Umakusudi huu ulifanyika baada ya kusikiza yaliyokuwemo katika usemi wa kila shabiki. Baada ya kunasa mazungumzo yote, mchango wa kila shabiki ulisikilizwa kisha kuteuliwa au kuchujwa kulingana na malengo ya utafiti. Kwa kuwa mtafiti alihitaji data zinazohusiana na upole, alilazimika kutupilia mbali data ambazo hazikuwa na uhusiano na mada. Uteuzi huo ulikuwa muhimu kwetu kwa minajili ya kupata data zinazohusiana na upole na ambazo zilitumika katika hatua ya uchanganuzi.

1.8.5 Vifaa vya Kukusanya Data

Tulihitaji vifaa fulani ili kukusanya data ya utafiti huu. Kwanza, tulihitaji kuwa na kinasa sauti kilichotuwezesha kupata data ghafi. Tulitumia kinasa sauti kunasa mazungumzo yote ya vipindi vinane vya *SK*. Pili, tulihitajika kuwa na simu ya rununu ambayo ilifanya kazi kama ya kinasa sauti. Sababu ya kunasa mazungumzo kwa kutumia simu na kinasa sauti ilisababishwa na haja ya kuwa na uhakika wa hifadhi mbadala iwapo nyingine ingepoteza data. Aidha, ni rahisi kurejelea au kusikiliza data iliyo kwenye simu wakati wowote kwa sababu inaweza kuchukuliwa popote.

Aina ya tatu ilikuwa kalamu na karatasi ambazo zilitumika kunakili mazungumzo ambayo yalihitajika katika uchanganuzi. Baadaye, kipakatalishi kilitumika kuhifadhi data kwa minajili ya kuzisetiri kutokana na uharibifu hadi wakati wa uchanganuzi. Sababu nyingine ya kuweka kwenye tarakilishi ni kwamba, uchujaji wa data muafaka zikiwa kwenye tarakilishi ni rahisi.

1.8.6 Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), kukusanya data ni kuweka pamoja habari mahsusi zinazothibitisha au kupinga ukweli fulani. Data hizo huwa zinahusiana na hivyo kuwekwa katika kikundi kinachothibitisha uhusiano huo. Katika ukusanyaji wa data hizo, mtafiti alisikiliza na kurekodi vipindi vya *SK*. Kusikiliza huko ni mbinu ya kukusanya data isiyoshirikishi. Mbinu isiyo shirikishi ni ile ambayo mtafiti hatagusani moja kwa moja na watafitiwa bali hupata habari kupitia njia zingine. Usikilizaji huu ulimpa nafasi mtafiti kuyakinisha mazungumzo ya *SK* na kufanya uteuzi wa data zilizohitajika.

Data kuhusu upole ziliteuliwa kutoka vipindi vinane vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*. Vipindi hivyo vilikuwa na mada nane tofauti kila mmoja. Tulirekodi mchango wa mwasilishaji mkuu, mwelekezi wa vipindi na maswali pamoja na maoni ya wasikilizaji. Mazungumzo yaliyorekodiwa yanaweza kucheza na kusikizwa tena iwapo mtafiti anahitaji kurejelea au kujikumbusha kitu fulani (Mugenda na Mugenda, 2003). Mchango huo ulihusisha masuala ya upole na kategoria mbalimbali kuhusiana na kanuni za mazungumzo. Aidha mtafiti alishiriki katika baadhi ya vipindi kwa njia ya utumaji ujumbe ili kuuliza maswali. Vipindi hivi vinane vilitupa data za kutosha na zilizotuwezesha kuendeleza uchunguzi wetu.

1.8.7 Unukuzi wa Data

Ukusanyaji wa data ulipokamilika, baadhi ya data hizo zilinukuliwa moja kwa moja na zingine zilifupishwa kutegemea urefu wa data. Uhakiki wa data ghafi kulingana na malengo na maswali ya utafiti ulifanywa ili kubaki na data muhimu pekee. Data zilizoteuliwa ziliainishwa katika makundi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole na mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Hata hivyo, data chache zinazohusiana na mkakati wa tano ambao ni mkakati wa kutosema kabisa jambo linalotishia uso, zilitumiwa lakini kwa uchache mno, na kuwekwa baada ya mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Hatua iliyofuata ilikuwa kutafsiri data za Kikalenjin katika Kiswahili.

1.8.8 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data

Baada ya kunakili kauli za mazungumzo kuhusiana na upole, data iliwasilishwa kwa kupangwa kwenye makundi ili kuwezesha na kurahisisha uchanganuzi. Uchanganuzi wa data ulifanywa kimaelezo. Kwanza, kauli hizo ziliainishwa kulingana na kategoria za mkakati chanya wa upole, mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati wa kuwa nje ya rekodi na mkakati hasi wa upole kulingana na mahitaji ya lengo la kwanza. Pili, data kuhusiana na athari za uzingatiaji wa mikakati ya upole kulingana na lengo la pili zilichanganuliwa. Tatu, kauli zilizohusiana na hali zinazoathiri uteuzi wa mkakati pamoja na changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mikakati ya upole zilichanganuliwa. Mwisho, kauli za mazungumzo hayo zilifafanuliwa kwa misingi ya Nadharia ya Upole na malengo ya utafiti.

1.9 Hitimisho

Kupitia sura hii, msingi wa utafiti huu umeonyeshwa. Sura hii imetoa mwelekeo kiupeo na pia mtazamo wa upole kulingana na wasemaji wa Kikalenjin kwa

kuzingatia mtazamo wa waasisi wa nadharia ya upole. Imeeleweka wazi kuwa kila jamii-lugha inachukulia upole kwa njia tofauti. Hata hivyo, imebainika kuwa jamii za Kiafrika hukumbatia sana suala la upole na mitazamo yao kuhusu upole huingiliana. Ni muhimu pia kutaja kuwa Wakalenjin, kupitia vipindi vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*, hunufaika kama jamii kupitia kwa uwasilishaji mzuri wa vipindi hivyo. Aidha, usuli wa utafiti umetuwekea mipaka kinadharia na kitaaluma. Sura inayofuata inahakiki mitazamo ya wataalamu wengi kuhusiana na mikakati ya upole na mihimili ya nadharia ya upole kwa ujumla.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Sehemu ya kwanza ya sura hii inaangazia baadhi ya maandishi yanayohusiana na mada na suala la utafiti. Kwa ujumla, tumepitia maandishi ya wataalamu waliotafitia mikakati ya upole katika mawasiliano kwa ujumla na kisha maandishi kuhusu mawasiliano kupitia vyombo vya habari. Upitiaji huo wa maandishi umetuwezesha kujadili na kutoa ufafanuzi wa jinsi kauli zao zinajenga utafiti wetu. Tumechunguza namna watafiti tofautitofauti wameangazia suala hilo la upole na kulinganisha mawazo yao na yetu.

Sehemu ya pili ya sura hii inaangazia nadharia iliyotumika katika utafiti. Uasisi wa nadharia hiyo na mitazamo ya watafiti wengi kuhusiana na suala la upole imefafanuliwa. Aidha, tumetalii namna ambavyo Kanuni Ushirika ya Grice inaingiliana na kuchangiana na Nadharia ya Upole. La muhimu ni kuonyesha jinsi watafiti wengine wamejaribisha Nadharia ya Upole kupitia tafiti zao. Nadharia ya Upole ndiyo msingi wa kubainisha na kuchanganua mikakati ya upole katika vipindi teule vya *SK* kupitia sura ya tatu, nne na tano kwenye tasnifu hii.

2.1 Dhana ya Upole

Dhana ya upole imefanyiwa uchunguzi na wanaisimu wengi na kutolewa maelezo mbalimbali. Miongoni mwa wanaisimu hao ni Goffman (1967), Lakoff (1973), Grice (1975), Brown na Levinson (1978,1987), Fraser na Nolen (1981), Leech (1983), Fraser (1990), Ilie (2001), Watts (2003) na Mills (2003). Maelezo kuhusu dhana ya upole na jukumu lake kuanzia karne ya ishirini hadi sasa ni suala la

mjadala mkuu. Wengi wameshughulikia maana halisi ya dhana ya upole na pia ubia wa dhana hii. Hata hivyo kila nadharia inayohusiana na dhana hii inatoa namna fulani ya kutathmini sio tu jinsi upole unavyoingizwa katika mawasiliano bali hata sababu zake.

Suala la upole lilipata kuchunguzwa sana miaka ya sabini. Hata hivyo, Goffman (1967) alishughulikia upole kabla ya miaka hiyo ya sabini. Goffman amejadili upole katika muktadha wa nadharia ya jumla ya tabia. Mtaalamu huyu alieleza kuwa upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kwa kutimiza au kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo. Maelezo ya Goffman yanaelekeza kuwa upole ni mbinu inayotumiwa na wazungumzaji kujaliana kimazungumzo ili kudumisha uhusiano wao.

Brown na Levinson (1978), wanaeleza upole kama namna ya kuokoa uso wa msikilizaji. Kwa maoni yao, watu hutumia upole kama njia inayojulikana, ya ujanja ili kuepuka kumfanya mtu mwingine kuhisi vibaya. Kwa hivyo upole ni aina ya udanganyifu unaotekelezwa na wasemaji ili kuhifadhi nyuso za wasikilizaji wao. Kwa mfano mtu anaweza kumkejeli mwingine kuwa ni mwerevu wakati anajua vizuri kuwa kauli hiyo ni kinyume cha ukweli. Hoja hii inaungwa mkono na Leech (1983) anaposema kuwa upole ni mkakati wa mawasiliano ambao watu hutumia kuanzisha na kuhifadhi mahusiano katika jamii zao. Utafiti wetu ulilenga kuchunguza namna ambavyo washiriki wa vipindi vya *Sobetab Kapchi (SK)* humudu au hukosa kuhifadhi nyuso za wenzao kupitia kwa mazungumzo.

Dhana ya upole katika karne ya Ishirini na moja imeelezwa na wanaisimu kama vile Watts (2003) ambaye anasema kuwa upole ni hulka ya kiasili ya tabia njema. Ni uwezo wa kufurahisha wengine kupitia matendo ya nje ya mtu husika.

Watts anaongeza kuwa upole ni dhana ya kiakili na kijamii ambayo hukuzwa kupitia mahusiano yetu ya kijamii. Watts hata hivyo anabainisha kuwa watu hawazaliwi na upole bali wanajifunza kwa kutazama jinsi watu wengine wanavyotagusana katika jamii zao.

Dai la Watts (2003) linatiwa nguvu na ukweli kuwa dhana ya upole ni tofauti katika jamii na tamaduni mbalimbali. Kwa mfano, kule Uchina, mtu akipewa zawadi hatakiwi kuichukua mara hiyo kwa sababu kwao kitendo kama hicho si upole. Kulingana na Wachina, kuchukua zawadi mara moja ni kuonyesha labda anayeichukua haithamini. Kinyume na ilivyo katika jamii za Kiafrika, Wachina huchukulia kuwa upole ni kukataa kuichukua zawadi hadi pale utakaporaiwa mara nyingi (Kautlaki, 2002). Hili lina maana kuwa kinachotambulika na kukubalika kuwa upole katika jamii moja kinaweza kuwa kinyume chake katika jamii nyingine. Uchunguzi wetu, umetumia kigezo hicho cha kijamii kuchunguza kile kinachothaminiwa kama upole katika jamii ya Wakalenjin ambao wanahusishwa na vipindi vya *SK*.

Mills (2003), anaunga mkono dhana ya Brown na Levinson (1987) kuhusu upole anaposema kuwa upole ni dhahirisho la hamu ya msemaji kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji na uso wake mwenyewe. Vitisho hivyo hutekelezwa na vitendo fulani vinavyotishia uso wa mtu mwingine. Tulilenga kutumia mawazo haya kutalii jinsi mikakati ya upole inabainika katika vipindi vya *SK*.

2.2 Mazungumzo kwenye Vyombo vya Habari

Kwa mujibu wa Ilie (2001), mjadala kwenye vyombo vya habari ni shughuli ya mazungumzo inayoongozwa na mtangazaji au mwasilishaji. Mjadala kama huo hupeva umbo na washiriki na kutathminiwa na watazamaji au/na wasikilizaji.

Maelezo haya yanamulika aina zote za mazungumzo katika vyombo vya habari kwa kuangazia washiriki na majukumu yao. Sifa za mazungumzo ya kawaida zinadhihirika kupitia ubadilishanaji wa papo hapo wa majukumu kwa njia rahisi ya maswali na majibu. Aina hii ya mazungumzo ndiyo Ilie (2001) anayaita nusu-rasmi. Utafiti wetu unahusu mazungumzo ya nusu rasmi kwa sababu yanaendeshwa na mtangazaji Winny pamoja na mhusika mkuu Rotich, na wasikilizaji. Wahusika hao hufuata kanuni fulani za mazungumzo ili kuwezesha maelewano.

Becker (2007) anafafanua kuwa mahojiano katika vyombo vya habari ni kategoria moja ya mazungumzo rasmi/ya kitaasisi. Kategoria hiyo ya mazungumzo rasmi ni dhana iliyobuniwa na wachanganuzi wa mazungumzo ili kuyatenga na mawasiliano ya kawaida. Washiriki katika aina hii ya mazungumzo huwa na majukumu mahsusi ambayo hayabadiliki katika muda wa mazungumzo. Ijapokuwa mazungumzo katika vyombo vya habari huzingatia kanuni za mazungumzo rasmi, mazungumzo haya pia husheheni ruwaza zinazohusishwa na aina nyinginezo za mazungumzo.

Kando na ukweli kuwa mazungumzo ya redio na mazungumzo ya ana kwa ana yanazingatia kanuni za mazungumzo, yale ya redio yana upekee wake. Upekee huo ni kwamba, wazungumzaji wanazingatia kanuni ya ubadilishanaji zamu kwa sababu wahusika hawaonani uso kwa uso na pia kwamba hakuna uwezo wa kuzungumza wakati mtu mwingine anazungumza. Ruhusa ya mratibu ndicho kibali pekee cha kutumika kwa sababu ana uwezo wa kukubali au kupuuza simu ya anayetaka kuzungumza. Mazungumzo ya redio ya vipindi vya *SK* hayaepuki ukweli huu na hii ndiyo sababu lengo mojawapo la utafiti wetu ni kubainisha na kuchanganua mikakati inayotumiwa ili kuzingatia urasmi huo.

2.3 Tafiti Zinazohusiana na Mada ya Utafiti

Tafiti chache sana zimefanywa kuhusiana na mazungumzo baina ya walio studioni na wasikilizaji. Tafiti nyingi zinazohusiana na upole zimejikita zaidi kwenye mazungumzo ya runinga. Mathalan, Kitamura (2000) kutoka ‘School of Europe’ alichunguza mazungumzo yasiyokuwa rasmi katika Kijapani. Alilenga kuonyesha namna ambavyo Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson inaweza kutumika katika mtagusano usio rasmi. Kitamura aligundua kuwa nadharia ya upole inatumika kwa mazungumzo rasmi na yasiyo rasmi. Kitamura anatoa msingi kwa utafiti wetu ambao ni wa mazungumzo yaliyochanganya yale yenye urasmi na yasiyo rasmi.

Uchunguzi mwingine ni wa Mukarromah (2002) ambaye alitafitia mikakati ya upole inayotumiwa na watangazaji habari wa kiume na wa kike katika Andalus FM kule Malang, Java Mashariki. Katika utafiti wake, aligundua kuwa kuna baadhi ya maneno ambayo hutumiwa na watangazaji wa jinsia zote. Pia, watangazaji wote wa Andalus FM wanatumia mikakati ya upole hasi na chanya. Utafiti wa Mukarromah una mchango mkubwa kwa utafiti wetu kwa sababu alichunguza mikakati ya upole katika mazungumzo ya redio. Tofauti tu ni kuwa lugha yao ya kichunguzi ilikuwa ya Kizungu ambayo inazungumzwa na jamii-lugha tofauti kabisa na ya Kiafrika. Kwa hivyo utafiti wetu utachangia katika ubainishaji wa mikakati ya upole katika jamii za Kiafrika na hasa wazungumzaji wa Kikalenjin.

Yuliana (2003) ambaye alichanganua mikakati ya upole inayodhihirika katika jamii ya Probolinggo kule Malang, Java, alibainisha mikakati ya upole inayotumika sana. Alieleza kuwa hali ya kutumia mikakati mingine kwa wingi huchangiwa na mahitaji ya utamaduni. Hayo yanashabihiana na maoni ya Grundy (2000) anayesema kuwa lugha haitenganishwi na mahitaji ya jamii husika. Utamaduni wa Kikalenjin nao

unasisitiza matumizi ya mikakati ya upole kimuktadha kama inavyodhihirika katika utafiti huu.

Aini (2003) alichunguza mikakati ya upole inayotumiwa na wauguzi wanapotoa matibabu katika hospitali ya Pare Kediri, Indonesia. Mtaalamu huyu alitaka kujua iwapo wauguzi hao huzingatia mikakati ya upole wanapowasiliana na wagonjwa. Ilibainika kuwa wauguzi wana mbinu ya kuwasiliana na wagonjwa ili kuwafanya wahisi kuwa watapona. Licha ya uchunguzi wake kuhusu miswada ya magonjwa, utafiti huo unahusiana na wetu kwa sababu ni uchunguzi wa mikakati ya upole katika mazungumzo. Hata hivyo, upekee wa utafiti wetu ni kwamba mazungumzo sio ya ana kwa ana na masuala ya mjadala inahusisha hadhira changamfu; sio wagonjwa.

Mtafiti mwingine ni Azza (2004) aliyechunguza mikakati ya upole katika filamu ya “Eiffel... I’m in Love” kilichotayarishwa na Rahmania Arunita. Azza aligundua kuwa wahusika katika dayolojia hiyo huhusisha mikakati fulani ili kukuza maelewano na kutekeleza mawasiliano baina yao. Ingawa kazi ya Azza inachanganua mikakati ya upole katika maandishi, kazi hiyo inahusiana na yetu kwa kiasi kikubwa katika sehemu ya kubainisha mikakati iliyotumika katika kuchora kazi hiyo. Aidha, mfumo wa dayolojia ni sawa na mfumo wa mazungumzo usio wa ana kwa ana kwa sababu yote huzingatia kanuni ya ubadilishanaji zamu na hivyo basi kuufanya mchango wa Azza kuwa muhimu kwetu.

Uchanganuzi mwingine wa mikakati ya upole ni wa Mustain (2005). Uchunguzi huu ulikuwa katika makala ya vikaragosi yanayochapishwa katika Jakarta, mji mkuu wa Indonesia. Katika uchunguzi wake, Mustain amebainisha mbinu walizotumia wahusika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Ameegemeza utafiti wake kwenye misingi ya nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1978). Utafiti huu ni tofauti na

wetu kwa kiasi kidogo sana kwa sababu unachunguza upole katika maandishi. Hata hivyo, uchunguzi wake unachangia sana utafiti wetu unaoshughulikia ubainishaji wa mikakati ya upole katika mazungumzo ya redio, kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Upole.

Yan (2010) naye alichunguza mikakati ya upole kwa misingi ya jinsia katika kipindi cha runinga cha 'Desperate Housewives'. Aligundua kuwa wanawake huwapongeza wanawake wengine na pongezi zao hupokelewa kama njia ya kuanzisha na kuimarisha mahusiano miongoni mwao. Anaeleza kuwa ni rahisi kwa wanawake kujidunisha kwa wenzao ili kuhifadhi nyuso za wenzao na hasa kuboresha mahusiano yao. Kwa upande mwingine, Yan (2010) anadokeza kuwa ni nadra sana kwa wanaume kuwapongeza wanaume wenzao kwa kujidunisha wenyewe kama wafanyavyo wanawake.

Utafiti huo wa Yan (2010) unabainisha kuwa wanawake hutoa mapendekezo kwa njia wazi ili kuimarisha mahusiano na wasikilizaji wao na mwisho, anahitimisha kuwa matumizi ya mikakati ya upole hutegemea mahusiano baina ya wazungumzaji wala sio masuala ya kijinsia pekee. Maoni yake yanaupa uzito utafiti wetu kwa sababu katika utafiti wetu, tulichunguza hali zinazopelekea uteuzi wa mikakati, jinsia ikiwa mojawapo. Licha ya uchunguzi wa vipindi vya *SK* kuzingatia zaidi uhusiano wa wahusika, masuala ya kijinsia yalichukua sehemu muhimu. Hata hivyo matokeo ya utafiti wake yalikuwa finyu kwa kuwa data yake iliegemea tu kipindi cha runinga. Kwa hivyo matokeo hayo hayangeweza kutumiwa kuelezea tabia za wanajamii wengine katika jamii zinginezo kwenye mazingira tofauti kabisa. Utafiti wetu unaangazia hasa mikakati ya upole katika mazungumzo ya vipindi vinavyolenga jamii-lugha halisi ya Wakalenjin. Utafiti huo ulituwekea msingi katika kuchunguza

jinsi wahusika wa umri na jinsia tofauti katika vipindi vya *SK* hukabiliana na suala la kuhifadhi uso katika mazungumzo.

Masuala ya upole pia yamechunguzwa na Petrickova (2012). Petrickova ameangazia mikakati ya upole katika maswali ya mahojiano kwenye runinga ya 'Cable News Networks'. Alitumia data kutoka vipindi viwili vya mahojiano ambavyo ni: 'State of the Union' na 'Piers Morgan Tonight'. Uchunguzi wake ulibainisha kuwa mikakati chanya na hasi ya upole ni dhahiri katika mahojiano hayo. Aidha Petrickova alifafanua kuwa uteuzi wa mikakati wa upole hutegemea sio tu uhusiano wa kijamii kati ya msemaji na msikilizaji bali pia jinsi msemaji anataka uhusiano huo udhihirike katika mazungumzo.

Aidha, Petrickova (2012) anakiri kwamba Nadharia ya Upole na hasa kipengele cha uso ni msingi tosha wa kufafanua mikakati ya upole inayotumika katika hali halisi ya maisha. Petrickova anasisitiza kuwa kanuni zinazotawala uteuzi wa mikakati wa upole zinatoa msingi mpana na sahihi wa kuchanganua mikakati ya upole katika hali halisi ya maisha. Ingawa utafiti wa Petrickova ni wa mazungumzo kwenye runinga, maoni yake yalikuwa muhimu kwetu. Utafiti huu ulituchoea kulishughulikia lengo letu la tatu la kuchunguza sababu za uteuzi wa mikakati inayotumiwa katika mazungumzo husika.

Putri (2013) amechunguza mikakati ya upole katika mazungumzo ya runinga katika kipindi cha Oprah Winfrey na kubainisha kuwa Oprah na mgeni wake Ricky Martin walitumia mikakati mbalimbali ya upole ili kuokoa nyuso zao katika mazungumzo waliyoshiriki. Putri anadai kuwa kuna uhusiano baina ya mikakati ya upole na masuala ambayo huathiri uteuzi wa mikakati hiyo. Putri anadokeza kuwa iwapo kwa mfano wazungumzaji ni mtu na mkewe, au labda wana uhusiano wa

karibu, mzungumzaji atajaribu kuonyesha upole lakini si kwa kiwango kikubwa na si katika hali zote. Utafiti wa Putri unahusiana na wetu kwa kiwango kikubwa. Uchunguzi huo ulituchoea kuchunguza jinsi mikakati ya upole inatumiwa na wahusika wa jinsia na umri tofauti katika mazungumzo kwenye vipindi vya *SK*. Hata hivyo, utafiti wetu unatofautiana na wa Putri kwa sababu wetu ni wa mazungumzo katika redio ilhali wake unahusu mazungumzo ya televisheni.

Opindi (2014) amechunguza upole na utambulisho katika lugha ya unyumba miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Moi. Matokeo ya utafiti wake yameonyesha kuwa muktadha huathiri maana na matumizi ya maneno. Ingawa utafiti wa Opindi umeegemea sana katika msamiati na sarufi, kazi yake inatoa mchango kwa utafiti wetu kwa sababu unaonyesha matumizi ya lugha kimuktadha kwa kuangazia masuala ya unyumba ambayo yanajadiliwa katika kazi yetu.

Vipindi vya *SK* vinavyoendeshwa na mwasilishaji Edward Rotich hutoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii katika asasi ya ndoa. Masuala hayo ni kama vile: sababu za kuvunjika kwa ndoa, sababu zinazochangia uke wenza, mavazi katika ndoa, mahusiano katika ndoa, talaka na mpango wa Kando miongoni mwa mengine. Kama wanavyoeleza Brown na Levinson (1987), kutoa ushauri ni kitendo kinachotishia uso wa msikilizaji. Kwa hivyo msemaji hulazimika kutumia mbinu mbalimbali za upole ili kuokoa uso wa msikilizaji. Kufanya hivyo kunaimarisha mahusiano baina ya wahusika na vilevile kuhakikisha kuwa mazungumzo hayo yanasonga mbele bila kukatika. Utafiti wetu uliangazia mbinu za upole zinazotumika katika kushughulikia masuala kama yale tuliyoyataja katika asasi ya ndoa.

Japo suala la upole limewashughulisha wanaisimu wengi kwa zaidi ya miongo mitatu sasa, watafiti daima watakuwa na mengi ya kutafitia katika uwanja mpana wa

upole. Lengo kuu la utafiti wetu ni kubainisha iwapo mazungumzo katika vipindi vya *SK* ambayo yanajadili masuala nyeti kwa uwazi mno, yanajali mahitaji ya uso. Aidha, tasnifu hii imebainisha na kuchanganua mikakati ya upole inayotumika katika vipindi hivyo vya *SK* kwa kutumia Nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson.

2.4 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Upole. Misingi ya nadharia hii iliwekwa na Lakoff (1973) ambaye anasema kuwa wazungumzaji wanafaa kuwa wazi wakati wa mazungumzo. Hata hivyo, Lakoff anasisitiza upole kuliko uwazi. Baadaye, Grice (1975) aliibuka na kanuni aliyoiita Kanuni Ushirika. Ijapokuwa hakutumia neno ‘upole’, kanuni hiyo ya Grice inahusiana kwa karibu sana na Nadharia ya Upole kwa sababu inaoana na mtazamo wa Lakoff (1973) kuhusiana na upole. Hata hivyo, Nadharia ya Upole, hasa mhimili wa kuokoa uso, inahusishwa sana na Brown na Levinson (1978, 1987). Wataalamu hao (Brown na Levinson) wanatazama upole kama mkakati wa kuokoa uso na ndio sababu tumechukua mtazamo wao kama kigezo cha uchanganuzi wetu. Nadharia hii iliendelezwa na kuboreshwa nao Fraser na Nolen (1981), Leech (1983) na Fraser (1990). Kimsingi, nadharia ya Upole inasisitiza kuwa mawasiliano yoyote yale hufanikiwa iwapo washiriki wa mazungumzo wanazingatia mikakati ya upole kwa makusudi ya kuokoa nyuso zao. Aidha, katika mazungumzo, kila mshiriki anatakiwa kuhisi kukubalika. Nadharia ya Upole iliendelezwa na wataalamu hatua kwa hatua kama inavyobainika katika sehemu inayofuata.

2.4.1 Upole Kulingana na Lakoff (1973)

Kwa mujibu wa Lakoff (1973), matumizi ya lugha huongozwa na kanuni za kipragmatiki za uwazi na upole. Kanuni ya uwazi inasema kuwa wahusika wa mazungumzo wanahitajika kuwasiliana kwa uwazi mno ili ujumbe ueleweke. Hata

hivyo, Lakoff anahitimisha kuwa ni muhimu zaidi kuzingatia upole kuliko uwazi. Lakoff anadai kuwa upole katika lugha una dhima ya kuepuka migogoro na hivyo unafaa kuzingatiwa kuliko uwazi. Baadaye, Lakoff aliigawa kanuni ya upole katika vitengo vitatu muhimu ambavyo ni: kutolazimisha ukweli, kutoa uhuru wa kuchagua na kumfanya msikilizaji ajihisi kukubalika.

Lakoff anazungumzia kitengo cha kutolazimisha ukweli kwa kudai kuwa msemaji hahitajiki kusema kila jambo bayana ili ukweli ukubalike. Anasisitiza kwamba msemaji anahitajika kubuni mbinu ya uwasilishaji itakayomfurahisha msikilizaji kwa sababu ukweli haufichiki bali hujitokeza hata usiposemwa kwa uwazi. Kuhusu uhuru wa kuchagua, Lakoff anamwelekeza msemaji kujali hisia za msikilizaji kwa kutumia usemi wenye kumpa msikilizaji nafasi ya kukubali au kukataa kutekeleza jambo. Hilo litamfanya msikilizaji kuhisi kuwa anakubalika katika mazungumzo husika.

Kwa ujumla, kanuni ya upole ya Lakoff inasisitiza mazungumzo yanayopunguza mikwaruzano katika mawasiliano baina ya wanajamii (Maricic, 2005). Kanuni mbalimbali zinatumiwa katika hali tofauti kwa umuhimu wa mitagusano, ama kubuni na kudumisha uhusiano mwema au kupitisha ujumbe ipasavyo. Mawazo ya Maricic ni muhimu kwa sababu ilibainika kuwa wahusika wa mazungumzo ya *SK* wanapozingatia kanuni za upole, mawasiliano yanafanyika kwa njia ambayo inakuza uhusiano kati ya wahusika wa mjadala na jamii inayolengwa na vipindi hivyo.

2.4.2 Upole kulingana na Leech (1983)

Kwa kuendeleza na kuboresha Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1978), Leech (1983) anatoa kaida sita za upole. Kaida alizozipendekeza ni mbinu zinazotumiwa na washiriki wa mazungumzo kwa minajili ya kuwasiliana bila mkwaruzano. Anatumia kaida hizi kuelezea upole kama hali ambayo wazungumzaji

wa jamii husika hutumia kuhakikisha kuwa kuna utulivu wakati wa mazungumzo. Kaida za Leech husisitiza kuwa upole hasi ni muhimu kuliko upole chanya. Anadai kuwa sio kaida zote zina umuhimu sawa. Kwa mfano, anasema kuwa kaida ya kumsifu msikilizaji ni muhimu kuliko ya kujitweza. Kaida za Leech ni pamoja na: kaida ya mkakati, kaida ya ukarimu, kumsifu msikilizaji, kujitweza, huruma na makubaliano na zinaangaziwa katika sehemu inayofuata.

2.4.2.1 Upole kama Kaida ya Mkakati

Upole kama kaida ya mkakati unamlenga msemaji. Inasema kuwa msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli zinazomgharimu msikilizaji na azidishe kauli zinazomfaidi msikilizaji. Kaida hii ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaendana sako kwa bako na maoni ya Brown na Levinson (1987) kuhusiana na mkakati hasi wa upole, ambayo inasisitiza kuepuka kumshinikiza msikilizaji.

Sehemu ya pili inakubaliana na mkakati chanya wa upole wa Brown na Levinson (1987) unaosisitiza kushughulikia mahitaji ya msemazwa. Kwa mfano, “Usijali, mimi nitakufulia nguo hizo”. Mfano huo unaonyesha kuwa msemaji anajali hisia za msikilizaji na yu tayari kumtekelezea jambo linalomsubiri. Huenda msikilizaji anawazia juu ya kutekeleza wajibu wake wa kufua na ndipo msemaji anajitolea kumshughulikia.

2.4.2.2 Upole kama Kaida ya Ukarimu

Kaida ya ukarimu inapendekeza gharama kwa msemaji. Inasisitiza kuwa msemaji azidishe uwasilishaji wa kauli ambazo humgharimisha yeye mwenyewe. Pia, msemaji anatakiwa kupunguza kauli zinazomnufaisha binafsi na kushughulikia zinazomnufaisha msikilizaji. Kwa mfano, ‘Naomba ulale, mimi nitamshughulikia

mgeni'. Usemi huu ni wa manufaa kwa msemazwa lakini unamgharimu msemaji kwa sababu amejitwika majukumu ya kumshughulikia mgeni. Msemaji anadhihirisha ukarimu kwa kujitolea kwa niaba ya msikilizaji.

2.4.2.3 Upole kama Kaida ya Kumsifu Msikilizaji

Kaida ya kumsifu msikilizaji inalingana na mkakati wa upole wa kuepuka kutokubaliana kama itakavyobainika katika sura ya tatu. Kaida hii hulenga kuwafanya wengine wahisi vizuri kupitia kwa ushirikiano wa msemaji. Kaida hii husema kuwa mzungumzaji azidishe kauli zinazotoa sifa kwa msikilizaji na apunguze uwasilishaji wa kauli zinazolenga kutomsifu msikilizaji. Ili kutimiza wajibu huu, msemaji anaweza kutumia tasfida kuepuka kusema lolote litakalozua hisia hasi kwa msemazwa. Kwa mfano, 'Inaonekana kuwa wewe u mwerevu'. Hoja hiyo inamwacha msikilizaji akihihi vizuri kwa kutambuliwa kuwa mwerevu. Huenda msikilizaji si mwerevu sana lakini kwa kuwa msemaji amempa sifa hiyo, msikilizaji atahisi vizuri.

2.4.2.4 Upole kama Kaida ya Kujitweza

Upole kama kaida ya kujitweza hueleza kuwa mzungumzaji anafaa kuzidisha kauli za kujitweza na kupunguza kauli zinazomsifu. Kwa mfano, "Jana nilizembea kweli, waweza kuniendea sokoni leo?" Msemaji ametumia ujanja kuomba msaada kwa msikilizaji lakini kwa kutojisifu. Matumizi ya maneno 'nilizembea kweli' yanayoonyesha kuwa anajitweza na kumweka msikilizaji katika hali inayomfanya kuwa ana uwezo wa kutekeleza jambo aliloshindwa kutekeleza msemaji.

2.4.2.5 Upole kama Kaida ya Makubaliano

Kwa kiasi kikubwa, kaida ya makubaliano inalingana na mkakati chanya wa upole wa Brown na Levinson (1987), wa kutafuta makubaliano na kuepuka kutokubaliana. Kaida hii inasema kwamba msemaji azidishe uwasilishaji wa kauli zinazoonyesha makubaliano kati yake na msikilizaji na apunguze zinazoonyesha ukinzani. Hii haimaanishi kuwa watu waepuke kutokubaliana kabisa na kuzidisha kauli za makubaliano. Kwa mfano, “Ninakubaliana nawe kuwa huyo ni nduguyo wa kiume lakini kwa wakati mwingine si lazima kumwamini sana”. Usemi huu unatoa onyo lakini kwanza kabla ya hayo unadhihirisha kukubaliana na msemazwa.

2.4.2.6 Upole kama Kaida ya Kumwonea Huruma Msikilizaji

Upole kama kaida ya kumwonea huruma msikilizaji ni mbinu aliyotumia Leech (1983) kuonyesha nafasi ya msikilizaji katika mazungumzo yoyote. Kauli inayojitokeza katika kaida hii ni kwamba, msemaji azidishe kauli zilizo na huruma kwa msikilizaji na aepuke kauli za uwazi zisizokuwa na huruma kwa msikilizaji. Mfano ufuatao unadhihirisha kauli hiyo; “Tuko pamoja katika janga hili”. ‘Tuko pamoja ni dhihirisho kuwa msemaji anamwonea huruma msikilizaji. Mbinu hii humpa msikilizaji nafasi ya kuhisi kuwa jambo lililompata linaeleweka kuwa na uzito katika maisha yake.

Hata hivyo, baadhi ya kaida za Leech (1983) zilikosolewa baadaye na Brown na Levinson (1987) kwa madai kuwa ni nyingi sana na hazionyeshi uwazi. Aidha, hazibainishi iwapo kaida hizo ni bia au za jamii husika zenye tamaduni mahsusi. Licha ya ukosoaji huo, kaida za Leech zinaingiliana sana na mikakati ya upole ya Brown na Levinson na zilifaa utafiti huu.

2.4.3 Upole Kulingana na Fraser (1990)

Katika wasilisho lake kwenye Jarida la Pragmatiki juzuu la 14, Fraser anabainisha kuwa dhana ya upole inaweza kushughulikiwa kwa kuzingatia mitazamo minne mikuu ambayo ni: (a) Mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii, (b) Mtazamo wa upole kama mkakati wa mazungumzo, (c) Mtazamo wa upole kama mkataba wa mazungumzo na (d) Mtazamo wa upole kama mkakati wa kuhifadhi uso.

2.4.3.1 Upole kama Kaida ya Kijamii

Kulingana na Fraser (1990), upole kama kaida ya kijamii ni mtazamo unaorejelea namna upole umekumbatiwa na watu katika jamii mbalimbali. Mtazamo huu huchukulia kwamba, kila utamaduni una kaida za kijamii ambazo husheheni kanuni zinazoelekeza tabia fulani, hali ya mambo na namna ya kuwaza katika muktadha maalum. Kulingana na mtazamo huu, upole huonyeshwa kama dhana inayohusiana na namna ya kuzungumza kimaridhiano kwa kuzingatia kaida na utamaduni wa jamii. Kwa kulinganisha na kaida za mazungumzo maalum kwenye redio, tulitumia mtazamo huu kuchunguza kaida wanazotumia Wakalenjin kama jamii katika kipindi cha *SK*. Kutokana na ulinganishi huo, ilibainika kuwa Wakalenjin kwa ujumla husheheni kanuni maalum ambazo zinaongoza mazungumzo yao.

2.4.3.2 Upole kama Mkakati wa Mazungumzo

Kwa kufafanua mtazamo wa upole kama mkakati wa mazungumzo, Fraser (1990) anaegemeza mawazo yake katika kazi ya Grice (1975). Fraser (1990) anatumia ufafanuzi wa Grice (1975) ambao unaeleza kwa kina zaidi kuhusu upole kama mkakati wa mazungumzo. Grice (1975) anadai kuwa wazungumzaji ni watu wenye akili razini na ambao haja yao kuu ni kupitisha ujumbe. Kwa hivyo, msemaji anafaa kusema jambo analotaka ipasavyo. Grice (1975) aliigawa kanuni ushirika

katika kaida nne ambazo hutawala mazungumzo yoyote yale. Kaida hizo ni: kaida ya kiasi, kaida ya ubora, kaida ya uhusiano na kaida ya namna. Kaida za Grice zinajibu swali ‘Ni nini kinachowasilishwa na vipi?’ Kiini cha swali hili ni kubainisha ujumbe mahsusi unaowasilishwa katika mazungumzo na namna ya uwasilishaji.

Urazini wa mja humwelekeza katika kutambua ni nini cha kusemwa na kusemwe vipi. Kutokana na hali hiyo, mzungumzaji lazima awe na uhakika wa kile anataka kuwasilisha (ujumbe) na vipi auwasilishe ujumbe huo (nyenzo). Hapa ndipo tunaona mwingiliano baina ya ujumbe na nyenzo za uwasilishaji wake. Suala la upole basi linakuwa muhimu katika kufanikisha mawasiliano katika mazungumzo, vinginevyo, mawasiliano hayo yanaweza kukatika.

Kimsingi, mtazamo wa upole kama mkakati wa mazungumzo unasisitiza kuwa mzungumzaji ana jukumu la kuwasilisha ujumbe maalum anapozungumza. Kutimiza lengo hili, msemaji anapaswa kutumia Kanuni Ushirika kwa kuzingatia kaida za kiasi, ubora, uhusiano na namna.

2.4.3.2.1 Kanuni Ushirika

Mtazamo wa Fraser wa upole kama mkakati wa mazungumzo ndio umefafanuliwa na Grice (1975) kama Kanuni Ushirika. Grice (1975) anashauri kupitia kanuni hiyo kuwa wanapozungumza, watu hushirikiana. Ili kufikia lengo hili, Grice alipendekeza kanuni ya jumla ya ushirikiano inayodai kuwa, “Msemaji anafaa kufanya mchango wake kuwa unaohitajika katika kipindi ambamo unatokea na katika mwelekeo unaokubalika katika mazungumzo anayoshiriki”. Hoja hiyo inahoji kuwa msemaji anafaa kusema jambo analotaka kupitisha kwa namna anayopaswa ili msemazwa afasiri maana inayokusudiwa. Kanuni Ushirika inasisitiza kuwa wahusika katika mazungumzo

hushirikiana kupitia kaida za kiasi, ubora, uhusiano na namna ili kuwe na maelewano (Lindblom, 2001).

a) Kaida ya Kiasi

Kaida ya kiasi hueleza kuwa msemaji anafaa kufanya mchango wake kwa kutoa kiasi kitakikanacho cha taarifa. Hii inamaanisha kuwa maelezo ya msemaji yaeleweke kadri inavyowezekana kwa kutoa taarifa inayotosheleza bila kutoa maelezo mengi yasiyohitajika. Ni muhimu kutambua kuwa bila Kanuni Ushirika, kuwasiliana kwa watu kungekuwa na matatizo mengi.

Msimamo wa Grice (1975) kwa wahusika wa mazungumzo ni kwamba wanapaswa kusema mambo kwa kiasi kinachotakikana. Hii ni kwa minajili ya kuzuia taarifa nyingi zisizo muhimu kwa mada husika. Iwapo msemaji atatoa maelezo marefu kwa muktadha wa swali linalohitaji neno moja tu 'ndio' au 'la' atakuwa anavunja kaida ya kiasi/idadi na hivyo kurefusha au kutinga mawasiliano bila sababu. Kaida ya kiasi ni muhimu kwetu kwa sababu tumeitumia kuchuja taarifa za washiriki kama njia ya kupata data inayotufaa tu.

b) Kaida ya Ubora

Kaida ya ubora inasisitiza kuwa msemaji hafai kusema mambo anayoamini kuwa ya uongo au mambo ambayo kwayo hana ithibati ya kutosha. Iwapo msemaji atatoa habari za kupotosha, mawasiliano yatakuwa na shida na yatakosa ukweli na hata kusababisha matatizo kati ya wahusika wa mazungumzo. Tumetumia kanuni hii kuchunguza iwapo wahusika katika vipindi vya *SK* humudu uwazi huku wakizingatia mikakati ya upole.

c) **Kaida ya Uhusiano**

Kaida ya uhusiano inaeleza kuwa, msemaji anafaa kusema mambo yanayohusiana na mada ya mazungumzo husika tu. Hafai kutoka nje ya mada inayozungumziwa. Wasikilizaji na wasemaji wanalazimika kuzungumza kiushirikiano na wote wakubaliane kueleweka katika njia fulani. Kanuni ushirika hivyo basi, hufafanua namna mawasiliano katika maongezi huafikiwa katika hali za kawaida za kijamii. Watu wanaozingatia kaida ya uhusiano katika matumizi yao ya lugha, huhakikisha kuwa jambo wanalosema katika mazungumzo linaendeleza lengo la mazungumzo hayo.

Kama anavyodokeza Grice (1975), kanuni ushirika kwa jumla huchukulia kuwa wasikilizaji kwa wasemaji wanazingatia kanuni hii. Jambo ambalo huzua suitafahamu ni kutoeleza bayana maana iliyokusudiwa na badala yake kuidokeza tu. Kaida hii imetufaa katika uchanganuzi wa namna mwasilishaji mkuu wa kipindi humudu kuwarejesha washiriki wanapotoka nje ya mada husika.

d) **Kaida ya Namna**

Kaida ya namna husisitiza umakinifu kwa upande wa msemaji katika kueleza jambo. Aidha, msemaji anapaswa kuwa mwangalifu anapotoa mahitimisho yake. Msemaji anafaa kujiepusha na kauli tata ambazo huweza kuibua fasiri tofautitofauti. Asitoe maelezo marefu ya kimzunguko bali maelezo yake yawe na mshikamano. Kwa hivyo, msemaji anafaa kueleza hoja zake kwa uwazi iwezekanavyo ili kuzuia utata.

Kwa kumuunga mkono Grice (1975), Yule (1996) anadai kuwa katika mazungumzo, mambo mengi huwasilishwa kuliko yanayosemwa, yaani usemi unaweza kupata maana nyingi kutegemea ufasiri wa msikilizaji. Mawazo hayo yanadokeza kuwa usemi huweza kubeba maana zaidi ya ile iliyokusudiwa na msemaji. Hii hutegemea

jinsi msemaji anatoa ujumbe na jinsi msikilizaji anaufasiri usemi husika (Malle, 2001). Kaida ya namna ya kueleza ilitumika kupima uwazi wa hoja za washiriki katika kipindi cha *SK*.

Grice alitambua kuwa kuna baadhi ya watu ambao hawafuati kanuni hizi kila wakati. Aligundua kuwa wao huzivunja kanuni hizo kimakusudi ili kukidhi mahitaji ya nyuso zao na za wenzao. Kuvunja kanuni hizi hata hivyo kunaweza kudokeza maana nyingine ya kauli husika. Ni kwa msingi huu ndipo utafiti huu umezingatia Nadharia ya Upole na kaida za ushirikiano za Grice kuhakiki maongezi katika vipindi vya *SK*. Utafiti huu umetathmini namna ambavyo kanuni hizi za Grice (1975) zinazingatiwa au kukiukwa na washiriki wa mazungumzo katika vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*.

Hata hivyo, kaida za ushirikiano za Grice zinafaa kujaribiwa na kuboreshwa kwa kuwa, upole katika mazungumzo ni jambo la kitamaduni na kwa hivyo kanuni yake siyo kanuni bia kutokana na tofauti za kitamaduni. Kwa mujibu wa Spencer-Oatey (2000) na Mills (2011), upole ni suala la ufaafu wa mazungumzo. Ufaafu huu hutegemea tofauti za kitamaduni kwa kila jamii. Inamaanisha kuwa utamaduni huchukua sehemu kubwa katika uamuzi wa kile kinachochukuliwa kuwa upole na kile ambacho si upole. Uboreshaji unatokana na tafiti zinazohusiana na upole kwa kuhusisha lugha chanzi kama ya Kikalenjin na zingine za Kiafrika ili kutathmini ubia wa kanuni hizo.

Mitazamo ya Fraser (1990) inajibu swali ‘vipi?’ Mitazamo hii inazingatia namna ambavyo ujumbe unawasilishwa. Ni muhimu kutaja kuwa, aghalabu watu wanapozungumza, lengo huwa ni kupitisha ujumbe. Bila shaka ujumbe huo hauwezi kueleweka iwapo washiriki wa mazungumzo hawatatumia njia fulani kuhakikisha

kuwa ujumbe uliokusudiwa umewasilishwa ipasavyo. Hapa ndipo pana muumano kati ya Nadharia ya Upole na kaida za Grice (1975) katika ukamilishaji wa mawasiliano.

2.4.3.3 Upole kama Mkataba wa Mazungumzo

Upole kama mkataba wa mazungumzo, ni mtazamo uliobuniwa na Fraser na Nolen (1981) na Fraser (1990). Fraser anaeleza kuwa mazungumzo yoyote yanapoanza, kila mshiriki huwa na uelewa wa mpangilio fulani wa haki na majukumu ambayo hubainisha, japo katika hatua za mwanzo, mambo ambayo kila mzungumzaji anatarajia kutoka kwa mwenzake. Mtazamo huu unafanana na kanuni ushirika ya Grice (1975) kuhusiana na kile ambacho msikilizaji anatarajia kutoka kwa msemaji. Mtazamo huu ulituelekeza kufafanua namna wazungumzaji wa vipindi vya *SK* hukidhi matarajio ya wenzao.

2.4.4 Upole Kulinganana na Brown na Levinson (1978, 1987)

Brown na Levinson wanaangalia upole kama mkakati wa kuokoa uso. Wataalamu hao wanaugawa upole katika makundi ya upole hasi na upole chanya. Huu ndio mkakati uliozingatiwa kwa kina na kupanuliwa kwa misingi ya aina mbili za uso. Brown na Levinson wanaweka wazi mipaka ya aina hizo za uso kwa kubainisha vitendo vinavyotishia uso chanya na uso hasi wa wahusika wa mazungumzo yoyote. Kama inavyobainika katika sehemu inayofuata, kazi hii imejikita sana katika mkakati huu wa kuokoa uso.

2.4.4.1 Upole kama Mkakati wa Kuokoa Uso

Mawazo ya Fraser (1990) kuhusiana na upole kama mkakati wa kuokoa uso yanaafikiana na yale ya Brown na Levinson (1987), ambao ni waasisi wa mtazamo wa upole kama mkakati wa kuokoa uso. Waasisi hao walitumia dhana ya uso ya

Goffman (1967) kubuni nadharia ya upole ya uso. Goffman (1967) anasema kuwa uso ni thamani ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na anavyotazamwa na wengine. Uso ni dhana bia na pia sura ya kibinafsi. Kwa ujumla, uso unarejelea kile ambacho mtu anatamani katika mawasiliano (Ting-Toomey, 2009). Kwa vile matamano ya washiriki wa mazungumzo hutofautiana, Brown na Levinson (1987) wanahoji kwamba dhana ya uso inaweza kugawanywa katika sehemu mbili: uso chanya na uso hasi. Uso chanya ni hali ya mshiriki wa mazungumzo kutamani kuwa hisia zake zikubalike na wenzake katika mawasiliano; nao uso hasi ni hali ambayo kwayo mtu hataki kuzuiliwa kujieleza anavyotaka. Aidha, Goffman (1967) anasema kuwa kutunza uso kunamfanya mtu kuhisi vizuri. Kwa upande mwingine, kupoteza uso kunasababisha kupotea kwa mhimili wa kihisia ambao huhifadhiwa katika hali za kijamii.

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa kuna taarifa ambazo hutishia nyuso za wasikilizaji. Hii husababishwa na uchache wa idadi ya majibu mbadala ya taarifa hizo. Hiyo ndiyo sababu mzungumzaji analazimika kuteua mikakati ya kuwasilishia ujumbe ili kupunguza vitisho kwa nyuso za wasikilizaji. Kama asemavyo Morand (2003) watu hutumia lugha kudhihirisha uso. Kwa vyovyote, wahasika wa mazungumzo huweza kuathirika kwa njia chanya au hasi na kwa hivyo kipengele cha uso ni cha kutiliwa maanani katika kuchunguza mazungumzo yoyote yale.

Kutokana na ukweli kuwa athari za kihisia za kupoteza uso zinaweza kuwa dhahiri, watu mara kwa mara hushiriki katika vitendo vya kuokoa nyuso zao na za wengine katika mazungumzo. Johnstone (2008) anasema kuwa wazungumzaji hawana budi 'kuokoa uso' wanapokabiliana na tendo linalotishia uso wa msikilizaji. Tendo hilo linaweza kuwa la kutishia uso chanya au uso hasi.

Kama wasemavyo Brown na Levinson (1987), ni muhimu kwa mja kuhifadhi sio tu uso wake bali hata nyuso za wenzake. Upole kama mkakati wa kuokoa uso unaafikiana na kaida ya Grice (1975) ya namna. Namna mtu anatoa ujumbe huathiri nyuso za wasikilizaji. Mkakati huu umetumika kubainisha jinsi washiriki wa mazungumzo katika vipindi vya *SK* wanavyowasiliana ili kuafiki maelewano baina yao na kuhakikisha kuwa wanadumisha mahusiano yao.

2.4.4.2 Vitendo Vinavyotishia Uso

Brown na Levinson (1987) wanabainisha aina nne za vitendo vinavyoweza kutishia nyuso za wazungumzaji na wasikilizaji katika mazungumzo yoyote yale. Vitendo hivyo huweza kuathiri uso wa msemaji au/na wa msikilizaji. Hii inamaanisha kuwa, baada ya usemi wowote kutolewa au kusikilizwa, msemaji na msikilizaji wanaweza kuathirika kwa njia hasi au chanya kwa pamoja au mmoja baada ya mwingine. Vitendo vinavyotishia uso hasi wa msikilizaji hutokea wakati msemaji anaingilia uso hasi wa msikilizaji kwa kutoa maagizo, kuonya au kuamrisha. Kwa mfano msemaji anapomwambia mtu anayeelekea msalani ifuatavyo: “Hakikisha umemwaga maji baada ya kutumia choo”. Usemi huo unatishia uso hasi wa msikilizaji. Ni usemi agizaji na kwa vyovyote vile, usemi huu unamletea msikilizaji aibu na hivyo kuhisi vibaya.

Kuna pia kategoria ya pili ambayo ni ya vitendo vinavyotishia uso chanya wa hadhira. Ni vitendo au kauli zinazoweza kumtia aibu msikilizaji. Kumtia aibu msikilizaji ni kuathiri uso chanya wake. Kauli hizo ni kama: kumtisha, kumtusi, kumdunisha msikilizaji au kuzungumzia mada mwiko katika jamii yake. Kwa mfano mwalimu darasani anapomwambia mwanafunzi “Wewe ni mjinga kama mamako”. Matusi hayo yanaathiri uso chanya wa msemazwa.

Aina ya tatu ni ya vitendo vinavyotishia uso hasi wa msemaji. Matendo kama vile kutoa ahadi kwa msikilizaji, kukubali kusamehe, kukubali pendekezo fulani kutoka kwa msikilizaji na kukubali shukrani zake hutishia uso hasi wa msemaji. Kwa mfano, iwapo watu wawili wamekosana na mpatanishi ahusishwe, kisha mpatanishi aseme “Ni vizuri kukubali kumsamehe mwenzako kwa sababu hata wewe utahitaji msamaha wakati mwingine”. Kauli hii ya mpatanishi inamlazimu mzungumzaji kukubali kutoa msamaha.

Kategoria ya mwisho ni ya vitendo vinavyotishia uso chanya wa msemaji. Mifano ya matendo hayo ni kama vile kujidunisha mbele ya msikilizaji, kumwomba msamaha msikilizaji, kukiri makosa na kukubali pongezi kutoka kwa msikilizaji. Hayo yote yanaathiri uso chanya wa msemaji. Kwa mfano, “Nisamehe, tafadhali”. Usemi huu unadhihirisha kuwa msemaji amejijweka katika nafasi ya kutojinasua mwenyewe ila kupitia kwa kitendo cha msikilizaji.

2.4.4.3 Kukabiliana na Vitendo Vinavyotishia Uso

Kuna mikakati mitano ya kukabiliana na vitendo vinavyotishia uso wakati wa mazungumzo kama inavyopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Wataalamu hao wanasema kuwa mikakati hii hutumiwa kutegemea ni uso gani unakabiliwa na tishio. Mikakati hiyo ni: kuwa kwenye rekodi, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati wa kuwa nje ya rekodi na mkakati wa kutosema ujumbe unaotishia uso.

2.4.4.3.1 Kuwa Kwenye Rekodi

Kuwa kwenye rekodi ni mkakati unaotumiwa na wahusika wa mazungumzo ambao wanafahamiana vyema (Arundale, 2006). Mkakati huu haulengi mahitaji ya uso au

vitisho kwa uso wa msikilizaji bali msemaji anatilia mkazo ujumbe anaouwasilisha. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi hutumika katika mazingira ya: kutoa ahadi kwa msikilizaji, kuwepo tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na msikilizaji, dharura au kutamauka na kutaka kumfaidi msikilizaji.

a) Kutoa Ahadi kwa Msikilizaji

Kutoa ahadi kwa msikilizaji ni mkakati wa kuwa kwenye rekodi ambao unaweza kutumiwa na msemaji kuokoa uso wa msikilizaji. Ni sawa na kujitweza ili kumkweza msikilizaji. Katika hali hiyo msemaji hahitaji kuwa mpole kwa sababu anayefaidika ndiye msikilizaji. Kwa mfano, ‘Lazima nikununulia nguo kesho asubuhi.’ Licha ya ulazima katika usemi huu, mfaidi wa kitendo kitakachofanyika ni msikilizaji na kwa hivyo hakuna haja ya msemaji kuwa mpole.

b) Tofauti za Kimamlaka

Kuwepo tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na msikilizaji ni aina nyingine ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Aina hii hutumiwa wakati kuna tofauti za kimamlaka kati ya washiriki wa mazungumzo. Kadiri umbali wa kijamii kati ya washiriki wa mazungumzo unavyoongezeka ndivyo kiwango kikubwa cha upole kinavyohitajika. Mzungumzaji mwenye mamlaka hahitaji kutumia upole anapozungumza na mdogo wake. Mfano mzuri ni wakati baba anamwambia mtoto wake ‘Nipe kitabu chako nione kazi yako.’ Baba anatumia mamlaka yake kama mzazi, kumwamuru mwanawe ampe kitabu na wakati uo huo, mwana hahisi kuwa ameamrisha bali huchukulia kuwa ni kawaida kwa mzazi kusema hivyo kwa sababu za kiumri na majukumu ya kiuwezo.

c) Hali ya Dharura

Mkakati mwingine wa kuwa kwenye rekodi ni katika hali ya dharura au kutamauka. Hali kama hii humhitaji msemaji kushughulikia manufaa ya msikilizaji wala sio uhifadhi wa uso wa msikilizaji huyo. Kwa mfano, ‘Pita haraka gari linakuja kasi’ ni kauli ya kuamrisha lakini msemaji hahitajiki kuwa mpole kwa sababu manufaa ni kwa msemazwa.

d) Kumfaidi Msikilizaji

Kumfaidi msikilizaji ni hali nyingine ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Kwa mfano ‘Leta fomu za mkopo nikujazie.’ Neno ‘leta’ ni amrifu lakini msikilizaji hahisi vibaya kwa sababu kitendo ni cha kumfaidi yeye mwenyewe. Msemaji huwa hasumbuki kutafuta maneno mbadala wakati wa hali kama hizi. Mbinu hii inasisitiza matumizi ya maneno ya uwazi kwa sababu msaada unaopatikana ni kwa msikilizaji na kwa hivyo kauli kama hizi hazihitaji upole.

2.4.4.3.2 Mkakati wa Upole Chanya

Kwa kutumia mkakati wa upole chanya, msemaji huashiria kuwa yeye pamoja na msemazwa ni washiriki wa jambo fulani na wote wana msimamo au nafasi sawa. Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa mkakati chanya wa upole huelekezwa kwa uso chanya wa msikilizaji na matamano yake kuwa mahitaji yake yanakubalika. Mkakati huu humfanya msikilizaji ahisi vizuri kuhusu hali yake na matamano yake. Msemaji hujaribu kuwa karibu na msikilizaji kwa kuanzisha ukuruba wa kuonyesha kuwa anamheshimu. Ujengaji huu wa ukuruba hufanyika kupitia msemaji kuzungumzia mambo ambayo yanampendeza msikilizaji na kujaribu kubuni mazingira yanayowatosheleza wote wawili. Brown na Levinson (1987) wanapendekeza njia kadhaa ambazo kwazo mkakati chanya wa upole hutekelezwa.

a) Kutumia Ucheshi

Mbinu ya kutumia ucheshi humfanya msikilizaji kuchangamka na kutekeleza wajibu wake bila kuhisi uzito wowote wa kazi inayopaswa kutekelezwa. Kwa mfano baada ya msikilizaji kumwambia msemaji kuhusu kazi nyingi alizo nazo, msemaji anaweza kusema, “Kwa kweli naona kuwa leo baadaye utapumzika sana!” Kauli hii inamfanya msikilizaji kuhisi wepesi wa kazi alizofikiria kuwa nyingi. Mbinu hii inanuia kumfanya msikilizaji kulegeza mawazo yake kuhusu shughuli kubwa inayomsubiri.

b) Kudhihirisha Urajua

Kupitia urajua, msemaji anaweza kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kumwelekeza amtekelezee agizo fulani. Mkakati chanya wa upole hutumika sana wakati wahusika wa mazungumzo wana uhusiano wa kimamlaka. Mfano mzuri ni mazungumzo baina ya mwalimu na mwanafunzi pale ambapo mwalimu anasema, ‘Utanisaidia kubeba mkoba huu, sivyo?’ Kuwa na urajua ni kutarajia jambo fulani litekelezwa na msikilizaji. Mwalimu anatarajia kuwa mwanafunzi wake atambebea mkoba wake. Hii ni kutokana na tofauti za kimamlaka kati yake na mwanafunzi.

c) Matumizi ya Utambulisho wa Makundi

Aina nyingine ya kutekeleza mkakati chanya wa upole ni kwa kutumia utambulisho wa makundi. Hii ni njia ya kutumia maneno yanayoonyesha uhusiano mzuri kati ya msemaji na msemazwa. Ili kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji wake, msemaji anaweza kusema hivi, ‘Mpendwa, ninatumai kuwa utanipeleka sokoni leo jioni.’ Usemi huu unamfanya msemazwa kuhisi vizuri kwa sababu ameitwa ‘mpendwa.’ Pia, msemaji anaweza kutekeleza upole chanya kwa kutaka idhini ya kutenda kitendo fulani lakini kwa njia ya maswali na kutoa sababu. Mfano, ‘Kwa nini usipike chapati leo na tunao unga wa ngano?’ Mkakati huu unakubalika kuliko kutoa amri kwa msikilizaji kutekeleza wajibu fulani.

d) Kumtambua na Kumshughulikia Msikilizaji

Mkakati chanya wa upole unaweza kutekelezwa pia kupitia kumtambua na kumshughulikia msikilizaji. Kwa kutumia mbinu hii, msemaji anamfanya msikilizaji kuhisi vizuri kwa mfano, kutambua na kumpongeza kwa bidii yake katika kutekeleza jambo fulani kama vile kuvaa vizuri, kuchukua nafasi ya kwanza darasani na pengine kuwa safi. Mfano mzuri ni wakati mzazi anamwambia mtoto wake; “Pongezi kwa umahiri wako, sasa umethibitisha kuwa wewe ni shujaa kweli.” au “Kazi ulizofanya ni nyingi sana na nina uhakika unahisi njaa, nikupikie chakula?” Kupitia kwa kauli hizo, uso chanya wa msikilizaji unahifadhiwa kwani anahisi vizuri kuwa anatambulika na kwamba mahitaji yake ni muhimu. Mbinu hii inafanana na mkakati wa kuwa kwenye rekodi.

e) Kutoa Ahadi kwa Msikilizaji

Kutoa ahadi ni njia nyingine ya kuokoa uso chanya wa msikilizaji. Hii ni njia nyingine ya kutekeleza mkakati wa upole chanya. Mzungumzaji anaweza kuahidi kumfanyia msikilizaji kitu fulani ambacho kitamfurahisha na kumfaidi. Kwa mfano, “Usitie shaka, nitakufulia nguo zako leo jioni.” Mbinu hii humfanya msemazwa kuhisi kuwa amethaminiwa kwa kupewa ahadi ya kufanyiwa kitu kilichosemwa.

2.4.4.3.3 Mkakati wa Upole Hasi

Mkakati wa upole hasi, unaelezwa na Brown na Levinson (1987) kuwa tofauti kabisa na mkakati chanya wa upole. Hii ni kwa sababu mkakati huu hautumiki kwa njia huria kama mkakati chanya wa upole. Lengo kuu la mkakati hasi wa upole ni kupunguza ulazimishaji wa kauli fulani kwa msikilizaji. Mkakati wa upole hasi unaweza kutumiwa na msemaji wakati anahitaji kitu kutoka kwa msikilizaji lakini

anajiepusha kuonekana kutumia ulazima na hivyo kumnyima msikilizaji uhuru wa kukataa.

Madai hayo yanaungwa mkono na Huang (2007) ambaye anasema kuwa mkakati wa upole hasi husisitiza uhuru wa msikilizaji japo msemaji atapata anachohitaji. Kupitia kwa mkakati huu, kuna chukulizi kuwa msemaji atakuwa analazimisha matamano yake kwa msemazwa. Hali hii huzua uwezekano mkubwa wa kumwaibisha msikilizaji kuliko mkakati wa kuwa kwenye rekodi au mkakati chanya wa upole. Zifuatazo ni njia ambazo msemaji anaweza kutumia ili kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji wake.

a) Kuomba Msamaha

Msemaji anaweza kuomba msamaha ili kuhifadhi uso hasi wa hadhira yake. Jambo hili hutokea kabla ya kutoa kauli ambayo msemaji anafikiria kuwa itamwaibisha msikilizaji au itamfanya ahisi vibaya. Ili kuepuka hayo, msemaji anaweza kusema, “Samahani Sarai, nitakwambia jambo hili hata ingawa hutafurahia.” Mfano huu unaonyesha namna ambavyo msemaji anajali mahitaji ya uso wa msikilizaji wake. Kwa kutumia neno ‘samahani’ msemaji anaonekana kumtayarisha msikilizaji kupokea ujumbe fulani usio mzuri ili atakapopata ujumbe huo asiabike au kuudhika.

b) Matumizi ya Maswali na Vidokezo

Aina nyingine ya kutekeleza mkakati hasi wa upole ni kwa kutumia maswali na vidokezo. Kwa mfano, “Ah...mm mwalimu, sijui...ii kama itawezekana uniazime kitabu chako tena?” Aina hii ya mkakati hasi wa upole huhifadhi uso hasi wa msemazwa kwa sababu msikilizaji atahisi kuwa ana uamuzi wa kukataa au kukubali. Uso wa msemaji pia utakuwa umehifadhiwa kwani anajihami na kutoonekana kulazimisha na pia kutarajia jawabu la ‘ndio’ au ‘la’.

c) Matumizi ya majina ya Heshima

Namna nyingine ya kutimiza mkakati hasi wa upole ni kwa kutumia usonde jamii. Hii ni mbinu ambayo msemaji anaweza kutumia majina ya kihonorofiki au vitambuzi rasmi wakati wa mazungumzo. Majina hayo ni kama vile Profesa, Daktari na Mwalimu. Haya ni majina ya kuonyesha heshima baina ya msemaji na msikilizaji ili kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji. Majina hayo yanatumika baina ya watu ambao hadhi zao ni tofauti. Kwa mfano katika mazungumzo baina ya mwanafunzi wa shahada ya uzamili na msimamizi wake, mzamili anaweza kusema, “Uniwie radhi Daktari, unaweza kupitia tasnifu yangu tena?”

d) Kutumia Kauli za Jumla

Kutumia kauli ya jumla ni mbinu nyingine ambayo msemaji anaweza kutekelezea mkakati hasi wa upole. Kulingana na Brown na Levinson (1987), msemaji anaweza kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji kwa kutumia kauli ambazo hazimlengi mtu yeyote hasa bali ni za kujumulisha. Mfano wa kategoria hii ni katika muktadha wa shule ya mabweni ambapo mwalimu wa zamu anaweza kusema, “Nisisikie kelele zozote bwenini.” Kauli hii haimlengi yeyote hasa bali ni wanafunzi wote kwa jumla. Kwa hivyo, uso wa hadhira unahifadhiwa kwa vile makali ya tamko hilo hayamwelekei mtu binafsi.

e) Kunominisha Vitenzi

Kunominisha vitenzi vinavyomhusu msikilizaji ili kuokoa uso wake hasi, ni kategoria nyingine ya mkakati hasi wa upole. Hii ni mbinu ya kutumia nomino badala ya vitenzi katika kuonya mtu au kumpasha habari muhimu. Mchungaji anaweza kusema kwa mwumini, “Larry, kutohudhuria ibada kila mara humfanya mtu kuzembea kiroho.” badala ya kusema, “Ulikosea kutohudhuria ibada hivyo utazembea kiroho”. Kupitia kwa unominishaji wa vitenzi, msemaji anahifadhi uso hasi wa msikilizaji. Neno

‘kutohudhuria’ ni heri kuliko matumizi ya maneno ya moja kwa moja kama vile kusema ‘hukuhudhuria’.

f) Kutumia Vitangulizi

Kadhalika, matumizi ya vitangulizi ni kategoria nyingine ya mkakati hasi wa upole ambayo msemaji anaweza kutumia ili kupunguza vitisho kwa uso hasi wa msikilizaji. Mfano mzuri ni wakati rafiki anaweza kumwonya mwenzake mwenye tabia ya kusema mambo ovyo ovyo kwa kusema, “Ninafikiria si vizuri kumwaga mtama penye kuku wengi maanake si kila mmoja ana uwezo wa kuficha siri.” au pengine, “Wajua, wanawake pia wana haki ya kuheshimiwa kama wanaume.” Kauli ‘ninafikiria’ na ‘wajua’ hupunguza makali ya usemi kwa msikilizaji kinyume na kusema wazi wazi kuwa, “Si vizuri, Wanawake wana”. Vitangulizi humfanya msikilizaji kuona kuwa halazimishwi kukubali kauli fulani ilivyo bali ni njia mojawapo ya kutafuta suluhisho kwa jambo.

g) Kuwa bila Rajua

Mkakati hasi wa upole unaweza kutekelezwa pia kupitia hali ya msemaji kuwa bila rajua. Hii ni hali ya kutotarajia mazuri na kupitia usemi wake, msemaji anajaribu kumwonyesha msikilizaji kuwa hatarajii kuwa anaweza kumsaidia lakini anahitaji msaada fulani. Kwa mfano, “Nina uhakika huna uwezo wa kunisaidia lakini nitakwambia tu, ninahitaji sana pesa za kusukwa nywele leo aduhuri.” Pia, msemaji anaweza kusema, “Kwa kweli wewe ni rafiki yangu mkuu na ungeweza kunisaidia kwa njia yoyote lakini sidhani una shilingi elfu sita ninazohitaji.” Kategoria hii ya mkakati hasi wa upole hulenga kuhifadhi uso hasi wa hadhira lengwa.

2.4.4.3.4 Mkakati Nje ya Rekodi

Mkakati nje ya rekodi ni mkakati wa upole usio wa moja kwa moja. Msemaji anaweza kukabiliana na vitisho kwa uso wa msikilizaji kwa kudokeza tu jambo na kumwachia msikilizaji kulifasiri anavyotaka. Mkakati huu unalenga kuwa msemaji asilazimishe matamania yake kwa hadhira yake bali atafute mbinu ya makubaliano. Kulingana na Brown na Levinson (1978), si rahisi kuhusisha maana moja wazi katika usemi wowote ule katika mkakati nje ya rekodi. Hii ina maana kuwa kuna uwezekano wa kuzuka utata katika usemi wowote. Utata huu aidha unatokana na kuvunjwa kwa kaida ya namna katika Kanuni Ushirika ya Grice.

Kulingana na Cutting (2008), utata katika usemi huokoa nyuso za wahusika wa mazungumzo. Iwapo msikilizaji atadokeza maana ambayo inamletea aibu, msemaji anaweza kuokoa uso wake kwa kukana kauli halisi iliyodokezwa na msikilizaji. Hata hivyo, utumiaji wa mkakati nje ya rekodi unatakiwa kufanyika kwa uangalifu sana kwa sababu msikilizaji anaweza kudokeza kauli ambayo haikukusudiwa na hii huenda ikamfanya msemaji asifaulu kupitisha ujumbe aliokusudia. Kwa mfano: “Ninashuku nimeangusha pesa njiani.” Iwapo msemaji ana nia ya kupewa pesa na msikilizaji, huenda asifaulu kwa sababu msikilizaji atafikiria labda msemaji hahitaji pesa bali kuhurumiwa tu. Kwa kumjali msemaji, msikilizaji anaweza kusema, “Pole dadangu kwa kupoteza pesa zako,” lakini asimpe msaada wowote. Kulingana na Brown na Levinson (1987), mkakati huu wa upole huokoa nyuso za wasikilizaji lakini mara nyingi msemaji huenda asifaulu katika kupitisha ujumbe aliokusudia au kutekelezewa jambo. Zifuatazo ni njia ambazo zinaweza kutumiwa katika utekelezaji wa mkakati nje ya rekodi:

a) Matumizi ya Kinaya au Kejeli

Ili kuhifadhi nyuso za wahusika wa mazungumzo, kinaya au kejeli zinaweza kutumiwa. Iwapo msemaji hataki kusema jambo moja kwa moja, anaweza kutumia mbinu hii ya kejeli. Kwa mfano, iwapo mtahiniwa amechukua nafasi ya mwisho katika mtihani wa hisabati, msemaji anaweza kuhifadhi uso wake kwa kusema, “Hata hivyo umejaribu.” Kauli hii inapunguza makali ya usemi wa moja kwa moja kama vile, “Umefeli sana mtihani huu.”

b) Matumizi ya vidokezo

Mbinu ya vidokezo inatumiwa na msemaji wakati anahitaji kutekelezewa jambo na msikilizaji wake. Msemaji huenda anahitaji maji ya kunywa lakini hataki kusema moja kwa moja. Atatafuta mbinu ya kuhifadhi uso wa msikilizaji wake kwa kumwambia, “Siku hizi jua linawaka sana hadi mtu huhisi kiu kila wakati.” Kauli hii huhifadhi uso hasi wa msikilizaji lakini huenda msikilizaji asifikirie kuwa msemaji anahitaji maji wakati huo. Kutekelezwa kwa kitendo cha kutoa maji kwa msemaji kunategemea namna msemazwa anafasiri ujumbe wa msemaji. Hapa ndipo kaida ya Grice ya na Nadharia ya Upole hujalizana.

c) Kutumia Sitiari

Watu wanapotumia sitiari huashiria kitu kingine ambacho hakihusiani na neno au kirai kilichotajwa. Matumizi ya sitiari humwezesha msemaji kuokoa sio tu uso wake bali hata uso wa hadhira lengwa. Kwa mfano mzee wa kanisa anaweza kuwatahadharisha washiriki kwa kusema, “Nimesikia kuna wachungaji wengine ambao ‘hula kondoo’, jihadharini msije mkaliwa nao.” Kupitia usemi huu, kiongozi huyu anatumia kirai kitenzi “hula kondoo” kumaanisha kufanya mapenzi na

washiriki. Ijapokuwa mchungaji hajatumia maneno ya moja kwa moja, ujumbe wake umepitishwa na hali kadhalika uso wa hadhira lengwa umehifadhiwa.

d) Kuzua Utata

Kuzua utata ni mbinu inayovunja kaida ya nne ya Grice ambayo inasisitiza uwazi wa usemi wowote. Hata hivyo, kama tulivyotanguliza katika sura ya kwanza, wakati mwingine msemaji anaweza kuvunja kaida fulani ili kutimiza lengo lake. Kuzuka kwa utata unatokana na usemaji wa jambo kwa njia ambayo jambo hilo huweza kufasiriwa kwa njia nyingi iwezekanavyo. Msikilizaji anaachiwa jukumu la kuutafutia usemi uliotajwa maana iliyokusudiwa. Mathalan, afisa wa idara fulani anaweza kutekeleza mkakati huu kwa kusema, “Nahitaji kushikwa mkono ili nitie sahihi fomu hii.” Kulingana na msemaji, kushikwa mkono ina maana ya kupewa ‘kitu kidogo’. Utata utazuka pale ambapo msikilizaji atafasiri maana tofauti na ile iliyokusudiwa na msemaji.

e) Matumizi ya Maswali ya Balagha

Matumizi ya maswali ya balagha ni kategoria nyingine ya mkakati nje ya rekodi. Mbinu hii hutumika kwa madhumuni ya kuokoa nyuso za wazungumzaji. Maswali hayo hutumiwa wakati msemaji anataka kuisisitiza jambo linalozungumziwa. Mfano, “Ni nani asiyelewa majukumu yake kama mwanamke?” Maswali kama hayo hayahitaji majibu kwa vile tayari msemaji ana majibu. Msemaji anatumia mbinu ya maswali ya balagha kumkinga msikilizaji dhidi ya kutoa majibu au maelezo kuhusiana na kitu fulani ambacho hakifurahishi.

2.4.4.3.5 Mkakati wa Kutosema Ujumbe Unaotishia uso

Tumejadili mikakati minne ambayo hutumika kukabiliana na vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika wa mazungumzo yoyote yale. Hata hivyo, kuna mkakati mwingine ambao unaonekana salama kuliko mikakati yote iliyozungumziwa. Brown na Levinson (1987), wanadai kuwa mkakati wa kutosema kabisa jambo linalotishia nyuso za wazungumzaji ni salama kwa sababu msemaji na msikilizaji hawataathirika kwa vyovyote. Mkakati huu unadai kuwa, iwapo msemaji anafikiria kuwa kile anataka kusema kitaathiri vibaya hisia za msikilizaji, basi hana lingine ila kutosema ujumbe huo. Mfano mzuri ni katika muktadha mbapo msemaji anahitaji chakula kutoka kwa msemazwa lakini anyamaze tu huku akifikiria msikilizaji atampa chakula. Licha ya usalama wa mkakati huu, matumizi yake yanaweza kusababisha kutofaulu kwa msemaji katika kutimiza lengo lake.

Kwa ujumla, wasemaji katika mazungumzo wanaweza kuokoa nyuso za wasikilizaji wao kwa kutumia mkakati wowote kati ya mitano ambayo imejadiliwa. Kwa mfano iwapo mtu anahisi njaa, anaweza kuchagua kutumia moja kati ya mikakati hiyo ifuatavyo:

- i. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi, “Nipe chakula nile.”
- ii. Mkakati chanya wa upole, “Mwandani wangu, nipe chakula nile.”
- iii. Mkakati hasi wa upole, “Nasikitika kukusumbua lakini itawezekana unipe chakula nile?”
- iv. Mkakati nje ya rekodi, “Kutembea kwingi kunamfanya mtu ahisi njaa sana.”
- v. Mkakati wa kutosema kabisa kitendo kinachotishia uso. Hii ina maana kwamba hataomba chakula kabisa.

Ingawa mikakati wa kutosema kabisa ndio una upole kwa kiasi kikubwa na salama kuliko mingine, kuna uwezekano mkubwa wa msemaji kukosa kufanikisha hitaji lake la kupata chakula. Tunafahamu fika kuwa chakula ni muhimu katika maisha ya binadamu na iwapo mtu hatapata chakula atakuwa amekosea mwili wake. Hivyo basi, mtu atalazimika kutumia mikakati minne ya kwanza ili kufanikisha lengo lake la kupata chakula na kwa wakati huo huo atakuwa ameokoa uso wa msikilizaji wake.

Ijapokuwa mitazamo ya upole iliyofafanuliwa na Brown na Levinson (1987) imekosolewa na baadhi ya wataalamu, mitazamo hii imechangia pakubwa katika utafiti wa suala la utafiti huu. Mathalan, Watts na wenzake (2005) na Werkhofer (2005) wanadai kuwa ni kosa kujumlisha kuwa lugha zote zina mikakati sawa ya kukadiria upole. Wataalamu hao wanaendeleza kuwa ujumlishaji huo hufungia nje ukweli kuhusiana na lugha nyingine. Ni kwa msingi huu ndipo tumeamua kujikita katika uchunguzi wa namna washiriki katika vipindi vya *SK* huzingatia au hupuuza kaida za Kanuni Ushirika na mikakati ya upole ili kuhifadhi nyuso zao.

Nadharia ya Upole na kaida za ushirikiano zimetufaa katika kutathmini mikakati ya upole inayotumika katika mazungumzo kwenye vipindi vilivyochunguzwa vya *SK*. Vipindi hivi vinaangazia masuala muhimu ya kijamii kama vile ngono, mapenzi, elimu katika jamii, siasa na ndoa, wakwe, ukosefu wa uaminifu katika ndoa na hata malezi. Masuala hayo yanahitaji kuzungumziwa kwa umakini ili washiriki wasikereke. Tumetumia mikakati ya upole kuchanganulia data iliyokusanywa kutoka kwa vipindi vinane vya *SK* kwa kuchunguza namna ambavyo mazungumzo hayo yanaendeshwa.

2.5 Hitimisho

Sura ya pili, imeonyesha namna wataalamu wengi wametumia Nadharia ya Upole kushughulikia suala la mawasiliano. Katika sehemu ya pili ya sura hii, tumeona namna ambavyo Nadharia ya Upole inaingiliana na Kanuni Ushirika ili kukamilisha mawasiliano. Kauli za watafiti wengi zimeonekana kuchangia utafiti wetu kwa namna moja au nyingine. Hata hivyo, hatukukosa kutofautiana na wengine kutokana na tofauti za lugha au jamii inayotafitiwa au miktadha ya uchunguzi.

Aidha, sura hii imefafanua mitazamo iliyobuniwa na wataalamu tofauti ili kulishughulikia suala la upole. Tumefafanua dhana ya upole kwa misingi ya wanaisimu wengi ambao wameeleza namna ambavyo upole unachukuliwa kulingana na jamii tofautitofauti. Nadharia ya Uso ya Brown na Levinson, Kanuni Ushirika ya Grice, mitazamo ya upole ya Fraser na kanuni za upole za Lakoff na Leech ni mbinu zinazotumika kushughulikia suala la upole katika mazungumzo ya kila siku. Hii ina maana kuwa hakuna nadharia iliyo bora kuliko nyingine isipokuwa mihimili ya nadharia hizo ndiyo hutofautisha miktadha ambamo nadharia hizi hutumika.

Kupitia kwa Nadharia ya Upole hasa mhimili wa ‘kuokoa uso’, imebainika kuwa masuala yanayohusu uso hutofautiana katika tamaduni mbalimbali japo dhana ya uso chanya na hasi hupatikana katika tamaduni zote. Mhimili wa kuokoa uso unafafanua namna ya kukabiliana na vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika wa mazungumzo. Ni kwa msingi huu ndipo mkakati wa kuokoa uso umefafanuliwa zaidi ya mikakati mingine, katika uchanganuzi wa mikakati ya upole, inayotumiwa na wahusika wa mazungumzo ya vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*. Kwa ujumla, sura hii imetuwekea msingi wa jinsi ya kulishughulikia suala la upole katika vipindi vya *SK* kwa kutumia Nadharia ya Upole kama inavyobainika katika sura ya tatu na nne.

Imebainika kuwa utenda kazi wa Nadharia ya Upole umejaribiwa na wanaisimu si haba. Imedhihirika kuwa nadharia hii imetolewa maelezo mengi ambayo yanajaribu kuonyesha ubia wake katika miktadha tofauti. Hata hivyo, wataalamu wanaonekana kukubaliana na kutofautiana kwa mengine. Tofauti hizo zinachangia kufanywa kwa chunguzi nyingi kuhusiana na upole kila uchao na kwa hivyo kuashiria kuwa lengo ni kuboresha nadharia hiyo ya upole. Licha ya tofauti hizo, ni dhahiri kuwa mikakati ya upole katika mazungumzo yoyote yale imeundwa kutokana na misingi ya Nadharia ya Upole.

Nadharia ya Upole imebainika kuwa mbinu tosha ya kuchanganulia mikakati ya upole katika mazungumzo. Sehemu ya mwisho ya sura hii imejadili maelezo na maoni mbalimbali kuhusiana na tafiti zinazohusiana na mada. Mawazo ya wataalamu wengi yamelinganishwa na hivyo kupata msingi wa utafiti wetu. Mawazo hayo yamekuwa msingi wa kuchanganua mikakati ya upole inayotumika katika mazungumzo ya *SK* kama inavyodhihirika katika sura inayofuata.

SURA YA TATU

MIKAKATI YA UPOLE KATIKA VIPINDI VYA *SOBETAB KAPCHI*

3.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data kuhusu mikakati ya upole inayotumika katika vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*. Ni uchanganuzi wa diskosi zinazohusiana na mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi, mkakati nje ya rekodi na mkakati ndani ya rekodi katika vipindi husika. Tumechunguza namna ambavyo wahusika wa mazungumzo katika vipindi vya *SK* wanakabiliana na vitisho kwa nyuso zao. Tumeorodhesha mbinu hizo na kuzifafanua kwa kutumia mifano ya kauli za washiriki wa mazungumzo hayo.

3.1 Upole Chanya Katika Vipindi vya *SK*

Mkakati wa upole chanya hulenga kudumisha uso chanya wa msikilizaji kwa kuepuka kufanya au kusema habari zinazoweza kumuudhi msikilizaji au kuhasiri uso wake chanya. Vilevile, mkakati huu kwa mapana hulenga kuusifu na kuufurahisha uso chanya wa msikilizaji kabla ya kufanya vitendo vya kiusemi. Jukumu kuu la mzungumzaji huwa ni kumtukuzi, kumheshimu na kumrai msikilizaji kiasi cha yeye kuhisi kuwa wa maana na thamani kubwa. Kadhalika, kupitia matumizi ya mkakati wa upole chanya, mzungumzaji hulenga kuibua, kukuza na kuyapalilia mazingira ambayo yanadumisha mahusiano baina ya washiriki wa mazungumzo, hivyo hutawaliwa na utoaji mwingi wa miadi chanya.

Mkakati huu hukubaliana na mawazo ya Lakoff (1973) kuwa jukumu kuu la washiriki katika mchakato mzima wa mawasiliano ni kudumisha mazingira ya uwiano. Washiriki hao hufanya hivyo kwa kujaribu kuepuka hali zinazoweza kuyavunja

mawasiliano. Madai hayo yanaashiria kwamba kudumisha mawasiliano ni muhimu kuliko kuzingatia upole. Hata hivyo, Lakoff (1973) anakubaliana na mawazo ya waasisi wa nadharia ya upole katika utoaji wa miadi chanya.

Mkakati huu hujaribu kupunguza umbali baina ya wahusika wa mazungumzo kwa kuzingatia ukuruba na hamu thabiti ya msikilizaji ya kutaka kuheshimiwa. Brown na Levinson (1987) wanadai kuwa mkakati wa upole chanya ni hulka ya kawaida miongoni mwa marafiki na watu wengine ambao wana uhusiano wa karibu. Wao wanapendekeza mbinu kumi na tano za upole chanya ambazo zinaweza kutumika kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji. Mjadala unaofuata unaonyesha namna ambavyo kategoria mbalimbali za mkakati chanya wa upole zimejitokeza katika mazungumzo ya vipindi teule. Ili kutoa taswira kamili ya jinsi mkakati huu ulivyotumika, tumetoa mifano mbalimbali inayothibitisha mbinu hizo za upole chanya.

Kutokana na data ya utafiti, ni bayana kuwa matumizi ya mkakati wa upole chanya yapo kwa wingi. Matumizi ya mbinu za upole yanaonyesha kuwa msemaji anashirikiana na msikilizaji na kwamba wote wana matarajio sawa ya kuelewana. Mkakati wa upole chanya una mawanda mapana kuliko upole hasi. Huku mkakati hasi wa upole ukitumiwa kwa uangalifu sana ili kupunguza tishio la uso kwa msikilizaji, mkakati chanya unaweza kutumika kwa namna huru katika mazungumzo. Hapa tunajadili kwa mifano mahsusni kategoria mbalimbali zinazotumiwa na wahusika wa mazungumzo ya *SK* kutekeleza mkakati wa upole chanya.

3.1.1 Kuepuka Kutokubaliana

Ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji, mkakati wa kuepuka kutokubaliana unamhitaji msemaji aepukane na kutokubaliana na msikilizaji. Hii ni kwa kutoa usemi ambao

unaonyesha makubaliano kati yao ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji. Mbinu hii inadhihirika katika vipindi vya *SK* kufuatia mifano ifuatayo inayothibitisha madai hayo.

Katika kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwanamume kuoia mke mwingine), ‘Pasta’ Rotich ambaye ni mwasilishaji mkuu katika vipindi vya *SK*, anajadili sababu za mwanamume kuoia mke mwingine. Anasema kuwa kwa kawaida, jamii hutarajia kupata watoto baada ya ndoa. Anakubaliana na ukweli kuwa watoto huleta furaha ndani ya nyumba. Hata hivyo, anaonyesha msimamo wake kwamba kuoia mke mwingine si suluhisho lakini hilo analisema baada ya kukubaliana na wazo kuwa bila watoto furaha katika ndoa haitakuwa kamili. Anasema:

Kal.

1. *Angen iman ale boiboiyet ne isuldaat lagok eng kapchi, ipkobate ma lazima kitun kwondo nebo aeng si koboiboitu biik amu biitu toiyeet kora.*

Kis.

Ninaelewa kuwa watoto hukamilisha furaha ya wanandoa, isipokuwa, si lazima kuoia mke wa pili kwani kufanya hivyo kutazua utengano.

Usemi wa Rotich unaonyesha makubaliano kati yake na wasikilizaji wa kipindi lakini mwishowe anaonya kuwa kuongeza mke mwingine si hakikisho kuwa kutakuwa na raha kamili. Matumizi ya maneno *angen iman ale* (ninaelewa kuwa) yanaonyesha makubaliano kati ya msemaji na msikilizaji. Kuepuka kutokubaliana ni mbinu inayohakikisha kuwa kuna maelewano na makubaliano kati ya wazungumzaji.

Kwenye kipindi cha *Tilyandit eng katunisiet* (Uhusiano katika ndoa), Rotich anatumza uso chanya wa msikilizaji wake Winny kwa kukubaliana naye kuwa baba ana majukumu ya kuwatunza na kuwapenda watu wa familia yake. Hata hivyo, ‘Pasta’

anaonyesha kuwa kuna kiwango cha kufanya mambo hayo. Anaonyesha mipaka ya mahusiano kati ya baba na bintiye kwa kusema:

Kal.

2. *Ayani ale kwandanyi iman ak konyolu kosigegei tilyandit ne kararan lakini, nyolu kora komi korogendoetab tilyandit amu mi tuguk alage che manyolu kogeer baba.*

Kis.

Ninakubaliana nawe kuwa ndiye babake, na pia kwamba wanatakiwa kuwa na uhusiano wa karibu, lakini pia, kuna mipaka ya uhusiano kwani kuna vingine baba hatakiwi kuviona kwa bintiye.

Kupitia kwa mfano huo, mwasilishaji huyu wa vipindi vya *SK* anaonyesha msimamo kuwa baba na bintiye hawatakiwi kuwa na mahusiano yanayovunja heshima. Lakini kabla ya hayo, anatumia kirai *ayani ale* (ninakubaliana nawe kuwa) kuonyesha makubaliano kati yake na Winny. Kukubali huko ni kuepuka kutokubaliana na wasikilizaji kuhusiana na majukumu ya kina baba katika kukuza uhusiano kati yao na binti zao.

Mfano mwingine wa kudhihirisha hali ya kuepuka kutokubaliana unapatikana katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa). Winny anawasihi wasikilizaji wa kiume waache kuwahusisha watu wa jamii zao kama vile wazazi na ndugu mambo yao ya familia. Winny anafanya hivyo lakini kwa kutumia usemi wenye makubaliano ili kuokoa uso wa hadhira yake kwa kusema:

Kal.

3. *Ayani iman iman ale sigiguk ak tupchosieguk bichoto, ipkobate magat otebegei murenik ole ii, tos ndawendi lakwanobochi kotos muitaenen bichoto betusiek tugul ii? Mi tilyanditab korotik iman **agomatiyotosi notok**, ago tinyei rerunet tilyandinoto amu mwaei Baibol kole bagaktoi chi kwanda ak kamet ak kotuiyogei ak osotiondenyi ak koek borto agenge. Kateeb ale ii pasta, kilya simetun murenik chepkametisikwak anan kotebiso eng gaa ametunis?*

Kis.

Kwa kweli kabisa ninakubaliana nawe kuwa wao ni wazazi na nduguzo isipokuwa wanaume mnapaswa kujiuliza kuwa, je huyo binti wa watu akiondoka, hao jamaa zako watakuvumilia siku zote? Kuna uhusiano wa damu **na hilo silipingi** lakini uhusiano huo una upungufu kwa sababu Biblia inasema kuwa mtu atawaacha wazazi wake na kuunganika na mkewe na kuwa mwili mmoja.

Usemi huo wa Winny una msimamo mkali dhidi ya wanaume lakini kwa kutaka maelewano nao, Winny anatumia maneno ambayo yanaonyesha hali ya kuepuka kutokubaliana. Virai *ayani iman* (kwa kweli kabisa ninakubaliana nawe) na *ago matiyosi notok* (na hilo silipingi) vinadhahirisha hali ya kuepuka kutokubaliana. Mbinu hii humwezesha msemaji kupitisha ujumbe ambao labda ungesemwa moja kwa moja bila kutanguliza sehemu ya makubaliano, ungekuwa tishio kwa uso wa msikilizaji.

3.1.2 Kutumia Utambulisho wa Usonde Jamii

Kulingana na Brown na Levinson (1987), juhudi za kuokoa uso chanya wa msikilizaji ni pamoja na mbinu ya kutumia majina ya makundi ya kijamii au kuwatambua wasikilizaji kwa njia ya jumla. Huu ni mkakati unaotumia uning'inizaji wa kauli. Majina yanayotumiwa kuashiria wasikilizaji ujumla wa wasikilizaji ni kama vile 'mpendwa', 'mwenzangu', 'profesa', 'mwalimu', 'daktari', 'mpenzi'. Dhima yamajina haya ni kupunguza makali ya vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji. Mbinu hii imedhihirika katika vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM* katika mifano ifuatayo:

Katika kipindi *Tuguk che butei katunisiet* (Sababu za kuvunjika kwa ndoa), Rotich anajibu swali la shabiki 'A' aliyeuliza iwapo wanawake husema shida zao kwa marafiki ili wasipatwe na msongo wa mawazo. Anasema:

Kal.

4. *Kass amwaun anyun **chebeiyo**, imuch ing'et kotakokaitit mising ak imustaate kila ilen icheng'e toretet kobun biik ako mengen ile kelityigei kipchabet.*

Kis.

Sikiliza nikwambie **dadangu**, unaweza kurauka mapema kama kungali na baridi, ukazunguka ukidhani unatafuta msaada bila kujua unajinolea mshale.

Kupitia kwa usemi huu, 'Pasta' anatumia jina la kijamii *chebeiyo* lililo na maana ya 'dadangu' kuonyesha uhusiano kati yake na msikilizaji husika. Ijapokuwa 'Pasta' anatoftiana naye kimawazo, anatumia neno hilo kupunguza makali ya kumweleza msikilizaji kuwa kuwaambia marafiki shida zako ni kujichimbia kaburi. Anamshauri msikilizaji kwa kutumia maneno sawa na methali 'kikulacho ki nguoni mwako' kwani siri si siri tena ajuapo mwingine.

Iwapo 'Pasta' Rotich angemwambia msikilizaji moja kwa moja kuwa hakuna suluhisho kwa kueneza shida zake, msikilizaji angeaibika na hilo lingekuwa tisho kwa uso chanya wake. Anapotumia neno *chebeiyo* (dadangu), msikilizaji anahisi kuwa amethaminiwa na msemaji kama mtu wa karibu. Jina hilo linaweza kutumika kumaanisha dadake msemaji au jina la heshima kwa kina dada.

Mfano mwingine wa utambulisho wa kimakundi unapatikana katika kipindi hicho cha *Tuguk che butei katunisiet* (Sababu za kuvunjika kwa ndoa). Mwasilishaji wa vipindi anaeleza kuwa wanaume wengine hutoroka nyumbani wanapokosa kulakiwa mlangoni na wake zao. Rotich anaonyesha majukumu ya mwanamke yakiwemo yale ya kuhakikisha kuwa mumewe anafurahia anachotendewa naye. Winny anaonekana kukerwa na jambo hilo na anamwuliza Rotich iwapo mume naye atampokea mkewe ajapo nyumbani akiwa amechelewa. Kwa kumjibu, Rotich anasema:

Kal.

5. *Ngalen ingen o chepkametinyu ile sikotonon ko ko kwony. Achi inye kou ole maktoi amemage kiy ngotaachin ana ko mataachin.*

Kis.

Dadangu, nina uhakika ya kwamba unaelewa kuwa nyumba huimarika kutokana na bidii ya mwanamke. Mtendee tu atakavyo na usijali iwapo atakupokea au la.

Ili kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji, Rotich hakutoa jibu lake moja kwa moja kuonyesha majukumu ya mwanamke aliyeolewa. Anatumia neno *chepkametinyu* (dadangu), ambacho ni kisawe cha *chebeiyo* (dadangu) kupunguza makali ya usemi wake. Neno hilo ni la heshima kwa kina dada. Hata hivyo, matumizi ya maneno ya utambulisho wa kimakundi hayapunguzi maana iliyokusudiwa. Ni njia ya kuepuka ulazimishaji wa mambo kwa msikilizaji.

3.1.3 Kuchopeka na Kurefusha Irabu [i] Mwishoni mwa Vitenzi amrifu

Kuchopeka na kurefusha irabu [i] mwishoni mwa vitenzi ni mkakati unaotumiwa na jamii za Kikalenjin ili kutomwamrisha msikilizaji kufanya jambo. Kupitia mbinu hii, msemaji anabadilisha sentensi amrifu kuwa rai. Kwa mfano katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Sababu za kuvunjika kwa ndoa), Winny anatofautiana na wazo la ‘Pasta’ kuhusu kudekezwa kwa wanaume kwa kuuliza:

Kal.

6. *Kaswoii ‘Pasta’, dunia ne kimi raini ko ng’wondet ne bo ‘scratch my back I scratch yours’ imugaksei iman iyachini chito tuguk che mayauini? Ingeleis a binadamu ak amache kechaman agane.*

Kis.

Nakuomba unisikilize ‘Pasta’, dunia ya leo ni ya nipe nikupe, itawezekana kweli umtendee mtu asivyokutendea? Unajua, mimi pia ni binadamu na ninataka kupendwa.

Kutokana na usemi huo, tunapata kuwa Winny halazimishi usikivu kutoka kwa Rotich bali anamrai amsikilize. Hili analifanya kupitia kwa matumizi ya neno *kaswoii* (nisikilize). Mzizi wa neno ni *kas* na *wo* ni kiambishi cha mtendewa katika nafsi ya kwanza umoja. Kitenzi *kaswo ni* amrifu. Ni sawa na ‘nisikilize!’. Irabu /i/ inapoongezwa na kurefushwa mwishoni mwa kitenzi *kaswo*, neno hilo linakuwa *kaswoii*. Hatua hiyo inabadilisha kitenzi hicho kutoka kwa hali yake ya kuamrisha na kuwa katika hali ya kurai. Matumizi ya mbinu hii yanamfanya msemaji kuepuka hali ya kumlazimisha Rotich kumsikiliza na hivyo ni kupunguza makali ya vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji.

Kwa kumjibu mwelekezi wa vipindi, Rotich pia anatumia mbinu hiyo ya uchopekaji na urefushaji wa irabu [i] mwishoni mwa kitenzi. Kwa kutumia swali la balagha anasema:

Kal.

7. *Ng’etii Winny, aguitosin ye kemwa ile ‘tit for tat’ ipkobate tos ng’o yekai ne mengen kole kiyai Jehovah muren ak tie ak kogochi age tugul boisionik che terchin! Kigilenji muren cham, kelenji kwony kas it, noto koboru kole magat igas it yaani, iyachi tuguk che mochei.*

Kis.

Winny, **fanya hivi**, nakuelewa unaposema nipe nikupe lakini je, ni nani asiyejua kuwa Mungu aliwaumba mume na mke na kuwapa majukumu yanayotofautiana! Mwanamume aliambiwa apende na mwanamke anahitajika kutii, na huko kutii ni kumfanyia mumewe atakavyo.

Usemi huo wa Rotich, kwa kuongeza na kurefusha irabu [i] mwishoni mwa kitenzi *ng’eeet* (fanya hivi!) ili kiwe *ng’etii*, unapunguza uamrishaji na kuzua urai. Kwa kufanya hivyo, mwasilishaji mkuu wa kipindi anatumia uso chanya wa msikilizaji ili kuwe na maelewano na uhusiano mzuri utakaoweza vipindi kuendelea.

3.1.4 Kumtambua Msikilizaji

Waasisi wa kipengele cha uso katika Nadharia ya Upole Brown na Levinson (1987), wanapendekeza kwamba mkakati huu unamhitaji msemaji kutambua hali za msikilizaji kama vile umiliki wa vitu fulani muhimu, mabadiliko yanayoonekana wazi, wadhifa alionao na chochote anachohisi kuwa msikilizaji anathamini na anataka kitambuliwe. Hali hii humfanya msemazwa kuhisi kuwa ametambuliwa na kushughulikiwa ipasavyo.

Kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka), kinadhihirisha mkakati huu wa kumtambua na kumshughulikia msikilizaji. Kupitia kipindi hiki, Winny anashughulikia uso chanya wa mwasilishaji mkuu kwa kutambua tajriba yake katika mambo yanayohusiana na ndoa. Anatambua wadhifa wa Rotich katika ushauri na pia ukomavu wake wa muda mrefu katika mambo ya ndoa kwa kuuliza:

Kal.

8. *‘Pasta’, ngakerin ko kiib kasarta ne koi iweny ak ing’alale ngalek che tinyegei ak sobetab kapchi, ngigeer inye ko tos torei biik kenyisiek olobo ata si kosirgei ak komach kobet lol?*

Kis.

‘Pasta’, ninaona kuwa umechukua muda mrefu kufanya uchunguzi na kuzungumzia mambo yanayohusu ndoa. Je, kwa mtazamo wako, unakadiria kuwa watu huishi kwa miaka mingapi kabla ya kukosana na kutaka kutalikiana?

Winny anaonekana kumshughulikia msemazwa kwa kutambua tajriba yake katika kazi ya ushauri kwa wanandoa. Kwa kumlimbikizia sifa za ukomavu katika kazi na kumwita ‘Pasta’ Winny anamshughulikia msikilizaji wake ambaye ni Rotich kwa wakati huo.

Mfano mwingine unaoweka bayana mkakati wa kumtambua na kumshughulikia msikilizaji ni katika kipindi cha *Amu nee che aei mren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwanamume kuo a mke mwingine). ‘Pasta’ anajaribu awezavyo kuwatambua na kuwashughulikia wasikilizaji wote wa kiume kwa kuwatambua kihadhi katika jamii za Kiafrika na hasa za Kikalenjin. Anaonyesha kuwa si rahisi kwa wanaume wa Kiafrika kuwaonyesha wake zao mapenzi kwa njia wazi. Anasema kuwa wao hawana mazoea ya kuomba msamaha wanapowakosea wake zao. ‘Pasta’ anasema:

Kal.

9. *Asome kwonyikyok chebo Afrika, chebo Kenya, chebo Rift Valley, ago mising ko chebo Kalenjin si koyan manong’otoikwak kou ole u, amu manaita ichek tugun che tounen kou kesom kwony nyoetabkaat ak ketaach eng’ gaa.*

Kis.

Nawasihi wake zetu wa Kiafrika, wale wa Kenya, wale wa Bonde la Ufa na zaidi ni wale wa jamii ya Kalenjin ili wawakubali waume zao jinsi walivyo kwa sababu waume hao **hawana mazoea ya tabia za kigeni** kama vile kuomba msamaha na kuwalaki wake zao nyumbani.

Utambuzi huu ni namna ya kuwaonyesha wanawake wasitarajie mengi zaidi kutoka kwa waume zao. Ni njia ya kuwahamasisha wasitarajie makuu ambayo yanatokana na hisia zao. Kupitia kwa utambulisho huo, ‘Pasta’ anawashughulikia wanaume Wakalenjin kuwa hawana mazoea ya mambo mengine ambayo ni mageni.

Katika mazungumzo hayo, ‘Pasta’ anatoa mfano wa kasisi aliyefumaniwa ‘akila kondoo’ wake ambaye ni mke wa mshiriki wake. ‘Pasta’ anasema kuwa hata baada ya kufumaniwa na mkewe, hakuchukua hatua ya kuomba msamaha. Mume huyo aliongozwa na chukulizi kuwa mkewe amemwelewa na kumsamehe. ‘Pasta’ anaeleza:

Kal.

10. *Kiib manong'otiondonoto koek kawaida kobek ngalechoto amu muren inendet. Moib kobogorisiek ole tinyei yoitio age tugul boisiek ipkobate atebenwa noto.*

Kis.

Mwanamume huyo alichukulia kuwa ni kawaida kwa mambo hayo kuisha bila yeye kuomba msamaha kwani yeye ni mwanamume. Nawaomba wanawake **msichukulie kuwa wana ubaya wowote** bali ni hali yao.

Usemi wa mwasilishi wa kipindi unawatambua wanaume wa Kiafrika kuwa wenye uwezo na ambao wanataka wakubalike walivyo. Utambuzi huo unashughulikia nyuso za wanaume kwa sababu wao watajua kuwa wanaeleweka na wanawake ambao watachukulia kuwa ni kawaida ya wanaume wote.

3.1.5 Kutumia Ucheshi

Matumizi ya ucheshi ni namna nyingine ya kuokoa uso chanya wa msikilizaji. Ucheshi huu unatokana na maarifa asilia na tabia zinazojulikana. Ucheshi hutumiwa kutilia mkazo usuli wa kitu au mtu. Mbinu hii katika kundi la mkakati chanya wa upole hutumiwa ili kumfanya msikilizaji achukulie mambo kwa wepesi. Ucheshi humfanya msikilizaji kurahisisha mambo yanayoonekana kuwa magumu. Ucheshi hutumiwa kama mbinu ya kupunguza vitisho kwa nyuso chanya za wahusika wa mazungumzo hasa msikilizaji. Katika vipindi vya *SK*, ucheshi unadhihirika kupitia mifano ifuatayo:

Kwenye kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwamume kuoia mke mwingine), Winny anaonekana kutofautiana kidogo na mwasilishaji mkuu wa kipindi. Mwasilishaji huyu anaposisitiza kuwa hata waume wanaobugia mvinyo na kutapika malazini wapendwe na kushughulikiwa,

mwelekezi anapinga kwa madai kuwa mama na baba ni watu wazima na wote wanafaa kuwa na hadhi sawa. Anatetea kuwa kufanya hivyo (kuwashughulikia wanaotumia mvinyo) ni kuwanyanyasa wanawake na kuwachukulia kama vyombo vinavyotumiwa na wanaume kujifurahisha.

Kwa kumjibu ‘Koriryo’, ‘Pasta’ anatumia ucheshi kupunguza makali ya vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji wake kwa kudokeza:

Kal.

11. *Winny, mamwa ale mamagat keachi kobogorio tuguk che kiachin muren, kobate chang’ murenik che mengeni kole tinyei ‘haki’ kobogorisiek keachi kou notok. Angen ale ngamwa kou notok kolen murenik che chang’ kikegono kwolilo lakini **angen ale tako aititaat.***

Kis.

Winny, mimi sijasema kuwa wanawake hawafai kutendewa kama wanaume, isipokuwa wanaume wengi hawajui kuwa wanawake wana haki ya kufanyiwa kama wao. Ninajua fika kuwa wanaume watasema ‘nimetulizwa’ lakini **ninajua ningali timamu.**

Kwa kusema *angen ale ta ko aititaat* (ninajua ningali timamu), wasikilizaji hawachukulii usemi huo kuwa na uzito bali wanaona kuwa ni mzaha tu. Hiyo ni hali ya kutoa kauli lakini kwa namna ya kimchezo ili kuepuka vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji. Mbinu hii ya mkakati wa upole chanya katika kuokoa uso, inachukua sehemu kubwa katika mazungumzo ya vipindi vya *SK*. Wahusika wa mazungumzo hayo wamekuwa makini sana ili kutunza nyuso zao na za wenzao kupitia kwa kutumia kauli ambazo zinaonyesha ucheshi ili kutekelezewa jambo.

3.1.6 Kutafuta Makubaliano

Wataalamu Brown na Levinson (1987), wanadai kuwa kutafuta makubaliano ni kategoria ya upole chanya ambayo hutumiwa kutosheleza tamani la msikilizaji la

kutaka kukubalika katika maoni yake. Wataalamu hao wanasema kuwa mbinu hii hutekelezwa kupitia msemaji kuzungumzia mada kubalifu kwa msemazwa. Ili kutimiza hayo, ni lazima msemaji awe anajua mengi kumhusu mhusika. Labda msemaji anajua anachopenda au kuchukia msikilizaji. Kumjua msikilizaji kunaimarisha uhusiano kati yake na msemaji.

Mkakati huu aidha huhusisha uepukaji wa kauli na mielekeo ambayo inadhihirisha kupinga msikilizaji au kupinga kauli zake. Uepukaji huu unamfanya msikilizaji ahisi kuwa anathaminiwa au anakubalika. Pia, mkakati huu huhusisha kukubaliana na msemaji katika mapendekezo yake na iwapo msikilizaji atayakataa afanye hivyo kwa njia inayodhihirisha sababu ya kukataa kutekeleza pendekezo lake. Hapa, msikilizaji huepuka kumpinga msemaji kwa njia ya moja kwa moja hasa kwa kuonyesha sababu ya kutowezezana kwa jambo lakini kwa namna ya kukubali kwanza.

Mbinu ya kutafuta makubaliano kati ya msikilizaji na msemaji inadhihirika kupitia kipindi cha *Kolokseet eng' katunisiet* (Mavazi katika ndoa). Mara nyingi, 'Pasta' anatoa kauli za makubaliano kabla ya kuonyesha msimamo wake ili kuwashughulikia wasikilizaji wake. Yeye anakubaliana na mwelekezi wake Winny kuwa watu hutofautiana kimawazo kwa kufafanua:

Kal.

12. *Terjin biik eng kataguret ak kolokseet, ago matiyosi notok. Iman chamei alage kolochi ngoroik che koen kochamei alage che nwagen mising. Tiegei noto Sobetab chi kong'ete mining'atenyi agoi etunatenyi ak etanutikab kaniset ne ilosune Kamuktaindet. Mie konaak nito kele ma lazima okergeitu ak biik alak eng' kiy tugul amu mi tugul alage che magat irarchigei.*

Kis.

Watu hutofautiana katika starehe na jinsi ya kuvaa **na hilo sipingi**. Wengine hupenda mavazi marefu na wengine hupenda mafupi sana. Hali hiyo hutegemea jinsi mtu alilelewa na pia maadili ya dini

anayomwabudia Bwana. Ni vizuri kujua kuwa si lazima ufanane na wenzako kwa kila hali kwani kuna mengine ya kujiamulia.

Katika mfano wa 12, ‘Pasta’ anaonekana kukubaliana na Winny ijapokuwa ana msimamo tofauti kidogo. Kwa kufanya hivyo, anadumisha uso hasi wa msikilizaji wake na kuepuka kutokubaliana naye. Ni dhahiri kuwa mwasilishaji wa vipindi anawaelewa wasikilizaji wake na anataka kudumisha uhusiano kati yake na wao ili kufanikisha mada katika vipindi teule vya *SK*.

Mfano mwingine wa kutafuta makubaliano upo kwenye kipindi cha *Suupsetab tibik ak kwonyik* (Ubakaji wa wanawake). Winny anamwelekeza mwasilishaji mkuu kuwa, watu wamebadilika kitabia na kimaadili na hivyo kuona dhambi kama kawaida. Anaeleza kuwa unyama umechukua nafasi ya ubinadamu na hali hiyo imesababisha watu kuwabaka watoto wao. Kwa kukubaliana na Winny, ‘Pasta’ anasema:

Kal.

13. *Unotok as Winny, kikotebi biik kou che makobwotitoi, kaigai agot tyong’ik cho kemwa. Tiong’ik kotinyei kasarta ne inegei ne ituitoskei, melen aei tuguk che aei kimugulmet ago notok amu nee si ngap ikase kelen mochei kirgit teta. Yaach biik iman Winny nga matugul.*

Kis.

Ni hivyo sasa Winny, watu wameishi kana kwamba hawafikirii tena, heri hata wanyama ambao umewataja. Wanyama wana muda mwafaka wa kukutanika kwa mfano: kuna wakati ambapo ng’ombe husemekana kuhitaji ndume. Wanyama hawafanyi kama vile ambavyo binadamu hufanya. Winny, japokuwa si wote, kusema kweli watu ni wabaya.

Kauli ya ‘Pasta’ inaonyesha makubaliano kati yake na msemazwa wake. Mbinu hii haimaanishi kuwa anayekubaliana na mwenzake hawezi kuonyesha msimamo wake. Katika sehemu ya kwanza ya usemi, msemaji anatumia maneno ambayo yanadhihirisha makubaliano na msikilizaji. Sehemu ya pili ya usemi inadhihirisha msimamo wa msemaji. Kwa mfano Rotich anapotumia neno ‘japokuwa’ anaonyesha

kuwa ana msimamo mwingine licha ya kukubaliana na msikilizaji kwa mambo mengine. Mbinu hii inatumika kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji.

Kwenye kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), tunapata dhihirisho lingine la mbinu ya makubaliano kati ya wahusika wa mazungumzo. Mjadala unazungumzia uchafu kama sababu mojawapo ya kuvunjika kwa ndoa. Winny anaungwa mkono na shabiki 'B' kupitia ujumbe unaosema:

Kal.

14. *Kemwa iman anyun 'Koriryo', magat kotililit kwony siko-chamak gaa. Ngot ko mekilgei kwony eng komostab tililindo koonei manong'otiony komanda sang. Ingen nee Koriryo, machamei murenik ole matilil, mweei kabisa agot nteripte ano eng' lainwek alak.*

Kis.

'Koriryo', hapo umesema kweli, mwanamke anatakiwa kuwa safi ili avutie nyumbani. Iwapo mwanamke hatajimudu katika hali ya usafi, mumewe atatorokea nje. Unajua wanaume hawapendi pahali pachafu, hivyo usipochukulia maanani atatoroka licha ya kujibidiisha kumtunza kwa hali zozote zingine.

Usemi huu wa shabiki 'B' *kemwa iman anyun 'Koriryo'* ('Koriryo', umesema kweli) unaonyesha makubaliano kati ya msemaji na msikilizaji. Japo 'B' anasisitiza usafi wa mwanamke pekee, anafanya hivyo baada ya kuonyesha makubaliano ambayo ni muhimu ili kuhifadhi nyuso za wahusika wanawake katika mazungumzo.

3.1.7 Kuwa Mrajua

Vipindi vya *SK* vimetumia mkakati wa urajua kwa wingi. Urajua ni hali ya kutarajia mazuri kutoka kwa mwenzako. Kauli zinazoonyesha urajua hupunguza viwango vya vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji. Kauli hizo huonyesha kuwa vitendo ambavyo vimetajwa si muhimu na huweza kupuuzwa kwa makubaliano ya msemaji na msikilizaji (Brown na Levinson, 1987). Upunguzaji wa vitendo hivyo huweza

kufanyika kupitia kwa kauli kama vile ‘kiasi’, ‘kidogo’, ‘chache’, ‘sekunde moja’ na ‘muda mfupi’. Katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), ‘Pasta’ anamrai Winny ampe nafasi amweleze anavyofikiria kuhusiana na swali alilouliza Winny kuhusu kile kinachosababisha watu kuwa na ‘mpango wa kando’. ‘Pasta’ anasema:

Kal.

15. *Kaswo kitigin oh Winny, kitigin kityo, mie konaak nito missing kele meyanat koombenot chi age tugul ne kigitun anan ko ne kigotunis. Chang biik che ibwotyin kole maya ko kamanda sang mureno, achicha! Maiman notok. Angen ale iyanwo nito, magatkoripkei chitugul amu kipsengwet kogerei biik tugul kogergeit ago ma kou muren anan ko kwony.*

Kis.

Winny nisikilize **kidogo, kidogo tu**, ni vizuri jambo hili lijulikane kwa kila mtu kwamba, yeyote aliyeoa na kuolewa hahitajiki kutangatanga. Wengi wanaamini kuwa si vibaya kwa mwanamume kutoka nje ya ndoa, la, si hivyo. Ninajua utakubaliana nami kwa hili kuwa, kila mmoja anatakiwa kujichunga kwa sababu mbingu inawatazama binadamu kwa usawa lakini si kwa mtazamo wa kijinsia.

Kupitia kwa mfano huo, Rotich anamrai Winny ampe nafasi kidogo ya kumwelezea kuhusu mpango wa kando, Rotich anatumia virai *kitigin, kitigin kityo* (kidogo, kidogo sana) na *angen ale iyanwo nito* (ninajua kuwa utakubaliana nami kwa hili) kudhihirisha urajua wake. Rotich anatarajia kuwa msikilizaji wake atakubaliana naye katika jambo hilo analozungumzia na pia kumrai amsikize kwa kutumia maneno yanayoonyesha anahitaji wakati mfupi sana.

Aidha, katika kipindi hicho cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa) msikilizaji ‘C’ kutoka sehemu za Chepyakwai katika kata ya Ngeria kaunti ya Uasin Gishu, anachangia mada lakini anatuma ujumbe mrefu unaochukua muda mwingi sana kusomwa. Rotich anawaambia mashabiki kuwa waandike jumbe fupi fupi na

zenye mada moja kila mmoja ili kuokoa wakati. Akisoma ujumbe huo, Winny anamrai ‘Pasta’ akisema kuwa bado ana jambo ndogo la kusoma lakini ananua kutumia muda mfupi sana kwa kusema:

Kal.

16. ‘Pasta’, asome *dakikaiyat agenge kityo asoman ng’olyo ne agase ale bo kamanut ne kasir kastoindoni, angen ale kaichamwo...*

Kis.

Pasta’, naomba **dakika moja tu** nisome jambo moja ninalofikiria kuwa la muhimu ambalo msikilizaji huyu ameandika, **najua umeniruhusu.**

Maneno *angen ale kaichamwo* (najua umeniruhusu) pamoja na *asome dakikaiyat agenge kityo* (naomba dakika moja tu) yanaonyesha urajua. Msikilizaji ‘K’ anatarajia mazuri kutoka kwa mwasilishaji wa kipindi kwamba atamsikiliza na kutendewa anavyohitaji. Ni vigumu kwa msikilizaji kukataa kumtimizia msemaji kitendo anachohitaji kwa sababu ya urajua wa msemaji.

3.1.8 Kujitambulisha na Kundi Moja na Msemezwa

Ili kutekeleza mkakati chanya wa upole, Brown na Levinson wanapendekeza kuwa msemaji anaweza kutumia kauli za ujumuishaji. Ni bayana kuwa katika mazungumzo yoyote watu hutumia vitenzi vya nafsi za kwanza, pili na tatu. Nafsi ya kwanza wingi inatumia kiambishi ‘tu’ ambacho kinamjumuisha msemaji pamoja na hadhira yake. Matumizi ya kauli za ujumuishaji ni namna ya kuonyesha ushirikiano kati ya msemaji na msemezwa. Ni njia ya kuonyesha kuwa wote wana msimamo mmoja na hivyo kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji. Ifuatayo ni mifano ya mkakati huu kutoka kwa mada tofautitofauti kama ilivyodhihirika katika vipindi vya *SK*:

Kwenye kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), Rotich anatoa ushauri kwa wasikilizaji wote kuwa mpango wa kando unasababisha magonjwa ya zinaa au virusi vya UKIMWI kwa wahusika. Anafanya hivyo kwa uangalifu sana ili asionekane kunyosha kidole kwa wasikilizaji. Kwa mfano anaposema:

Kal.

17. *Kingen **achek tugul** kele ye kakoit borto noto matinyei kerichoo komugaksei kwalda chito tuguk tugul che katabo lagok si keribe inendet. **Biik tugul** kongen kora kole ye kagobek tuguk ak kwo chichotok kong'etu lagok ko kibananok che bonon.*

Kis.

Sote tunajua kuwa ugonjwa huo unapozuka, mtu anaweza kuuza mali ambayo watoto wangerithi kwa ajili ya matibabu. **Watu wote** wanafahamu pia kuwa mali yakiisha na aage dunia, watoto watabaki mayatima, tena maskini.

Rotich anatumia maneno *achek tugul* (sote) na *biik tugul* (watu wote) inayoonyesha ujumuishaji wa wahusika wote wa mazungumzo. Mkakati huu wa kujumuisha msikilizaji katika kundi moja na msemaji unafaa muktadha huu kwa sababu msikilizaji anajiona kuthaminiwa na kukubalika kwenye kundi la msemaji. Matumizi ya maneno yanayomtenga msemaji na kundi lake (la msemaji), hupelekea msikilizaji kuhisi kuwa hakubaliki. Mwari (2014) anasema kuwa msikilizaji atahisi vizuri iwapo msemaji atamtambua kuwa yeye ni mwanakikundi. Machira (2015) anamuunga mkono Mwari kwa kusema kuwa makundi haya yanaweza kuwa na uhusiano katika misingi ya umri, jinsia, siasa, jamii, utamaduni au matabaka. Majina ya sifa yanayoenda na utambulisho wa kimakundi ni pamoja na: Rafiki yangu/yetu, mwenzangu, mwanachama mwenzangu, ndugu yangu, mwenzetu, kaka yetu, dada yetu, baba yetu miongoni mwa majina mengine.

Kwa kumaliza maelezo kuhusu UKIMWI na mpango wa kando katika ndoa, mwelekezi wa kipindi, Winny, anamjumuisha mwasilishaji mkuu katika usemi wake kwa kusema,

Kal.

18. *Kitinye kamang'unet kele kakonyoor boroindo kastoikyok che chang' nga makimuch ...*

Kis.

Tuna matumaini kuwa wengi wa **wasikilizaji wetu** wamepata nafasi ya kuzungumza ingawaje **hatukuweza...**

Anaposema *kitinye* (tuna), kiambishi cha kwanza *-ki-* cha kitenzi hicho ni cha nafsi ya kwanza wingi na kisawe chake ni kiambishi '-tu-' katika Kiswahili. Maneno *kastoikyok* (wasikilizaji wetu) na *makimuch* (hatukuweza) yanaashiria kuwa msemaji anawashirikisha wengine katika kitendo cha 'kutoweza'. Ni njia ambayo mzungumzaji ('Koriryo') anamjumuisha mwasilishaji mkuu (Rotich) katika utoaji wa shukrani kwa wasikilizaji na kutoa hitimisho la kipindi. Iwapo msemaji angetumia vitenzi vya nafsi ya kwanza umoja kama 'nina, nitafanya, ninajua' miongoni mwa vitenzi vingine, msikilizaji angehisi kutengwa na kwa hivyo uso wake chanya kudhurika. Hilo linadhihirisha kuwa kiambishi 'tu' cha vitenzi katika nafsi ya kwanza wingi ni muhimu katika utekelezaji wa mkakati wa msemaji kumjumuisha msikilizaji katika kundi lake.

3.1.9 Kumchenga Msikilizaji

Mbinu nyingine ya kutimiza upole chanya ni kumchenga msikilizaji. Mbinu hii inamhitaji msemaji kutumia ujanja ili atimiziwe haja yake. Hali hii husisitiza kujitweza kwa msemaji na kutumia usemi ambao unamfanya msikilizaji ahisi kuwa ana uwezo wa kutenda jambo kuliko msemaji. Mkakati huu humwezesha msemaji

kufaulu lakini unahitaji umakinifu sana ili msikilizaji asije akafikiria ametumiwa vibaya. Vipindi vya *SK* vimedhihirisha mbinu hii kupitia mifano mingi.

Katika kipindi cha *Kolokset eng' katunisiet* (Mavazi katika ndoa), Winny na mwasilishaji wa kipindi wanajadili suala la mavazi na namna watu wengi wamevunja maadili ya jamii nyingi. Wao wanadai kuwa siku hizi watu hutembea uchi. Wanaeleza kuwa mavazi ya kisasa yanaonyesha yale yasiyotakiwa kuonekana. Rotich anaeleza kuwa kulingana na maadili ya kale ya jamii ya Wikalenjin, watu hawakuruhusiwa kuona uchi wa wenzao. Anaendeleza kuwa kwa bahati mbaya mwanamume angemwona mwanamke akioga, angekimbia bila kutazama nyuma. Hata hivyo, siku hizi badala ya kukimbia, mtu atasimama na kutoa maelezo yote kuhusu mwili wa mwanamke huyo. Tazama mfano huu:

Kal.

19. **Rotich:** *Tos ilen nee agobo nitok oh Winny?*

Kis.

Winny, unasemaje kuhusu hili?

Kal.

Winny: *'Pasta', uyo ui mising' eng ane anai ak amwa agobo Sobetab keny lakini angen ale itinye ng'omnatet nebo barak agobo atebonoto, mwawech oh.*

Kis.

'Pasta', inaonekana sina uwezo wa kujua na kuzungumzia sana maadili ya kale lakini ninajua una maarifa ya hali ya juu kuhusiana na maadili hayo, hebu tuambie.

Kupitia kwa usemi wa Winny, Rotich amechorwa kama mjuzi wa mengi kuhusiana na maadili ya jamii ya Kikalenjin. Sentensi *uyo ui mising' eng ane anai ak amwa agobo Sobetab keny* (inaonekana sina uwezo wa kujua na kuzungumzia sana maadili ya

kale) na *angen ale itinye ng'omnatet nebo barak* (ninajua una maarifa ya hali ya juu) zinadhihirisha ukweli huo. Winny anatumia ujanja ili kupata usaidizi kutoka kwa mwasilishi wa kipindi kwa kujitweza kimaarifa na kumkweza mwenzake. Njia hii inamsaidia msemaji kufanyiwa kitu na msikilizaji lakini kupitia njia ya kuhepa ulazimishaji wa kauli ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji.

Mfano mwingine wa kutekeleza mkakati wa kuchenga msikilizaji ili atekeleze jambo unadhihirika katika kipindi cha *Suupsetab kwonyik ak tibik* (Ubakaji wa wanawake). Mwasilishaji na mwelekezi wa kipindi wanafafanua sababu zinazopelekea wanawake kubakwa. Wanakubaliana kuwa wakati mwingine wanawake wenyewe hujisababishia shida kwa kuvaa mavazi yasiyositiri mwili wote. Winny anatoa nafasi kwa wasikilizaji kutoa maoni kuhusiana na jambo hilo. Msikilizaji 'D' kutoka Kitale anachangia kupitia ujumbe wake unaosomwa na Winny hivi:

Kal.

20. *Kang'etii 'Pasta' ak 'Koriryo', iman ng'olyondono komwa amu betusiechu koyomei bich oindet kobun koloksetab kwonyik ak tibikwak. Makomi kondit agot kitigin. Nginyoru bichuto kobendoti buch ak komugaksei kosuub ichek biik che memuchi koboi kabwatutikwak nga ngab abwoti ane ale chito agine ne suupsei ko chubot amu moyani ale aei choto chito ne timam. Agot ngano ii, ko mamuchi amwa kiy amu matinye naet agobo yotok mising, okwek che omwoiywech.*

Kis.

'Pasta' na 'Koriryo', mlilosema ni kweli kwa sababu hali ilivyo, shetani huwajaribu watu kupitia kwa mavazi ya wanawake. Hamna heshima hata kidogo. Wanawake siku hizi hutembea uchi na kuna uwezekano wa wao kubakwa na wanaume wasiotawala mawazo yao japokuwa mara nyingi huwa ninafikiria kuwa wale wabakaji wamelaaniwa kwa sababu vitendo kama hivyo hufanywa na wasio na akili timamu. Hata hivyo, siwezi kusema chochote kwa sababu **sina ujuzi sana wa mambo hayo, ila ni ninyi mtakaotueleza.**

Msikilizaji ‘D’ anaposema kuwa hana maarifa kuhusiana na mambo yanayozungumziwa, na kutoa fursa kwa viongozi wa kipindi kuelezea, anawapa hadhi ya kuwa na uwezo au maarifa kuhusiana na jambo linalozungumziwa. Usemi huo unamtweza msemaji na kumfanya msikilizaji kuhisi kupewa heshima au uwezo fulani. Hali hii pia hutunza uso wa msemaji kwa vile hakuonekana kutofautiana na wasikilizaji wake. Kama ‘D’ angeonyesha kuwa ana ujuzi wa mambo yanayozungumziwa kwa kutofautiana na mwasilishaji na mwelekezi wa kipindi, nyuso zao (mwelekezi na mwasilishaji) chanya zingetishiwa. Mkakati huu wa upole chanya ni mbinu tosha ya kutunza uso chanya wa msikilizaji.

3.1.10 Kudai Hali ya Kutendeanana

Kudai hali ya kutendeanana ni mkakati wa upole chanya. Hutumika wakati msemaji anataka kufanyiwa jambo na msikilizaji lakini kwa kukubali kuwa hata yeye atamfanyia msikilizaji kitendo kingine. Ni hali ya kutendeanana mambo kwa maridhiano au hali ya nipe nikupe. Msemaji anaahidi kumfanyia msikilizaji kitu lakini yeye pia anahitaji afanyiwe kingine. Hali hii inajitokeza katika kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwamume kuo a mke mwingine). ‘Pasta’ anafafanua kuwa, iwapo mwanamke ameajiriwa na mumewe hana kazi, mara nyingi mwanamke kama huyo humdharau mumewe kwa sababu hana chake. Anasema

Kal.

21. *“Winny, angen ale kiyai Mungu muren koek ne baei bikyik eng ko. Imugaksei itoche mushara kila arawa ko matache lakini abatisiei is. Tos memugak kegashine iyaiywo alak ayaun alak ne kategeremushareguk kityo Winny?”*

Kis.

Winny, ninajua kuwa Mungu alimuumba mume na kumpa majukumu ya kukidhi mahitaji ya familia yake. Inawezekana uwe umeajiriwa na unapata mshahara kila mwezi na miye nisiwe nao lakini ninafanya ukulima. Je, haitawezekana **unisaidie nami nikusaidie kwa mengine** badala ya kuona mshahara wako tu?

Kwa kutumia maneno *'iyoiywo alak ayaun alak'* (unisaidie nami nikusaidie kwa mengine), 'Pasta' Rotich anaonyesha hali ya kudai kutendana. Anatekeleza hili kupitia kwa maelezo anayomtolea mwelekezi wa kipindi kuwa watu katika jamii wanafaa kutendana mambo ili kuondoa mkwaruzano. Mbinu hii husababisha msemaji na msikilizaji kutendana mambo pasi na vitisho kwa nyuso zao chanya. Mbinu hii hutoa nafasi ya maridhiano kwa wahusika wa mazungumzo ili kukidhi mahitaji ya uso wa msemazwa. Kupitia kwa mfano huo, tunaona kuwa washiriki wa mazungumzo ya vipindi vya *SK* wanatilia maanani mkakati huu ili kudumisha mahusiano mema baina yao.

3.1.11 Matumizi ya Chuku

Katika mkakati wa kutumia chuku, msemaji analazimika kutumia maneno ambayo yanampa sifa msikilizaji lakini kwa njia ambayo sifa husika imesemwa kwa maneno yanayozidi uhalisia wa mambo. Mara nyingi, mkakati huu unatumika wakati msemaji anajua hakika kuwa kile anachosema labda si kweli au ametia chumvi nyingi ukweli uliopo. Mkakati huu wa upole chanya hutumika kupitisha habari fulani kwa msikilizaji lakini habari hiyo haisemwi moja kwa moja. Kufanya hivyo ni njia mojawapo ya kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji. Katika kipindi cha *Kolokset eng' katunisiet* (Mavazi katika ndoa), Rotich anatumia chuku kueleza uzuri wa mwili wa mwanamke. Anaonyesha kuwa mwanamke ameumbwa vizuri na haitaji kufanya lolote ili kuwa zaidi ya alivyoumbwa.

Ili kuonyesha uzuri huo, Rotich anasema,

Kal.

22. *Kwonyikyok ak tibikyok, kingen komie kele okaroron mising, kingen kapsaa kele kikiyaak eng, ung'otiet ne inegei. Kingen kele otinye suenutik che ng'ing'inen kou chelilyat, kingen kele alak eng' okwek kotinyei kelyek che biriren kot ko yelo anan kilen lelach. Heehee, oiye okororon iman! Lakini kata mie mising ndakoboru tegisto eng kolokseng'wong.*

Kis.

Wanawake na binti zetu, tunajua vizuri kuwa ninyi ni warembo sana, tunajua fika kuwa mliumbwa kwa siri ya kipekee. Tunajua kuwa mna viuno vyembamba mithili ya nyigu, tunajua kuwa kati yenu mna wale walio na **miguu myeupe hata mingine ni manjano**. Heehee, ninyi ni warembo kweli! Lakini ingekuwa vema zaidi kama mngeonyesha adabu kupitia kwa mavazi yenu.

Maneno ya Rotich kwenye kirai '*biriren kot ko yelo*' (myeupe hata mingine ni manjano) ni ya chuku, uzuri unaozungumziwa umepita kiasi cha kawaida. Mbinu hii imetumika ili kuifanya hadhira ya msemaji kuhisi vizuri na kufurahia urembo wao. Hata hivyo, ujumbe uliotakiwa kupitishwa (wa kutotembea uchi) utakuwa umefanikiwa bila kutishia uso wa msikilizaji kwa sababu lugha imerembeshwa kupitia kwa chuku.

Mkakati huu wa kutumia chuku umedhihirika pia kupitia kwa kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa). Rotich anafafanua jinsi ukosefu wa usafi ndani ya nyumba husababisha mume kutoroka na kupelekea kuvunjika kwa ndoa. Mwasilishaji huyo wa vipindi anasema:

Kal.

23. *Changianjin kwonyik agichek komanda manong'otoik Winny. Ngap ko kamusta mureno kota ko karon kocheng'jinot lagok beek ak fis ndalen koit koskolony komachamu gaa. Bendoti kikombook kong'ete jikoni akoi 'gate'. Ma notok kityo, koi ndait ole kiruei kong'utoi lugumekab lagok, 'chamu nding' oloto! Kemwa nee ibak kwondo ne masite kelek, mi ndisyot ne kiamei betut age, mi marakwek che kiamei ain, mi*

mayaiyat ne koamei amut koskoleny yaani bulot kutit chamu koriik cho mengech Winny cho kitoretegei.

Kis.

Winny, pia wanawake huchangia kutoka nje kwa wanaume. Mwanamume anaweza kuondoka asubuhi na mapema kuwatafutia watoto chakula na karo. Arejeapo, anapata nyumbani hakuvutii. Vikombe vimesambazwa kote kuanzia jikoni hadi langoni mwa ua. Sio hilo tu, afikapo mahala pa kulala anakaribishwa na uvundo wa mkojo wa watoto, huko kunanuka po! Tuseme nini kuhusu mkewe asiye piga mswaki meno, kuna mabaki ya ndizi ya siku nyingine, kuna maharage aliyokula juzi na kuna mabaki ya yai alilokula jana jioni, Winny, yaani **mdomo unanuka kama vyumba vidogo vya kujisaidia.**

Mfano huo unaonyesha jinsi mwasilishi wa kipindi ameelezea jinsi ukosefu wa usafi ndani ya nyumba husababisha mwanamume kutafuta mke mwingine au kuwa na ‘mpango wa kando’. Rotich ametumia chuku anapotumia kirai *chomu koriik cho mengech cho kitoretegei* (unanuka kama vyumba vidogo vya kujisaidia).

Mfano mwingine wa kutumia chuku kama mkakati wa upole chanya ni katika kipindi cha *Tetetab sigisiet* (Mpango wa uzazi). Winny anamwambia Rotich kuwa mwanzoni, jamii ya Wakalenjin haikukumbatia mpango wa uzazi kwa sababu iliaminika kwamba mpango huo ulikusudiwa kusimamisha uzazi. Anaeleza kuwa imani ya wanajamii kuhusiana na dawa za kupanga uzazi ilikuwa kwamba watoto watakozaliwa baada ya kutumia mpango huo hawangeweza kuzaa. Rotich anakubaliana naye kwa kusema kuwa imani hiyo ilisababisha watu wengi kuzaa watoto wengi kupiku uwezo wao. Anatumia chuku kwa kutaja idadi ya watoto wanaofuatana kama siku za juma akisema:

Kal.

24. *Keer iman oh Winny kit ne kibit amu kayananotok bo buch o, kisich biik lagok che rubugei kou Monday, Tuesday, Wednesday, Thursday... ei, kibiit nyalilda kot!*

Kis.

Winny, angalia kweli kilichotokea, kupitia kwa imani hiyo potovu, watu walizaa **watoto wanaofuatana kama Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi...** ai, kulitokea shida!

3.1.12 Kumwelewa Msikilizaji

Wakati wa kutekeleza upole chanya, msemaji anaweza kutumia usemi unaoonyesha kuwa anamwelewa msikilizaji. Usemi huo unalenga kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji wake na wakati uo huo msemaji awe amepitisha ujumbe aliokusudia. Kwenye kipindi cha *Korgrtab yugoi ak ingamatisiek eng sobetab kapchi* (Mashemeji katika maisha ya ndoa), msikilizaji ‘E’ kutoka Naivasha anauliza iwapo ni lazima mume awachukie wazazi wake ndipo mkewe aelewe kuwa anampenda.

Kwa kumjibu msikilizaji ‘B’ mwasilishaji wa kipindi anasema:

Kal.

25. *Angen ale ochame sigikwok ago bo iman notok. Ayani icham kabisa ago ngatesun ale cham koigeny. Mamwa ale iwech sigiguk ipkobate magat inai ile ye kaitunisie konyolchinin inet sigiguk, mising ko mama neng’ung, konai kole kakoit chito age ne magat koib kebeber neo eng sobeng’ung.*

Kis.

Ninajua kuwa mnawapenda wazazi wenu na hiyo ni haki. **Ninakubali** kuwa mwapende kabisa na mfanye hivyo hata milele. Sisemi uwachukie wazazi isipokuwa unatakiwa ujue kuwa unapooa, unatakiwa kuwafahamisha wazazi wako, zaidi ni mama mzazi, ajue kuwa aliyeolewa anachukua sehemu kubwa na ya kipekee katika maisha yako.

Rotich anaonyesha, kupitia kwa usemi ‘*Angen*’ (ninajua) kuwa anawaelewa wanaume. Ili kupitisha ujumbe wake kuhusu hali ya kuwatunza wake zao na kuzuia migogoro kati yao na wakwe zao, Rotich anatoa kauli ya kukubaliana nao na pia kuonyesha makubaliano kupitia kwa maneno ‘*angen... ak ayani*’ (ninajua... na

ninakubali). Kukubali huku kunaokoa uso wa msemzwa kwani anahakikishiwa kuwa hisia zake zinakubalika.

Aidha, hali hii inamwezesha msemzwa atulie na aweze kumsikiza msemaji zaidi. Hali hii isingefikwa iwapo msemaji angeonyesha kumpinga msemzwa moja kwa moja au kumlaumu. Watu huwa radhi kushiriki katika mazungumzo iwapo watahisi kuwa wameelewewa. Hata hivyo, pindi wakihihi vingenevyo, huenda ukaibua ugomvi au hata msemzwa anyamaze na hivyo kukatiza mazungumzo.

Kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka) pia kinadhihirisha mkakati wa kumwelewa msikilizaji. Winny anasoma ujumbe wa msikilizaji ‘F’ kutoka Kapenguria unaodhihirisha kuwa anawaelewa viongozi wa kipindi (Rotich na Winny). Ujumbe huo unasema:

Kal.

26. *Iman mabotok amu omoche ak okwek orip sait, notok amu nee si olen dakikainik aeng’. Ochamwoo amwa ... nitok kityo.*

Kis.

Ni kweli, si kosa lenu, kwa sababu mnataka kutunza saa na ndio sababu mnasema dakika moja. Nikubalieni niliseme ... hili tu.

Msikilizaji ‘F’ anaonyesha kuwa anawaelewa wasimamizi wa kipindi wanapotoa dakika mbili kwa kila anayetaka kuuliza swali au kuchangia mada. Anaposema *iman mabotok amu omoche orip sait* (ni kweli, si kosa lenu kwa sababu mwataka kutunza saa), ‘F’ anadhihirisha kuwa anajua nia ya waelekezi wa kipindi wanapowaharakisha au kuwanyima muda. Mbinu hii ni njia ya kutunza uso chanya wa wasimamizi wa kipindi husika. Msikilizaji ‘F’ anaepuka kuwaaibisha wasimamizi wa kipindi kwa kuwaambia wazi kuwa hawapaswi kuwakatizia muda.

Kumwelewa msikilizaji ni pamoja na kushughulikia mahitaji yake. Mtu anapomwambia msikilizaji kuwa ‘ninajua’ au ‘ninakubali’ anaonyesha kuwa anaungana na msikilizaji kwa kile kinachozungumziwa. Mbinu hii humfanya msikilizaji kuona kuwa anathaminiwa na kukubalika. Kwa kufanya hivyo, msemaji hahifadhi uso wa msemazwa tu bali pia anaonyesha kuwa mazungumzo ni kadhia ya ushirikiano. Kwa kumwelewa msikilizaji, msemaji anadhihirisha kaida ya namna ya kuwasilisha ujumbe kama ilivyofafanuliwa na Grice (1975).

3.1.13 Kutoa Ahadi kwa Msikilizaji

Kutoa ahadi ni namna nyingine ya kuokoa uso chanya wa msikilizaji. Kuahidi kunamfanya msemazwa kufurahi kwa sababu anajua atapokea au atatendewa kitu fulani na msemaji. Vipindi vya *SK* vimesheheni matukio ambamo wazungumzaji wanatoa ahadi ili kukabiliana na tishio kwa nyuso zao chanya. Kwenye kipindi cha *Tetetab sigisiet* (Mpango wa uzazi), Rotich anatoa ahadi kwa wasikilizaji wao kuwa atawatembelea ili waonane uso kwa uso na kuzungumza na wanaume. Tazama mfano huu:

Kal.

27. *Atinye kamang'unet ale chang' che tebege kole tia chichi mwaei ng'alechu tenin chu, angen ale ui eng murenik koyan tetetab sigisiet. Ogas o, otet tuiyet ak oguro nyo kengalal ak murenik, anyone kabisa.*

Kis.

Ninatumai kuwa wengi wenu mnajiuliza maswali mengi kuhusiana na kimo changu kwa kulinganisha na maneno ninayoyasema. Ninajua ni vigumu kwa wanaume kukubali kutekeleza mpango huu wa uzazi. Hebu sikilizeni, pageni mkutano kisha mniite tuzungumze na wanaume, **kwa kweli nitakuja.**

Anyone kapsa (kwa kweli nitakuja) ni usemi wenye ahadi. Rotich anasema hivi ili kuwafurahisha wasikilizaji wake kwa sababu wana hamu ya kumwona. Kwa

wasemezwa, ahadi hii inabeba dhima ya kuonyesha kuwa Rotich anawathamini kwa vile yuko tayari hata kukutana nao.

Pia, katika kipindi cha '*Korgetab yugoi ak kamatisiek eng sobetab kapchi*' (Wakwe katika maisha ya jamii), Winny anamshughulikia msikilizaji 'G' kutoka Chepyemit katika kaunti ya Elgeiyo Marakwet ambaye analalamika kuwa hakupewa nafasi kuchangia wakati wa kipindi kilichopita, kwa kumhakikishia kuwa angeongezewa muda. Anamjibu msikilizaji:

Kal.

28. *Meimge ane tupchenyu, testai, atesun rani dakikaisiek alak aeng.*

Kis.

Usisumbuke kakangu, endelea, **leo nitakuongezea** dakika zingine mbili.

Sehemu ya usemi wa Winny *atesun rani* (leo nitakuongezea) unatoa ahadi kwa msikilizaji. Huku kutoa ahadi kunaokoa uso chanya wa msikilizaji kwa sababu hatakuwa na wasiwasi wa kuishiwa na muda. Pia, msikilizaji anaona kuwa uhusika wake katika kipindi unakubalika na kuthaminiwa. Aidha, msemazwa anahisi kuwa hakukosea kutoa lawama yake. Uso wake unahifadhiwa anapohisi kuwa yeye anathaminiwa na msemaji wake.

3.1.14 Kutanguliza Mawali kabla ya Kutoa Sababu ya Kitendo

Waasisi wa nadharia ya upole, Brown na Levinson (1987), wanasema kuwa msemaji anaweza kutekeleza upole chanya kwa kuuliza au/ na kutoa sababu za kutenda kitendo fulani. Mkakati huu unakubalika kuliko ule wa kumwamrisha au kumshurutisha msikilizaji kutenda jambo husika. Mkakati huu unadhihirika vyema kupitia kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka). Mwasilishi wa kipindi anatoa

hadithi ya mama mmoja aliyezungumza naye kuhusiana na masaiibu aliyokuwa akipitia. Mama huyo anamwambia ‘Pasta’ kuwa mume wake alimwuliza watekeleze kitendo cha ndoa kwa kutumia sehemu ya kuendea haja kubwa. Rotich anaripoti taarifa hiyo akisema:

Kal.

29. *Kale kwonyotok kilenji manong’otionyi ‘koba korutochi chitab kokwet’ betunotok. Alen kibwat is kole kalya si ‘makirutochi chitab kokwet’ ago mi ‘kibunguetab koyotok?’*

Kis.

Mama huyo aliniambia kuwa siku moja mumewe alimwambia ‘wamtembelee jirani’, labda mumewe alijiuliza **mbona nyumba ya jirani isitembelewe hali walikuwa na ufunguo wa nyumba hiyo?**

Sehemu ya kati ya usemi wa ‘Pasta’ Rotich “*kalya si makirutoch chitab kokwet*” (Mbona wakose ‘kumtembelea jirani’) ni kama swali lakini ni la kibalagha. Sehemu ya mwisho ya usemi huo “*ago mi kibunguet*” (na hali walikuwa na ufunguo) inatoa sababu ya kufanya kitendo husika. Kuwa na ‘ufunguo’ ndiyo sababu kuu ya kutaka kumtembelea jirani. Mbinu hii inapotumiwa, matokeo yake huokoa uso chanya wa hadhira lengwa. Kwa mujibu wa mfano huo wa 29, kutanguliza swali kabla ya kutoa sababu ya kufanyika kwa jambo kunamfanya msikilizaji kuhisi vizuri kwa sababu hahitajiki kutolea jibu swali lililoulizwa. Iwapo angehitajika kutolea jawabu, angeaibika kwa sababu jambo linalozungumziwa ni la aibu na linatishia uso wake chanya. Mbinu hii huwapa wasikilizaji nafasi ya kujiokoa kutokana na aibu inayobebwa na usemi.

Mbinu hii ya kutanguliza swali na kutoa sababu ya kutekeleza kitendo fulani imetekelezwa pia kupitia kwa kipindi cha *Kitun kwondo age* (Kuoja mke mwingine). Kwa kuchangia mada, msikilizaji ‘H’ kutoka Ziwa anaonekana kutofautiana na Winny ambaye anakataa katakata kuwa si vyema kuoja mke mwingine kwa sababu

kuoa huko kutasababisha ufukara. Winny anaeleza kuwa watoto watakapoongezeka mahitaji yatakuwa mengi kwa mwanamume na atamwachia mama watoto majukumu hayo. Isitoshe anaendeleza kuwa upendo wa mume kwa wake wote hautakuwa kwa viwango sawa.

Winny anaendelea kuteta kuwa hata mwanamume akiwa na mali nyingi, mali hiyo haitanunua upendo na hivyo anapendekeza kuwa ni vyema mtu akiwa na mke mmoja. Msikilizaji ‘H’ anamjibu Winny kwa kusema,

Kal.

30. *Kongoi ‘Koriryo’ amu iribe laindap kwonyik. Achame kityo ateb ale ii, kalya si machomwo kwondonyuatun kwondo age ago tomo korerchi tugukyuk?*

Kis.

‘Koriryo’, ninashukuru kwa sababu unachunga laini ya wanawake. Napenda tu kuuliza kuwa **mbona mke wangu asiniruhusu** nimwoe mke mwingine **hali hajapungukiwa na mali yangu?**

Msikilizaji ‘H’ anajaribu kutoa sababu zake zinazomfanya kufikiria kuwa kuoa mke mwingine si shida. Anapitisha ujumbe wake kwa kuuliza swali kisha kutoa sababu ya kutaka kutekeleza jambo husika. *Kalya si machomwo* (mbona mke wangu asiniruhusu) ni swali la balagha na *ago tomo korerchi tugukyuk* (hali hajapungukiwa na mali yangu). Mfano huu unadhihirisha namna msemaji anajaribu kuokoa uso wa msikilizaji kwa kutumia maswali ya balagha kama kitangulizi cha kusema kitendo cha kutishia uso. Mkakati wa maswali ya balagha unaokoa uso wa msikilizaji kinyume na kutoa sababu ya kitendo moja kwa moja. Msikilizaji anajipata katika hali ya kuelewa mapema kinachofuata. Mbinu hii huwasaidia wazungumzaji kujiepusha na hali ya kutoa sababu ya kitendo moja kwa moja bila kujali hisia za wasemezwa wao.

3.1.15 Kuzidisha Kauli Zinazomshawishi Msikilizaji Kukubaliana na Msemaji

Uzidishaji wa kauli zinazomshawishi msikilizaji kukubaliana na msemaji ni mbinu mojawapo ya kutekelezea mkakati chanya wa upole. Msemaji anahitajika kusema jambo na kumaliza kwa usemi unaomfanya msikilizaji kukubaliana naye. Mbinu hii inaweza kutekelezwa kwa kutumia maswali mwishoni mwa usemi. Maswali hayo yanatakiwa kutangulizwa na maneno kama ‘*tos*’ (si), ‘*iyani yekai ile*’ (unakubaliana nami kuwa) na ‘*ingen*’ (unajua) miongoni mwa mengine.

Katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), Rotich anamweleza Winny kuwa mara nyingi wanaume hutafuta mpango wa kando kwa sababu wake zao wanawanyima haki zao au hawatosheki. Rotich anasema kuwa wanawake wanapofikia umri fulani huamua kuwatesa waume zao kwa sababu watoto wamekuwa wakubwa na hivyo wanaume wataogopa kuwaadhibu. Winny anatofautiana naye kwa kusema:

Kal.

31. ‘*Pasta*’, *mongen ale amu nee si iteteanjini murenik mising, imugaksei koesio mureno kogochi imandanyi kwony. Ago amu notok komugaksei kosiimda kwonyotok ako mata komage kiy ngalechoto bo itok, iyani yekai ile imugaksei notok ii?*

Kis.

‘*Pasta*’, Sijui ni kwa nini unapenda kuwatetea wanaume sana, inawezekana mwanamume kumnyima mkewe haki yake. Na kwa sababu hiyo, inawezekana kwa mwanamke kukosa hamu kabisa ya mambo hayo ya kitandani, **je unakubaliana nami kuwa hilo linawezekana?**

Winny anatumia swali mwishoni mwa usemi ili kumshawishi msikilizaji kukubali hoja lake. Swali *iyani yekai ile imugaksei nitok ii?* (je, unakubaliana nami kuwa hili linawezekana?) linampa msikilizaji nafasi ya kukubaliana na msemaji. Licha ya

tofauti katika mawazo yao, msikilizaji, kupitia kwa swali hilo linalokuja mwishoni mwa sentensi anashawishika kukubaliana na mawazo ya msemaji. Uamilifu wa matumizi ya maswali mwishoni mwa usemi unadhihirika kupitia usemi wa Rotich katika mfano ufuatao:

Kal.

32. *Winny, **maesioi** agot kitigin ale imugaksei kwaak notok, bo iman ng'olyondono kemwa. Kit ne kamache amwa ko atkaan kora ko chang' korik che butoksei amu kwonyik. Nganda simdoi kwonyik agobo katuiyonoto bo katunisiet, ko mate chong'indonywa nebo murenik. Kora komachang' murenik che sasei kwonyikwak kot koete kotuiyetab katunisiet, tos mau notok o Winny? Lakini anyun **Ayanun** inye ng'olyondono kemwa.*

Kis.

Winny, **sikatai** hata kidogo kuwa hilo linaweza kufanyika. Jambo nililokusudia kulisema ni kwamba mara nyingi nyumba nyingi huvunjika kwa sababu ya kutowajibika kwa wanawake. Ingawa wanawake hukata tamaa kuhusiana na jambo hilo la ngono, idadi yao si kubwa kama ya wanaume. Isitoshe, sio wanaume wengi ambao huwadharau wake zao hadi kuwanyima haki ya ndoa, Winny, si hilo ni kweli? Lakini **ninakubaliana nawe** kuhusu ulichosema.

Kupitia mfano huu, tunapata kuwa Winny na 'Pasta' Rotich wanamalizia usemi unaowafanya wakubaliane. Maneno *maesioi* (sikatai) na *ayanun* (ninakubaliana nawe) yanadhihirisha kuwa Rotich anakubaliana na Winny. Shauku ya msemaji inazidishwa kwa msikilizaji ambaye hana lingine ila kukubaliana na msemaji. Hii ni mbinu mojawapo ya kuwafanya wasemaji watekelezewe mambo au mawazo yao kukubalika bila kutishia uso chanya wa msikilizaji.

3.2 Upole Hasi Katika Vipindi vya SK

Kama tulivyotanguliza katika sura ya pili, mkakati huu wa upole hasi hulenga kupunguza vitisho kwa uso hasi wa msikilizaji wakati wa mazungumzo. Kama wasemavyo Brown na Levinson (1987), upole hasi huwakilisha jambo linaloeleweka

kama tabia njema na unaohusishwa na maelezo ya kawaida kuhusu jamii. Lengo kuu la upole hasi ni kupunguza ulazimishaji wa kauli fulani inayotishia uso wa msikilizaji.

Brown na Levinson (1987), wanaeleza kuwa mkakati wa upole hasi hutumiwa ili kuutambua uso hasi wa msikilizaji kwa kuonyesha tofauti iliyopo baina ya msikilizaji na mzungumzaji. Huang (2007), anasisitiza mawazo ya Brown na Levinson kwa kusema kuwa, katika utumiaji wa mkakati huu mzungumzaji hana uhuru mkubwa wa kumwingilia msikilizaji ukilinganishwa na mkakati wa upole chanya. Huang anaendeleza kuwa, mkakati huu hudhamiria kuondoa ulazimishaji wa kauli zinazotishia uso wa hadhira. Katika vipindi vya *SK*, matumizi ya mkakati hasi wa upole na wahusika wa mazungumzo kama njia ya kuhifadhi nyuso hasi za wasikilizaji wao, yanabainika kupitia mbinu zifuatazo:

3.2.1 Kuwa Bila Rajua

Kuwa bila rajua ni kutotarajia mazuri. Hii ni mbinu mojawapo inayotumika katika mazungumzo kutekeleza upole hasi. Mbinu hii ilidhihirika kupitia kipindi cha *Tetetab Sigisiet* (Mpango wa Uzazi). ‘Pasta’ Rotich anatofautiana na Winny ambaye anadai kuwa kuzaa watoto wengi kunachangia utajiri mwingi katika jamii. Winny anatoa sababu kuwa watoto hao wanapomaliza masomo yao huajiriwa na kupata fedha nyingi. Rotich anamjibu,

Kal.

33. *Makinae ng’alechu Winny, imuch kotemene sigindet konet lagok tugul ipkong’etyo alage koek choriik, koek alage chelesos kotomo kemwa che supsei. Aaksei chutok amu manyor lagok tuguk che yomei eng gaa amu sigisiet ne makipangan, notok amu nee si kalenjin imuch memugak ng’olyong’ung.*

Kis.

Winy, huwezi kubashiri mambo haya, kuna uwezekano wa mzazi kushindwa kuwasomesha watoto wake wote hadi wengine wakaamua kuwa wezi na wakora, kando na wabakaji. Hayo hufanyika watoto hao wanapokosa mahitaji ya kutosha kutokana na kutopangwa kwa uzazi, na hiyo ndiyo sababu nimesema **huenda ulilosema lisiwezekane**.

Mfano 33 unadhihirisha hali ya kutokuwa na urajua. Rotich anaposema “*imuch memugak*” (labda halitawezekana) anaonyesha hali ya kutotarajia mazuri. Kwa hivyo, jambo lililosemwa huenda lisiwe kama ilivyotarajiwa.

Mfano mwingine ni katika kipindi hicho cha *Tetetab Sigisiet* (Mpango wa Uzazi). Pasta Rotich anaeleza kuwa wanaume nao wanatakiwa kujihusisha na mpango wa uzazi kwa kuchukua hatua ya kufanyiwa upasuaji au kutumia madawa. Msikilizaji ‘I’ kutoka kijiji cha Ndonyo Ngaria, kaunti ya Uasin Gishu anasema,

Kal.

34. *Korom yotok ‘Pasta’, abwati ale ui koyan mureno koek inendet ne masigisie. Iyani murenik che chang kole chepyosok che magat kwam kerichek anan koai kiy age tugul ne kemugak amu memugaksei eng muren kongen kole masigisie.*

Kis.

‘Pasta’ hilo **ni gumu**, ninafikiria kuwa **si rahisi** kwa mwanamume kukubali ya kwamba yeye ndiye asiyeweza kutunga mimba. Wanaume wengi wanaamini kuwa wanawake ndio wanaotakikana kutumia madawa au chochote kile kinachowezekeka kwa sababu **haiwezekani** kwa mwanamume akae akijua hana uwezo wa kupata mtoto.

Mfano huu unatumia maneno yanayodhihirisha kutowezekeka kwa jambo au ugumu wa utekelezaji wake. Kupitia kwa matumizi ya maneno *korom yotok* (ni ngumu) na *ui* (si rahisi), msemaji anamtayarisha msikilizaji kutotarajia mazuri au kutekelezewa jambo. Sehemu ya mwisho ya mfano huu inaonyesha matumizi ya neno *memugaksei*

(haiwezekani) kama kiashiria cha kutowezekana kabisa kwa jambo. Mbinu hii humtayarisha msikilizaji ili asitarajie mazuri kutoka kwa msemaji.

Kuwa bila rajua pia inadhihirika kupitia kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka). Shabiki 'J' kutoka Kapsabet anauliza ni kwa nini wanawake wasiwasamehe waume zao wanapopatikana 'wakiiba' ilhali mume ni kichwa cha nyumba. Anauliza,:

Kal.

35. *'Angii Pasta' ak Winny, tos manyolu iman kogas it kwony muren ak konyochi kaat inendet bila masharti agot indanyor 'kochorsei?' Amwae kou notok amu mwaei baibol kole muren ko metitab kot. Mongen sine ngot ko iman nitok amu tomo aweny komie bukuit.*

Kis.

'Pasta' na Winny, ninauliza hivi, je mwanamke hafai kumtii mumewe na kumsamehe bila masharti hata akipatikana 'akiiba'? Ninasema hivyo kwa sababu Bibilia inasema kwamba mume ni kichwa cha nyumba. **Sijui kama hili ni kweli kwa sababu sijachunguza sana Bibilia.**

Mfano huu ni dhihirisho kuwa shabiki 'J' hatarajii kuwa mwendelezi wa kipindi pamoja mwasilishaji watakubaliana naye kwa vyote. Hili linathibitishwa na sentensi ya mwisho *mongen sine ngot ko iman nitok amu tomo aweny komie bukuit* (sijui kama hili ni kweli kwa sababu sijachunguza sana Bibilia). Maana ya usemi huu ni kuwa msemaji amejitaweka katika nafasi ya kutarajia majibu chanya au hasi kutoka kwa msikilizaji. Kategoria hii ya upole humpa msikilizaji uwezo wa kukubali au kukataa mawazo ya msemaji. Kwa kufanya hivyo, msemaji atakuwa amejitayarisha kupokea matokeo yaliyo sambamba au kinyume na matarajio yake.

Kwa kumjibu, Winny anasema:

Kal.

- 36.** *Acha akinye chorwenyu, ngo u yo omoche okwek kegasak it agot eng tuguk che manyolu. Mwaei baibolinotong'ung kole ogas it eng Kiptaiyat yaani, eng tuguk che ma kiptuibatoi ak magetab Mungu, ui inye yotok. Agot nga no kemwoe kityo amu kimwoei ang buch angen ale mondoigei ng'onny murenik.*

Kis.

Rafiki yangu, hilo si kweli, inaonekana ninyi mnataka tu tuwatii hata kama haifai. Bibilia hiyo yako inasema pia kuwa tunapaswa kutii katika Bwana yaani, katika mambo yasiyo kinyume na mapenzi ya Mungu, inaonekana hilo ni gumu. **Hata hivyo tunasema tu kwa nia ya kusema lakini tunajua ninyi hamnyenyekei hata kidogo.**

Usemi wa Winny katika mfano 36 unabainisha hali ya kutotarajia mazuri. Anathibitisha kuwa kuna mambo ambayo ni magumu kwa wanaume kutekeleza. Sehemu ya mwisho ya usemi huo *agot nga no kemwoe kityo amu kimwoei ang buch angen ale mondoigei ng'onny murenik* (hata hivyo tunasema tu kwa nia ya kusema lakini tunajua ninyi hamnyenyekei hata kidogo) ni dhihirisho la kukubali kutowezekana kwa jambo. Kwa kutumia maneno yanayoonyesha ugumu wa kutendeka kwa jambo, washiriki wa mazungumzo wanatekeleza mbinu ya kutokuwa na urajua. Hayo yanafanyika kwa makusudi ya kupunguza vitisho kwa uso hasi wa msikilizaji.

3.2.2 Matumizi ya Kauli za Jumla

Kauli za jumla hutumiwa ili kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji. Ni mbinu ya kutumia kauli zisizohusishwa na mtu maalum. Kwa njia nyingine, mbinu hii humhitaji msemaji kutotumia viwakilishi vya nafsi. Msemaji anapotoa kauli kama hizo, atakuwa

anaokoa uso hasi wa msikilizaji kwa sababu kauli hizo haziathiriwi na hisia. Mifano inayofuata inafafanua mkakati huu.

Katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), Rotich anatoa mausia kuwa wanawake wanafaa kuzingatia usafi ili waume wasitafute ‘mpango wa kando’. Anasema:

Kal.

37. *Atechini kobogorisiek tugul konai kole ma bo iman atebet ne makiunegei. Kalya si mang’et mama ak kochokyi boisionik ndaityo kochorchigei beek konegit koit manong’otiondenyi! Mabo iman konyastagei chi amu mweenen chorueng’ung no kitemechini nda kikakietenen.*

Kis.

Ninawashauri **wanawake** wote wajue kuwa si haki kukaa bila kuoga. Mbona **mama** asifanye kazi zake haraka haraka kisha aoge mara moja kabla ya kufika kwa mumewe! Si haki kujiachilia kwa sababu yule rafiki yako, ambaye ungemfia iwapo ungekatazwa kuolewa naye atakutoroka.

Katika mfano huo, matumizi ya maneno *kabogorisiek* (wanawake) na *mama* (mama yeyote) inaonyesha hali ya kutomlenga mtu binafsi. Hali hii humfanya msikilizaji, hata kama atagundua kuwa yeye ni mzembe katika hali ya usafi, kujigundua mwenyewe na hatahisi vibaya. Iwapo mtu mchafu angenyoshewa kidole na kuambiwa azingatie usafi, uso wake hasi ungeathirika kwa sababu ya kauli inayomlenga, yaani matumizi ya kauli zinazolenga mtu binafsi.

Mfano wa pili katika kutekeleza mbinu ya matumizi ya kauli za jumla ni katika kipindi cha *Subseetab tibik ak kwonyik* (Ubakaji wa wanawake). Rotich na Winny wanatoa ushauri kwa wasikilizaji kuwa ubakaji wa baba kwa binti zao ni dhahiri. Wanashikilia kuwa hali hii hutokana na watu ambao labda wengine hawafikirii vizuri.

Wanaeleza kuwa baba mwingine anaweza kupendezwa na umbo la bintiye ambalo humkumbusha juu ya mkewe akiwa msichana. Rotich anasema:

Kal.

38. *Mayaach metowek **biik tugul** che supsei Winny. Imuch kogeer **baba** ateptab bortab cheptanyi kobwatyi agobo ole kiu kwondonyi ko chepto. Imugaksei kong'eet baba inotok ak konam cheptanyi amuu tamaa ne keyanie chito lakwet kamet. Yaach **murenikalage** Winny, utyegei.*

Kis.

Winny, sio kwamba **watu wote** wanaobaka wana akili punguani. Baba anaweza kuona umbo la bintiye, ukamkumbusha umbo la mkewe akiwa msichana. Kuna uwezekano wa baba huyo kumbaka bintiye kutokana na tamaa inayosababishwa na fikra ya kumfananisha bintiye na mkewe. Winny, **wanaume wengine** ni wabaya tu, hujisahau.

Matumizi ya *biik tugul* (watu wote), *baba* (baba) na *murenik alage* (wanaume wengine) ni kauli za kijumla kwa sababu hazimlengi yeyote. Hata Rotich anaposema “*Yaach murenik alage Winny, utyegei*” (Winny, wanaume wengine ni wabaya, hujisahau), haonyeshi kumlenga mwanamume yeyote. Anaweka kijumla usemi wake ili wanaume wasihisi vibaya. Mbinu hii ni mwafaka katika kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji.

3.2.3 Matumizi ya Vitangulizi

Ili kutekeleza mkakati hasi wa upole, msemaji anaweza kutumia vitangulizi katika usemi wake. Mbinu hii hupunguza makali ya usemi wenye kuonyesha msimamo fulani. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kitangulizi ni sehemu ya usemi ambao huweza kuwa kweli kwa kiwango fulani au kwa namna fulani pekee. Pia wanaongeza kuwa, kitangulizi kinaweza kuwa kweli zaidi ya inavyotarajiwa. Hata hivyo, wao wanaonya kuwa hatari ya kitendo kinachotishia uso mara nyingi hutokana na chukulizi. Chukulizi hizi ni zile zinazohusishwa na kitendo husika. Mfano ni katika

kumwuliza mtu jina lake, msemaji anachukulia kuwa msikilizaji yuko tayari kumpa habari hizo za kibinafsi. Kutokana na maoni hayo tunaona kuwa matumizi ya vitangulizi ni njia mojawapo ambayo kwayo msemaji anaweza kujifunga na chukulizi hizo.

Kwa mujibu wa Allot (2010), matumizi ya vitangulizi yanaweza kuchukuliwa kama njia rahisi ya kujiondoa kwa msikilizaji. Hii ina maana kuwa mchango wa kauli itakayofuata kitangulizi utavunja kaida za Grice za uhusiano na namna. Maoni hayo yanatujaza kuwa sababu mojawapo ya kutumia vitangulizi ni kutamka wazi utambuzi wa kitendo kinachotishia uso wa msikilizaji na kuonyesha kuwa msemaji anamwelewa msikilizaji. Murphy (2010) anaunga mkono wazo hilo kwa kusema kuwa matumizi ya vitangulizi yanaonyesha kuwa msemaji amekosa neno sahihi la kutumia au kwamba uteuzi wake wa maneno sio kama inavyopaswa kuwa.

Mzungumzaji hulenga kufanikisha mkakati hasi wa upole kwa kutumia vitangulizi na vidokezi ambavyo humtayarisha msikilizaji kuupokea ujumbe wake hata kama ni hasi. Kaida hii hutambulishwa na matumizi ya maneno ya kuomba msamaha pamoja na matumizi ya dhamira tegemezi kama vile: labda, samahani, nafikiri, huenda, -weza miongoni mwa mengine. Matumizi ya vidokezi hivi pia hudhamiria kuonyesha majuto kwa habari ambazo mhusika anataka kuzisema. Katika vipindi vya *SK* kaida ya matumizi ya vitangulizi inadhihirika katika miktadha mbalimbali.

Katika kipindi cha *Kolokseet eng katunisiet* (Mavazi katika ndoa), Winny anatumia vitangulizi kuonyesha jinsi wanawake wanathamini mavazi. Anasema kuwa wanawake huhisi vizuri wanapooneka warembo mbele ya wengine. Anasema:

Kal.

39. *Ingenii ‘Pasta’, makiyaach sinyen mi...ising kou ole obwotitoi, kaek kityo amu kichame urembo.*

Kis.

‘Pasta’ unajua sisi si wabaya sa...ana kama mnavyofikiria, ni vile tu tunapenda urembo.

Matumizi ya kitangulizi *ingenii pasta* (‘Pasta’ unajua) yanamtayarisha ‘Pasta’ kupokea ujumbe unaofuata bila kukisia ukali wa usemi huo. Kitangulizi hiki kinamsaidia Winny katika kupunguza ukali wa usemi wake. Hii ni kwa nia ya kutomkasirisha msikilizaji wake kupitia kwa ujumbe unaofuata kitangulizi hicho. Ni mbinu muhimu katika kumtayarisha msikilizaji kupokea ujumbe mbaya au unaomgharimu furaha na raha yake.

Mfano mwingine wa kutumia vitangulizi unadhihirika katika kipindi cha *Korgetabyugoi ak ingamatisiek eng katunisiet* (Wakwe katika ndoa). Rotich anawashauri wasikilizaji, ambao ni kina baba, kuwa wanatakiwa kuonyesha msimamo kwa watu wa jamii zao ili kuwakinga wake zao. Anaeleza kuwa mara nyingi kumetokea vita kati ya jamii nyingi kwa sababu mwanamume haonyeshi mipaka kwa wazazi, ndugu na dada zake. Mwasilishi huyu mkuu wa kipindi anadokeza:

Kal.

40. *Eng kasarwek alak ko ngap komamage kiy murenik tuguk alak chebo kamanut mising. Amu eng kasarwek che chang koumiandos chepyosok amu murenik che meboru kiwotet. Tonon ko i muren ak imwachi sigiguk ilenji kwondong’ung ko kwondong’ung amat kotangoe chi.*

Kis.

Wakati mwingine wanaume wanaweza kupuuza mambo muhimu sana. Kuna nyakati wanawake huumia kwa ajili ya wanaume wasioonyesha mipaka kwa wazazi, simama kama mwanamume na uwaeleze wazazi wako kuwa mkeo ni mkeo na hafai kuchezeza na yeyote.

Mwanzoni mwa usemi huu, msemaji (Rotich) anaonekana kutolenga chochote. Anazungumza kimzunguko kwa kutotaja bayana lengo Lake. Anaposema *eng kasarwek alak ko ngap komamage kiy murenik tuguk alak chebo kamanut missing* (wakati mwingine wanaume wanaweza kupuuza mambo muhimu sana), Rotich anatanguliza usemi wake kwa maneno yasiyo bayana. Sentensi ya mwisho *tonon ko i muren ak imwachi sigiguk ilenji kwondong'ung ko kwondong'ung amat kotangoe chi* (simama kama mwanamume na uwaeleze wazazi wako kuwa mkeo ni mkeo na hafai kuchezewa na yeyote) inaonyesha msimamo tofauti na ulio katika sentensi tangulizi. Msimamo huu unaonekana baada ya kumtayarisha msikilizaji ili asiudhike akipata ujumbe unaofuata. Mbinu hii inatunza nyuso za wahusika wa mazungumzo hasa msikilizaji ambaye vinginevyo angehisi vibaya.

3.2.4 Kuuliza Maswali

Msemaji pia anaweza kuendeleza mkakati hasi wa upole kwa kutumia mbinu ya kuuliza maswali. Mzungumzaji anaweza kumwuliza msikilizaji maswali kama njia ya kupata majibu na kumwezesha kuwasilisha hitaji lake bila mkwaruzo kwa msikilizaji. Mifano ifuatayo inadhihirisha mbinu hii katika kipindi cha *Sobetab Kapchi*. Kwenye kipindi cha *Tetetab sigisiet* (Mpango wa uzazi), Winny anazua utata kwa kuteta kuwa mpango wa uzazi unatakiwa kufanywa na kila mhusika katika ndoa. Analalama kuwa wanawake wameumizwa na madawa ya kupanga uzazi huku wanaume wakila raha na wao ndio wanahitaji 'kula' kila wakati. Winny analalama,

Kal.

41. *Amu nee si onyalili murenik kwonyik o 'Pasta'?Nda kikoyan koyam laisetab arawek sogol ana olen raisi! Imuktoi ano kwony kola tuguk tugul eng ngony? Kalen kata kaikai koboisie murenik kerichek agichek si konyumnyumchi kwonyik mila no te no.*

Kis.

‘Pasta’, mbona wanaume mnawatesa wanawake? Si mngemwacha abebe tu mzigo wa miezi tisa, ama mnafikiria ni rahisi! Inawezekanaje kwa mwanamke kubeba mzigo wote duniani? Ninafikiria ingekuwa vema iwapo wanaume wangetumia madawa za kupanga uzazi ili kuwapunguzia wanawake mizigo.

Kutokana na usemi huo wa Winny, maswali matatu muhimu yanajitokeza. *Amu nee si onyalili murenik kwonyik o ‘Pasta?’* (‘Pasta’, mbona wanaume mnawatesa wanawake?) limetanguliza usemi wote. Swali hili linaonekana la jumla na kutomlenga mwanamume yeyote binafsi. Swali la pili *nda kikoyan koyam laisetab arawek sogol ana olen raisi!* (si mngeacha abebe tu mzigo wa miezi tisa, ama mnafikiria ni rahisi!) inaonyesha kuwa msemaji ana machungu kutokana na majukumu mazito ya mwanamke. Hata hivyo, swali la mwisho *imuktoi ano kwony kola tuguk tugul eng ngony?* (inawezekanaje kwa mwanamke kubeba mzigo wote duniani?) si bayana lakini linamtayarisha msikilizaji kusikia kinacholalamikiwa.

Maswali hayo yanalenga kupata maoni ya wasikilizaji lakini kwa kutumia mbinu isiyo dhahiri. Mbinu hii inaficha udhahiri wa usemi kwa kutumia maswali. Wasikilizaji wanaposikia usemi kama huo, wanajaribu kutoa maoni yao kwa sababu makali ya usemi yamepunguzwa. Kuuliza maswali kunawasisimua wasikilizaji kutaka sana kuchangia mjadala husika kwa sababu kauli zinazotumiwa zinahitaji majibu kutoka kwa yeyote yule asiyetajwa.

Mbinu ya maswali pia imedhihirika katika kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwanamume kuoia mke mwingine). Rotich anaeleza kuwa wanaume wengi wameamua kuoia mara ya pili au ya tatu kwa sababu wanawake wamewanyima haki za ndoa. Anatoa mfano wa mwanamke ambaye alikuwa akimnyima mumewe kitendo cha ndoa na kuamua kulala chumba tofauti. Anaeleza kuwa mzee, mumewe huyo mwanamke, aliteseka katika hali hiyo

kwa muda mrefu hadi akashindwa kuvumilia. Baadaye, maji yalipozidi unga, mzee alikuwa akimhonga mkewe kwa kumpa ng'ombe bomani ili amkubali. Alifanya hivyo kwa muda mrefu hadi ng'ombe aliokuwa nao bomani wakawa wa mkewe. Alipoona hivyo, mzee huyo aliamua kujinyonga kwa sababu hangeweza kujamiiana na mkewe tena bila ng'ombe wa kumpa. Rotich anauliza:

Kal.

42. *Winy ak kostoikyok che kwonyik, tos nyolu itesan ching'ung kou notok? Yo irwe eng rumit age ibwatitoi ano ago kikoba tukyuk agot chepsitie ak miso koing'wong?*

Kis.

Winy pamoja na wasikilizaji wetu wanawake, **je ni ungwana kumtesa mtu wako hivyo? Ulalapo katika chumba kingine unafikiria nini huku unajua ng'ombe wangu, 'chepsitie' na 'miso', walipelekwa kwenu?**

Mfano wa 42 unadhihirisha kuwa Rotich anachukua jukumu la kuwatetea wanaume kutokana na kunyimwa haki zao. Anaonyesha kuwa tendo la ndoa ni muhimu kwa mwanamume kwa sababu amelipa mahari. Maswali anayotumia yanaonyesha kuwa mwanamume ana haki ya kupata chochote kutoka kwa mkewe. Maswali hayo yanapunguza makali ya usemi dhahiri ambao labda ungeonekana kutishia uso wa wanawake. Matumizi hayo ya maswali ya balagha ni muhimu ili kumwacha msikilizaji akiwaza na kutafuta namna ya kurekebisha tabia husika kuliko kumwambia moja kwa moja kuwa ana kosa.

3.2.5 Kutokuwa Bayana

Mbinu ya kutokuwa bayana ni sawa na kusema kitu kimzunguko. Msemaji anatumia mbinu hii kwa minajili ya kuokoa uso hasi wa msikilizaji. Ni mbinu ya kukwepa kutaja mambo bayana. Mbinu hii inavunja kaida ya Grice (1975) ya namna na ya Lakoff (1973) ya uwazi. Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, kaida hizi zinaweza

kukiukwa ili kukidhi mahitaji ya uso. Kwa mtazamo wa Lakoff (1973), upole ni muhimu katika mazungumzo kwa lengo la kuepuka kumkosea msikilizaji kuliko kutafuta uwazi. Ili kuokoa uso hasi wa msikilizaji na kupunguza ulazimishaji, msemaji analazimika kueleza jambo husika kwa njia ya mzunguko. Kwa mfano wakati mtu anapashwa habari ya kufariki kwa jamaa wake, msemaji anaweza kusema, ‘dunia hii tuliomo, mambo mabaya hutupata ghafla kwa sababu ya kazi zake shetani ...’. Mbinu hii ya kutokuwa bayana imetumika kwa wingi katika *SK*.

Katika kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka), mwasilishaji mkuu wa kipindi anatumia mbinu ya mzunguko kukashifu kitendo cha kufanya mapenzi kwa kutumia sehemu ya mwili ya kuendea haja kubwa. Analalamika:

Kal.

43. *Ngap kasarta age kolenji mureno kwondonyi koba tuwa ‘korutochi chitab kokwet’. Kilenjo kwondo age kilazimishan manong’otionyi kwai kou noto. Ongen tugul ole ‘rutoito ne kibendi kap chitab kokwet’ ko kiptuibotoi nebo magetab Jehovah.*

Kis.

Wakati mwingine mwanamume anaweza kumwambia mkewe ‘**wamtembelee jirani**’. Mwanamke mmoja aliniambia kuwa mumewe alimlazimisha wafanye hivyo. Nyote mwajua kuwa ‘**safari ya kumtembelea jirani**’ ni kitendo ambacho ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

Mfano huo wa 43, unadhihirisha mbinu ya mzunguko kwa uwazi kabisa. ‘Pasta’ Rotich anasema mambo machungu, lakini anatumia mbinu hii ili kuepuka kuwaaibisha mashabiki. Mbinu ya mzunguko inamwezesha kupitisha ujumbe lakini kwa kuwa makini sana asitishie uso wa hadhira yake. Licha ya mzunguko huo wote, ujumbe unafika vizuri.

Mbinu ya maelezo ya kimzunguko ni bayana pia katika kipindi kiki hiki cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka). Winny anaeleza hatua na kiwango cha

kutii. Anasema kuwa wanawake wengi wametii hadi wakapatwa na ugonjwa wa kiharusi. Anaeleza kwamba kuna hatua za kutii na iwapo mambo yatakuwa magumu, mtu asivumilie mpaka afe. Jambo hilo analieleza kimzunguko ifuatavyo:

Kal.

44. *Mochei konai kwonyik kole **makiegu Job mising**. Kiegu sine eng tuguk alak ago chotok ko che imugaksei lakini agot Job ko kiit kowach kot kole kialel nee ne ten ni kot kobiro Kamuktaindet ne te ni? **Kitwegu, makisisei kot 'kityar kitonget**.*

Kis.

Wanawake wanatakiwa kujua kuwa **hawatakikani kuvumilia sana kiasi cha kuwa Ayubu**. Unaweza kuwa lakini kwa mambo yanayowezezana. Ulifika wakati ambapo hata huyo Ayubu alilalama sana kwa kuuliza kile alichomkosea Muumba wake hadi akateseka kiwango kile. **Zungumza, usivumilie hadi 'ugonge kikapu'**.

Ili kuokoa nyuso za wasikilizaji, Winny anatoa maelezo ya kimzunguko humtayarisha msikilizaji kukabiliana na kitendo fulani kinachotarajiwa kutajwa. Msikilizaji huandaliwa mapema kwamba litakalosemwa si kulingana na matarajio yake ya wakati huo. Jambo hilo hufanyika ili kuokoa uso hasi wa hadhira. Iwapo Winny angesema moja kwa moja kuwa wanawake wasikubali kuteswa, wanaume wangekereka na kumwona Winny kama mwalimu mbaya wa wanawake. Pia, wanawake wengine wangemchukulia kuwa mchochezi na kuwa anataka kuvunja ndoa zao. Winny anatomia mbinu hii kupitisha ujumbe ambao ni tatanishi kidogo ili kurahisisha mambo. Mzunguko huu humtayarisha msikilizaji kupokea habari isiyofurahisha.

3.2.6 Kutaja Kitendo cha Kutisha Uso kama Kanuni ya Ujumla

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa, mzungumzaji anaweza kushughulikia tendo la kutishia uso hasi wa msikilizaji kwa kutaja kitendo kinachotishia uso kama kanuni ya jumla au ukweli unaojulikana. Brown na Levinson wanaendeleza kuwa

kutaja kitendo hicho kama kaida ya kijamii kunaokoa uso kwa sababu msikilizaji anachukulia kuwa jambo husika halimhusu yeye binafsi bali wanajamii wote. Katika vipindi vya *SK*, wahusika wanatumia kanuni ya jumla katika mazungumzo yao na wengine kwa nia ya kuokoa nyuso zao hasi. Wahusika wa mazungumzo katika kipindi cha *Amunee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwanamume kuoa mke mwingine), wanadhihirisha mfano mzuri wa matumizi ya ujumla kama kitendo cha kuokoa uso. Winny anasoma arafa ya msikilizaji ‘K’ kutoka Laikipia inayosema,

Kal.

45. *Kamoche amwa ale ii ‘Pasta’, magat konai chepyosok kole muren komenyei orit chepyoso ama eng kot. Mamage kiy goriik che kororon anan ko mbareik che echen anan ko kitandet no irwe ole kemakte ak mutoit no nyigis. Achek kemache kechamech kityo ak keribech, ingen ile makitinye murenik ng’al che tia! Ngap igere muren ne kameto kot neoo nebo koita ak kwo kobaigei ak chepyoso ne menyei kot kitigiin nebo suswek. Kora ko ngap kometo mureno kitandet ne o kot ago tinyei mutoit ne bo kwong’ut ak kwo kosyep rechait eng kap mosoget ne matinyei kiy. Mekwong’e kora kwo baba ipkorip lagokab chito age ak kometo chechiik amu chomyet ne manyor eng gaa, tos mau notok o ‘Pasta?’*

Kis.

‘Pasta’ ninataka kusema hivi, **wanawake** wanatakiwa kujua kuwa mwanamume anaishi ndani ya mwanamke na wala si nyumba. hana haja na vyumba vikubwa, mashamba makubwa au kitanda kikubwa ambacho waweza kulala utakavyo na godoro nzito. Twahitaji kupendwa na kutunzwa tu kwa sababu **sisi** wanaume hatuna mambo mengi. Wakati mwingine unaweza kushuhudia kisa cha mwanamume aliyeacha chumba chake kubwa cha mawe na kwenda kulalia malazi mabaya kwa **mjane** anayeishi katika nyumba ndogo ya nyasi. Aidha, **baba** huyo anaweza kuacha kitanda kikubwa na godoro nzito na kwenda kulalia kitu kichafu kwa mjane asiye na chochote. Pia usishangae anapowaacha watoto wake na kuwatunza wa **mtu mwingine** kwa sababu amekosa upendo nyumbani, ‘Pasta’, si hilo ni kweli?

Katika mfano wa 45, maneno ya kijumla kama vile *chepynosok* (wanawake), *chepyoso* (mwanamke), *muren* (mwanaume), *muren* (mwanamume), *achek* (sisi), *mosoget*

(mjane), *baba* (baba), *lagok* (watoto) na *chito age* (mtu mwingine), yametumika. Maneno hayo hayamlengi mtu maalum binafsi bali yanalenga ujumla wa watu. Kauli kama hizo zinapotumika, wasikilizaji hawajali kwa sababu viwakilishi vya nafsi au majina hayakutajwa wala hakuna aliyenyoshewa kidole. Mbinu hii hutekeleza upole hasi kwa kuokoa uso hasi wa msikilizaji.

Mfano wa pili katika utamkaji wa kitendo kinachotishia uso kama kanuni ya jumla ni katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa). Mwasilishi mkuu wa kipindi anachukua muda mrefu kuzungumzia yale ambayo husababisha kuvunjika kwa ndoa. Kwa kueleza hatari ya kutowajibika kwa wanawake, Rotich anasimulia kisa cha mama mmoja aliyesahau nafasi yake kwa mumewe. Anasema kuwa mama huyo alikuwa na mazoea ya kumwambia msaidizi wa nyumbani ampelekee mumewe maji bafuni. Ilikuwa mazoea kwa msaidizi huyo kumpata mume wa mwajiri wake akiwa amejifunga taulo kiunoni.

Siku moja, huyo mwanamume akaona hakukuwa na sabuni huko bafuni na akamwita mkewe ampelekee. Mkewe akamwamrisha msaidizi wake achukue sabuni bafuni lakini alimpata mume wa mwajiri wake akiwa uchi wa mnyama kwa sababu alitarajia mkewe ampelekee sabuni. Msaidizi wa nyumbani alishtuka lakini yule mzee akamvuta kifuani na kumkumbatia. Yule mzee akamweleza huyo msichana kuwa kwa sababu ameona kila kitu, hakuna ambacho kingewazuia wasikamilishe mapenzi na ndivyo ilivyokuwa. Baada ya siku chache, yule kijakazi alishika mimba na huyo mwanamke alipotaka kumfukuza, mumewe akakiri kuwa mimba ilikuwa yake. Kwa kuwaonya wanawake dhidi ya matokeo kama hayo, Rotich anashauri:

Kal.

46. *Ngamwaiywok kwonyikyok, molen ki malaikainik. Muren ngokakoro kiy ak kocham, ko ui kometo. Kityem cheplakwanotok koiyweis lakini*

maimugak amu kigeer manong'otiondonotok kole ye kakoro kiy age tugul eng bortanyu ko nee ne kang'et!

Kis.

Acha niwaambie **wake zetu, sisi** si malaika. Mwanamume aonapo kitu na kukipenda ni vigumu aachilie. **Kijakazi huyo** alijaribu kuogopa lakini haikuwezekana kwa sababu **mwanamume huyo** aliwaza kuwa iwapo ameona kila kitu mwilini mwangu kilichosalia ni nini!

Maneno *kwoyikyok* (wake zetu), *ki* (tu), *muren* (mwanamume), *cheplakwanotok* (kijakazi huyo), na *manong'otiondonotok* (mwanamume huyo), yametumika katika hali isiyolenga yeyote hasa. Wanawake na wanaume wametambuliwa kijumla ili kuhifadhi nyuso za wasikilizaji wa kipindi husika. Mbinu hii huhakikisha kuwa wahusika katika mazungumzo yoyote yale hawakereki kwa njia yoyote. Hata hivyo wanaupata ujumbe ulokusudiwa.

3.2.7 Kupunguza Ulazimishaji wa Kauli

Ili kutekeleza upole hasi, msemaji anaweza kutumia maneno ambayo hupunguza ulazimishaji kwa msikilizaji wake. Mzungumzaji hutumia kauli hizo ili msikilizaji ahisi kuwa halazimishwi kuupokea ujumbe husika. Katika vipindi vya *SK*, wahusika wakuu wanathibitisha matumizi ya mbinu hii kwa namna kadhaa. Kwa mfano 'Pasta' anapowaomba wasikilizaji wake wasitumie muda mrefu kwa sababu wengine nao wanahitaji kupewa nafasi anasema,

Kal.

47. *Ngasomok anyun ra ale moip kasarta ne koi amu machei chitugul kong'alal.*

Kis.

Acha niwaombe leo kwamba msichukue muda mrefu kwa sababu kila mmoja anahitaji kuzungumza.

Kauli ya msemaji katika mfano 47 inaonyesha kuwa hakuna ulazimishaji wowote. Ni kana kwamba Rotich anawabembeleza wasikilizaji wake. *Ngasomok* (acha niwaombe) ni kauli yenye urai. Iwapo Rotich angewalazimisha wasikilizaji wachukue muda mfupi, wasikilizaji hao wangedhurika kwa madai kuwa uso wao hasi ungekuwa umeingiliwa. Aidha, Rotich kama mwasilishaji mkuu angesababisha wasikilizaji wengine kuacha kuchangia au kuuliza maswali.

Kuokoa uso wa msikilizaji kupitia mbinu ya kupunguza ulazimishaji wa kauli, unadhihirika pia katika muktadha wa kipindi cha *Suupsetab tibik ak kwonyik* (Ubakaji wa wanawake). ‘Koriryo’ anawapongeza kina mama kwa kuwafundisha binti zao hatari za kutembea pekee njiani au mwituni. Anasema kuwa iwapo kuna wakati ambapo wasichana wadogo wamebakwa ni wakati wakiwa pekee yao na labda wakiwa mwituni wakichunga mifugo au kutafuta kuni. Anasisitiza kuwa ni muhimu kumpa mtoto msichana mwenzake wa kuambatana naye ili chochote kikitokea aweze kutoa taarifa kwa wazazi au kwa yeyote yule aliye karibu. Ufuatao ni ushauri wake:

Kal.

48. *Alen kongoi eng kwonyik che kikonet tibiikwak kobendat ak choronokwak che tibiik. Ndemugaksei yekai komagat koba mama ak cheptanyi ui tugul ole atal amu chang bunik. Ngasomook sigik tugul che kwonyiik ale moyokte lagok sanda ko kakoimen.*

Kis.

Ninawashukuru wazazi wa kike ambao wamewafundisha binti zao kutembea na rafiki zao ambao ni wasichana. **Ingewezekana**, mama angeandamana na bintiye kote kote kwa sababu adui ni wengi. **Ninawaomba** wazazi wote wa kike kwamba, msiwatume watoto madukani wakati kumekuwa giza.

Mfano huo wa ushauri wa ‘Koriryo’ kwa wanawake kuhusiana na ubakaji ni mfano bora wa matumizi ya kauli zinazopunguza ulazimishaji wa kauli kwa msikilizaji. Kinyume na kusema kitu dhahiri, Winny anatumia maneno *ndemugaksei*

(ingewezezana) *na ngasomook* (ninawaomba), kuwarai wasikilizaji wamsikie. Hata hivyo, Winny anafaulu kupitisha ujumbe wake muhimu kwa wasikilizaji baada ya kutumia maneno ya kurai. Kupitia kwa hekima yake, Winny anatimiza lengo lake na wakati uo huo kushughulikia nyuso za wasikilizaji wake.

3.2.8 Kudhihirisha Staha/Heshima Baina ya Msemaji na Msikilizaji

Tofauti kihadhi na kimamlaka kati ya msemaji na msikilizaji huhitaji mbinu hii ya kuonyesha staha baina ya wahusika wa mazungumzo. Kaida hii hukubaliana na mawazo ya Leech (1983) kuhusu kanuni ya upole ya kujitweza ambapo mzungumzaji hujidunisha na kumsifu msikilizaji. Lengo hasa la kujitweza na kumsifu msikilizaji ni kuhifadhi uso wake ambao uko kwenye hali ya mazingira ya kuingiliwa.

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kaida hii hudhamiria kuondoa ulazimishaji wa mzungumzaji kwa msikilizaji ili atekelezewe jambo fulani. Mbinu hii hutumiwa wakati msikilizaji ana hadhi ya juu kuliko msemaji. Ni kwa sababu hii ndipo msemaji hawezi kulazimisha kauli kwake kwani msikilizaji anahisi kuwa hadhi yake ni kinga dhidi ya ulazimishaji. Katika vipindi vya *SK*, kaida hii inabainika katika matumizi ya lugha ya wahusika wakuu katika miktadha kadhaa.

Winny, katika kipindi cha *Kolokset eng katunisiet* (Mavazi katika ndoa), anaonyesha staha kati yake na wasikilizaji wake kwa kusema kuwa anajua kati ya wasikilizaji kuna watu walio na hadhi za juu tofautitofauti. Anaeleza kuwa anawaheshimu sana wasikilizaji kwa kuchukua muda wao mkubwa kusikiliza kipindi chao huku akijua wana majukumu makubwamakubwa. Anaendeleza kuwa yeye na mwasilishaji mkuu wa kipindi wana furaha isiyo kifani kwa kusikizwa na watu wakubwa kama wasikilizaji wao. Kwa upole Winny anachangia:

Kal.

49. *'Pasta' Rotich, ingeleis nyolu amwa nitok eng tegisto kot amu kostoikyok alak ko chemogenik eng kapkasi. Kongoi kastoikyok amu angen ale eng kwenung'wong komi **propesaek ak dakitarinik koboto mwalimoek ak ogilini**. Kigonyitok kot mi...ising kastoikyok amu ogasech agot nga o bik che echen. Otestai okwek kou notok amu mwoei baibol kole age tugul ne iming'inigei kekanaptoi.*

Kis.

'Pasta' Rotich, unajua ninasema hili kwa heshima sana kwa sababu baadhi ya wasikilizaji wetu ni wakubwa kazini mwao. Asanteni wasikilizaji wetu kwa sababu ninajua kuwa kati yenu mna **maprofesa, madaktari, walimu na mawakili**. Tunawaheshimu sana kwa sababu mnatusikiliza hata ingawaje mna vyeo vikubwavikubwa. Endeleeni hivyo kwa sababu Bibilia inasema kwamba ajishushaye atakwezwa.

Mfano wa 49 unaonyesha jinsi mbinu ya kuonyesha staha kwa wasikilizaji imetekelezwa. Winny anawajali sana wasikilizaji wake kwa sababu hawajui wote. Matumizi ya majina ya kihonorofiki katika kirai *propesaek ak dakitarinik koboto mwalimoek ak ogilini* (maprofesa, madaktari, walimu na mawakili) yanaonyesha kuwa Winny anawaheshimu wasikilizaji wake. Ana uhakika kuwa baadhi yao ni watu wakuu serikalini na kwokwote wanakofanyia kazi na hivyo ilimpasa awasifu kwa kuwalimbikizia sifa kupitia majina yao ya heshima. Utekelezaji wa upole hasi kwa kuonyesha heshima kati ya wasikilizaji humpa msikilizaji kuhisi vizuri kwani ametambuliwa na msemaji.

Aidha katika mfano uo huo wa 49, Winny anamtambua mwasilishaji mkuu kwa kumwita 'Pasta'. Neno Pasta lina maana ya mhubiri ambaye ni mtumishi wa Mungu katika dini la Kikristo na anawaheshimu sana wafuasi wa dhehebu analosimamia. Hata hivyo, Rotich si kasisi hasa bali alipata jina hilo kutokana na umaarufu wake katika utoaji wa ushauri kwa mambo ya kiroho na asasi ya ndoa. Winny anapotumia jina 'Pasta', anaonyesha kuwa anamheshimu na kumtambua sana mwasilishaji mkuu wa vipindi.

Mfano mwingine wa kuonyesha staha kati ya msemaji na msikilizaji ni katika kipindi cha *Kasarta ne kibete lol* (Wakati wa kupeana talaka). ‘Pasta’ anatoa ushauri kwa wanaume wanaotoka nje ya ndoa lakini kwa kuwatambulisha kwanza kihadhi. ‘Pasta’ anasema:

Kal.

50. *Achame aweekyi kongoi manong’otoik tugulche kikosoman. Maraisi somanet sinyen Winny kou ole iptoi alage.*

Kis.

Ninapenda kuwashukuru **wanaume wote waliosoma**. Kusoma si rahisi kama vile wengine wanavyochukulia.

Kupitia kwa mfano 50 hapo juu, kirai *manong’otoik tugul che kikosoman* (wanaume wote wasomi) inaonyesha kuwa Rotich anawajali sana wasikilizaji wake kwa kuwatambua wanaume waliosoma. Licha ya kuwa anawaonya dhidi ya utamu wa mapenzi nje ya ndoa, anafanya hivyo kwa kutanguliza usemi wenye kuwasifu. Hali hii imesababishwa na ukweli kuwa wasikilizaji wa vipindi hivi vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM* ni wa viwango tofauti kihadhi. Utekelezaji wa mbinu ya kuonyesha staha kati ya wahusika wa mazungumzo ndiyo sababu mojawapo ya vipindi hivi kuendelea bila kukatika.

3.3 Mkakati Ndani ya Rekodi

Mkakati ndani ya rekodi hutumika wakati msemaji ana mamlaka ya juu kuliko msikilizaji. Hutumiwa na wanajamii wanaofahamiana vizuri au kuwa na uhusiano wa namna fulani. Mkakati huu hutumika kwa mapana katika mawasiliano ya kila siku. Brown na Levinson (1987) wanasema kuwa mkakati ndani ya rekodi hufuata kanuni za utaratibu wa mawasiliano kama anavyoeleza Grice (1975). Kutokana na msingi huu, mzungumzaji anapaswa kuzungumza kwa namna ya moja kwa moja na kwa

uwazi zaidi ili kuzuia utata wowote katika usemi wake. Hii ina maana kuwa kauli zinazotumiwa ni fupi, huhusiana na mazungumzo, hazina habari zaidi ya zinazohitajika na kwamba hazina utata.

Wakati wa kutumia mkakati huu, la muhimu kwa msemaji ni kuwasilisha ujumbe wala si kujali mahitaji ya uso wa msikilizaji. Mkakati ndani ya rekodi hutumika zaidi wakati wa kushughulikia jambo la dharura. Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa wakati msemaji anataka kumshughulikia msikilizaji labda kwa jambo la dharura, anaacha kushughulikia mahitaji yake (msikilizaji) ya uso na kutumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Yafuatayo ni mazingira yanayohitaji matumizi ya mbinu ya kuwa kwenye rekodi kama yalivyobainika katika vipindi vya *SK*.

3.3.1 Wakati Washiriki wa Mazungumzo Wanahusiana kwa Karibu

Mazingira ya mawasiliano baina ya watu wenye uhusiano wa karibu hudhihirika katika mazungumzo baina ya wanafamilia, mahirimu, marafiki au watu ambao wamefahamiana kwa muda mrefu. Kwa msingi huu, msemaji halazimiki kutumia kauli zote zenye kuhifadhi uso wa msikilizaji. Hii ni kwa sababu ya mahusiano yao yanayowaruhusu kuamrishana, kutumana na kuagizana bila upande mmoja kuhisi vibaya.

Katika kipindi cha *Amunee che ipchin kitun kwondo age* (Sababu za kuoja mke mwingine), Rotich na Winny wanadhihirisha uhusiano wao wa kirafiki. Uhusiano huu unatokana na mtagusano wao wa kila Jumatano wanaposhirikiana kupeperusha vipindi vya *SK*. Mazungumzo baina yao yanaonyesha kuwa hawaogopani wala kuzingatia sana mipaka kati yao. Rotich anahitaji maji na anatumia maneno ya kawaida kuhakikisha kuwa amepata maji kutoka kwa Winny, kwa kusema:

Kal.

51. *Inagaa beek Winny, ngashokwama meel buch, iboru kole koromen ra ng'alek che kemwoe.*

Kis.

Winny, nipe maji, sijui mbona kiu kimenianzia leo mapema, inaonekana mambo tutakayoyasema leo ni muhimu.

Kutokana na kauli katika mfano 51, kirai *'inagaa beek* (nipe maji) ni amrifu. Hata hivyo, msikilizaji hachukulii kuwa ameamrisha na msemaji. Anaona kuwa ni kawaida kwao kuzungumza hivyo kwa sababu ya uhusiano wao. Iwapo amri hiyo ingeelekezwa kwa mtu mwingine asiyehusiana na Rotich kwa ukaribu, kwa mfano mtu ambaye hajawahi kukutana naye, ingekuwa tishio kwa uso wa wake.

Mfano mwingine wa mahusiano ya karibu ni katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiyet* (Vitu vinavyovunja ndoa). Rotich anazungumzia jinsi wanawake wanawasumbua waume zao wakati wa kujamiiana. Rotich anaeleza kuwa wengi wa wanawake walikuwa wakipitia dirishani walipokuwa wasichana kwenda kuwatafuta wapenzi wao. Analalama kuwa anashangazwa na wao kwa sababu walipopewa kibali cha kuishi na kufurahia maisha ya ndoa, wao huwasumbua waume zao. Winny na Rotich wanaonekana kutofautiana kidogo kwani Rotich anataka kuwa wazi zaidi kwa kutaka kufafanua kwa undani. Kwa kumkanya Rotich, Winny anasema:

Kal.

52. *Acha matimwa, kot ko matataimwaa mising. Ingen ile achek biikab Kalenjin ko ki kiptagurin matakichame tugun che king'anyei mising. Metoe yotok si konachigei chi kityo.*

Kis.

Hapana, usiendelee kusema sana. Unajua sisi Wakalenjin ni wastaarabu na huwa hatupendi mambo yanayofunuliwa zaidi. Achia hapo ili kila mmoja ajing'amulie.

Mfano 52 unadhihirisha uhusiano uliopo baina ya washiriki wa mazungumzo. Maneno yaliyotumiwa ni tisho kwa nyuso za watu ambao mahusiano yao si ya karibu. Matumizi ya maneno *achicha* (hapana) na *'matataimwa'* (usiendelee kusema) yanasikika kuwa amrifu lakini kwa walio na uhusiano wa karibu au waliozoeana ni maneno ya kawaida tu. Rotich hahisi kukereka kwa sababu wamezoeana na Winny na kwa hivyo sentensi amrifu hizo ni kama utani tu.

3.3.2 Katika Mazingira ya Dharura

Mkakati ndani ya rekodi hutumika wakati kuna dharura. Jambo hili la dharura huwa ni la kumfaidi msikilizaji. Katika kutumia mbinu hii, lengo kuu la msemaji ni kumtahadharisha msikilizaji kutokana na jambo linaloweza kumdhuru na hivyo hana haja ya kuzingatia upole kwani anayefaidika ni msikilizaji. Mkakati ndani ya rekodi katika mazingira ya dharura ulidhihirika kwenye vipindi vya *SK*.

Kwenye kipindi cha *Tetetab sigisiet* (Mpango wa uzazi), mwasilishaji mkuu wa kipindi anatoa maonyo kwa wazazi wanaopenda kuzaa watoto bila mpango. Ushauri wake anautoa bila kuzunguka kandokando hivi:

Kal.

53. *Ngamwaiywok iman bikyok, ongemwee atebet ne makichalani tugun. Machei ngemwa ng'al ko matkeegu chebo let kisuldoe. Amu nee si ngemwa kele ngotet biik sigisiet keib kou yo kakile ongeiye ketesage? Ngateiywok, mongeiye kot koi chepkildet amu agoi kotemenech ripseetab lagok.*

Kis.

Acheni niwaambie ukweli, **tukimbie** tabia ya kutojali. Tunahitajika kuwa watu wasiokuwa wa mwisho kutimiza jambo linalosemwa. Mbona inaposemekana kuwa watu wapange uzazi tunachukulia kana kwamba tumeambiwa tuzae na kuongezeka? Mausia yangu ni kwamba, **tusizae** hadi 'kidole kidogo' pia kizae kwa sababu ulinzi wa watoto utatushinda.

Kupitia kwa mfano wa 53, Rotich anawatahadharisha wasikilizaji wake moja kwa moja bila kupitia kando. Anafanya hivyo ili watilie maanani upangaji wa uzazi. Asemapo *kot koi chepkildet* (hadi kidole kidogo pia kizae), Rotich anamaanisha kuzaa bila mwisho au hadi pale uzazi utakapokatika. Hakwepi kwa lolote lile bali anatumia maneno yaliyo wazi na bayana. Maneno kama vile ‘*ongemwee*’ (tukimbie) na ‘*mongeiye*’ (tusizae) ni makataa ya moja kwa moja. Anapotoa tahadhari hiyo, Rotich hajishughulishi sana na uhifadhi wa uso wa msikilizaji kwa sababu anayefaidika ni huyo msikilizaji. Hata hivyo, anatumia usemi unaomjumulisha na wasemezwa kwenye kikundi kimoja. Hapa ndipo tunapata mwingiliano kati ya mikakati miwili, ya upole chanya na ya kuwa ndani ya rekodi

Kutoa maonyo au tahadhari ni kama kumshughulikia msikilizaji. Msemezwa anapata hisia kuwa msemaji anamjali wala si kumwamrisha. Iwapo maneno kama hayo yangetumiwa katika mazingira yanayomfaidi msemaji, msemezwa angehisi vibaya na hivyo uso wake kuathirika. Hali ya kutaja kitendo kinachotishia uso kama kauli ya kumfaidi msikilizaji ni mbinu tosha ya kutekelezea mkakati ndani ya rekodi.

3.3.3 Wakati Msemaji na Msikilizaji Wanatofautiana Kimamlaka

Katika mazingira ambapo msikilizaji na msemaji wanatofautiana kimamlaka, mkakati ndani ya rekodi hutumiwa kama mbinu ya kutimiza na kudumisha mawasiliano. Mbinu hii ni mwafaka kwa msemaji na msikilizaji wanaotenganishwa na hadhi au uwezo fulani. Msemaji aliye na hadhi au mamlaka makubwa kuliko msikilizaji, ana uwezo wa kumwamrisha mdogo wake ambaye kwa muktadha huu ni msikilizaji. Lengo la mawasiliano katika muktadha huu ni kuwasilisha ujumbe bila kujali hali ya uso wa hadhira. Hii ni kwa sababu yule anayezungumza hatawaliwi na kaida ya

kutakiwa kujizuia kwa namna yoyote. Mbinu hii ilibainika katika vipindi vya *SK* kupitia mifano ifuatayo.

Katika kipindi cha '*Korgetabyugoi ak kamatisiek*' (Wakwe katika ndoa), mwasilishaji mkuu wa kipindi anadhihirisha tofauti za kimamlaka anapoangazia namna mama mkwe anadhihirisha uwezo wake mbaya dhidi ya mkazamwana. Rotich anadai kuwa chanzo cha kuvunjika kwa ndoa nyingi ni mama mkwe. Anahadithia kisa cha msichana aliyelazimishwa na mama mkwe kumnyima mumewe tendo la ndoa, kwa ufupi anasema:

Kal.

54. *Kimwawolakwetabchi kole ii Winny ak kostoikyok tugul, kale kilenji kogo koyan kotuiyo ak manong'otionyi agenge eng arawa. Ko kingatebe ngo kiisub kounotok ko kile kwonyoto kiiyai kou notok amu kimakotinyei kamug'o ine amu ki korom korgrtabyugoi.*

Kis.

Winny na wasikilizaji wetu wote, msichana huyo aliniambia kuwa mama mkwe alimwamrisha kukutana na mumewe mara moja kwa mwezi. Nilipomwuliza kama alifuata masharti hayo akakubali kuwa alifanya hivyo kwa sababu **hakuwa na uwezo juu ya mama mkwe.**

Kutokana na mfano 54, tofauti kati ya mamlaka na uwezo ni dhahiri ndani ya hadithi iliyosimuliwa na Rotich. Mama mkwe alikuwa na uwezo mkubwa dhidi ya mkazamwana na kwa hiyo alimwaamrisha. Mfano huo unaonyesha kuwa tofauti za kimamlaka ulimkandamiza msichana huyo. Amri aliyoitoe mama mkwe ilitokelezwa kwa sababu ya tofauti za kiumri/kimamlaka kati yake na msemzwa. Hii ilitokana na hisia za mama mkwe huyo kuwa ndiye mkubwa na mwenye uwezo mwingi kuliko binti huyo.

3.4 Mkakati Nje ya Rekodi

Katika utekelezaji wa mkakati wa upole nje ya rekodi, msemaji huwa hawasilishi ujumbe wake kwa msikilizaji kwa njia wazi au ya moja kwa moja. Kitendo huwasilishwa kwa namna ambayo si rahisi kuhusisha lengo au maana moja mahsusi na usemi husika. Kwa msingi huu, mzungumzaji hutumia maneno au kauli zinazodhamiria msikilizaji kudokeza lengo au maana iliyokusudiwa. Mkakati nje ya rekodi humpa msikilizaji nafasi kubwa ya kufasiri anachokusudia msemaji. Kwa hivyo, msemaji wa kitendo ana nafasi mkubwa wa kujikinga iwapo fasiri litaonekana kumdhuru msikilizaji. Mkakati huu una misingi yake katika uelewa na ufasili wa maana ya msikilizaji katika kufafanua kinachosemwa.

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), mkakati nje ya rekodi unakabiliwa na hatari ya ufasili potovu wa maana. Hii inatokana na sababu kuwa msikilizaji anakisia maana kutokana na usemi wa msemaji usio wa moja kwa moja. Wataalam hawa wanaendelea kufafanua kuwa, mkakati huu huzivunja kaida za utaratibu wa ushirikiano kama zinavyoelezwa na Grice (1975). Kwa msingi huu, msikilizaji hutarajiwa kuwa na elimu-awali au uelewa wa kile kinacholengwa na msemaji hasa kwa kurejelea kwa kina vidokezo katika kauli ya msemaji. Vipindi vya *SK* vimedhihirisha matumizi ya mbinu mbalimbali zinazotumiwa wakati wa kuokoa uso hasi kwa kutumia mkakati nje ya rekodi ifuatavyo:

3.4.1 Kutumia Maelezo Pungufu

Mara nyingi, maelezo pungufu yana utata mwingi. Kwa msingi huu, msemaji huzua kauli fulani yenye maana mbalimbali kwa msikilizaji na kumwachia msikilizaji kujitafutia maana lengwa. Kwa kutumia mbinu ya maelezo pungufu, msikilizaji anakusudia kuokoa uso wa msikilizaji. Katika kipindi cha *Kolokset eng katunisiet*

(Mavazi katika ndoa), Rotich anaeleza kuwa kusudi la kuvaa mavazi ni kusitiri uchi wa mwanadamu. Anatumia mfano katika Bibilia wa wakati Adamu na mkewe Hawa walipolila tunda lililokatazwa na Mungu na kujipata uchi. Anaeleza kuwa walijificha kwa sababu walijua kuwa utukufu wa Mungu ulikuwa umetoweka na wakajiona uchi. Mungu aliwatengezea mavazi kutoka kwa ngozi ya kondoo ili wasione aibu tena. Rotich anatumia mfano huo kuonyesha kuwa binadamu hakukusudiwa kutembea uchi. Anaeleza:

Kal.

55. *Kima ko magetab kipsengwet kobendat biik ach ngor, notok amu nee si kotuch Kamuktaindet biik che tai eng kabungutab **Eden. Ngoboru inye..ee kole meguitos biik kole mamagat keryokyi tugun che tounen.***

Kis.

Hayakuwa mapenzi ya mbingu wanadamu kutembea uchi, hiyo ndiyo sababu Muumba aliwavika mavazi watu wa kwanza katika shamba la Edeni. **Inaoneka...naaa** watu hawafahamu kuwa hatupaswi kukimbilia mambo mapya.

Katika kauli hii, msemaji hataki kusema moja kwa moja kuwa baadhi ya wasikilizaji hawapaswi kuvaa kama wafanyavyo. Kwake, kuvaa vizuri au kusitiri mwili ni mapenzi ya mbinguni na anatoa hoja zake kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili msikilizaji asije akakereka. Badala ya kutaja mambo moja kwa moja, anatumia kirai *ngobaru inye kole* (inaoneka...naa) kutoa kijisababu cha watu wengine kuvaa vibaya. Mkakati huu unalenga kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji.

3.4.2 Matumizi ya Vidokezo

Mbinu ya kutoa vidokezo ili kumwelekeza msikilizaji ni njia nyingine muhimu ya kutekeleza mkakati nje ya rekodi kwa makusudi ya kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji. Vidokezo hivyo vitamwelekeza msikilizaji kung'amua lengo la msemaji na kumshughulikia. Kwa mfano katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu

vinavyovunja ndoa), Winny anaeleza kuwa wanawake Wakalenjin hawana ujasiri wa kudai au kuuliza mapenzi kwa waume zao moja kwa moja bali hutumia mifano ya watu wengine au ‘kuwapiga teke’ waume wanapotaka kulala. Anasema:

Kal.

56. ***Mabotech ‘Pasta’ Rotich, achek kwonyik ‘Wakale’ ko makimugune tebsetab ngalechoto bo kitanda.*** *Ngemache kityortoi kityo kolen chito ketuchegei lakini ndepkogas nebo aeng konai kiit ne kemache. Imuch kong’et agot kwondo ak komwochi manong’otionyi agobo kwony ne cham ngomanagat ‘koamei rubet’ mising tamangap konai manong’otionyi kole kamochei katuiyetab katunisiet.*

Kis.

Sio kosa letu ‘Pasta’ Rotich, sisi wanawake ‘Wakale’ hatuwezani na mambo ya kuuliza wazi wazi mambo hayo ya kitandani. Wakati mwingine tunapohitaji, tunatupa mateke tu kitandani na mzee labda akafikiria unajifunika. Likifanyika mara ya pili, atajua unachohitaji. Njia nyingine ni mke kumsimulia mumewe kisa cha mwanamke ambaye akiwa mjamzito ‘huhisi njaa’ sana kwa makusudi ya mumewe kuelewa anahitaji kitendo cha ndoa.

Mfano huo wa 56 unaonyesha jinsi wanawake wa Kikalenjin wanachukulia mambo ya kuuliza mapenzi kuwa mwiko. Licha ya masomo na kubadilika kwa nyakati, ni nadra sana kumpata mwanamke wa lugha husika akimwuliza mumewe ampe mapenzi. Winny anatumia kidokezo *mabotech ‘Pasta’ Rotich, achek kwonyik ‘Wakale’ ko makimugune tebsetab ngalechoto bo kitanda* (sio kosa letu ‘Pasta’ Rotich, sisi wanawake ‘Wakale’ hatuwezani na mambo ya kuuliza wazi wazi mambo hayo ya kitandani) kutanguliza usemi wake. Kidokezo hiki kinampa msikilizaji nafasi ya kujiandaa kupokea ujumbe unaotishia uso bila kukereka.

3.4.3 Kutumia Maswali ya Balagha

Katika kuokoa uso wa msikilizaji, msemaji anaweza kutumia maswali ambayo hayahitaji majibu. Kusudi la mzungumzaji kutumia maswali ya balagha sio tu kuokoa uso wa msikilizaji husika bali hata kusisitiza au kutilia mkazo kile

kinachozungumziwa. Maswali ya balagha humwachia msikilizaji nafasi ya kuelewa kwa undani kile alichokusudia msemaji. Matumizi ya maswali ya balagha yamebainika kwa wingi katika vipindi vya *SK*.

Anapofafanua mpango wa kando kama sababu mojawapo ya kuvunjika kwa ndoa nyingi, Rotich anatumia mfano mzuri wa msaidizi wa nyumbani ambaye alikuwa akitafuta kazi kwa yule aliyekuwa mpenzi wake katika siku za ujana. Anampa mwanamume huyo jina la *X* na msichana jina *Y*. Kwa sababu ambazo hazikuwezekana, hao wawili hawakuoana. *Y* alikosa mume na akapata mtoto wa mwanamume huyu ambaye hakumwoa. *X* alimpata mke msomi kwa sababu hata yeye alikuwa msomi lakini mwishowe kisomo kile hakikuzuia vikwazo vingi katika ndoa yao.

Baada ya siku nyingi, *Y* na *X* walikutana mjini na wakakumbushana penzi lao. Kwa vile *Y* alijua udhaifu wa wanaume, alitumia ujanja wake wa kumbusu *X*. *X* alikumbuka na kutamani siku zile za awali walipopendana na baada ya maongezi ya muda mfupi walibadilishana nambari za simu. *X* alikuwa akimpatia *Y* fedha za kujisaidia mara kwa mara. Siku chache baadaye, *X* alianza kulalamika kwa mkewe kuwa msichana aliyekuwa akiwasaidia alikuwa mkali kwa watoto. Mama watoto kusikia hivyo akakubali pendekezo la mumewe la kumwachisha kazi na *X* akaahidi kumsaidia kutafuta msaidizi mwingine bila kudokeza kuwa alikuwa na mtu akilini.

Majuma mawili yalipoisha, *Y* aliajiriwa kwa *X* na mapenzi yao yaliendelea kama kawaida. *Y* akaonekana mwema sana hadi mkewe *X* akawa akimwachia watoto na kwenda shughuli zake za biashara hata kwa juma zima bila kurejea nyumbani. Ikawa ni kawaida kwa *X* kumsifu *Y* kwa mkewe kuwa yu mkamilifu. Baadaye *X*

alipachikwa mimba na X na mkewe alipofunguliwa macho mtoto alipozaliwa, mambo yalikuwa balaa. Pasta anasema:

Kal.

57. *Ongemwa iman yutok anyun Winny, ngiwendi inye kabisa wikit msima ilen kemetochi ng'o boiyot? Auiyo kituiyo kimagetiet ak artet ak kenyor tugul kochamegei?*

Kis.

Winny, tulizungumzie hili sasa, **unapoenda kwa muda wa juma zima utakuwa umemwachia nani mumeo? Ni lini fisi na mbuzi wameachwa pamoja kisha wakapatikana wakiwa salama?**

Kwa kuwa maswali yaliyotumiwa katika mfano wa 57 hayahitaji majibu, wasikilizaji wanapata fursa ya kujing'amulia mambo bila kuashiriwa moja kwa moja. Uso wa msikilizaji unatunzwa kwa sababu hatagharamika kutolea majibu maswali hayo. Kwa kusisitiza kutowajibika kwa wanawake kuhusiana na jambo hilo, Rotich katika kipindi hicho cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa) anatumia maswali ya balagha kusisitiza mawazo yake ifuatavyo:

Kal.

58. *Chepkametisikeyuk, tos mongen okwek iman ole muren ko mebwoti konyil aeng ngiborchi chomnyet anan koro 'opportunity'? Anan olen memugaksei amu cheplakwet? Olen tangoita ngalechu is? Ng'o ne mengen, ng'o iman ne meguitos kole makimetochin lakwet sugaruk eng ole ityin ak kelenji mat aitu ko keam sugaruk kininen? Moberbergei kwonyichu kaigai ngasomok, tos mongen okwek ole anyiny kiy ne kechorei, ne maneg'ung'i? Ongen is ole mautie moset katwalet!*

Kis.

Dada zangu, si hata ninyi mnajua kuwa mwanamume hafikirii mara mbili anapoonyeshwa mapenzi au aonapo 'mwanya'? Ama mnafikiria haiwezekani kati yake na msaidizi wa nyumbani? Mnafikiria mambo haya ni mchezo ee? Ni nani asiyejua, kwa kweli ni nani asiyelewa kuwa haiwezekani kuweka sukari anakofikia mtoto kisha kumkanya asithubutu kuilamba? Nawaomba wanawake msijidanganye tafadhali, je hamjui kuwa

kile kinachoibwa, kisicho chako ni kitamu? Mnajua nini, nyani hasahau kuruka kwake.

Kupitia kwa mifano ya 57 na 58, tunaona kuwa Rotich ametumia maswali ya balagha kuokoa uso wa hadhira yake na pia kisisitiza suala la mada husika. Kwa usemi mmoja, Rotich ametumia maswali mengi ya balagha na hii imekuwa mbinu mwafaka aliyotumia kuwasilisha hoja yake kuu ambayo ni kuwaonya kina mama dhidi ya kuwaamini sana wafanyi kazi wa nyumbani. Ni mbinu ya kuhakikisha kuwa wasikilizaji wamechukulia kwa uzito kile ambacho kinasemwa.

3.4.4 Udondoshaji wa Kauli

Udondoshaji au kusema kauli zisizo kamilika ni njia nyingine ya mkakati nje ya rekodi. Mbinu hii inalenga kuwa msemaji asikamilishe usemi wake iwapo anajua utatishia uso wa hadhira lengwa. Kulingana na Brown na Levinson (1987), msemaji anapaswa kumjali msikilizaji wake na atafanya hivyo tu kupitia uteuzi wa maneno yake kwa ufasaha au kudondosha sehemu za usemi ambazo zinaweza kumkera msikilizaji. Usemi kama huo huwa unaonyeshwa kimaandishi kwa kutumia alama za dukuduku.

Katika kipindi cha *Korgrtabyugoi ak ingamatisiek eng katunisiet* (Mashemeji katika ndoa), Rotich anafafanua kisa cha binti mmoja aliyeolewa na mwanamume aliykuwa mwana wa kipekee kwao. Rotich anasema kuwa binti huyu aliposhika mimba, akawa na matamanio kama ya wanawake wengine. Alikuwa anapenda sana matunda ya kila aina na soda aina ya 'sprite'. Kila jioni, mumewe alikuwa akimletea vitu hivyo na kumpa kwa furaha. Furaha hiyo ilikatika punde tu mamake mvulana alipoona hayo na alipogundua kuwa huyo binti alikuwa na mimba. Mama mkwe alimfumania huyo msichana akiwa na mumewe na kumtusi kuwa alipata mimba mapema na kwamba

kuna uwezekano aliibeba kabla ya ndoa. Sio hilo tu, mamake mvulana aliendeleza kuwa mimba hiyo haikuwa ya mwanawe.

Ili kupata hifadhi, yule binti aliegemeza kichwa chake kwenye kifua cha mumewe lakini ghafla akapata kichapo mgongoni. Kwa bahati mbaya, yule mwanamume alipoinuka kukabiliana na mamake, mkewe akaanguka na kuumizwa na jiwe tumboni. Msichana huyo alipolalama kuwa alikuwa anahisi uchungu mwingi, mama mtu alijitoa kumpeleka hospitalini kwa kizingizio kuwa hizo zilikuwa shughuli za wanawake. Walipofika njiani, yule binti akamlalamikia mama mkwe kuwa alihisi uchovu na alimrai watafute gari ili liwabebe. Mama mkwe alimkemea kwa kuteta kuwa alikuwa na mpango wa kumfilisisha mwanawe. Yule msichana alishindwa kutembea na mara mama mkwe akakasirika na kumchapa sana. Mimba ilimtoka yule binti na cha kustaajabisha, mama mkwe alisheherekea. Rotich anatumia udondoshaji anaposema:

Kal.

59. *Mutyo bikyok, wooui mutyo ne bo iman, mutyo eng chebo chi ne kimakongen kole ketun korgetabyugoi ak werit. Kastoikyok, ngateb as ale ii, aisuru, ngotebi, mamache amwa amu tos amwa tugun che yaach. Kalya yegai*

Kis.

Jameni ninasema pole, wooui pole kabisa, pole kwa binti wa watu ambaye hakujua kuwa ameolewa na mtu na mamamtu. Wasikilizaji wetu, niulize hivi, aidhuru acha tu, sitaki kusema kwa sababu huenda nikasema vibaya. **Sasa, mbona**

Kupitia mfano huo, Rotich anadondosha maneno ambayo yangemletea shida. *Kalya yekai....* (sasa mbona) ni sehemu ya mwisho ya usemi wa Rotich inayothibitisha udondoshaji. Udondoshaji huu umefanyika ili kuepuka kutamka maneno ambayo labda yangedhihirisha kukereka kwa msemaji lakini anatumia udondoshaji kuzuia matamshi mengine. Mbinu hii ni mwafaka katika utekelezaji wa udondoshaji. Pia, anakata usemi wake kwa nia ya kuwajali wasikilizaji.

3.3.5 Matumizi ya Kejeli yenye Ucheshi

Kadhalika, mkakati wa kutumia kejeli yenye ucheshi hubainika lakini kwa namna chanya. Mkakati huu unaoana na mawazo ya Leech (1983) kuhusu matumizi ya kinaya. Leech anaeleza kuwa, mzungumzaji anaweza kuwasilisha ujumbe hasi kwa msikilizaji kwa kutumia lugha ambayo haidhihirishi uhasi kwa njia ya moja kwa moja. Kwa mfano, mwanafunzi aliyefeli mtihani anaweza kuambiwa hakufeli sana ikitiliwa maanani kuwa yeye hufanya vizuri kwenye spoti kuliko masomo. Kejeli itabainika tu katika kauli hii iwapo mwanafunzi husika si mwanaspoti. Hivyo basi, mkakati huu hutumika katika uwasilishaji wa kauli zenye dhihaka.

Matumizi ya kejeli yalibainika katika kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka). Rotich anafafanua nafasi ya mwanamke katika mchakato wote wa kupeana talaka. Anawaeleza wasikilizaji kuwa si jambo la busara kwa wanawake kukimbilia talaka wanapoulizwa na waume zao. Anatoa sababu kwamba mwisho wao ndio huumia. ‘Pasta’ Rotich anatumia kejeli kuwakosoa wanawake kama hao kwa kusema:

- Kal.**
60. *Ingen nee Winny, ng’omen chepyosok cho ruochin besiet nebo kwangut, ee ng’omen akinye. Kelen berber iman biik che kikoba Beijing ndaweek nyokobarchigei kechop ng’atutik che keerei magutikwak ii!*

Kis.
 Winny, unajua nini, wanawake wanaokimbilia talaka ni werevu sana, **ee ni werevu kweli. Unafikiria ni wajinga kweli** watu walioenda Beijing na waliporudi wakupigania kuwekwa kwa sheria inayojali maslahi yao!

Mfano huu unaonyesha jinsi msemaji amefaulu kupitisha ujumbe wake kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Rotich anawaonya wanawake dhidi ya kukimbilia talaka kwa sababu watapata hasara. Kisha, ‘Pasta’ anatumia kejeli kuwasuta wanaofanya hivyo

lakini anakwepa, kwa kutumia kinaya kuwa wao ni werevu. Mbinu hii inaokoa uso wa msemaji na zaidi ni msikilizaji kwa sababu hawatachukuliana makosa.

3.5 Hitimisho

Sura ya tatu imeangazia kategoria za mikakati ya upole katika vipindi vya *SK*. Uchanganuzi umefanyika kwa kutumia mifano maridhawa kuonyesha jinsi mikakati hiyo ya upole imetumika katika vipindi teule. Imebainika kuwa vipindi hivi vya *SK* vimetumia mikakati anuwai ya upole kufanikisha mazungumzo kama ilivyoangaziwa na Brown na Levinson (1987). Ufafanuzi wa jinsi kategoria za mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi, mkakati wa kuwa ndani ya rekodi na mkakati wa kuwa nje ya rekodi hutumiwa na wahusika wa mazungumzo ya *SK* kushughulikia nyuso zao umefanyika kwa kina.

Vipindi vinane vya *SK*, vilivyotumika katika uchanganuzi wa upole vimeonyesha jinsi msemaji anaweza kushughulikia uso wake na uso wa msikilizaji. Kupitia kwa nadharia ya uso, tumeona jinsi ambavyo msemaji anaweza kutumia mbinu tulizozitaja ili kuwasilisha ujumbe wake. Kwa kufanya hivyo, msemaji atakuwa anahifadhi uso wake na wa msemazwa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa katika mazungumzo yoyote yale, uso wa mhusika yeyote huweza kuathirika. Mikakati hiyo imefafanuliwa kwa misingi ya nadharia ya upole ya uso na kile kinachokubalika kama upole katika jamii ya Wakalenjin. Sura inayofuata ni uchanganuzi wa athari za uzingatiaji na ukiukaji wa mikakati ya upole katika vipindi vya *SK*.

SURA YA NNE

ATHARI ZA UZINGATIAJI NA UKIUKAJI WA MIKAKATI YA UPOLE KATIKA VIPINDI VYA *SOBETAB KAPCHI*

4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia aina nne za mikakati ya upole. Mbinu za kutimiza mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi, mkakati ndani ya rekodi na mkakati nje ya rekodi zimejadiliwa kwa upana. Aidha mkakati wa tano, wa kutosema kabisa jambo linalotishia uso wa msemaji umeelezwa kwa ufupi. Mikakati hiyo huhitaji kuzingatiwa ili kukuza uhusiano mzuri baina ya washiriki wa mazungumzo. Wakati mwingine, wazungumzaji huweza kukiuka matumizi ya mikakati ya upole kwa sababu moja au nyingine. Kutokana na hali hiyo, sura hii inaangazia athari zinazojitokeza wakati wazungumzaji wanazingatia au kukiuka mikakati ya upole katika vipindi husika vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*.

Brown na Levinson (1978) ambao ni waasisi wa Nadharia ya Upole, wanadai kuwa mtu anapozungumza anafaa kuwa mwangalifu ili asimuudhi au kumuaibisha msikilizaji. Wanasema uso hasi na uso chanya wa msikilizaji unafaa kuhifadhiwa. Kwa kushadidia mawazo hayo ya Brown na Levinson, Grice (1975) anaibuka na kanuni ushirika ambayo anaigawa katika kaida nne. Anatumia kaida hizo kuonyesha jinsi msemaji anafaa kuwa mwangalifu ili kukuza maelewano na uhusiano mzuri wakati wa mawasiliano. Kaida hizi ni: kaida ya kiasi, ubora, uhusiano na kaida ya namna. Kama tulivyodokeza katika sura ya pili, kaida ya kiasi inasema kuwa mtu anapozungumza asitumie maneno mengi ambayo hayaongezi umuhimu wowote kwa anayosema. Kaida ya ubora inasema kuwa msemaji anafaa kusema jambo ambalo ana uhakika nalo, wala asiseme jambo ambalo hawezi kulithibitisha. Kaida ya uhusiano

inasema kuwa mzungumzaji asiseme mambo ambayo hayahusiani na mada ya mazungumzo. Nayo kaida ya namna inasema kuwa jambo linalosemwa liwe wazi ili msikilizaji asitatanike kupata maana iliyokusudiwa na msemaji.

Sura hii, inapambanua athari zinazoibuka wakati wahusika wa mazungumzo katika vipindi vya *SK* wanazingatia au kupuuza mikakati ya upole. Tumeangazia athari hizo kwa uwazi kupitia uchanganuzi wa sehemu za mazungumzo ya wahusika ili kutoa maelezo kamili.

4.1 Athari za Uzingatiaji wa Mikakati ya upole

Kama inavyohibitika katika sura ya tatu na nne, wahusika katika mazungumzo ya *SK* wamejaribu sana kutumia mikakati ya upole wanapowasiliana. Hali hii inatokana na sababu kwamba wahusika hao ni wa umri tofauti, hadhi na mamlaka tofauti, jinsia tofauti na hali za kiuchumi tofauti. Uzingatiaji wa mikakati ya upole una athari kadhaa katika mazungumzo ya *SK* kama ambavyo tumeeleza katika sehemu ya 4.1.1.

4.1.1 Kukuza Heshima Baina ya Wahusika wa Mazungumzo

Kila mja huhitaji sana kuheshimiwa na wenzake. Kuna uwezekano kuwa wakati wa mazungumzo, mzungumzaji huweza kumkwaza msikilizaji kupitia kwa usemi wake. Hali hii hutokana na usemi au maneno ambayo yanaudhi. Watu wanapotumia maneno kama hayo hukoseana heshima na hiyo husababisha mlahaka mbaya kati yao. Ukawaida wa maisha ya kila siku ni pamoja na mchakato wote wa mahusiano ya binadamu ambao huenda sako kwa bako na lugha ya heshima.

Lugha ya heshima ni kipengele muhimu sana cha utamaduni, tabia na mazungumzo yoyote yale. Mahusiano ya kijamii na kaida za tabia njema hutegemea sana lugha ya heshima. Kaida za kiheshima zimefichwa ndani ya misemo, methali, vitendawili na

virai teule. Ili kukuza na kudumisha heshima baina yao, wahusika katika mazungumzo ya *SK* wanazingatia kaida hizo kupitia utekelezaji wa mbinu tofautitofauti.

4.1.1.1 Matumizi ya Misemo

Misemo ni kauli fupifupi zinazotumiwa na jamii kuisitiza ukweli wa jambo fulani. Ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii fulani kwa lengo la kutoa msisitizo wa maadili fulani (TUKI, 2014). Misemo hii inaweza kutumika wakati mtu anataka kusema kitu lakini hataki kukisema kwa uwazi. Kwa mfano mtu anaweza kumwona mtu mwingine akimdhulumu mwenzake kisha akasema ‘heshima ya mtu ni utu’. Msemaji anamaanisha kuwa yule anayemdhulumu mwenzake hana utu na kwa hivyo hapati heshima zake licha ya uwezo wake kinguvu. Mwasilishaji mkuu, mwelekezi wa vipindi na mashabiki wa vipindi vya *SK* walitumia misemo kwa wingi wakati wa mjadala.

Katika kipindi cha *Kalokset eng Katunisiet* (Mavazi katika ndoa), ‘Pasta’ Rotich anamjibu msikilizaji ‘L’ kutoka Kapsabet kuwa urembo hausaidii sana bali tabia njema. Shabiki huyu anasimulia hadithi ya msichana aliyependa kuvaa mavazi mafupi sana yaliyomwacha nusu uchi. Nia ya msichana huyu ilikuwa kunasa hisia za mwanamume mmoja tajiri, ambaye alikuwa kijijini mwao, ili amwoe. Shabiki huyu anaelezea kuwa mambo hayakumwendea vyema yule msichana kwa sababu mwanamume huyo alimpendelea binti mwingine aliyekuwa mpole sana, mwenye adabu na aliyetoka katika jamii ya wachochole. Alimtwaa na kufunga ndoa naye kwa sababu alikuwa na tabia njema na alionyesha tabia yake kupitia kwa namna alivyovaa mavazi yaliyofunika mwili wake vizuri. Baada ya kusikia hadithi hiyo, Rotich anajibu:

Kal.

61. *Achame ole kearorto kastaindenyo. U notok kabisa, amu 'yebo kimng'ulya kobo', matinye 'kebutyi berer'.*

Kis.

Ninapenda mfano wa msikilizaji wetu. Ni hivyo kweli kwa sababu **kilichokusudiwa kuwa kitakuwepo** hata **kikitafuliwa vijisababu**.

Katika mfano 61, Rotich anatumia msemu 'yebo kimng'ulya kobo' (kilichokusudiwa kuwa kitakuwepo). Mfano huu unaonyesha jinsi Rotich ametumia msemu kuonyesha heshima kati yake na wasikilizaji. Licha ya ufupi wa msemu huo, mambo mengi yamefichika ndani yake. Pasta Rotich amechagua kutumia msemu huo badala ya maneno yenyewe ambayo yanaweza kuudhi.

Sehemu ya mwisho ya mfano huo wa 61 inabeba msemu mwingine 'Kebutyi berer' (kutafutiwa vijisababu). Huu ni msemu wa Kikalenjin unaomaanisha kutolea vijisababu mfanyiko wowote. Lengo ni kuonyesha kuwa hakuna kinachoweza kuzuia kutendeka kwa jambo lililopangwa na Maulana. Misemo hulenga kupitisha ujumbe usokuwa wazi kwa wasikilizaji ili kila mmoja aweze kujitafutia maana yake.

Matumizi ya misemo pia ilibainika katika kipindi cha *Tililindo eng katunisiet* (Usafi katika ndoa), 'Koriryo' anatumia msemu ili kuonyesha jinsi wanaume wengine hujisahau. Anasema kuwa wanaume wengi wanategemea tu usafi wa wanawake bila kujua hata wao wanahitajika kuwa wenye kujali usafi wa miili yao ili kuvutia wake zao. Koriryo anafafanua umuhimu wa usafi katika jamii kwa ujumla kuwa ni jukumu la kila mwanajamii kwa kusema:

Kal.

62. *Magat kotililit chitugul eng kapchi. Makele kwonyik ichegei Pasta che magotin kotililitu amu agot ichek kogasei kong'wan kong'utoi*

manong'otoikwak. Ngap kelen kaesyo kwony boiyonyi ago ngaga chamu 'nding' ago notok ne igochin ichek kobet 'appetite'.

Kis.

Kila mmoja katika jamii anahitajika kulinda usafi. Pasta, sio wanawake pekee wanaohitajika kuwa safi kwa sababu hata wao huhisi vibaya wakati waume zao hunuka vibaya. Wakati mwingine inachukuliwa kuwa mwanamke amemkataa mumewe kumbe **ananuka 'nding'** na ndio sababu wanawake hupoteza hamu.

Mfano 62 unatumia msemu '*chamu nding*' (ananuka 'nding'). Msemu huu umetumika kuonyesha harufu mbaya sana ya wanaume wanapokosa kuzingatia usafi. Kupitia kwa matumizi ya msemu, Winny anakuza na kudumisha heshima baina yake na wasikilizaji wake. Ikumbukwe kuwa, wengi wa mashabiki wa kipindi cha *SK* ni wanaume na wao ndio huchangia mjadala kwa wingi. Winny anatumia msemu huo ili wasikilizaji wenyewe wajipambanulie uzito wa mnuko unaozungumziwa. Mbinu hii ni mojawapo ya njia za kukuza heshima baina ya wasemaji na wasikilizaji. Ukuzaji wa heshima unajenga uhusiano mzuri baina ya wanajamii.

Mfano mwingine wa matumizi ya misemo unadhihirika katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Sababu za Kuvunjika kwa Ndoa). Winny anauliza sababu ya wanaume kuoja wake wengine licha ya kutunzwa vizuri? Kwa kumjibu, 'Pasta' Rotich anatoa orodha ya hali zinazomfanya mwanamume aoe mara nyingine hivi:

Kal.

63. *'Koriryo', ingen ile murenik ko biik alak che makielewani. Ngap kotemene bich kele kobetyi nee yekai si kotunis kogeny. Ngap kotinyei age kwondo ne susyin age siyet kole ndakikaek nenyi lakini itunisiei kora, makiguitos bichu Winny, makiguitos iman. Agot nga no, ko bororyetab Kalenjin kotinyei ngalek che chang. Ngap kotunis chito amu cheserwet kwondonyi, kora ko amu tinyei mbaret neo, anan ko matinyei **olo bo sang** eng lagokyik anan ko kikisimji inendet kotun lakwa ne labda kiburon ago kima kochamei.*

Kis.

‘Koriryo’, unajua wanaume ni watu wasioeleweka. Wakati mwingine watu hushindwa kile wengine hukosa ndipo huo tena. Pia, mwanamume anaweza kuwa na mke ambaye mwanamume mwenzake anatamani angekuwa wake lakini bado atataka kumwoa mwingine. Hawa ni watu wasioeleweka Winny. Hata hivyo, Wakalenjin wana mambo mengi kama sababu za kuoa tena. Mtu anaweza kuoa mke mwingine kwa sababu mke wake ni mzembe, au mtu huyo ana shamba kubwa, au hana ‘**nje**’ kati ya watoto wake au hata labda alilazimishwa kumwoa msichana asiyempenda kwa sababu alimpachika mimba.

Msemo ‘*olo bo sang*’ (nje) katika mfano wa 63 una maana ya mtoto wa kiume. Katika Kikalenjin, neno *sang* linamaanisha nje. Kwamba, mtoto wa kiume huwa anatekeleza mambo magumu na mazito ya nje huku wa kike akitekeleza shughuli zinazopatikana ndani ya nyumba. Mtoto huyu wa kiume anachukuliwa kuwa mtoto wa kipekee kwa sababu anaweza kufanya mambo mengi magumu kando na kuendeleza ukoo wa babake. Shughuli za nje kama vile ujenzi na ulinzi wa wanyama na watu huchukuliwa kuwa kazi ngumu.

Hata hivyo, jambo linalozingatiwa sana ni lile la kuendeleza uzazi wa jamii. Kwa hivyo jamii husika huamini kuwa ni lazima mtoto wa kiume azaliwe katika jamii ili kuendeleza kizazi cha jamii. Rotich anatumia msemo huo kuonyesha mojawapo ya sababu za wanaume kuoa wake wengine zaidi. Badala ya kutumia maneno ya moja kwa moja ya mtoto mwanamume, ‘*Pasta*’ Rotich anatumia msemo kudhihirisha heshima baina yake na mashabiki wa kipindi na jamii ya Kikalenjin kwa ujumla.

4.1.1.2 Matumizi ya Methali

Labda kwa vipaji vyote alivyopewa mwanadamu, lugha ndiyo ya kushangaza kwa sababu ya upekee na uwezo wake. Maneno yanaweza kutumika kwa njia nyingi kumaanisha vitu vingi. Maneno ni kama moyo wa kila lugha kwa sababu hapo ndipo ubongo hutolea maana viashiria vya lugha. Kwa njia nyingine, maneno huzalisha

lugha. Maneno hayo hutumika kila siku kuwasilisha mawazo katika kumbukumbu za watu.

Maneno yanaunganishwa katika sintaksia sahihi ya lugha husika ili kutoa maana inayokubalika kwa wasemaji wa lugha hiyo. Wakati mwingine, watu hutumia methali katika mawasiliano. Methali ni tungo fupifupi ambazo hutumika wakati wa mawasiliano kutoa ujumbe kwa njia isiyokuwa wazi. Methali humlazimu msemaji kutoa ujumbe kwa njia iliyofichika ili msikilizaji atoe fasili yake.

Methali hizi hutumika kisitiari kuonya, kurekebisha, kusifu, kuzawadi, kutahadharisha na kurembesha lugha (Kiruki, 2014). Licha ya ufupi na usaili wake, methali ni kipengele muhimu cha busara kinachoashiria ukweli ulio na msingi wake katika utekelezaji wa tajriba ya kila siku ya binadamu. Pia, methali huonyesha kile kinachoaminiwa na jamii pamoja na tamaduni zao katika historia. Wasemaji wa Kikalenjin hutumia methali katika mazungumzo ya kuendesha shughuli zao za kila siku ili kuwasilisha mawazo na hisia zao. Sababu kuu ni kwamba inaaminika kuwa methali huhusishwa na hekima. Hivyo basi, methali kama tungo ni sehemu ya lugha husika ya Kikalenjin na pia sehemu muhimu ya tamaduni za Wakalenjin.

Kila lugha ni kama hekalu kwani inahifadhi nafsi ya waizungumzayo. Mawasiliano ya lugha ni njia ya kupata wazo kutoka kwa akili ya mtu hadi kwa mwingine bila upasuaji. Ni kama damu ya nafsi ambayo huingiza na kukuza mawazo (www.omniglot.com/languages/proverbs/language.htm). Hii ni kutokana na imani ya watu kuhusu lugha yao. Kwa kuambatana na hayo, ni dhahiri kuwa lugha ni msingi wa kila mawasiliano katika lugha husika.

Wahusika wa mazungumzo katika vipindi vya *SK* wanatumia methali kwa wingi ili kudumisha heshima baina yao. Kila wanapozungumza, methali hujipenyeza kwenye usemi wao ili kurahisisha ujumbe na kutunza nyuso zao na za wasikilizaji wao. Mfano mzuri ni katika kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka). Shabiki ‘M’ kutoka Tavina, katika kaunti ya Trans Nzoia, alionekana kufurahishwa na wazo la Rotich kuwa mambo katika ndoa hayafai kutajwa na kufanywa ovyo ovyo. Alishereheshea wazo hilo kwa kutoa onyo kuwa ndoa nyingi huvunjika kwa sababu ya uwazi unaozidi kiasi katika mambo ya ndoa. Alidokeza:

Kal.

64. *Kacham ole kemwaite iwe! Ingen ile bikyok ko kikoutie ateptab keny. Makomage kiy biik kosub tyegutik che kibo kwanisyekyok. Kongoi ‘Pasta’ amu eng iman kieli tany kong si kechorei.*

Kis.

Ninapenda sana ulivyosema. Unajua, watu wetu wamesahau mwenendo wetu wa kale. Hawajali tena kufuata nyayo za babu zetu. Asante ‘Pasta’ kwa sababu hakika hata **ng’ombe hufumbwa macho ndipo atolewe damu.**

Mfano wa 64 unaonyesha jinsi methali imetumika kutunza nyuso za wazungumzaji wa *SK*. Methali *kieli tany kong si kechorei* (Ngombe hufumbwa macho ndipo atolewe damu), ina maana ya kuwa mambo mengine hayafai kufanywa wazi wazi. Wakalenjin kwa ujumla wanapenda kunywa damu ya ng’ombe. Wakati wa kutoa damu ng’ombe hupigwa mshale ili damu inapotiririka iwekwe katika kibuyu maalum. Kwa sababu Wakalenjin wanawaenzi sana wanyama wao wa kufugwa, wanaona ni vyema kumtoa damu ng’ombe lakini pasi na ng’ombe kuuona mshale unaotumiwa. Ng’ombe husika hushikwa na wengine lakini yule wa kumpiga mshale huficha uta na mshale wake usionekane ili ng’ombe asishtuke.

Matumizi ya methali hiyo katika mfano 64 ni mbinu tosha ya kukuza heshima baina ya wazungumzaji wa *SK*. Mbinu hii ni njia mbadala ya kutoa ujumbe bila kumkera yeyote. Mara nyingi, methali hii hutumiwa na jamii ya Wakalenjin kuwaonya watu dhidi ya kuzungumza au kusema kila kitu hadharani.

Mfano wa pili wa matumizi ya methali ni katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Sababu za kuvunjika kwa ndoa). ‘Pasta’ Rotich anatumia methali kuwakosoa wanaume wanaozingatia mtazamo wa kibabedume na wanaofikiria kuwa mateso kwa wanawake ni njia mojawapo ya kuwafanya wawaheshimu waume zao. Rotich anaeleza kuwa dhuluma dhidi ya wanawake ni mtazamo duni wa kijadi ambao unachangia kuvunjika kwa ndoa nyingi. Akisimulia kisa cha mwanamke aliyezomewa kila kukicha na mama mkwe kwa kumkosoa mumewe, Rotich anasema kuwa huyu binti wa watu aliteseka sana. Mama mkwe alikuwa akimsingizia mke wa mwanawe kuwa ndiye mkosa. Tazama mfano huu:

Kal.

65. *Wooi, ng’wan we Winny, ng’wan nebo koitita. Kele inye kang’eeet chopyoaset age ne kibunu koin ak kous age ne kergei tuwai amu nee! Ibwotitoi ano korgetab yugoi bo lakwani iman yekai! Kalya si mager kong werinyi matiny kongen kole makenu lakwetab chito! Eiting’o, nga iman, ng’wan kobo chi tandus kobo tiony.*

Kis.

Winny, woi inaumiza kweli. Yaani mwanamke aliyetoka nyumba nyingine anaamua kumtesa mwenzake anayefanana naye kwa nini! Huyu mama mkwe anafikiria nini akifanya hivyo! Mbona asimwonye mwanawe hali anajua kuwa lalama za mke wa mwanawe ni kweli! Haidhuru, kumbe ni kweli kuwa **ni uchungu mzaliwa akiwa wa binadamu lakini si kwa mzaliwa wa mnyama.**

Sehemu ya mwisho ya mfano 65, ‘*Ng’wan kobo chi tandus kobo tiony*’ (ni uchungu mzaliwa akiwa wa binadamu lakini si kwa mzaliwa wa mnyama) ni methali. Kulingana na Wakalenjin hasa jamii ya Wanandi, methali hii inaashiria kuwa watu

huhisi vibaya watu wao wanapotendewa vibaya ilhali hawahisi kukereka wengine wasio wao wanapotendewa unyama. Methali kama hizi hutumika kumkosoa mama wa kambo anayewatesa watoto ambao labda mama yao aliaga dunia. Kwa kutumia methali hii ya kijumla, ‘Pasta’ Rotich anakuza heshima baina yake na wasikilizaji wake kwa kutokuwa bayana zaidi. Kutumia maneno bayana kuna uwezo wa kuathiri nyuso za wasikilizaji.

4.1.1.3 Matumizi ya Ubadilishaji Msimbo

Wakati mwingine, ni vigumu kwa watu kutaja maneno fulani katika lugha yao. Hii ni kwa sababu maneno kama hayo huonekana kukosa heshima miongoni mwa wanajamii. Wazungumzaji hujipata katika hali ya kupenyeza maneno ya lugha nyingine ndani ya lugha yao. Kwa sababu ni sharti mtu apitishie ujumbe aliokusudia, ubadilishaji msimbo huja kama njia ya kipekee ya kumsaidia mtu kama huyo kutekeleza uwasilishaji wa ujumbe. Myers-Scotton (1993) anatoa dhana ya ubadilishaji msimbo kama hali ya kutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo.

Hivyo basi, ubadilishaji msimbo humsaidia mzungumzaji kujiepusha kutaja mambo anayokisia kuwa yatafunja heshima baina yake na msikilizaji. Wahusika wa mazungumzo ya *SK* wanatumia ubadilishaji msimbo kama mbinu ya kukuza heshima baina yao. Rotich na Winny wametumia ubadilishaji msimbo kwa wingi wakati wa mazungumzo ili wasiwakere wasikilizaji wao.

Kwenye kipindi cha *Tilyandit eng Katunisiet* (Uhusiano katika Ndoa), Rotich anasema hivi:

Kal.

66. *Ngalen ingen o Winny ile makanye bikyok komwachi lagokwak tuguk che tinyegei ak 'sex'. Aegei sigik kou ne mengen lagok kole sikobit lakwa ko ke- 'practise'-n ng'alechoto.*

Kis.

Winny, ninajua unafahamu kuwa watu wetu wanaogopa kuwaambia watoto wao mambo kuhusiana na **ngono**. Wazazi wanadhani kuwa watoto hawaelewi mtoto hupatikana kupitia utekelezaji wa**kitendo cha ngono**.

Neno 'sex' katika mfano 66 ni la Kiingereza na limetumiwa kimuktadha kumaanisha ngono. Wasemaji wa Kikalenjin wanaogopa sana kuyataja mambo kama hayo hadharani na ndiposa Rotich anatumia neno la Kiingereza ili neno hilo lisionekane kuwa la aibu. Iwapo Rotich angetumia neno la Kikalenjin '*Keruiyo*'(kulala), lingonekana kuwa hatari kwa sababu wasikilizaji wangeogopa kuchangia. Wakalenjin ni wastaarabu sana na hupenda kujitenga na matumizi ya maneno yanayoonekana kuaibisha. Hii ndiyo inapelekea wao kutumia msimbo mwingine kuelezea mambo mengine.

Sehemu ya mwisho ya mfano huo wa 66, ina neno *Ke-practise-n* ambalo limeundwa kwa kuchanganya Kikalenjin na Kiingereza. Neno hili linabeba maana ya kufanya zoezi hilo la ngono. Imeonekana vigumu kwa Rotich kusema sentensi yote kwa Kikalenjin kwa sababu kwake yeye na jamii yote husika, maneno kama hayo hayatajwi hadharani. Ubadilishaji msimbo basi umemsaidia msemaji Rotich kupitisha ujumbe wake lakini kwa kutunza heshima baina yake na hadhira.

Pia, ubadilishaji msimbo ulibainika katika kipindi cha *Supsetab tibik ak kwonyik* (Ubakaji wa wanawake). Winny anasema:

Kal.

67. *Kegas iman ii ‘Pasta’? Nga makenu kapsaili kolen **nyani haoni kundule**. Kegas komie ole kamwaita kastaindenyo? Kamwa komie kole kimakongen chepyosonotok kole kima ko kararan kaloksetab tibikyik. Kale kicham komwoe kila agobo lagokab **jirani** kobwatyin kole matinyei **kasoro** chechik, **lakini mwisho msichana alibakwa nani!***

Kis.

Umesikia kweli ‘Pasta’? Kumbe Waswahili hawakukosea waliposema **nyani haoni kundule**. Umesikia vizuri alivyosema msikilizaji wetu? Amesema vizuri kuwa huyu mama hakuona tabia na hali ya mavazi ya wanawe kuwa haikupendeza. Amesema kuwa huyu mama alikuwa na mazoea ya kuwakosoa binti za **jirani** akifikiria wake hawakuwa na **kasoro, lakini mwisho, msichana alibakwa nani!**

Katika mfano huo, baadhi ya maneno yaliyotumiwa kuwasilisha ujumbe ni ya Kiswahili. Ya kwanza ni methali **nyani haoni kundule**. Baada ya msikilizaji huyo kutoa maoni yake kuwa kina mama ndio wanachangia kubakwa kwa binti zao kwa kutowaonya dhidi ya kuvaa vibaya, Winny ‘analipuka’. Anafanya hivyo kwa kubadilisha msimbo ili kurahisisha mawasiliano na kujenga uhusiano mzuri kati yake na wasikilizaji. Anafanya hivyo kwa sababu ni vigumu kwake kutaja mambo hayo bayana.

Pili, ni katika sentensi ya mwisho katika mfano huo wa 67 ambayo ina maneno ya Kiswahili **jirani** na **kasoro**. Licha ya kuwa maneno hayo hayahusiani moja kwa moja na lugha ya heshima, yanazua wepesi fulani wa ujumbe kinyume na matumizi ya maneno ya Kikalenjin ambayo yangeonekana kupitisha ujumbe lakini kwa uzito.

4.1.1.4 Kuzungumza kwa Zamu

Kuzungumza kwa zamu ni njia mojawapo ya kuonyesha heshima baina ya wahusika wa mazungumzo. Yang (2007) anahoji kuwa washiriki wa mazungumzo wanakabiliwa na tatizo la kuzungumza na kusikiliza kwa wakati mmoja. Naye Crystal

(1995) anaafikiana na Yang kwa kudokeza kuwa mojawapo ya sifa za lugha ya mazungumzo ni kule kuzungumza kwa zamu au kukatizana usemi. Kuna uwezekano kuwa mzungumzaji anaweza kukatizwa usemi wake na msikilizaji. Jambo hili hutokea wakati labda msikilizaji anataka kurekebisha jambo alilolisema msemaji, kushadidia wazo la msemaji au hata kukerwa na ujumbe wa msemaji. Ili kuthibiti tatizo la ukatizaji za zamu, washiriki wa mazungumzo wanapaswa kuheshimiana kwa kubadilishana zamu.

Dubois na wenzake (1996) pamoja na Sacks na wenzake (1994) wanaelezea ushikaji zamu kama tendo la kimtagusano kupitia mazungumzo na ambalo hudhihirisha ushirikiano wa watu wawili au zaidi. Hii ina maana kwamba, ubadilishanaji zamu hutokea wakati kuna mtoa habari na yule wa kuupokea ujumbe huo. Mazungumzo katika vipindi vya *SK* hayaepuki sifa hii ya mazungumzo. Ubadilishanaji wa zamu ulibainika kwa njia nyingi kupitia kwa mazungumzo baina ya mwelekezi, mwasilishaji mkuu na mashabiki wa vipindi husika.

Ilibainika kuwa, wahusika wa mjadala katika vipindi vya *SK* wanapeana heshima kwa kusubiri muda wao. Kila Rotich anapokuwa akizungumza, Winny pamoja na mashabiki wanamsikiliza kwa makini. Winny naye, anapoelekeza kipindi, anasikilizwa kwa makini na mwasilishaji pamoja na wasikilizaji wa vipindi. Nao 'Pasta' Rotich na Winny huwapa masikio mashabiki wanapochangia. Aidha, mwasilishaji wa vipindi anasisitiza kila wakati kuwa ni muhimu kuwapa wengine nafasi kwa sababu maoni ya kila mmoja yanafaa. Wakati mmoja Winny anasikika akisema:

Kal.

68. *Kastoikyok, ongigochinigei okwek nafas. Ongekas maoni chebo biik alak agichek amu kaswech chechok. Ye imache imwa kiy ago kakakegonin nafas isir asikesoman kokait kasarta ne yamatkei.*

Kis.

Wasikilizaji wetu, ninaomba **tuwe tukiwapa wengine zamu**. Tuyasikie maoni ya wenzetu kwa sababu wametupa nafasi. Iwapo umepewa nafasi na bado unataka kuchangia, ninaomba uandike ujumbe ili tuusome wakati unaofaa utakapofika.

Mfano huu unaonyesha kuwa mwelekezi wa vipindi anawajali wasikilizaji wote. Mwelekezi hategemei kuwa maoni ya watu fulani ni bora kuliko ya mashabiki wengine. Ni mbinu nzuri ya kusawazisha mawazo ya mashabiki na pia wao kuhisi kuwa wote wanaheshimiwa. Iwapo Winny angetoa nafasi kwa watu wachache wanaojulikana kuchangia kila wakati, huenda wasikilizaji wengine wangejiondoa kwenye mjadala. Vipindi hivi vya *SK* vimekuwa vikiendelea bila kukatika kwa sababu wasikilizaji wote wanachukuliwa kwa usawa. Mbinu hii ya ubadilishanaji zamu inakuza na kudumisha heshima baina ya washiriki wa mazungumzo ya *SK*.

‘Pasta’ Rotich pia anachukua wakati mwingi kuwarai wasikilizaji wake dhidi ya kuchukua muda mwingi. Anawaambia kuwa ni vyema mtu kuwapa wengine nafasi ili wachangie. Ananukuu kifungu cha Bibilia kwa kusema:-

Kal.

69. *Ogero tupchosiekyok, ‘mie ne tia ak ko kararan ne tia, ye meng’jindos che tupcho eng yamdaet agenge’. Kararan nebo kwong’ut ye kagikaskai it kou lagokab korgonak. Ongigojinigei boroindo agot nga matia kasarta keamdoi kaptililei kot koyamech tugul.*

Kis.

Ndugu zetu, ‘tazama jinsi ilivyo vema, na kupendeza, ndugu wanapokaa pamoja kwa umoja’. Itakuwa vema sana tukiwatii wenzetu na kushirikiana kama watoto wa mama mmoja. **Tubadilishane zamu, na hata ingawa wakati ni mfupi, tutagawana muda hadi ututoshe.**

Kwa njia ya heshima, Rotich anawarai wasikilizaji wawape nafasi wenzao na anafanya hivyo kwa kunukuu kifungu katika Bibilia. Bibilia ni kama mwongozo kwa watu na si wengi wanaopinga maneno yake. Kwa sababu ‘Pasta’ Rotich ni mcha Mungu, anatumia kifungu hicho kuwaelekeza mashabiki wa vipindi kuthibitisha umoja na wema wao kupitia ubadilishanaji wa zamu.

Kwa ujumla, ubadilishanaji zamu kama mbinu ya kutekelezea heshima kati ya washiriki wa mazungumzo, hutoa nafasi kwa kila mshiriki kujiwasilisha. Hata wasipopewa muda kwa wakati huo, wao husubiri kipindi kinachokuja kwa sababu wanajua mwasilishaji na mwelekezi wa vipindi hawana mapendeleo. Mashabiki wa *SK* wanafurahia sana vipindi hivi kutokana na juhudi za viongozi wanaotumia hekima kusawazisha mawazo yao.

4.1.1.5 Matumizi ya Sifa za Kiarudhi

Crystal (2003) anaeleza kuwa, lugha ya mazungumzo husheheni sifa za kiarudhi kama vile toni na kiimbo. Sifa hizi huonyesha namna mzungumzaji anahisi wakati anazungumza. Obuchi na Mukhwana (2010), wanatoa dhana ya sifa za kiarudhi kama sifa za sauti ambazo hubainika katika vipashio vikubwa kuliko kipande sauti kimoja. Tuna vipande sauti kama vile kiimbo, mkazo na toni. Katika mjadala wetu, tutaangazia namna kiimbo na toni zinajitokeza katika mazungumzo.

Kiimbo ni sauti maalum inayojitokeza wakati wa kutamka maneno fulani. Ni kule kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti ya lugha wakati wa mazungumzo. Kiimbo husaidia kuleta maana kamili ya sentensi iliyokusudiwa. Kwa kutamka sentensi kwa sauti fulani ya ‘kiwimbo’, tunaweza kubainisha kauli ya kawaida, swali, hisia miongoni mwa zingine (Toboso, 2016). Wakati mtu anatamka maneno au sentensi kwa viimbo mbalimbali, sentensi hiyo au maneno hayo hutoa dhana tofauti.

Katika uandishi, viimbo huwakilishwa na alama za uakifishaji ili kumwelekeza msomaji kusoma kwa kiimbo kilichokusudiwa. Katika mazungumzo, msikilizaji huwa makini kusikiliza ili ajue mahali msemaji amesema kwa kiimbo (www.kcse-online.info).

Kwa upande mwingine, toni ni kiwango cha kidatu pamoja na mabadiliko ambayo hutokea wakati mtu anatamka silabi au maneno. Katika lugha za toni, mabadiliko ya toni hubadili maana ya yale yanayosemwa (Mgullu, 2008). Waja wanapozungumza, ni kawaida wao kubadili sauti ndani ya usemi. Sauti inapobadilika, maana inayojitokeza ni tofauti. Hivyo basi, mtamkaji anapobadilisha sauti ya silabi moja ya neno au neno moja katika sentensi, maana hubadilika. Vipindi vya *SK* vilishuhudia matumizi ya kiimbo na toni kama inavyodhihirika katika mifano inayofuata.

Katika kipindi cha *Tilyandit eng katunisiet* (Mahusiano katika ndoa), Winny anachangamkia wazo la ‘Pasta’ Rotich anayewaonya kina mama dhidi ya kuwaachia wanaume watoto wasichana. Anasema kuwa wanaume wengine wamefumbika ndani ya mawazo na hawana uwezo wa kujizuia licha ya uhusiano wa damu kati yao na watoto wao. Rotich anaendelea kusema kuwa wanaume kama hao wamesikika wakiwafanya binti zao kuwa wake zao wakati wake zao wametoroka kwa sababu moja au nyingine. Winny anasema:

Kal.

70. *Oiye unotok kabisa ‘Pasta’, kale ndengen inye chepyosok kole tiong’ik murenik! Imugoksei koyoni chito boiyonyi mising kot ko mebwotyin kole imuch kwam lagokyik. Wooowoi, akonyiti mising murenik ipkobate mutyo bikyok, kilen mutyo eng murenik, yani korotiguk kapsa kapsa!*

Kis.

Haki ‘Pasta’, ni hivyo kabisa, laiti kinamama wangejua kuwa wanaume ni wanyama! Kuna uwezekano mtu anamwamini mumewe

sana hadi hafikirii kuwa anaweza ‘kuwala’ walio wake. **Wooowoi**, nawaheshimu sana wanaume lakini pole sana, tunasema pole kwa ajili ya wanaume, yaani damu yako kabisa kabisa!

Mfano 70 unaonyesha jinsi Winny anatoa hisia zake kuwahusu wanaume. Licha ya kuwa wanaonekana wanyama, Winny bado anasema kuwa anawaheshimu kwa sababu wao ni wanaume. Katika jamii ya Kikalenjin, mwanamume akikosa bado ataheshimiwa. Hata afanye jambo baya kiasi gani, mwanamume atabaki kuwa mwanamume. Hiyo ndiyo sababu Winny anasikika kukerwa na tabia ya wanaume lakini kwa namna nyingine anakwepa kuonekana mkosa heshima kwa wanaume.

Sehemu ya kwanza ya mfano 70 inaonyesha mshangao na kuudhika kwa Winny kupitia kwa sauti yake. Lakini anaposema neno *wooowoi* sauti yake inashuka ili wanaume wasimwone kana kwamba yeye hana heshima. Kama wasemavyo Obuchi na Mukhwana (2010), kila lugha ina utaratibu wake maalum wa kupanga mawimbi ya sauti zake. Katika muktadha wa usemaji, kila lugha ina utaratibu wake maalum wa kupanda na kushuka kwa mawimbi-sauti zake. Ikumbukwe kuwa wengi wa mashabiki wa vipindi vya *SK* ni wanaume na hivyo Winny hangependa kuwaudhi au kuwakasirisha. Sauti ya chini inadhihirisha heshima kwa wasikilizaji.

Kupitia kipindi cha ‘*Mpango wa kando*’ (Mpango wa kando), ‘Pasta’ Rotich anaelezea machungu wanayopitia wana wa kike. Anatumia mfano wa mtu fulani aliyekuwa akimtesa mkewe bila sababu. Mkewe alipojaribu kumwuliza sababu ya kumtesa, mwanamume alimjibu kuwa hajui kumbembeza mwanamke. Rotich anaeleza kuwa baada ya uchunguzi, iligunduliwa kuwa mwanamume alikuwa ‘akila nje’ na hivyo hakuwa na haja na nyumbani. Anasema:

Kal.

71. *Nga kicham komi ole 'amisye' chito ak kelen iimi nee o Winny. Eiting'o we chepyosochu, akonyitok nebo iman amu omuitoi. Kale kwonyoto kiiisub betut agenge agoi kotab lakwa age ne ki maitun chi ago kitinyei lagokyik. Ki 'single lady' Winny, ngamwa kou notok si iguiye ak koguiyo kastoikyok che kikomeny olin bo taon. Ingen is ile ane aelewani amu abunu olin bo Rift Valley, olin bo Eldoret, ee olin bo Segero, gaa is oo Winny ole ta keng'alali kutitab chego. As, ngemete cho korok Winny si tun amutin olinyo...wei ngekonyit kostoikyok korok si kemwa choto betutage...*

Kis.

Winny, kumbe mtu alikuwa na mahala pa 'kukulia' na huku watu wakiuliza kilichokuwa kikimsumbua. **Poleni kinamama, ninawaheshimu kwa kuwa ninyi ni wavumilivu.** Mke wa huyo mtu anasema kuwa siku moja aliamua kumfuata mumewe kisirisiri hadi kwa msichana mmoja ambaye alikuwa na watoto lakini hakuolewa. Winny, nitamwita mama aliye peke yake ili wewe pamoja na wasikilizaji wetu mnaoishi mijini mwelewe. Unajua kuwa mimi ninaelewa kwa sababu ninatoka Bonde la Ufa, mjini Eldoret, naam kule nyumbani Segero mahali bado inazungumzwa lugha ya maziwa. Haya, Winny, tuyaache hayo kwanza halafu siku moja nitakupeleka huko kwetu... **naam, tuwaheshimu wasikilizaji wetu kwanza ili tuyaseme hayo wakati mwingine...**

Mfano wa 71 unaonyesha vile 'Pasta' Rotich anawaheshimu wasikilizaji wake, Pasta anatumia neno la Kinandi *eiting'o* (ninasikitika) ambalo linatamkwa kwa sauti ya chini. Ameanza usemi wake kwa kuelezea kisa kilichotukia lakini ghafla, sauti yake inashuka ili kuonyesha kuwa anasema jambo hilo kwa heshima ya kina mama. Sehemu ya mwisho ya mfano huo unaonyesha jinsi Rotich anavyowajali wasikilizaji, anamwambia Winny, *ngekonyit kostoikyok korok* (tuwaheshimu wasikilizaji wetu kwanza na anasema hivyo kwa kushusha sauti chini. Heshima kwa wasikilizaji inajitokeza kupitia kwa maneno anayosema Rotich na anavyoyasema maneno hayo.

4.1.1.6 Udondoshaji wa Maneno/kauli

Udondoshaji ni uondoaji wa kitu mahali Fulani (Kamusi Elezi, 2016). Udondoshaji wa maneno ni kule kuondoa neno au baadhi ya maneno katika sentensi. Mbinu ya

udondoshaji hutumika wakati mzungumzaji anafikiria kuwa neno au maneno fulani hayafai au yanaaibisha. Udondoshaji wa maneno husaidia kuhifadhi hali nzuri ya wahusika wa mazungumzo ili kuwe na mwendelezo mzuri wa mazungumzo. Mara nyingi, msemaji hudondosha maneno mengine wakati anajua kuwa msikilizaji ameelewa au anajua ujumbe anaokusudia kupitisha. Hata hivyo, mchakato wa udondoshaji haufanyiki ovyo ovyo bali msemaji huwa makini ili asipoteze maana aliyokusudia kwa msikilizaji.

Udondoshaji wa maneno unabainika katika mazungumzo ya *SK* wakati mwasilishaji mkuu na mwelekezi wa vipindi wanatoa maelezo ya mambo nyeti ambayo yangewakera au kuonekana ya kukosea heshima mashabiki wa vipindi vyao. Mfano mzuri ni katika kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazomfanya mwanamume kuoia mke mwingine). Winny anasimulia kisa cha rafiki yake aliyeletewa mke mwenza baada ya miaka miwili katika ndoa. Winny anasema kuwa mumewe rafiki yake alilalama kuwa mkewe hakuwa tayari kila wakati kumpa haki yake ya ndoa. Winny anamwambia ‘Pasta na wasikilizaji’:

Kal.

72. *Milei bich murenik alage, ngole chito yekai mekochin kwondonyi imandanyi sait age tugul ye kamach i, kwani imuchi ine chichoto mm aa wei, ne mang’etei i! Metiny amwa ‘Pasta’ angen ale kakoelewan kostoikyok ole kamache amwaita. Nda kiane kwonyo ko kita acherugei amuita wigit agenge kityo angen ale kobegune chito mmm mmm ee, kobegune chito...*

Kis.

Wanaume wengine wanashangaza sana, mtu asemapo kuwa mkewe hampi haki yake kila wakati anapotaka, kwani huyo mtu anaweza **mm aanaam**, bila kuchoka! ‘Pasta’, acha nisiseme, ninajua wasikilizaji wetu wameelewa ninachokusudia kusema. Ningekuwa huyo mwanamke ningejitolea kuvumilia juma moja tu kwa sababu nina uhakika mtu huyo angeishiwa na **mmm mmm ee, mtu angeishiwa...**

Mfano huu unaonyesha kuwa Winny amedondosha maneno mengine katika usemi wake. Anaposema *kwani imuchi ine chichoto mm aa* (kwani huyo mtu anaweza mm aa) anaashiria kuwa amekosa maneno muafaka, ya heshima, ya kutumia ili asiwakosee wasikilizaji wake. Anadhihirisha hali hiyo kwa kuendelea kusema *metiny amwa 'Pasta'* ('Pasta', acha nisiseme). Winny anamalizia kwa kusema *kobegune chito... (Mtu angeishiwa...)*. Iwapo wasikilizaji hawangeelewa alichosema Winny, wangeulizia 'nini?' Lakini kwa kuwa wao wanaelewa sababu ya Winny kudondosha maneno mengine, wanaendeleza mjadala.

Mfano mwingine wa udondoshaji unadhihirika kupitia usemi wa Rotich ambaye kila wakati anapenda sana kuwatilia maanani wasikilizaji. Rotich, katika kipindi cha *Katunisiet ak koolokset* (Mavazi katika ndoa), analalama kuwa kina dada wamezembea sana katika hali ya kuvaa. Anaeleza kuwa wazee wengine wanawaaibikia wake zao kutokana na jinsi wanavaa. Hoja yake ni kuwa wanawake wanavaa mavazi makubwa sana ambazo zinaficha uzuri wa miili yao. Rotich anahoji kuwa mwanamke anatakiwa kumvutia mumewe kwa njia yoyote ile na iwapo atavaa mavazi makubwa sana, mumewe ataaibika kutembea naye. Anadokeza:

Kal.

73. *Maboto murenik Winny, ngab kolachkei agichek kwonyikyok eng oret ne ngigeere ilen kogo nebo lagok. Muren ko makanyei ama chame aibu. Esioi murenik che chang kobendat ak kwonyikwak amu ngoma ngoroik che chang che kelach, ko koen ak koechen kosiir kiasi. Kalya si melach ngoroik che yomin, che ngobendoti ak boiyot ak kosubun let kobaibai kole nga atinye kwondo iman e! Amache iimajinan oo Winny, chito ne kelach mm mm kit age kondoita eng olo borei, korup age ne tinyei netit ne tenden eng kapkelyen, korup marindet, korup pestit anan nga kikure neng'wong topit oe Winny, korup blausit korup chosit, ndaityo kolach chambait, kotamne cheketit ne tinye chepkulet ak komi kitmbaetab metit ne kakirat! Chamu nee okwek maya tinye chicho! Kamugulit chito kot ko matogu kele tinyei agot suet, ho! Winny! Igase kong'al i!*

Kis.

Winnie, siwalaumu wanaume. Wakati mwingine, wake zetu waweza kuvaa kwa njia ambayo utadhani ni wakongwe sana. Mwanamume huogopa na hapendi aibu. Wengi wa wanaume huogopa kutembea na wake zao kwa sababu ya mavazi. Iwapo si mengi kwa mwili ni ndefu kupita kiasi. Mbona usivae mavazi yanayokutosha vizuri, yale ambayo ukitembea na mumeo na labda anakufuata nyuma, hufurahi kisirisiri kuwa kumbe ana mke kweli! Ninataka ufikirie kweli Winnie, mtu ambaye ametanguliza **mm mm kitu kingine** sehemu ya chini, akafuatisha nyingine iliyo na neti sehemu ya chini, kisha rinda, kisha nyingine mnayoiita ‘top’, kisha blausi, ikifuatwa na fulana, nyingine inayoitwa ‘jumper’ bila kusahau jaketi iliyo na kofia na kumbuka hiyo inavaliwa juu ya kichwa kilichofungwa kitambaa! Joto nyingi kiasi gani! Mtu amevaa vitu vingi hadi haijulikani kama ana kiuno, lo! Winnie, ni maneno kweli!

Kupitia mfano huo, Rotich anatupa taswira ya jinsi wanawake wazembe huvaa. Picha hiyo inajitokeza mawazoni. Hata hivyo, kuna mengine ambayo ‘Pasta’ Rotich anaogopa kutaja bayana. Anaposema *mm mm kitu kingine* (Mm mm kitu kingine sehemu ya chini), Rotich anadondosha maneno ya uwazi kama vile ‘chupi’ au ‘suruali’. Hii ni kwa sababu ya heshima baina yake na wasikilizaji. Jamii ya Wakalenjin hujiepusha na kule kutaja mambo kama hayo na badala yake hutumia maelezo ya kimzunguko ili kudumisha heshima baina ya wasemaji wa lugha husika.

4.1.2 Kufurahisha na Kuwavutia Mashabiki

Kando na kukuza na kudumisha heshima baina ya wahusika wa mazungumzo ya SK, athari nyingine ya uzingatiaji wa mikakati ya upole ni kuwavutia na kuwafurahisha mashabiki ili kuwe na mwendelezo wa vipindi.

Kulingana na Pring (1999), wawasilianaji hupigania kuonekana na kukubalika. Hali hii huwalazimu wazungumzaji kutumia lugha ya kuwavutia na kuwafurahisha wasikilizaji. Wazo hili linashereshewa na Crystal (2004), ambaye anasema kuwa ushindani huu husababisha wazungumzaji kutumia mtindo wa lugha yenye kunata wakati wa kuwasilisha ujumbe. Inadhihirika katika vipindi vya SK kuwa, kila

mhusika azungumzapo, hujaribu kutumia lugha ya kufurahisha na kuteka mawazo ya wenzake wanaomsikiliza.

Wakati wa mazungumzo kila mhusika hutaka kukubalika mbele ya wenzake. Haja hii husababisha watu kutumia maneno yanayojenga lugha safi yenye kuvutia. Lugha yenye mnato hujengwa na maneno ya upole na ucheshi. Ucheshi husababisha uhusika wa wasikilizaji kwa sababu maneno yanayotumiwa yanachekesha na kufurahisha. Upole husababisha usikivu mwingi kwa sababu wasikilizaji wanahisi kuwa lugha inayotumiwa inajali matakwa na hisia zao.

Mbinu ya kufurahisha mashabiki imedhihirika kati ya wahusika wa mazungumzo ya *SK* kwa njia nyingi. Mashabiki wameonekana kufurahia sana ucheshi wa mwasilishaji wa vipindi na Winny ambaye ni mwelekezi wa vipindi husika. Viongozi hao wanajitahidi sana kutumia lugha ya kufurahisha ili kuendeleza kipindi chao. Hii ndiyo sababu mojawapo ya vipindi husika kuendelea bila kukatika. Katika kipindi cha *Mpango wa kando* (Mpango wa kando), Winny anaelekeza kipindi kwa kutanguliza hivi:

Kal.

74. *Kastoikyok, betutab ra ko betut ne inegei amu king'alale kiit ne kingen tugul kele kikobut korik che chang. Tetutietab rani kegure 'mpango wa kando'. Angen ale ngamwa nitok koaragendos cheleos amu len kaking'ang'da ng'alekwak. Ago i, kane inye, ngalen kakinyoigei tugul. Machei sikomwoweche 'Pasta' amu nee che aei biik kotoi 'mipango ya kando', we...we! Angen ale anyiny ra kipindit nitok kot ak angen ale chomei kastoikyok mi...iii...sing. Mangen ale kilya inye siko tugun che etan kwonyiny! Karibu 'Pasta' Rotich amu chobotin kostoikyok koepchi it tetutietab mpango wa...aaa kando...ooo!*

Kis.

Wasikilizaji wetu, leo ni siku ya pekee kwa sababu tunazungumzia kile tukijuacho wote kuwa kimevunja ndoa nyingi. Leo tutazungumzia 'mpango wa kando'. Ninajua fika kuwa ninapotaja hili 'majambazi' huwa na wasiwasi kwa sababu wanafikiria mambo yao yanafichuliwa. Lakini mbona wasi wasi na wote tunatafuta tiba! Mchungaji yuko

tayari kutujua sababu zinazopelekea watu kutafuta ‘mipango ya kando’. **We...we!** najua kipindi cha leo ni kitamu **sa...aaa...na** na sijui mbona ni kawaida kwa kinachokatazwa kuwa kitamu!. Karibu mchungaji Rotich kwa kuwa wasikilizaji wetu wako tayari kwa kipindi cha mpango **wa...aaa... kando...ooo!**

Maelezo ya Winny katika mfano wa 74 yanaonyesha ucheshi wake. Winny anadhihirisha uelekezi mzuri kwa sababu lugha yake ina mnato mwingi. Anapenda kutia chumvi nyingi usemi wake ili wasikilizaji wafurahi na kuwa tayari kuendeleza kipindi husika. Anaposema *we...we! Miiiising, waaaa, na kandoooo, (we...we! Saaaana, waaaa na kandoooo)* Winny anaonyesha ucheshi. Hali hii inawafurahisha mashabiki sana na wanakuwa na ari ya kutaka kikisikiliza kipindi tena na tena. Pia, kwa kusema *mongen ale kilya inye si ko tugun che etan kwonyinyen* (sijui mbona vitu vinavyokatazwa ni vitamu), Winny anawachekesha wasikilizaji wake na kuwatia ari ya kutaka kusikiliza kipindi kinachofuata.

Kama wasemavyo Jost na Burgess (2000), Hoffman na Centeno (2003), Keltner na wengine (2003) na Krueger (2006), furaha huwafanya waja kuishi bila mawazo mabaya na kutaka kuendeleza utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Hii ndiyo sababu Winny anajikakamua kutia chumvi lugha yake ili mashabiki wa kipindi wawe tayari kumsikiliza mwasilishi mkuu. Ucheshi ni mbinu muhimu sana katika mazungumzo kwa sababu inaashiria urajua wa msemaji.

Imedhihirika pia kuwa Rotich anatumia lugha ya ucheshi. Kila anapoelezea kitu, Rotich anajaribu kuwavutia na kuwafurahisha mashabiki wa vipindi vyake. Kwa muda mrefu watu wengi wamechukulia kuwa watumishi wa Mungu kama vile wachungaji hutumia lugha sahili isiyotiwa chumvi. Rotich anakiuka mtazamo huo kwa kutumia lugha yenye wingi wa vichekesho ili kuwafurahisha wasikilizaji. Mashabiki wa vipindi hivi wamekuwa wakitazamia sana siku ya Jumatano saa nne

usiku ili wakisikize kipindi. Ucheshi wa Rotich unamwezesha kuwashughulikia wasikilizaji ambao ni wa umri tofauti, lahaja tofauti za Kikalenjin, dini tofauti na hadhi au mamlaka tofauti.

Akifafanua mahitaji ya wanaume katika kipindi cha *Tililindo eng katunisiet* (Usafi katika ndoa), Rotich anadhihirisha ucheshi wake anaposema:

Kal.

75. *Ngamwaun anyun Jepkorir ak kostoikyok che kwonyik. Achek murenik kechome tuguk che tililen. Kichome **kompoun ne tilil, jikoni ne tilil, mesa ne tilil, ole kirue ole tilil, kurere ne tilil, kamwa ale kurere ne tilil** Winny, kurere kitanda is oo amu oloto ole mi tuguk tugul. Amwoe kou notok Winny amu ngap koboisie alage tuguk cho kiribegeri si manam bich musar anan ko borwek cho yaach ak kowirchi oloto. Kalechin mi kwonyik as Winny che kekwong'e. Kikwong'e iman amu, pto! Makimwoe agot, aisuru ngamwa kityo. Mi kwonyik che wijchin kurere tukyoto ak koutye kowirta ye kaeech. Ko amu muren ko mamache kiy ne ng'utoi ne samis, komuchi komwei eng koyoto ak kocheng biik che mi ichegei che len ak koro ng'o. **Yaani tililen kot kot kibiyo buch ama kiam kiy.***

Kis.

Winny pamoja na wasikilizaji wetu wa kike, sikilizeni niwaeleze, Sisi wanaume tunapenda vitu safi. Tunapenda **mazingira safi, jikoni safi, meza safi, mahala safi pa kulala, mvunguni safi, Winny, ninamaanisha, mvunguni, yaani chini ya kitanda** kwa sababu humo ndimo mlimo kila kitu. Winny, ninasema hivyo kwa sababu wengine wanaweza kutumia mipira ya kuzuia ushikaji mimba na magonjwa mabaya na kutupa mvunguni. Nakwambia Winny kuwa kuna wanawake wa kushangaza. Wanashangaza kweli kwa sababu pto!, Hata haisemekiki lakini aidhuru acha niseme tu. Kuna wanawake wanaotupa vitu hivyo mvunguni usiku kisha husahau kuzitoa asubuhi. Kwa sababu mwanamume hapendi mnuko mbaya, kuna uwezekano kuwa atatoroka na kutafuta wanawake wasio na waume, wanaotamani kuwa na mmoja. Yaani walio safi **hata waweza kushiba bila kula chochote.**

Usemi huu wa mfano 75 unabeba ucheshi mwingi. Licha ya kuonya dhidi ya uzembe, unachekesha sana kwa vile mambo mengine yamefafanuliwa kupiku ukweli au uhalisia wa mambo hayo. Anapofafanua usafi kwote kwote, 'Pasta' anatumia sehemu zote za mazingira kama vile: *kompoun* (mazingira), *jikoni* (jikoni), *mesa* (mezani),

kitanda (kitandani), na *kurere kitanda* (mvunguni). Anafafanua kupita kiasi kile ambacho kinawafanya wanaume kutoroka na kuwatafuta wanawake walio tayari kuwapokea kwa mikono miwili. Anatia chumvi kuwa wale wasio na waume ni safi hadi mtu anaweza kushiba bila ‘kula’. Usemi huo ni wa kuchekesha na kufurahisha. Unanata mawazo ya wasikilizaji na kwa vile unatumia lugha ya mafumbo, unajali mahitaji ya nyuso za wasikilizaji wa viwango tofautitofauti.

Kama mbinu mojawapo ya upole, ucheshi unalenga mahitaji ya uso wa msikilizaji. Msemaji hataji tu mambo kwa nia ya kuchekesha bali huwa makini sana asitoe usemi unaotishia uso wake au wa msikilizaji. Licha ya kuwa nia kuu ya kuzungumza ni kupitisha ujumbe, msikilizaji anatakiwa kuwa mwangalifu sana asichochee hisia mbaya kati yake na msikilizaji (Sanberg, 2010).

4.2 Athari za Ukiukaji wa Mikakati ya Upole katika Mazungumzo ya SK

Lugha na binadamu ni mambo mawili ambayo hayatenganishwi. Iwapo binadamu ataishi bila lugha, basi hatakuwa tofauti na wanyama wa mwituni. Hata hivyo, matumizi ya lugha huathiri mawasiliano iwapo jinsi ya kuitumia haitazingatiwa kimuktadha. Neno, kirai, kishazi, sentensi au matini yoyote yale yanaweza kumaanisha kitu kizuri au kibaya katika miktadha tofautitofauti. Kiuamali-jamii, lugha hupata maana kimuktadha. Maana ya lugha hutegemea nia ya msemaji na ufasiri wa msikilizaji.

Lugha husheheni mambo mengi. Matumizi ya lugha ndiyo huonyesha kile kinachokusudiwa katika lugha husika. Lugha hubeba uzuri au ugaidi kulingana na jinsi inavyotumiwa. Mara nyingi tumekuwa tukifikiria kuwa ugaidi ni matendo ya kutisha tu lakini hata lugha ni chombo cha ugaidi. Iwapo msemaji atasema jambo kisha msikilizaji alifasiri neno hilo kama lenye kuogopesha au kutisha, basi lugha

aliyotumia msemaji itakuwa ya ugaidi. Hii ina maana kuwa, anayesikiliza ndiye huipa lugha maana.

Kwa mujibu wa Watts (2003), ukosefu wa upole umeshughulikiwa kwa muda mrefu uliopita, unashughulikiwa sasa na utaendelea kushughulikiwa. Hii ni kwa sababu maana kamili ya kuwa mpole na kutokuwa mpole, hutegemea kaida za jamii, na kwa vile jamii nyingi zina kaida tofauti, kinachochukuliwa kama upole na kisicho upole bado kinatafitiwa. Haugh (2003, 2007, 2010) anasema kuwa hakuna nadharia kamili au kanuni bia inayoweza kutumika kwa jamii zote kulingana na mada ya upole. Hata hivyo, umuhimu wa kazi ya Brown na Levinson kuhusiana na nadharia ya upole ni kubwa mno. Na kama anavyosema Eeelen (2001), majina yao, Brown na Levinson, karibu yanachukuliwa kuwa sawa na nadharia yenyewe ya upole. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) ambayo ina msingi wake katika dhana ya uso ya Goffman (1967, 1972), na kaida za Grice (1975), inajaribu kuelezea kile ambacho kinahesabiwa kama upole au si upole. Mills (2003) anakiri kuwa kiunzi chao Brown na Levinson kuhusiana na upole kimeathiri karibu kila kazi inayochanganua mikakati ya upole. Kwa mujibu wa nadharia ya upole, kila tabia inayojaribu kulinda uso wa msikilizaji ni ya upole na kila tabia au jambo linalotishia uso wa msikilizaji ni ukosefu wa upole.

Culpeper (2008) anafafanua ukosefu wa upole kama mbinu za uzungumzaji ambazo hulenga kudhuru uso na kwa hivyo husababisha mgongano na ukosefu wa upatanifu katika jamii. Ukosefu wa upole hutokea wakati msemaji anasema kimakusudi kile ambacho kinadhuru uso wa msikilizaji moja kwa moja au/na msikilizaji kuchukulia kilichosemwa kuwa kibaya au yote mawili (Culpeper, (2011)). Kwa ujumla, maoni hayo yote yanalenga msimamo mmoja kuwa kile kinachochukuliwa kuwa upole au

ukosefu wa upole hutegemea uelewa wa msemaji na msikilizaji kuhusiana na jambo linalozungumziwa.

Matumizi ya lugha isiyopendeza hutokana na ukiukaji wa mikakati ya upole. Hata hivyo, kule kutokuwa mpole hutegemea uwepo wa kipimo sanifu wa kaida za upole (Yuli, 2007). Vipindi vya *SK* vinashuhudia ukiukaji wa mikakati ya upole kwa njia moja au nyingine. Kutokana na ukweli huo, sehemu inayofuata inajaribu kutoa kategoria za matumizi ya lugha na ambazo zimedhihirisha ukiukaji wa mikakati ya upole katika vipindi vinavyotafitiwa vya *SK*.

4.2.1 Matumizi ya Lugha Mwiko

Kwa mujibu wa Gao (2013), lugha mwiko ni matumizi ya maneno ambayo kulingana na jamii-lugha husika, hayakubaliki au yamewekewa vikwazo vya kutotajwa hadharani. Maneno kama hayo huweza kutajwa tu kati ya makundi ambayo yana ukawaida fulani. Kulingana na Gao, maneno kama hayo huhesabiwa kuwa machafu na ya kuaibisha. Mbaya (2002) anaeleza lugha mwiko kama matumizi ya maneno au mada ambazo labda kwa mtazamo wa watumiaji lugha hiyo, huzua mtafaruku. Trudgil (1986) anashadidia mawazo hayo kwa kusema kuwa lugha mwiko haiweki wazi mipaka ya kihadhi na kiumri kati ya wazungumzaji.

Lugha mwiko si matumizi ya maneno machafu tu bali wakati mwingine hutumika kama mkakati wa kupitisha ujumbe na kutumika kama mbinu ya kuthibiti lugha ili kukuza na kuendeleza imani na maadili ya jamii. Wataalamu kama vile Adebileje (2012), na Chigidi (2009) wamejaribu sana kuonyesha kuwa matumizi ya lugha yoyote ile huenda sako kwa bako na maadili ya watumiaji lugha husika. Wao wana maoni kuwa lugha ndiyo hudhibiti mahusiano ya kijamii. Inadhihirisha kuwa

watumiaji wa lugha wanatakiwa kuwa waangalifu ili wasiende kinyume na maadili hayo.

Wanajamii-lugha hutekeleza mahitaji ya imani yao kwa kuzingatia mikakati ambayo itawathibiti wasiwakwaze wenzao. Pamoja na mikakati hiyo ni ile ya upole ambayo inapozingatiwa hukuza uhusiano mwema. Watu wanapokiuka matumizi ya mikakati ya upole huwakosea wenzao kimazungumzo. Licha ya kuonyesha ukomavu wao wakati wa mazungumzo, wahusika wa mazungumzo ya *SK* hawaepuki matumizi ya lugha mwiko katika mazungumzo hayo.

Katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), shabiki ‘N’ anathibitisha kukereka kwake anapotumia maneno mwiko kuelezea uzembe wa wanawake ifuatavyo:

Kal.

76. *Igere i ‘Pasta’, mi karusiek isinyen che serkwetin ne matinyei kikaigai. Ngamwa nito eng kainet amu sait age konyitei biich nitok mising. Kalya kwonyik che mengen amut aka ra eng ole iloktoge! Agot nga kiribe tegisto ko ma kele kilach ambururu kele si keek cheptagurin, magat konai chepyosok kole kikwo kasarta no ketuchei agot **kubesto** ye mitei ak manong’otaikwak. Magat kogono ‘appetite’ kalooksetab kwondonyu si mageer nebo chito age.Pto! Yaach cheserwetinik ‘Pasta’.*

Kis.

Unaona nini ‘Pasta’ kuna **wanawake** (*kwa madharau*) kwa kweli ambao ni **wazembe kupindukia**. Acha tu nilitaje hili kwa jina kwa sababu linakera sana. Mbona wanawake wengine wanaonekana kutopambanua kati ya jana na leo kupitia kwa namna wanavaa! Hata ingawa ni kutunza heshima sio eti wavae mavazi makubwa ndio waonekane wastaarabu, wanawake wanatakiwa kujua kuwa wakati ule wa kufunika **paja** hata mbele za waume zao ulipita. Kuvaa kwake mke wangu kunafaa kunipe hamu ya mapenzi ili nisimwone wa mwingine. Pto! Wazembe ni wabaya ‘Pasta’.

Kupitia usemi wake ‘N’ katika mfano huu, mambo mawili yanajitokeza. Kwanza, anakuwa mkweli ili apitishe ujumbe wake bila kupoteza maana. Pili, ‘N’ ni msemaji

asiyependa maelezo ya kimzunguko, anataja kitu kwa jina lake. Anapotumia maneno *karusiek* na *kubesto* (wanawake na paja) anaonekana kukosa heshima kwa wanawake. Neno *karusiek* katika Kikalenjin linaashiria ‘wanawake’ lakini si jina la heshima. Neno hilo si la heshima hata kidogo. Neno *kubesto* (paja) halitajwi wazi katika jamii husika. Inawakera sio tu wanawake bali na jamii nzima ya Wakalenjin.

Shabiki ‘N’ anaonekana mtovu wa heshima kwa sababu anavunja kaida za jamii ya Kikalenjin. Usemi huo unaleta hisia mbaya na huweza kupelekea kujiondoa kwa wasikilizaji ambao labda watoto wao, wakubwa ambao ni wazazi, pia ni mashabiki wa kipindi cha *SK*. Hii ni kwa sababu ‘N’ hajazingatia umri na hadhi za wahusika wote wa mazungumzo. Athari inayojitokeza hapa ni kuwa wasikilizaji wengine labda wanaaibikia usemi huo na hata wengine huogopa kuchangia.

Mfano mwingine wa matumizi ya lugha mwiko ni katika kipindi cha *Supseetab tibik ak kwonyik* (Ubakaji wa wanawake). Maelezo ya Winny kuhusiana na namna ubakaji unatukia yanaonekana kumkera msikilizaji ‘O’ ambaye ni mwanamke. ‘O’ anahisi kuwa Winny anawalaumu wanaume pekee katika kosa hilo. Kulingana naye, wanawake pia huchangia katika ubakaji wao. Anasema:

Kal.

77. *Ngotogu inye kele itetanjini olo bo ko o Winny. Ngamwaun anyun, yaach kwonyik ak tibik agichek. Ngamwa ale ndelachigei komie bichoo ta mami kiy ne yaei kesuub ichek. Amu is i Winny, ae nee chito ne kararan metit kot konam chi buch! Ma lazima kero kiy ne kelal mat eng bortanyi ak katemene kotise kiy age ipkobate koboisie ‘beek’ che ichegei kotise kityo!*

Kis.

Winny, waonekana kuwatetea wanawake sana, acha nikwambie kuwa hata wanawake na wasichana ni wabaya pia. Nitasema hivi, iwapo kina dada wangevaa vizuri, hawangebakwa. Ninauliza hivi Winny, ni nini kitamfanya mtu mwenye akili timamu ambake mwenzake? Si ni lazima ameona kitu ambacho **kimewasha ‘moto’ndani ya mwili**

wake, na ambao hangeweza kuuzima kwa njia yoyote isipokuwa atumie ‘maji’ maalum kuuzima!

Maneno yaliyotumiwa katika mfano 77 ni wazi mno. Baadhi ya maneno ambayo shabiki ‘O’ anatumia ni mwiko katika Kikalenjin. Kwa mfano kishazi *kelal mat eng bortanyi* (kuwasha moto ndani ya mwili wake) ni cha kuaibisha. Mambo kama hayo hayatajwi kabisa panapo watu wasio wa rika moja. Ni wazi kuwa, katika nyakati tulizomo baadhi ya watu hasa vijana hawajali sana matumizi ya lugha kwa sababu wanaona kuwa wameendelea. Hata hivyo, wengi wa Wakalenjin bado wanazingatia maadili ya jamii. Mambo yanayoelezea kuhusu mapenzi hayasemwi na hata imewapasa wanajamii kuchukulia kuwa hayafanyiki. Ni nadra sana kuwapata Wakalenjin wakizungumzia mambo kama hayo kwa sababu yanachukuliwa kuwa mwiko.

4.2.2 Kukatizana Zamu

Licha ya kuwa mazungumzo mengi ya *SK* yamezingatia ubadilishanaji zamu, baadhi yalidhihirisha ukatizaji zamu. Ukatizaji zamu unatokana na msikilizaji kukosa subira au kukerwa na jambo alilosema msikilizaji na anataka kulirekebisha. Ni bayana kuwa kukatizana zamu kunampelekea msemaji kuhisi kuwa anachosema hakithaminiwi. Kama wanavyoelekeza Brown na Levinson (1987), msikilizaji anafaa kutulia hadi msemaji anyamaze na kumwelekeza msikilizaji azungumze. Uelekezi huo ni kupitia maneno kama: ‘nieleze sasa’, ‘maoni yako?’, ‘kazi kwako sasa’, ‘jieleze’, na ‘unasemaje’ miongoni mwa mengine.

Kukatizana zamu ni sifa mojawapo ya mazungumzo ya ana kwa ana au kupitia upigaji simu. Hata hivyo, Kukatizana zamu kulidhihirika katika vipindi vya *SK* japo kwa uchache sana. Sababu kuu ni kwamba, zamu ya kuzungumza kwa mashabiki

ilidhibitiwa na mwasilishaji na mwelekezi wa vipindi. Kukatizana zamu huku kulifanyika baina ya Winny na Rotich.

Katika kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka) Rotich na Winny wanaelekeza kipindi kimpangilio. Hata hivyo, kunatokea wakati ambapo wawili hao hukatizana zamu. Iwapo Rotich anazungumza na Winny labda anataka kuchangia wazo alilozungumzia Rotich, Winny anamkatiza Rotich na kutoa mawazo yake. Vivyo hivyo kwa mwasilishaji wa vipindi, kwamba, Winny anapozungumza na Rotich ana jambo la kurekebisha, Rotich anamkatiza Winny ili asitoe ujumbe tofauti kwa wasikilizaji. Tazama mfano ufuatao:

Kal.

78. **Winny:** *Ngu yo mi ubaguzi sobetab Kalenjin o 'Pasta'. Kalya inye si kou yo matinye kwony sauti. Kele inyalilin chito isise amebute kut i!Yani imuitoi kityo amu ikwondonyi! Uyo ma...*

Kis.

'Pasta', ni kama asasi ya Kikalenjin ina ubaguzi. Yaonekana kuwa wanawake hawana sauti. Yaani mtu anakutesa na unakimya hata hutoi sauti! Unavumilia tu kwa kuwa u mkewe! **Ni kama si...**

Kal.

Rotich:(*akimkatiza*) *Mamanishani kou notok Winny. Imugaksei komanden age eng kong'ung amu aegai kou yo karirenen kot ak kolenji mete chito nani. Ngigere ane ile atebiot ko matinye chi, kelen amache tangoita!' Makergei bi...*

Kis.

Simaanishi hivyo Winny. Kwa kujifanya kukuhurumia kuna uwezekano wa mwingine kukwambia umwache mumeo na uondoke kwako. Atakwambia, 'si unaona mimi ninakaa vizuri bila mume, mimi sitaki mchezo!' **Watu si sa...**

Kal.

Winny: (*akimkatiza*) *Akwong'e kit agenge 'Pasta', kilya inye si koyoni murenik kole iberberegei kwonyik?*

Kis

Ni kitu kimoja kinachonishangaza ‘Pasta’, imani ya wanaume kuwa wanawake hudanganyana.

Mfano huu unadhihirisha ukatizaji zamu katika mazungumzo ya *SK* kwenye redio ya *KASS FM*. Winny na ‘Pasta’ wanachukuliana kama marafiki wa karibu na kwa hivyo kukatizana zamu ni jambo la kawaida. Hata hivyo, hawafanyi hivyo kila wakati. Wao wanazingatia sana upeanaji wa zamu kwa sababu wanataka kuwa mfano mwema kwa wasikilizaji wao. Wanapowarai wasikilizaji kuwapa wengine nafasi, wao hutolea sababu ambazo huwafanya mashabiki wachukulie kuwa wote wanathaminiwa. Ukatizaji wa zamu unavunja sifa mbili za mazungumzo ambazo ni kanuni ya ubadilishanaji zamu na kanuni ya usikivu. Uvunjaji wa kanuni hizi husababisha wahusika wengine wa mazungumzo kukosa nafasi ya kujieleza na hilo si tendo jema. Wasemaji na wasikilizaji wanafaa kuwaheshimu wenzao kwa kuwa wasikivu ili kipindi kipate kuendelea kwa heshima.

Kanuni ya usikivu inaonekana kukiukwa mara nyingi katika vipindi vya *SK*. Hili linadhihirika kila ambapo msemaji anataka kudokeza jambo ambalo msikilizaji labda hakubaliani nalo au kutaka kulishadidia. Mara nyingi, Rotich anaonekana kuingilia kati usemi wa Winny ili kulainisha jambo lililoleweka vinginevyo au kujibu swali aliloulizwa. Rotich anaonekana kuelewa mambo mengine hata kabla ya Winny kumaliza kusoma maswali ya mashabiki wa vipindi vya *SK*. Mfano ufuatao katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa) unadhihirisha ukiukaji wa kanuni ya usikivu na umakinifu. Winny anasoma swali la shabiki mmoja kutoka Chepyakwai katika kata ya Ngeria kaunti ya Uasin Gishu:

Kal.

79. **Winny:** *Kateeb kastoindoni kole, amu nee si ngomanda mureno sang'utab katunisiet komakikerei ko kiy...*

Kal.

(Msikilizaji huyu anauliza hivi, mbona mwanamume akitoka nje ya ndoa haionekani **kuwa jambo ...**)

Kal.

Rotich: *(Akimkatiza) Angen ole tokyingei tebutionoto Winny amu...*

Kis.

(Winny, najua linakoelekea swali hilo kwa **sababu...**)

Mfano 79 unaonyesha kuwa Rotich amekosa kumsikiliza Winny kwa sababu anajua anachotaka kusema. Hali hii inatokea pasi na msikilizaji kukusudia. Mtu hujipata katika hali hii bila mapenzi yake kwa sababu watu wengi hushindwa kujizuia kusema wakati wenzao wanazungumza. Hata hivyo, ni vizuri kuzingatia kanuni ya usikivu na umakinifu kwa sababu mzungumzaji anahisi kuwa mambo yake yanakubalika. Iwapo anakatizwa kila wakati, huenda atahisi kuwa labda usemi wake haumfaidi au hauna thamani kwa msikilizaji.

4.2.3 Matumizi ya Kauli Zinazolenga Kundi Maalum

Wazungumzaji wanapotekeleza mbinu ya upole katika mawasiliano, wao hutumia kauli ambazo ni za kijumla na ambazo hazimlengi yeyote. Hata hivyo, wazungumzaji hawaepuki kutumia kauli zinazolenga kundi maalum kabla ya kumaliza mazungumzo. Hali hii inatokana na sababu tuliyoitoa awali kuwa, kuna baadhi ya wazungumzaji ambao hutaja kitendo cha kutishia uso kimakusudi. Aidha, msikilizaje anaweza kufasiri ujumbe wa msemaji kama wenye kuathiri hisia zake.

Vipindi vya *SK* vimeshuhudia huu ukiukaji wa mikakati ya upole wakati wa mazungumzo. Sana sana, ni mwasilishaji na mwelekezi wa vipindi ambao wametumia kauli kama hizo lakini kwa uchache sana. Hali kwamba wao wanatumia kauli hizo inatokana na sababu kuwa wao wametagusana kwa muda mrefu na kwa hivyo umbali wa kirafiki kati yao ni mdogo sana. Brown na Levinson (1987) wanasema kuwa utekelezaji au ukiukaji wa mkakati wa upole unategemea ukaribu au umbali wa kirafiki kati ya wahusika wa mazungumzo. Wakati mwingine, wahusika wa mazungumzo hasa wasiklizaji, wanaweza kupuuza kitendo cha kutishia uso kwa kuuona kama mzaha na badala yake kujaribu kuelewa anachomaanisha msemaji. Kecses (2010) anaonyesha jinsi watu wanaweza kufanya kitendo kinachotishia uso kuonekana cha kawaida. Anatumia mfano wa mazungumzo kwa lugha ya Kiingereza kati ya Mchina (mhudumu hotelini) na mwenzake kutoka Australia (mteja) ifuatavyo:

Mhudumu : *Can I get you some more coffee Sir?* (Bwana mkubwa, nikuongezee kahawa?)

Mteja : *Who is stopping you?* (Nani anakukataza?)

Mhudumu : *You want to stop me?* (Unataka kunikataza?)

Mteja : *Oh no, just bring me your damn coffee.* (Ah hapana, leta tu hiyo kahawa yako).

Mfano huu unaonyesha jinsi ukosefu wa upole katika usemi wa mteja umemezwa na mhudumu wa hoteli (Mchina) ambaye ameelewa kile ambacho tamko linamaanisha kuliko kile ambacho tamko hilo la mteja lingeweza kuzua. Kutokana na habari hiyo, ‘Koriryo’ na ‘Pasta’ wanafanyiana utani na hivyo kuonekana kutotishia nyuso zao. Katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), ‘Pasta’ Rotich anamweleza Winny jinsi wanawake wanawaonea wanaume. Anahoji kuwa kuvunjika kwa ndoa hokusababishwi na wanaume pekee. Anasema:

Kal.

80. *Ngap sait age otinye ng'alek Winny, ochame olaumeni murenik eng kiy age tugul. Ngotwek mureno, ole kakobol, koteb kiy, ole kakobol, kokon dairekshon, ole kakobol. Ara ii, sikosis kityo chichi ne makotinye sauti ak kelen metitab kot i!*

Kis.

Winny, hata **ninyi mna** mambo wakati mwingine, **mnapenda kuwalaumu** wanaume kwa kila tendo. Mwanamume akisema kitu, **mwasema** amepiga makelele, akiulizia chochote, **mwasema** amepiga makelele, akitoa mwelekeo, **mwasema** amepiga makelele. Sasa, huyu mwanamume anyamaze tu bila kutoa sauti na hali ndiye kichwa cha nyumba!

Mfano 80 ni usemi wa Rotich kwa Winny ili kuonyesha kosa la wanawake. Rotich anatumia maneno yanayolenga kundi fulani maalum na ambayo yanaonyesha kuwa Winny ni mmoja wa kundi hilo. Maneno *otinye* (m-na), *ochame* (m-napenda), *olaumeni* (m-nawalaumu) na *ole* (m-nasema) ni ya nafsi ya pili wingi. Kiambishi awali 'o' katika Kikalenjin ni sawa na kiambishi awali 'm' cha Kiswahili ambacho huashiria nafsi ya pili wingi. Katika mifano ya maneno hayo, kiambishi 'o' (m) kinamjumuisha winny pamoja na wanawake wengine wanaozungumziwa na Rotich.

Iwapo uhusiano kati ya Rotich na Winny ungekuwa mbali, maneno hayo yangetishia uso wa Winny. Hii ni kwa sababu Rotich ametumia maneno ambayo yanalenga mtu au kundi maalum. Kama Rotich angetaka kujiepusha na mambo ya kutishia uso wa msikilizaji, angetumia maneno ya jumla kama vile: *kwonyik* (wanawake), *olo bo go* (wale wa ndani ya nyumba), *kwonyik alak* (wanawake wengine) miongoni mwa maneno mengine. Hata hivyo, hamna madhara kwa hisia za hao wawili kwa sababu wamezoeana sana.

4.2.4 Kuzungumzia Mada Zinazotishia Uso wa Hadhira

Brown (1990) anaeleza kuwa uso wa msikilizaji unafaa kutiliwa maanani kabla mzungumzaji hajasema lolote. Anasema kuwa uso ni haja ya kutolazimishiwa kitu. Dhana ya uso ni msingi wa nadharia ya upole kwa sababu inachukua sehemu kubwa katika uchanganuzi wa upole. Pamoja na matendo yanayotishia uso chanya wa msikilizaji ni kuzungumzia mada ambazo ni mwiko. Msemaji anaposema kile anajua kuwa kulingana na kaida za jamii husika si vizuri kutaja, atakuwa anatekeleza kitendo cha kutishia uso wa msemazwa.

Vipindi vya *SK* vinajaribu sana kuhepa mada ambazo zinatishia nyuso za wahusika wa mazungumzo. Kwa kawaida, msemaji na msemazwa hujaribu wawezavyo ili kuendesha mazungumzo kwa heshima na amani. Hata hivyo hapana chema kisicho na dosari. Wahusika wa mazungumzo haya ya *SK* wanajipata japo kwa mara chache wakizungumzia mada ambazo kwa wengine zinazua hisia za kukera. Kuna uwezekano kuwa wazazi wengine ambao labda umri wao unapiku ule wa mwasilishaji, wanakosa kuchangia mada zingine ambazo wanaaibika kuzijadili.

Mada mwiko huathiri nyuso za wahusika wa mazungumzo kwa njia hasi. Winny na Rotich wanataja mada kama hizo kimzunguko lakini wakati mwingine wanalazimika kutaja mengine kwa majina kamili. Hilo linafanyika wakati ambapo wanakosa neno au maneno mbadala. Kwa mfano katika kipindi cha *Kolokset eng katunisiet* (Mavazi katika ndoa), Winny anasimulia kisa cha baba aliyekuwa akimnunulia bintiye mavazi mafupi mno. Kwa kutaja sehemu za mwili, Winny anatoa taswira kamili ya jinsi mapaja ya msichana huyo yalionekana alipokuwa akitembea na Rotich anamkatiza kwa sababu maelezo yake yalikuwa wazi mno.

Kal.

81. **Winy:** *Kimi boiyo oliny ne kicham kwolchin tibikyikyik ngoroik che nwogen mising kot ko kiga kokwong'e biik. Kicham kotogu kubesoik che birireeen kot ak ko kima komi 'space'katikati nebo kelyekyik. Yaani hee, mongen ole amwoitoi agot ale...*

Kis.

Kulikuweco na mzee mmoja huko kwetu aliyependa kumnunulia bintiye nguo fupi fupi hata watu wakashangazwa naye. **Mapaja meupe yalikuwa yakionekana** na kuharibu zaidi **hakukuwa na nafasi katikati ya miguu yake**. Yaani sijui nisemeje...

Kal.

Rotich: *Ngoyam Winy, oiye matata imwa, ingele matachomei bikyokchebo Kalenjin kemwa lagok is. Ingele matachamei kemwa kebeberwek alak chebo borto is. Mangele kikewalak ilen kiwalagis tuguk tugul Winy, ta koribei tegis chitab Kalenjin ngachang'an ko Nandiindet.*

Kis.

Winy, itoshe, usiendeleo kusema, unajua watu wetu, Wakalenjin, hawapendi sana unapozungumzia watoto. Pia, unajua kuwa hawapendi kuzungumzia sehemu zingine za mwili. Usije ukafikiria kuwa inaposemekana kuna mabadiliko ukadhani vitu vyote vilibadilika, Wakalenjin bado wanatunza heshima na hasa Mnandi.

Kupitia kwa mfano huu, Rotich anamtahadharisha Winy dhidi ya kutaja mambo mengine bayana. Ni muhimu kutaja kuwa, umri wa Rotich na Winy unatofautiana kidogo na ndio sababu kuu ya Rotich kuwa makini sana. Vipindi vya *SK* vinazungumzia mada ambazo mara nyingi huchukuliwa kuwa mwiko katika jamii za Kiafrika. Mada kama vile: sehemu nyeti za mwili, ngono, magonjwa yasio na tiba kwa kutaja machache, ni mada mwiko katika jamii ya Wakalenjin hasa Wanandi.

Mfano mwingine wa mada inayotishia uso chanya wa msikilizaji ni katika kipindi cha '*Mpango wa kando*' ('Mpango wa Kando'). Rotich na Winy wanazungumzia sababu za wanaume kuwa na mipango ya kando. Mojawapo ya sababu hizo ni wanawake

kutoonyesha upendo kwa waume zao. Winny anaeleza kuwa wanawake husahau majukumu yao punde tu wanapozaa. Anaendeleza kuwa wanawake huhisi kuwa hawana haja ya kuwa makini tena kwa mahitaji ya waume zao kwa sababu wamezaa watoto na hivyo kuweka mizizi thabiti bomani. Winny anadokeza:

Kal.

82. *Igeere ii 'Pasta', chepyosok isinyen kobwati kole kikimutu nyo kosigis kityo. Haja nenywa ko kobiit keswekap koi kitun. Agot ndawendi boiyot kasi kenyit, ko mamage kiy bora koribogis lagok. **Ingen as kosigis, kosigis kityo!***

Kis.

Unajua nini 'Pasta', wanawake wanafikiria kuwa waliolewa kuzaa tu. Haja yao ni kutunza 'mbegu' ya jamii iliyomwoa ili kuwe na mwendelezo wa uzazi. Hata mumewe akienda kazini mwaka mmoja, mke hajali mradi watoto wawe na malezi mazuri lakini **kuzaa sasa ndio wanajua sana, kuzaa tu!**

Kutokana na mfano 82, sentensi *Ingen as kosigis, kosigis kityo!* (Kuzaa ndio wanajua sana, kuzaa tu!) ni yenye kutishia uso wa wanawake. Hata hivyo, ujumbe huo hautishii uso wa wanawake pekee bali hata wanaume kwa sababu uzazi unachukuliwa kuwa jambo la kiasili na huaminika kuwa ni majaliwa kutoka kwa Maulana. Hiyo ndiyo sababu Wakalenjini hukwepa kutaja idadi kamili ya watoto walio nao. Mtu akiuliza idadi ya watoto wa mtu fulani, jawabu atakalopata ni *sere* yaani wengi tu. Inaaminika kuwa ni mwiko kutaja idadi ya watoto kwa sababu ni kama kujivunia watoto na inaaminika kuwa kitu kibaya kinaweza kuwapata watoto hao.

4.3 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia athari zinazojitokeza wakati ambapo wazungumzaji huteua kutumia au kupuuza mikakati ya upole wanapowasiliana. Kutokana na mchakato wote wa uchanganuzi, ni bayana kuwa matumizi ya kila mkakati yanazua athari chanya na hasi. Jambo hili hutokea kwa sababu wazungumzaji hutofautiana kimawazo na hii

hupelekea kutofautiana wakati wa kuwasiliana. Wazungumzaji katika vipindi vya *SK* wameteua kutumia mikakati ya upole ili kukidhi mahitaji ya nyuso zao. Hata hivyo, sura hii imeonyesha kuwa baadhi ya wahusika wamelazimika kupuuza mikakati ya upole ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa bila utata.

Iliyobainika, matumizi ya mikakati ya upole hayafanyiki bila mzungumzaji kujua. Wakati wa mazungumzo, msemaji hupanga maneno yake ili yalete maana lakini kwa kuzingatia hisia za msemazwa. Wazungumzaji katika vipindi vya redio vya *SK* wamedhihirisha uwezo huu wa kutekeleza au kupuuza mikakati ya upole kimuktadha kutegemea athari na hali ya wakati wa mazungumzo. Sura inayofuta imeshughulikia hali anuwai zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole pamoja na changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mikakati hiyo.

SURA YA TANO

HALI ZINAZOATHIRI UTEUZI WA MIKAKATI YA UPOLE NA CHANGAMOTO ZA MIKAKATI HIYO KATIKA VIPINDI VYA *SOBETAB KAPCHI*

5.0 Utangulizi

Sura ya nne imechanganua athari za uzingatiaji na ukiukaji wa mikakati ya upole katika vipindi vinavyotafitiwa. Athari hizo hutokana na hali ambazo haziepukiki. Ni kwa msingi huo ndipo sura hii ya tano inashughulikia malengo ya tatu na ya nne ya utafiti kwa kuainisha na kuchanganua hali zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole, na changamoto za mikakati hiyo. Kwa kuangazia hali za uteuzi wa mikakati ya upole, mtafiti ameinisha hali kama vile tofauti za kijinsia, kimamlaka na kiumri kama vigezo vikuu vya uteuzi katika sehemu ya kwanza ya sura hii. Mtafiti ameelezea namna washiriki wa mazungumzo hulazimika kutumia mkakati mmoja kuliko mwingine kwa kutegemea hali na muktadha wa mazungumzo.

Sehemu ya pili ya sura hii imeangazia changamoto wanazokumbana nazo wazungumzaji wa *Sobetab Kapchi (SK)* wanapotekeleza mikakati ya upole. Mtafiti ameinisha na kufafanua changamoto hizo kwa kuchanganua mazungumzo baina ya wahusika katika vipindi husika vya *SK*. Ufafanuzi unaotolewa ni kwa mtazamo wa Nadharia ya Upole na kanuni za mazungumzo ambazo zina muumano na Nadharia ya Upole. Aidha, changamoto hizo zimeangaziwa kwa misingi ya hali zinazolazimisha matumizi ya mkakati hata wakati ambapo ni dhahiri kuwa una uwezo wa kutishia uso.

SK ni vipindi ambavyo vina wahusika wa umri tofautitofauti na kwa hivyo mahusiano ni tofauti. Maingiliano baina ya wahusika hao, hutegemea hadhi zao pamoja na kuzoeana kwao. Mazungumzo baina ya mwasilishaji mkuu, mwelekezi wa vipindi na

mashabiki wa *SK* hudhibitiwa na hali mbalimbali za kijamii. Aidha, hali hizi zina mchango mkubwa katika uteuzi wa lugha inayotumiwa baina yao. Katika mchakato wote wa kuchanganua hali hizo, mtafiti amejikita katika mazungumzo kati ya Pasta Rotich ambaye ni mwasilishaji mkuu na Winny Jepkorir ambaye ni mwelekezi na mashabiki wa vipindi husika vya *SK*.

5.1 Hali Zinazoathiri Uteuzi wa Mkakati wa Upole

Matumizi ya mikakati ya upole huathiriwa na hali nyingi. Hii ina maana kuwa kuna mwingiliano mkubwa baina ya matumizi ya mikakati ya upole na masuala ya kijamii. Masuala kama vile: jinsia, hali za kiuchumi, umri, hadhi ya wazungumzaji katika jamii husika na malengo yao ni baadhi yazo. Maoni hayo yanaafikiana na ya Brown na Levinson (1987) wanaosema kuwa kila wakati mzungumzaji anapotekeleza kitendo kinachotishia uso, huongozwa na seti ya kanuni zinazobainishwa na uzito wa kitendo hicho.

Brown na Levinson (1987) wanabainisha hali muhimu za kijamii, zinazomwongoza msemaji kuteua mkakati atakaotumia kuwasilisha ujumbe wake. Hali hizi ni pamoja na: uhusiano wa kijamii kati ya msemaji na msikilizaji, hali ya tendo la kutishia uso na uhusiano kimamlaka wa wahusika wa mazungumzo. Hali hizi humwongoza msemaji kuteua jinsi ya kuzungumza kimpangilio ili kukidhi mahitaji ya uso wa msikilizaji wake. Kwa kuyatilia nguvu mawazo ya Brown na Levinson, Yule (1996) anasema kuwa mtagusano wa kiisimu kwa kawaida huwa ni aina ya mtagusano wa kijamii. Kwa kusisitiza wazo hilo, Yule anadokeza kuwa lazima masuala ya ndani na nje, yanayotawala mahusiano husika, yatiliwe maanani.

Masuala ya ndani huhusisha maingiliano ya kijamii yanayohusisha mtu binafsi kama vile uhusiano wake na wengine. Masuala ya nje huhusu hadhi mbalimbali

zinazoshikiliwa na wanajamii. Hata hivyo, Brown na Levinson (1987) wanaweka hali hizo zote katika hali mbili kuu ambazo ni faida apatazo msemaji kwa kutumia mkakati fulani na hali za kijamii.

5.1.1 Faida za Mkakati

Msemaji hutumia mkakati wa upole kwa sababu una faida kwake. Msemaji ana uwezo wa kupunguza vitisho kwa uso kwa kumhakikishia msikilizaji kuwa anampenda na anataka kumtimizia mahitaji yake. Hivyo, uso wa msikilizaji hautatizwi na msemaji kwa kuwa wote wanahitaji kujaliana. Kwa mfano: **twende tunywe soda**. Mfano huo unaoyesha kuwa msemaji amepunguza vitisho vya uso kupitia usemi wake ambao unaonyesha kitendo kinachomjumuisha pamoja na msemaji. Zifuatazo ni faida azipatazo msemaji anapotumia kila mkakati wa upole:

5.1.1.1 Faida za Mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi unamhitaji msemaji kutaja mambo yalivyo bila kujali vitisho kwa uso wa msemajwa. Sababu kuu ni kuwapa nafasi wasikilizaji kupata ujumbe kamili uliokusudiwa na msemaji. Mkakati huu una faida kwa msemaji kwa sababu: kwanza, anaonekana mwaminifu kwa kutaja mambo yalivyo bila kuficha lolote. Pili, msemaji anaonekana kumwamini msemajwa kwa kumwambia kila kitu ilivyo. Tatu, msemaji anapata sifa kwa kuzungumza bila uoga, nne, hutoa nafasi nzuri kwa msemaji na msikilizaji wa kueleweka na mwisho, msemaji ana uwezo wa kurejesha uso wa msikilizaji kwa kutumia maelezo baada ya usemi wenye kutishia uso.

Wahusika katika mazungumzo ya *SK*, hasa mwasilishaji mkuu na mwelekezi wa vipindi, wanatumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi kwa kuzingatia faida zake. Katika kipindi cha *Suupsetab tibik aka kwonyik* (Ubakaji wa wanawake), Winny na

Rotich wanajadiliana kuhusu tabia ya kinyama ambayo imekithiri miongoni mwa wanaume. Kwa njia huru kabisa, Rotich anakemea tabia ya ubakaji kwa kutumia maneno halisi ya kitendo hicho bila kukwepa lolote kwa kusema:

Kal.

83. *Matinye keuny chuto Winny, yaach murenik alage iman ne matinye kerop taban. Kalya si kochut chito oik kot ko makongen amut ak ra! Kele ng'etei chito iman ak koregune ngorietab orit lakwenyi ne kisichei i! Korotikyik i! kot koyaat kabisa long'it ak kotoi kasit i! uyo memukaksei Winny. Aiya kikorukan metit chito is! Kalya okwek o kastoikyok! Kalya iman o murenono iyae ng'olyondono, rektaun kasinotok iman? Ingen nee Winny, kasinotok isinyen komochei koyan biik tuwai si korekto, ambuch i, ot ot ot ot, **luktoi bich moo** kaiya is ngot ko ter ole kigiyaita biik alak.*

Kis.

Hili halifichiki Winny, bila kupitia kando, kwa kweli wanaume wengine ni wabaya. Mbona mashetani wamwingie mtu hadi hajui tofauti ya leo na kesho! Ni kweli mtu ana ujasiri wa **kumvua nguo bintiye aliyemzaa! Damu yake! Hata akafungua suruali na kuanza kazi!** Winny, ni kama haiwezekani, labda tu kama amerukwa na akili. Wasikilizaji wetu, mbona hivyo kweli! Kwa mwanaume unayefanya hivyo, una hata hamu? Winny, unajua nini, hali hiyo inahitaji ukubalifu au maridhiano ya wawili ndipo kazi iendelee, la sivyo, oh oh oh oh, **hamu itapotea kabisa** labda tu iwapo watu wengine waliumbwa tofauti.

Mfano 83 unadhihirisha jinsi 'Pasta Rotich' ametumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi kueleza kile ambacho wanaume wabakaji hufanya. Rotich amesema mambo kinagaubaga bila kuficha lolote. Kupitia usemi huo, Rotich amefaulu kupitisha ujumbe usiokuwa na utata. Aidha, amefaulu kutumia ujasiri wake kutoa taswira ya jinsi mambo yalivyo mabaya wakati wa utekelezaji wa jambo kama hilo. Mbinu hii, licha ya kutishia uso wa msikilizaji, inakubaliana na kaida ya kiasi na kaida ya namna katika kanuni ushirika kama ilivyopendekezwa na Grice (1975). Grice anapendekeza mbinu ya kuwa wazi ili kuzuia utata ambao unapelekea msikilizaji kufasiri ujumbe kwa maana ambayo haikukusudiwa na msemaji.

Mfano wa pili uliozingatia faida ya kutumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi ni katika kipindi cha *Tilyandit eng katunisiet* (Uhusiano katika ndoa). Mwasilishaji mkuu pamoja na mwelekezi wa kipindi wanajadiliana kuhusu marafiki katika ndoa. Winny anamwuliza Rotich iwapo jamii mbili zinaweza kuwa marafiki hadi mwanamume 1 anaweza kwenda kumtembelea mke wa mwanamume 2 bila uwepo wa mkewe au mwanamume 2. Kwa kumjibu, Rotich anaweka wazi hatari zilizopo kwa mahusiano yaliyozidi kiasi kama hayo. Kwamba, hali kama hiyo husababisha kukosana kwa marafiki wengi kutokana na sababu kuwa “mambo yanaweza kubadilika” wakati wowote. Anasema:

Kal.

84. *Maya chorwandit Winny. Kararan ye kakosyin choronok amu lochingei milosiek. Agot nga no anyun komugaksei Winny kelochigei milet kot kela che machamndootin kelochigei. Ingen is ile nganyo koing'ung kila ko mami boiyong'ung i Winny, koitei kenaitegei kot kemwochigei shideshek che kitinye... ingen ile egu ngalek otomatik is Winny, kinyoche ko kikechor tugukab bich ama kinai amu kikerikyigei mising.*

Kis.

Winny, urafiki si mbaya. Ni muhimu kwa marafiki kujaliana kwa sababu wanabebeana mizigo. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kubebeana visivyokubalika. **Unajua, nikija kwako mara nyingi bila uwepo wa mumeo, itafika wakati ambapo tutazoeana hadi tukafunuliana siri au kusema shida tulizo nazo... Winny, nakwambia mambo yatafanyika bila kupangwa! Tutajipata tumeiba ‘vitu vya wenyewe’ bila kujua kwa sababu ya ukuruba wetu.**

Mfano huo unaonyesha jinsi Rotich anachukua muda mrefu kumfafanulia Winny athari za uhusiano wa karibu sana kati ya familia. Pasta Rotich anasema maneno jinsi yalivyo na yanavyotendeka bila mzunguko wowote. Wasikilizaji pamoja na mwelekezi wa kipindi wanapata kwa njia ya moja kwa moja anachomaanisha Rotich bila utata wowote. Mbinu hii haizingatii uokoaji wa uso kwa sababu faida ni kwa

msemazwa. Aidha, msemaji naye anafaidika kwa kutumia maneno machache kueleza jambo. Pia, msemaji hana gharama ya kujali uso wa msikilizaji.

5.1.1.2 Faida za Mkakati wa Upole Chanya

Mkakati wa upole chanya unawaweka msemaji na msikilizaji kwenye kiwango kimoja. Mkakati huu unasisitiza kuwa msemaji amzingatie msemaji wakati wa mazungumzo ili msikilizaji asihisi kutengwa. Faida za mkakati huu ni kwamba vitendo vya kutishia uso vinaweza kupunguzwa kupitia usemi wa msemaji ambao unadhihirisha kuwa yuko katika hadhi au nafasi sawa na msikilizaji. Hii ina maana kuwa msemaji atajaribu awezavyo kupenda apendacho msikilizaji, atajitolea kwa mambo mengine licha ya kutoa maelekezo kwa msemazwa na kwamba msemaji ajihusishe na msemazwa kama wahusika katika nafasi sawa. Mkakati wa upole chanya hutoa nafasi kwa msemaji kukidhi mahitaji ya uso chanya wake na wa msikilizaji.

Kipengele muhimu katika mkakati wa upole chanya ni udhihirishaji wa hali sawa kati ya msemaji na msikilizaji. Brown na Levinson (1987), wanadai kuwa kutaka kuwa na nafasi sawa katika mawasiliano ni muhimu sana katika upole chanya. Hii inawezekana tu iwapo kuna mazungumzo yanayozingatia mahitaji ya wahusika wote wa mazungumzo kwa njia ya udhihirisho wa sifa za ufanano. Sifa hizi ni pamoja na ufanano wa: mawazo, mapendeleo, nia, mtazamo na ujumuishaji wa kimakundi (Lyons, 2007).

Katika Vipindi vya *SK*, wahusika wakuu ambao ni Rotich na Winny wanatumia mkakati wa upole chanya katika mazungumzo yao na hadhira husika. Kupitia kipindi cha *Kasarta ne kibetei lol* (Wakati wa kupeana talaka), Winny anaeleza jinsi wanawake wengine hukimbilia mambo ya talaka pasi na kufikiria yatakayowapata

watoto. Winny anasema kwamba wanawake wengi wanakumbatia sehemu ya katiba mpya inayozungumzia ugawaji wa mali kati ya mume na mke wanapotalikiana. Anaendeleza kuwa bila kujua muktadha wote wa kipengele hicho cha sheria, kina mama hao huwatafutia makosa waume zao ili wakosane na kutaka talaka. Anaeleza hivi:

Kal.

85. *Mabotech 'Pasta', kiyai Mungu muren ak kong'at kobois. Achek ko kigilenjech kinyal manong'otoikyok engkiy age tugul amu makitinye kiy ne nenyoy. Nguno ngekas kele mi ng'atutiet ne ribech ak koyoni kesige kiy, kegase kotakibesio haraka si kenyoru tugun che chechok.*

Kis.

Sio kosa letu 'Pasta', Mungu alimuumba mwanamume na kumwamuru afanye kazi. **Sisi** tuliamriwa kutazamia chochote kutoka kwa waume zetu na pia watutawale kwa sababu hatuna kilicho **chetu**. Sasa tukisikia kuwa kuna sheria **inayotulinda** na kutupa uwezo wa kupata kitu, tunatamani tutalikiane haraka ili tufaidike.

Kupitia kwa mfano 85, Winny anajijumuisha pamoja na kikundi chote cha wanawake. Licha ya kuwakosoa, Winny anapata faida ya kukubalika kwa wanawake wenzake kwa kujijumuisha nao kama unavyodai mkakati wa upole chanya. Faida nyingine ni kwamba, wasikilizaji wote kwa ujumla wanapata mtazamo mzuri kuhusiana na mwelekezi wa kipindi kwa sababu anawaelekeza wanawake kuona makosa yao.

Faida nyingine ya mkakati wa upole chanya unadhihirika katika kipindi cha *Tililindo eng Katunisiet* (Usafi katika ndoa). Winny anatoa pendekezo lake kwa Rotich kuwa wanaume wanafaa kuwajibika katika usafi wa wake zao. Anasema kuwa wanaume wengine wana mazoea ya kuwamezea mate wake za watu wengine ambao wameng'ara bila kujua wameng'arishwa na waume zao. Winny anahoji kuwa kila mwanamume anapaswa kumvisha na kumtunza mkewe ipasavyo ili kila mtu atosheke

na maji ya “kisima chake”. Kwa kumjibu, Rotich anawatetea wanaume kwa kutumia maneno yanayomjumuisha pamoja na wao ifuatavyo:

Kal.

86. *Wooi, moborotech missing ibogei Winny. Ngaortotech missing nga sine mi iman murenik cheu choto kemwa. Mi sinyen agichek chepyosok cheu chukai kamwae Winny. Che matiny kakiipchi sabunit, omo, ‘downy’ ak ngoroik che kororon kolochi ngoriet agenge ipkochomit nding!*

Kis.

Wooi, haki Winny **msitulemee** sana. Ni kama **mmetusingizia** sana hata hivyo, kuna pia wanaume walio na tabia kama hizo ulizozitaja. Kuna pia wanawake ambao hata wakiletewa sabuni, omo, ‘downy’ na mavazi mazuri, wana mazoea ya kuvaa nguo moja mpaka inanuka nding!

Usemi huu wa Rotich unaonyesha kuwa Rotich anajiweka katika kategoria moja na wanaume wenzake. Yeye hajitengi na wao hata ingawa anajihusisha nao kwa jambo linalowakosoa. Rotich anafaidika kwa vile wanaume watakuwa na imani naye kwa sababu anawaelewa. *Moborotech* (msitulemee) na *ngaortotech* (mmetusingizia) ni ya nafsi ya kwanza wingi. Kiambishi -tu- katika maneno hayo yanamshirikisha Rotich pamoja na wanaume wengine. Aidha Rotich anafaulu kupitisha ujumbe wake kwa wanaume wanaopuza mahitaji ya wake zao. Faida nyingine ni kwamba, kupitia kwa usemi wake, wanawake watarekebisha tabia zao za kuwa wachafu bila kuhisi kuwa wanatengwa. Mbinu ya kutumia mkakati wa upole unawanufaisha wahusika wote wa mazungumzo kupitia usawa katika nafasi zao.

5.1.1.3 Faida za Mkakati wa Upole Hasi

Mkakati wa upole hasi unadai kuwa msemaji awe na mahitaji ya msikilizaji katika mawazo yake. Kwamba, ajue kuwa msikilizaji ana mahitaji ambayo anataka yakubalike na kutekelezwa. Mkakati wa upole hasi una faida kama vile: msemaji

ataonekana kuwa na heshima kwa msikilizaji, msemaji atadumisha urafiki kati yake na msikilizaji na matumizi ya maneno yasiyo ya moja kwa moja yatamfanya msemazwa kuonekana kumjali msikilizaji. Msemaji anapotekeleza mambo hayo anaonyesha kuwa anajua mahitaji ya msemazwa.

Mbinu ya mkakati wa upole hasi inalenga kupunguza vitisho kwa uso hasi wa msikilizaji kwa kuepuka ulazimishaji wa mambo kwake. Mkakati huu humhitaji msemaji kupunguza matumizi ya maneno ya moja kwa moja, kuomba radhi, kutumia maswali kama vitangulizi, kutumia viwakilishi vya wingi na kuwa mrajua. Ni vyema pia kutaja kuwa lengo kuu la mkakati wa upole hasi ni kwamba msikilizaji atekelezewe jambo na msemazwa bila ulazimishaji na pia kwamba unadumisha heshima kati ya wahusika wa mazungumzo. Aidha, inazuia kuzoeana sana kwa wahusika wa mazungumzo ili kila mmoja awe na nafasi yake.

Vipindi vya *SK* vilishuhudia matumizi ya upole hasi mara kadhaa. Mwelekezi wa vipindi alidhihirisha matumizi ya mbinu hii katika kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwondo age* (Sababu zinazompelekea mwanamume kuo a mke mwingine). Winny anawalaumu wanaume kwa tabia ya kukimbilia kuo a mke mwingine badala ya kutafuta makubaliano. Anatetea kuwa kuo a sio suluhu bali ni kukimbia shida ambayo labda wangekabiliana nayo na wangepata suluhu. Rotich anamjibu Winny kwa upole:

Kal.

87. *Nyoiwo kaat 'Koriryo' ee ak kwonyik tugul amu kiy ne awendi amwoe. Ng'wan iman eng kwonyik lakini aisuru ngamwa ane sionyoivo kaat. Ma chametab murenik kotunis kogeny ipkobate ngap komi kwonyik che makonu agot nafas ne king'olole.*

Kis.

'Koriryo' na wanawake wote kwa ujumla, **nisameheni** kwa kile ninaenda kusema. Ninajua ni uchungu kweli kwa wanawake lakini

haidhuru, acheni niseme tu **kisha mnisamehe**. Si mapenzi ya wanaume kuoja tena bali kuna wanawake wengine ambao hawatoi hata nafasi ya mazungumzo.

Maneno *nyoiwo kaat* (nisameheni) na *si onyoiwo kaat* (kisha mnisamehe) yanaonyesha uombaji radhi. Kwa unyenyekevu, Rotich anawakosoa wanawake kwa kutotoa nafasi ya mazungumzo lakini hilo analifanya kwa uangalifu sana asije akatishia uso hasi wa msikilizaji. Faida anazopata Rotich ni kwamba anafaulu kupitisha ujumbe aliokusudia kwa wanawake kwa kupunguza vitisho kwa uso hasi wa msikilizaji. Aidha, msemaji amedumisha heshima baina yake na msikilizaji kupitia ukwepaji wa kusema mambo bayana. Msikilizaji naye amefaidika kwa sababu mahitaji ya uso wake yamekidhiwa na msemaji.

Mfano wa pili katika mkakati wa upole hasi unapatikana katika kipindi cha *Mpango wa kando* (Mpango wa kando). Winny anashereheshea wazo la Rotich kuwa wanaume wengine hawatosheki hata wake zao wakikubali kuwatosheleza kimapenzi katika tendo la ndoa. Winny anahoji kuwa miaka inapobadilika, watu pia hubadilika. Anaendeleza kwamba wanaume wa siku hizi wana mazoea ya kufanya mapenzi na wanawake zaidi ya mmoja. Anasema:

Kal.

88. *Angen ale iyanwo nito murenik tugul 'Pasta', tugul koboten sinyen amu agot nga i Pasta ko i chito kora ago i muren. Tos meyani akinye ile kokoziden murenik i! Ingen kochulchul komosi ak komosin amu mengem kotebi ak kwondo agenge. Chomei koyaei che kile 'comparison'.*

Kis.

Ninajua wanaume wote watakubaliana nami kwa hili 'Pasta', yaani wote pamoja na wewe kwa sababu licha ya kuwa u mchungaji, wewe ni binadamu mwanamume. **Je, si hata wewe pia unakubali** kuwa wanaume wamezidi! Wanajua kupita huku na huku kwa sababu hawajui kukaa na mwanamke mmoja. Wanapenda kulinganisha wanawake.

Mfano 88 unatoa taswira kamili ya wanaume. Winny anaonyesha jinsi mambo yamebadilika. Hata hivyo, anafanya hivyo kwa kuzingatia uso wa hadhira. Hilo anatekeleza kwa kutumia usemi unaodhihirisha urajua. Kama tulivyotanguliza katika sura ya pili, kuwa mrajua ni kutarajia mazuri. Kirai *angen ale iyanwo nito murenik tugul* (ninajua wanaume wote watakubaliana nami kwa hili) ni usemi wenye urajua. Winny anatarajia kuwa wanaume watakubaliana naye.

Vilevile katika mfano huo wa 88, Winny anatumia maneno *tos meyani akinye ile* (je, si hata wewe unakubali kuwa) kama vitangulizi kabla ya kutaja kitendo kinachotishia uso. Vitangulizi hivyo huwa ni maswali ambayo mara nyingi hayahitaji majibu. Kusudi la maswali hayo ni kumtayarisha msikilizaji kusikia kitendo kinachotishia uso lakini hakina makali sana.

Matumizi ya viwakilishi vya wingi ni mfano mwingine wa matumizi ya mkakati wa upole hasi. Mbinu hii inadhihirika katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Sababu za kuvunjika kwa ndoa). Rotich na Winny wanaongoza mjadala kwa kuelezea sababu zinazopelekea ndoa kuvunjika. Akieleza kwa undani, Rotich anatumia kielelezo cha mwanamume mmoja aliyekuwa akimlazimisha mkewe wafanye kitendo cha ndoa kupitia sehemu ya kwendea haja kubwa. Anaendeleza hadithi hiyo kuwa mwanamke huyo alilazimika kutoroka baada ya kuumizwa na mumewe siku zote na hangeweza kuvumilia tena kitendo hicho. ‘Pasta’ anasema:

Kal.

89. *Arirenok kwonyikyok, arirenok iman. Okwek oloe miletab lagok, manong’otoikwok ak tilyanutik tugul. Cholwok murenik amu inyalilok ako magerei boisionicho te cho. Achek kemoche kityo kenyorchigei magutikyok agot che yachen. Ingorire kipsengwet ak konyochi kaat murenik che u chotok amu ichek ko mengen kit ne yaei.*

Kis.

Nawahurumia sana kina mama, nawahurumia kweli. **Ninyi** mnabeba mizigo ya watoto, waume zenu na wanajamii wote. Wanaume ni wachokozi kwa sababu wanawatesa bila kuona kazi nyingi mnazotekeleza. **Sisi** tunataka tu tujipatie mahitaji yetu hata yale mabaya. Hebu mbingu iwahurumie na kuwasamehe wanaume kama hao kwa sababu **wao** hawajui watendalo..

Mazungumzo ya Rotich katika mfano huu yanaonyesha jinsi mkakati wa upole hasi unaweza kushughulikiwa kupitia matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza, pili na ya tatu uwingi. Viwakilishi *achek* (sisi), *okwek* (ninyi) na *ichek* (*wao*) havimwashirii au kumlenga mwanamke au mwanamume yeyote maluum. Kupitia kwa mifano hiyo mitatu, wazungumzaji na wasikilizaji wanapata faida ya kuhifadhi nyuso zao kutokana na vitisho vya uso. Faida nyingine ni kwamba msemaji hatakuwa katika hatari ya kutoeleweka kwa sababu usemi wake ni wa kijumla. Aidha, msikilizaji anapata fursa ya kujirekebisha mwenyewe bila kutajwa jina.

5.1.1.4 Faida za Mkakati wa Kuwa Nje ya Rekodi

Kama wanavyodai Brown na Levinson (1987), mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaeleza kuwa msemaji anapaswa kuwa mwangalifu kwa kutotaja mambo bayana ili asiye akamkera msikilizaji. Kwamba, msemaji anapaswa kutaja mambo kimzunguko au kimaelezo ili msikilizaji aweze kung'amua maana ya usemi. Kwa kutumia mkakati huu, msemaji atapata sifa kwa kuwa mjanja, ataonekana asiyelazimisha, atapendwa na wengi kwa kuonekana mwema na atahepa lawama iwapo msikilizaji atafasiri usemi wake vingine. Aidha, msemaji ana uwezo wa kumfanya msikilizaji amtekelezee kitendo bila kuhisi kulazimishwa. Kwa mfano:

Msemaji: Ni baridi sana

Msikilizaji: Basi nitafunga dirisha

Mfano huu unaonyesha kuwa msikilizaji amefaidika kwa kushirikiana na msemaji na msemaji amefaidika kwa kutekelezewa jambo na msikilizaji bila kulazimishwa.

Mkakati wa kuwa nje ya rekodi unadhihirika katika vipindi vya *SK*. Viongozi wa vipindi wanajaribu wawezavyo kuhakikisha kuwa wanajali uso wa hadhira lengwa. Ikumbukwe kuwa kipindi hiki kinahitaji mashabiki wanaojitolea. Kwa hivyo, yafaa viongozi wawe makini wasije wakawaudhi. Hii ndiyo sababu kuu inayowalazimu Rotich na Winny kutumia mikakati ya upole ili kudumisha uhusiano mwema baina yao na mashabiki wa vipindi vya *SK*.

Kwenye kipindi cha *Tililindo eng katunisiet* (Usafi katika ndoa), Winny na Rotich wanawaeleza mashabiki namna uzembe ulivyo na gharama. Ili kuonyesha taswira kamili, Rotich anasimulia kisa kuhusu ndoa iliyovunjika siku kumi na saba tu baada ya harusi kwa sababu ya uzembe. Rotich anasema kuwa asubuhi ya siku ya kumi na saba baada ya ndoa, mwanamke aliamka mapema kutengeneza kiamsha kinywa. Mumewe alipokuwa akilala chali kitandani, akitazama paa la nyumba, akaona nyumba ya buibui karibu na neti ya kuzuia mbu. Alimnyamazia mkewe kwa masaa manne hadi mkewe akamwuliza sababu ya ukimya huo. Kwa kujibu, mumewe alielekeza kidole kwa buibui kisha akamwuliza mkewe, “Kwani kazi yako hapa ni nini? Mbona hujali usafi wa hii nyumba?” Yule mwanamke, akakusanya vitu vyake na kuondoka kwa sababu hakutarajia kukasirikiwa na mumewe wa muda mfupi badala ya kumwambia pole pole shida aliyooona. Rotich anasema:

Kal.

90. *Ndaki ane murenono ii kostoikyok, kota kiacheru kotab kiproroktet kogere kwondo si konam aibu. Kiyait agine murenono amu kiwir boror kwen. Kimatamwoei kou notok. Kiteborchin koyoto bo kiproroktet anan kolenji 'uyo kokomeny kiproroktet yu'. Kitagerei ktyo kwondonyi kocheru kabukyot ak kubukto kiproroktet. Ngo cham kelen kieli tany kong' si kecharei o bikyok.*

Kis.

Wasikilizaji wetu, ningekuwa huyo mwanamume, ningetoa hiyo nyumba ya buibui akiona huyo mwanamke ili aabike. Mwanamume huyo alifanya vibaya kwa sababu ‘alipasua chungu’ papo hapo. Hangesema hivyo, **angemwonyesha mkewe hiyo nyumba ya buibui au amwambie ‘ni kama buibui amejenga hapa’**. Hilo lingemfanya mkewe achukue ufagio na kuondoa hiyo nyumba ya buibui. Wasikilizaji wetu, si hata msemu wetu husema ukitaka damu kwa ng’ombe, usimpige mshale akiona!

Mfano 90 unashadidia matumizi ya mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Usemi wa Rotich unaonyesha kuwa anaelewa faida za kutosema jambo wazi. Sentensi *kiteborchin koyoto bo kiproroktet anan kolenji ‘uyo kokomeny kiproroktet yu’* (angemwonyesha mkewe hiyo nyumba ya buibui au amwambie ‘ni kama buibui amejenga hapa’) ni mfano tosha wa mbinu hii. Faida kwa msikilizaji ni kuwa halazimishiwi kitendo kwa msemaji na faida kwa msemaji ni kuwa hakuathiri kihasi uso wa msikilizaji.

Mfano mwingine wa mbinu ya kuwa nje ya rekodi unapatikana katika kipindi hicho cha *Tililindo eng katunisiet* (Usafi katika ndoa). Winny anatofautiana na Rotich wakati wa kuelezea ni nani anapaswa kushughulikia usafi wa mwanamume. Rotich anawatetea wanaume kuwa wanapaswa kushughulikiwa na wake zao. Winny anapjaribu kuonyesha msimamo tofauti, Rotich anamkatiza usemi. Winny anajaribu kupitisha ujumbe wake lakini hawezi kwa sababu anakatizwa kila wakati na ‘Pasta’ Rotich. Ili apate nafasi, Winny anasema:

Kal.

91. **Winny:** *Heehe,kale alyon inye, ndakanyoru kasrta kitigi...iin amwa kiy ne atinye ko temuchi koguiyo murenik kole ma kasitab kwony inegei kosuldae tililindab manong’otionyi.*

Kis.

Heehe, **sijui nifanyaje, ningepata tu muda mdo...ogo** niseme nilicho nacho, kuna uwezekano wanaume wangeelewa kuwa si kazi ya mwanamke pekee kutimiza usafi wa mumewe.

Kal.

Rotich: *Ongeep it anyun kostoikyok, testai Winny, ng'alal.*

Kis.

Wasikilizaji, hebu tusikize, Winny endelea, zungumza.

Mfano huo unaonyesha jinsi Rotich amemtekelezea Winny kitendo cha kumpa nafasi ya kuzungumza bila kushurutishwa. Kishazi *kale alyon inye, ndakanyoru kasarta kitigi...in* (sijui nifanyaje ningepata tu muda mdo...ogo) haimlengi yeyote lakini hali hii inamfanya Rotich kushughulikia mahitaji ya mwelekezi wa kipindi. Usemi wa Rotich *ongeeep it anyun kastoikyok, testai Winny, ng'alal* (wasikilizaji hebu tusikilize Winny endelea, zungumza), unaonyesha kuwa Winny amepata kibali cha kuzungumza. Mbinu hii imemfaidi Winny kama msemazwa kwa sababu ametekelezewa kitendo cha kupewa nafasi ya kuzungumza. Pia, Rotich amefaidika kwa sababu hahisi kulazimishwa kumpa Winny nafasi ya kuzungumza.

5.1.1.5 Faida za Mkakati wa Kutosema Kabisa Jambo la Kutishia Uso

Mkakati wa kutosema kabisa jambo linalotishia uso ni mbinu ambayo msemaji anakatiza usemi au kutosema kwa kuhofia kutishia uso wa msikilizaji. Mbinu hii ni salama kabisa kuliko mikakati mingine ya upole kwa sababu msikilizaji hana uwezo wa kujua mawazo ya msemaji. Faida za mbinu hii ni kuwa msemaji hapati lawama kwa kutishia uso wa msikilizaji. Aidha msikilizaji hatabashiri kuwa msemaji alikuwa tayari kutaja kitendo cha kutishia uso wake. Mkakati huu hutumika tu iwapo si lazima mtu atekelezewe kitu na msikilizaji.

Matumizi ya mkakati wa kutosema kabisa kitendo kinachotishia uso umetumiwa mara chache sana katika vipindi vya *SK*. Hata hivyo, tutaangazia mifano miwili tu ya

mkakati huo kutoka kipindi cha *Tilyandit eng katunisiet* (Mahusiano katika ndoa). Mwelekezi wa vipindi pamoja na mwasilishaji mkuu wanaonekana kutumia mkakati huu wakati wanaona kuwa jambo watakalo kulisema lina uwezo wa kutishia uso wa msikilizaji kwa kiwango cha juu. Akionyesha kuwa baba hapaswi kuona uchi wa bintiye, ‘Pasta’ Rotich anasema:

Kal.

92. *Kastoikyok, Tos chomei konyekab kwan kogeer cheptonyi komi yaach ngor? Ma notok kityo, agot nga kikirikyin ko tos nda amei kiy lakwet olo booo olo booo, ngotebi Winny matikany amwa notok amu konyit ko toror. Ibwat koro chito kit ne makikanyei agot kemwa, bo kwong’ut biik Winny. Agot nda maendeleo i, ko ngotebi, makikuro kelenjino nyo iro lakwet amei iin iin woi angen ale kakonai kastoikyok kit ne ang’alale.*

Kis.

Wasikilizaji wetu, je, macho ya baba yana ujasiri wa kumwona bintiye akiwa uchi? Sio hilo tu, hata kama ni kukaribiana, je mtoto msichana akiumwa **sehemu yaa...aa ya...aa, acha nisiseme hilo** Winny kwa sababu heshima si utumwa. Hata kama ni kuendelea, acha tu ikae, sitaitwa kuambiwa nimwone mtoto anayeumwa...aa...aa, **woi nafikiria wasikilizaji wetu wamejua ninachomaanisha.**

Tumeona kupitia mfano wa 92 kuwa mambo mengine hayafai kutajwa moja kwa moja. Katika jamii za Kiafrika hasa jamii husika ya Kikalenjin, sehemu zingine za mwili ni mwiko kuzitaja. Hiyo ndiyo sababu Rotich anaonekana kuyakwepa. Virai *olo boo olo boo, ngotebi Winny matikany amwa notok* (sehemu yaa...aa ya..., acha nisiseme hilo) na *iin iin woi angen ale kakonai kastoikyok kit ne ang’alale* (...aa...aa, woi nafikiria wasikilizaji wetu wamejua ninachomaanisha) ni dhihirisho kuwa ‘Pasta’ amedondosha maneno mengine. Maneno yaliyodondoshwa ni viashiria vya sehemu za mwili ambazo hazitajwi ovyo.

Kupitia ukwepaji wa kutamka maneno mengine, msemaji amefaulu kupunguza vitisho kwa uso wake na wa msikilizaji wake. Faida nyingine ni kwamba hadhira kwa ujumla

imemwelewa msikilizaji na kwamba sio lazima waambiwe kila kitu. Wakati mwingine mtu anafaa kuelewa kilichokusudiwa kusemwa bila kutajwa kwa kuzingatia muktadha wote wa mazungumzo.

Uteuzi wa mkakati kutokana na faida inayotokana na matumizi yake, ni hali ambayo hukumbatiwa na wahusika wa mazungumzo yoyote yale. Kwamba, wazugumzaji wanafaa kufikiria sana kabla ya kuteua mkakati wa kutumia wakati wa kupeana ujumbe. Kutokana na mifano hiyo, wahusika wa mazungumzo katika vipindi vya *SK* wamefanya uteuzi wao kimkakati ili kukidhi mahitaji ya nyuso zao. Hata hivyo, faida ya mkakati pekee haitoshi kutumiwa kama kigezo cha uteuzi wa mkakati na ndio sababu sehemu inayofuata inachanganua hali za kijamii kama sababu ya pili ya kuteua mkakati mmoja badala ya mwingine.

5.1.2 Sababu za Kijamii

Sababu za kijamii ni hali zinazotokana na mtagusanao wa aina tofauti ya watu. Kwa mujibu wa Moland (2014), hali hizi huwekwa kwa makundi ya umri, jinsia, muktadha na tabaka/hadhi. Hali tulizotaja humpelekea mzungumzaji kutambua muktadha na mada ya mazungumzo wakati wa mawasiliano. Vipengele hivi vya kijamii, huwaweka wahusika wa mazungumzo katika hali ya kutaka kuridhiana licha ya vingine kutishia uso kwa kiwango kikubwa.

5.1.2.1 Tofauti za Kiumri Kati ya Wahusika wa Mazungumzo

Karibu jamii zote za Kiafrika huafikiana kuwa heshima huandamana sako kwa bako na umri. Inaaminika kuwa waja wana kanuni inayorithiwa kijamii, inayomwezesha mtu wa umri mdogo kumheshimu anayempiku kiumri. Kwa kawaida, matumizi ya lugha huongozwa na yale yanayozungumziwa. Hata hivyo, umri wa wahusika wa mazungumzo huathiri matumizi ya lugha kwa namna moja au nyingine.

Tofauti baina ya wahusika wa mazungumzo yoyote yale ni kipengele muhimu. Akishadidia hoja hiyo, Bell (2003) anadai kuwa umri ni raslimali ya utamaduni wa jamii na huathiri pakubwa matumizi ya mikakati ya upole katika jamii husika. Kama anavyodokeza Maclagan (2005), umri wa watu husababisha tofauti za lugha katika mazungumzo. Mwasilishaji, mwelekezi na mashabiki wa vipindi vya *SK* wanatofautiana kiumri. Ni kwa msingi huu wa tofauti za kiumri ndipo tunaona kuwa wao wanateua lugha inayowafaa na inayoweza kudumisha heshima baina yao. Udumishaji huo wa heshima unatekelezwa kupitia uteuzi wa mkakati mwafaka wa upole.

Wahusika wakuu wa mazungumzo ya *SK*, 'Pasta' Rotich na Winny 'Koriryo', wanazingatia sana suala la umri katika kuyadhibiti matumizi ya lugha. Katika kipindi cha *Mpango wa kando* (Mpango wa kando, Rotich anamshawishi Winny kuwa wanawake nao wana mipango ya kando. Anajaribu kumwonyesha sababu za mipango hiyo ya kando lakini kwa kumwonya asithubutu au kujaribu jambo hilo. Mjadala ufuatao kati yao unathibitisha hayo:

Kal.

93. **Rotich:** *Kas as ateun chepkametinyu, nyalilda ne aei chepyosok kocheng mpango wa kando, ndabuch ko kimatemugune yegai ng'alechoto. Ndakiribei murenik kwonyikwak komie ta kimatami ngala che ucho. Ki eng keny ko kima kegase kwony ne tinyei mpango wa kando lakini ra, ho, indoi is agot ngamwaun.*

Kis.

Sikiliza nikushauri dadangu, shida ndizo ziwafanyao wanawake kuanza mipango ya kando, bila shida hizo hawangekuwa na haja nayo. Iwapo wanaume wangewajibika kuwatunza wake zao vizuri, hakungekuwa na mambo kama hayo. Zamani, hangesikia kuhusu mwanamke aliyekuwa na mpango wa kando lakini leo he...he, hata wako mstari wa mbele.

Kal.

Winy: *Hapo sasa, ingen ile kiawege saa nane is ak agas tuguk che kilen 'chokoza nyuki uone' ak alak che kilen, 'mjinga akierevuka mwerevu yu mashakani'. Ingen is ile ngeng'emin iegu aribika...*

Kis.

Hapo sasa, unajua nilirudi saa nane na nilisikia vitu kama 'chokoza nyuki uone' na 'mjinga akierevuka mwerevu yu mashakani'. Unajua nini, ukiharibiwa utakuwa haribika.

Kal.

Rotich: *Angii Winny, ngu ilen ibak agot choto koboibochin, muitoi kityo amu nyalilda ako agot nga no korwokyin kabwatutikwak. Metyem kot ko metyem we lakwaninyo, inye kota isetu ago ta ko I ming'in.*

Kis.

Winny, unafikiria hata wao wanafurahia! Wanavumilia tu kwa sababu ya shida, la sivyo dhamiri zao zinawahukumu. **Mwanetu**, usijaribu na usijaribu, bado una mwendo mrefu kwa sababu **ungali mdogo**.

Mdahalo huo, kati ya Rotich na Winny unathibitisha kuwa wanatofautiana kiumri. 'Pasta' anaposema *kas ateun chepkametinyu* (sikiliza nikushauri dadangu) *metyem kot ko metyem* (usijaribu na usijaribu) anabainisha kuwa umri wake unapiku ule wa Winny. Sentensi hizo ni amrifu na zinathibitisha kuwa msemaji ni mkubwa kiumri kuliko msikilizaji. Aidha, maneno *lakwaninyo* (mwanetu) na *ta ko I ming'in* (ungali mdogo) yanathibitisha tofauti kati ya umri wa Rotich na Winny. Mifano hiyo inaonyesha kuwa Rotich ana mamlaka ya kumwamrisha Winny naye Winny hana haki ya kukataa kumsikiza Rotich kwa sababu ya tofauti katika umri wao. Hii ni dhihirisho kuwa Rotich ameteua mkakati wa kuwa kwenye rekodi kwa sababu ana mamlaka juu ya msemazwa wake.

5.1.2.2 Tofauti za Kijinsia kati ya Msemaji na Msemazwa

Lakoff (1973), ni mmoja wa watafiti wa awali waliobobea katika uchunguzi wa uhusiano baina ya jinsia na matumizi ya mikakati ya upole. Lakoff anadai kuwa

wanawake hutumia mikakati ya upole kuliko wanaume. Anasema kuwa udunishwaji na ukosefu wa uwezo kwa wanawake hujitokeza kupitia wanavyotarajiwa kuzungumza na jinsi wanavyozungumziwa. Tangu nyakati za Lakoff (1967), karibu chunguzi zote kuhusiana na tofauti za kijinsia zimepata mahitimisho yanayoafikiana.

Kwa mujibu wa Tannen (1990) na Harisah (2012), wanawake wamepewa nafasi zisizo za kimsingi katika jamii. Kando na hayo, wanawake na wanaume wana mitazamo tofauti kuhusiana na hali ya maisha. Hii ina maana kuwa kila jinsia ina mtazamo wa kipekee na ulio tofauti na wa jinsia nyingine. Tannen anasema kuwa wanaume wanachukulia kuwa ulimwengu ni uwanja wa mapigano na wenye mpangilio wa nguvu na uwezo. Kwa wanaume, mpangilio huu unamruhusu mhusika kuwa katika nafasi moja kwa wakati mmoja katika mapigano au mapambano ya maisha. Yaani, awe katika nafasi ya juu au chini, kushinda au kushindwa. Kwao, mazungumzo ni mijadala ambayo kwayo kila mmoja hupigania kushinda na kupewa atakacho.

Kwa upande mwingine, wanawake hujichukulia kuwa watu walio katika ulimwengu wenye mtandao wa makubaliano. Wanawake huchukulia kuwa ulimwengu wao unawahitaji kufanya mazungumzo yanayolenga mahusiano mema na yatakayosababisha maafikiano (Ediyani, 2010). Holmes (1995) anahoji kuwa wanawake ni wepesi wa kuomba msamaha, kutumia lugha ya upole, kuonyesha heshima kwa msemzwa na kutoa pongezi.

Kama asemavyo Putri (2013), masuala ya kijinsia hubainisha wanaume na wanawake. Putri anasema kuwa wanawake hutumia lugha ya upole kuliko wanaume. Vipindi vya *SK* vilisawiri tofauti hizi kwa sababu wahusika wa mazungumzo ni wa jinsia tofauti. Winny na Rotich wanapoendeleza vipindi, utagundua kuwa lugha wanayotumia ni

tofauti. Hali hii inatokana na tofauti za kijinsia. Kwa mfano, katika kipindi cha *Katunisiet ak kolokset* (Mavazi katika ndoa), Winny na Rotich wanajaribu kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji kuwa mavazi yanaathiri mawazo ya wanaume. Mazungumzo kati ya wawili hao ni kama yafuatavyo:

Kal.

94. **Winny:** *Kale kiam nee murenik inye iman si ngoro 'skatit' age tugul kosirtoi kobotonso? Lakini malaumeni mising amu une aenwa. Ingen ile nyochin kaat Mungu chitugulis. Tos ma kikiyai murenik kou notok o 'Pasta'?*

Kis.

Sijui wanaume wana shida gani, sijui mbona hutetemeshwa na 'sketi' yoyote ipitayo? **Lakini sitaki kuwalaumu sana kwa sababu inaonekana ni maumbile. Unajua Mungu humsamehe kila mtu? 'Pasta', si ni ukweli kuwa waliumbwa hivyo?**

Kal.

Rotich: *Acha Winny, ngu kemach igochi murenik inye chomjinet kwai kiy age tugul. Ingen ile ngogaas alage kou notok koberbergei kolen tinyei amu nee nebo kwai tuguk alak agot che maiyonotin. Amache amwa ale ingoboi chi kabwatutikyik si ma kitigin kokweri kaseetab miat ne bunu kaloksosiekap kwonyik. Amache kokasak ni Winny, mami sababu nebo tengek, ama chechuk ngalechoto, sirotin eng Bukuit.*

Kis.

Hapana Winny, ni kama unataka kuwapa wanaume kibali cha kutenda lolote. Unajua, wengine wakisikia hivyo hujidanganya kuwa wana sababu ya kufanya mambo mengine hata yasiyokubalika. **Nataka kusema hivi,** kila mtu atawale mawazo yake ili asije akaongozwa na tamaa ya macho kutokana na mavazi ya wanawake. **Nataka hili lisikike Winny,** hakuna sababu ya dhambi, na maneno hayo si yangu, yameandikwa kwenye Biblia.

Mfano huo unaonyesha tofauti kati ya usemi wa Winny na Rotich. Usemi wa Winny ni wa kuashiria unyenyekevu. Hili linadhihirika kupitia mistari *Lakini malaumeni mising amu une aenwa* (Lakini sitaki kuwalaumu sana kwa sababu inaonekana ni maumbile), *Ingen ile nyochin kaat Mungu chitugul is* (Unajua Mungu humsamehe

kila mtu?), na *Tos ma kikiyai murenik kou notok o 'Pasta'?* ('Pasta', si ni ukweli kuwa waliumbwa hivyo?). Matumizi ya maswali yasiyohitaji majibu kama vitangulizi na maneno ya kuonyesha urajua ni dhihirisho kuwa Winny ameteua mkakati wa upole hasi.

Kwa upande mwingine, usemi wa 'Pasta' unadhihirisha uamrishaji. Mistari *Acha Winny* (hapana Winny), *Amache amwa ale* (nataka kusema hivi) na *Amache kokasak ni Winny* (nataka hili lisikike Winny) ni udhihirikaji wa uwezo wa kiume. Usemi wa Rotich unaonyesha kuwa msemaji ana haja ya kutumia uamrishaji kutekeleza mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Lugha yake inabeba uwezo fulani wa kiamri kama ilivyo na wanaume wengine. Hata hivyo, 'Koriryo' na 'Pasta' wanaelewana kwa vyovyote vile bila mkwaruzano.

5.1.2.3 Uwezo wa Kitabaka/Kihadhi kati ya Msemaji na Msikilizaji

Ili kubainisha tabaka la mtu, ni kawaida kwa waja kuhusisha kiwango cha elimu na cheo chake. Milroy na Milroy (1995) na Trudgill na Anderson (1990) wana mtazamo kuwa hali ya mtu kijamii huathiri uteuzi wake wa lugha. Urefu wa usemi, toni na njia ya kuwasilisha ujumbe hutegemea cheo cha mtu (Maclagan, 2005). Maoni ya wataalamu hao yanaelekeza kuwa lugha na tabaka la watu linafaa kuzingatiwa wakati wa kuwasiliana. Uteuzi wa maneno na vitengo vyote vya lugha ni njia mwafaka ya kukuza na kudumisha uhusiano na mlahaka mzuri kati ya wahusika wa mazungumzo yoyote yale.

Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa mahusiano ya kimamlaka baina ya wahusika wa mazungumzo ni mojawapo ya masuala yanayobainisha mkakati wa upole utakaotumiwa. Suala hili la mamlaka linaweza kujidhihirisha kwa njia

tofautitofauti kama vile: hadhi ya mhusika, nguvu za kiuchumi, mamlaka kutokana na nguvu za kimwili miongoni mwa mengine.

Morand (2014) anasema kuwa, walio na uwezo mdogo kimamlaka wanapozungumza na wenye uwezo mkubwa, wanahitaji kutumia kiwango kikubwa cha upole. Iwapo msemaji ana mamlaka ya juu kuliko msemazwa, msemaji atadumisha kiwango kidogo tu cha upole ama hata asiwe mpole kabisa. Kwa mfano, hautaonekana ukosefu wa upole mwajiri akisema kwa mwajiriwa: **‘Sina shaka hutajali nikivuta sigara’**. Usemi huo unaonyesha kuwa msemaji hana haja ya kudumisha uso wa msikilizaji kwa sababu mamlaka yake yanamruhusu kumtawala msemazwa kiusemi. Msemaji ametaja kitendo kinachotishia uso bila uoga na hata asipojibiwa, ana uwezo wa kuvuta sigara bila idhini ya msikilizaji.

Kwa upande mwingine, msemaji wa mamlaka ya chini anahitaji kupata ruhusa ya msemazwa aliye na mamlaka ya juu ili atekeleze jambo fulani. Iwapo anahitaji kuvuta sigara atatumia upole hasi ambao unaonekana kuwa na upole mwingi kuomba idhini ya kuvuta sigara. Anaweza kusema **‘Tafadhali mkubwa, utakuwa sawa nikivuta sigara?’** Bila idhini ya msemazwa, msemaji hatavuta sigara. Mifano hiyo inaonyesha tofauti za kiuwezo kati ya washiriki wa mazungumzo kutegemea mamlaka yao.

Katika mazungumzo ya *SK* tofauti za kimamlaka zinashuhudiwa kati ya wahusika wa mazungumzo. Tofauti hizo zinasawirika kati ya wahusika wakuu ambao ni Rotich na Winny, na mazungumzo kati ya mashabiki na wahusika wakuu. Licha ya majukumu yao ya kuongoza vipindi, wao wanatofautiana kimamlaka. Rotich ndiye mwasilishaji mkuu na pia umri wake unabeba uwezo mkubwa hivyo kuonekana kuwa na mamlaka ya juu kuliko Winny. Aidha, Rotich ana tajriba kubwa katika kazi ya kutoa ushauri kwa wana ndoa kwa vile amefanya kazi hii kwa muda mrefu hata akapewa jina

‘Pasta’. Kutokana na hayo, tofauti zao kimamlaka zinadhihirika kupitia mazungumzo husika.

Pia, kuna tofauti za kimamlaka kati ya wahusika wakuu na mashabiki wa vipindi husika. Kwa kuwa hatuna uwezo wa kujua mamlaka ya baadhi ya mashabiki, tumechukulia tu kuwa wote ni watu wa kawaida na kwamba mwasilishaji mkuu pamoja na mwelekezi wa vipindi wana tajriba hivyo kuwa na mamlaka makubwa. Tumegundua kuwa, mashabiki wachache tu ndio huuliza maswali ya kudadisi tajriba ya mwasilishaji mkuu. Kupitia maswali mengi na nyongeza ya mashabiki wengi, kuna dhihirisho kuwa wengi wanakubaliana na mwasilishaji mkuu kwa mambo mengi.

Katika kipindi cha *Suupsetab tibik ak kwonyik* (Ubakaji wa wanawake), Rotich na Winny wanatoa ushauri kwa wanawake kuwa wasitembee mahali ambapo kuna msitu au kutembea mwendo mrefu wakiwa pweke pweke. Rotich anadhihirisha mamlaka yake ifuatavyo:

Kal.

95. *Nganetak kastoikyok mising ko tibik ak kwonyik. Mewendote kityo eng ole imen anan ko banda ne koi anan ko ole mi timdo.*

Kis.

Acheni niwafunze wasikilizaji wetu hasa wana wa kike. Usitembee pekee mahala pa giza, mwendo mrefu au mweituni.

Kupitia mfano huo, ‘Pasta’ anatumia neno *nganetak* (acheni niwafunze) kuonyesha kuwa ana mamlaka ya kutoa mafunzo kwa wasikilizaji wake. Ana uwezo dhidi yao kwa sababu ya uelewa wake wa mashauri yanayohusiana na ubakaji. ‘Koriryo’ ni kati ya wanawake kwa hivyo anashirikiana na wanawake ambao ni wasikilizaji kupata ushauri. Hili linathibitishwa na majibu yake ifuatavyo:

Kal.

96. *Kitinye tabu kwonyik iman 'Pasta'. Kilen kongoi amu konetisieng'ung ne iboru kole kiichigil mising agobo tuguk che imuch konyanyasanech. Abwoti ale kakekas kwonyik tugul kit ne imuch koyaak ye kewendote kityo. Ongeripkei amu ki 'vulnerable' mising.*

Kis.

'Pasta', kwa kweli wanawake tuna shida. Tunashukuru kwa mafundisho yako yote yanayodhihirisha **tajriba yako katika utafiti wa mambo** yanayoweza kutunyanyasa. Sasa nina uhakika wanawake tumesikia kuhusu kinachoweza kutendeka ukitembea pekee. Hebu tuwe makini kwa sababu kutokana na hali yetu lolote linaweza kutupata wakati wowote.

Majibu ya Winny katika mfano 96 yanaonyesha kuwa Rotich ana mamlaka juu yake na wanawake wenzake. Anakubaliana na mwasilishaji mkuu na anawarai wanawake kutilia maanani mashauri hayo ili waepukane na mambo mabaya yanayoweza kuwapata. Maneno anayotumia Winny katika kirai *kiichigil mising agobo tuguk* (tajriba yako katika utafiti wa mambo) yanadhihirisha uwezo wa Rotich.

5.1.2.4 Mukstadha wa Mazungumzo

Uamali ni uchunguzi wa maana katika lugha kwa kuhusisha mukstadha. Kama yalivyo matendo yanayodhihirisha adabu, lugha ya upole ni kitu ambacho wahusika wa mazungumzo hujifunza kutegemea namna wanavyohusishwa na kujumuishwa kijamii na kimazingira. Hali hii hutokea kwa sababu kila mazingira ni mukstadha tofauti wenye wahusika tofauti. Kila mukstadha una jumuiya tofauti na kila jumuiya-lugha ina namna ya kipekee ya matumizi ya lugha.

Mukstadha ni kitengo muhimu sana katika mazungumzo. Sababu kuu ni kwamba lugha hupata maana kimukstadha. Pasipo uhusishaji wa mukstadha mawasiliano yoyote yale yanaweza kuzua utata kati ya wazungumzaji. Grice (1975) akielezea kaida ya namna ya kanuni ushirika, anahoji kuwa wahusika wa mazungumzo wanahitajika kufanya

kila wawezalo ili kuepuka maneno au miundo isiyoeleweka. Yaani waseme kwa ufupi na kwa mpangilio mzuri ili kuepuka utata. Hivyo basi muktadha ni kipengele muhimu sana katika mazungumzo yoyote.

Muktadha huathiri uteuzi wa mkakati wa upole. Wakati mwingine, mzungumzaji hulazimika kutumia zaidi ya mkakati mmoja wakati mmoja au hata kulazimika kutumia mkakati fulani ili kupitisha ujumbe aliokusudia. Muktadha wa mjadala wa vipindi vya *SK* ni wa masuala ya ndoa. Mara nyingi, mwasilishaji mkuu anajikita katika masuala ya wana ndoa na jamii kwa ujumla. Mambo yanayozungumziwa huhitaji muktadha usiojumuisha watoto na vijana. Hiyo ndiyo sababu kuu ya vipindi hivyo kufanyika saa nne hadi saa sita usiku.

Mbali na hayo, vipindi vya *SK* hujumuisha wazazi wa viwango tofautitofauti kiumri lakini mambo yanayozungumziwa huwafaidi wote. Rotich na Winny wanazingatia sana muktadha wakati wa mjadala. Wao wanateua lugha inayowapendeza wasikilizaji wa vipindi ambao hujitolea katika masaa ya usiku. Rotich yuko makini sana anapowasilisha katika miktadha tofautitofauti. Mfano mzuri ni katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa). Rotich anaonekana kuhepa matumizi ya maneno mengine kwa sababu muktadha haumruhusu kuyasema wazi. Akiwaeleza wasikilizaji kuwa pande zote mbili, za baba na mama, zinachangia kuvunjika kwa ndoa, Rotich anasema:

Kal.

97. *Ngap ilen ile matinyei nafas chepyosok lakini **acha, serwenatet notok.** Kalya si kobendat kikombok che kaamisie lagok end kompaun? Kalya si monet lagok koweek chitugul kit ne kaamisie amawo koureren. Pto! Ya notok mising chepyosok amu agoi komweenok boisiek.*

Kis.

Wakati mwingine unaweza kuchukulia kuwa kina mama hawana nafasi lakini **la, huo ni uzembe**. Mbona vikombe vinavyotumiwa na watoto

vitapakae kila mahali katika maeneo ya nyumbani? Mbona watoto wasifundishwe kurejesha vyombo baada ya kutumia? **Ah! Kina mama, hilo ni baya sana** kwa sababu waume zenu watawatoroka.

Mfano wa 97 unaonyesha kuwa muktadha wa mazungumzo unamlazimu Rotich kuzungumza kinagaubaga bila mzunguko. Ametumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi kuwakosoa kina mama. Brown na Levinson (1987) wanadokeza kuwa msemaji anaweza kutumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi iwapo kitendo kinachotishia uso kinamfaidi msikilizaji au katika hali ya dharura. *Acha, serwenatet notok* (la, huo ni uzembe) na *pto! Ya notok mising chepyosok* (ah! Kina mama, hilo ni mbaya sana) ni sentensi zinazothibitisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Wanaofaidika kutokana na usemi huo ni kina mama kwa sababu wakiacha uzembe, watapendwa na waume zao.

Mfano wa kutumia zaidi ya mkakati mmoja wakati mmoja ni katika kipindi hicho cha *Tuguk che butei katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa). Winny anafafanua sababu za kuchapwa kwa wanawake na waume zao. Anaeleza kuwa kuna wanawake ambao wanastahili kuchapwa. Anasema:

Kal.

98. *Maunye nitok chepyosok, yomei kebirok kapsa amu kutuswek che koen. Mi chepyosok che masistos kot ko masistos. Nda a agenge eng chotok, kotanyebuti beek ye kageronu manongotionyu konyonei ko kakobogit.*

Kis.

Kina mama, sitaficha hili, mnastahili kuchapwa kabisa kwa sababu ya midomo mirefu. Kuna kinamama ambao hawanyamazi hata kidogo. **Ningekuwa mmoja wao, ningeweka maji mdomoni** nimwonapo mume wangu mlevi akija.

Kupitia mfano huo, Winny anatumia zaidi ya mkakati mmoja kwa wakati mmoja.

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi unadhihirika katika sentensi *maunye nitok*

chepyosok, yomei kebirok kapsaa (kinamama, sitaficha hili, mnastahili kuchapwa kabisa). Winny anatumia mkakati huu kwa sababu anataka kupitisha ujumbe unaomfaidi msikilizaji. Hata hivyo, msemaji anatumia mkakati mwingine ndani ya usemi mmoja ambao ni wa kuwa nje ya rekodi. Anaposema *nda ane ko inye, kotanyebuti beek* (ningekuwa mmoja wao, ningeweka maji mdomoni), Winny anamwachia msikilizaji kutafuta maana ya usemi badala ya kumwambia moja kwa moja. Mfano huu unaonyesha kuwa uteuzi wa mkakati/mikakati hutegemea muktadha na kiwango cha tishio kwa uso. Hivyo basi, ni muhimu kwa wahusika wa mazungumzo yoyote kuzingatia kipengele cha muktadha.

5.1.2.5 Mada ya Mazungumzo

Mazungumzo yote yana mada rasmi. Mada ya mazungumzo hutegemea mahali, wakati na hali za wahusika kwa wakati huo. Watu huyarekebisha mazungumzo yao kila siku ili yalingane na hali mbambali. Wahusika wa mazungumzo wanaweza kujitwalia uhuru wao wakiwa miongoni mwa marafiki na kusema vitu ambavyo miongoni mwa wageni vitaonekana vya kuaibisha. Kwa kawaida, tutangamanapo na marafiki tunajiepusha na urasmi uliozidi. Hii ni kwa sababu wakati wowote wa mazungumzo, wahusika hufanya mazungumzo yao kwa mkataba unaokubalika kwao.

Mkataba wa mazungumzo hutokana na hali kwamba kila kunapotokea mazungumzo, wahusika wanaafikiana kwa namna inayowaleta pamoja. Kuafikiana huku kunatokana na uzingatiaji wa sheria fulani za mahusiano hata ingawa sheria hizo hazijaandikwa popote. Vipindi vya *SK* vinashuhudia mazungumzo katika mada tofaututofauti. Wahusika wa mazungumzo husika wanateua mikakati ya upole kulingana na mada ya siku. Mada nyingi katika kipindi hiki huhusiana na masuala nyeti katika ndoa na hii

ndiyo sababu uzingatiaji wa lugha unafaa ili kutunza nyuso za wahusika wa mazungumzo.

Katika kipindi cha *Tuguk che butei katunisiet*, (Vitu vinavyovunja ndoa), Rotich anaeleza kuwa ndoa nyingi huvunjika kwa sababu ya laana. Anaendeleza kuwa binti za watu huolewa kwa jamii ambazo historia yao haijulikani. Kwa bahati mbaya, msichana mwingine anaweza kuolewa kwa jamii iliyo na laana kwa sababu ya kutenda mambo kinyume na matakwa ya jamii. Labda binti huyo atakuwa akipata watoto wanaokufa baada ya muda fulani. Wakati utafika wa huyu binti kurudi kwao kwa sababu ya shida hiyo kubwa. Rotich anawahurumia kina dada kwa kusema:

Kal.

99. *Arire chepyosok Winny, woo woi, eiting'o amu ipkotakoiye lakwetab chito ye kabiit kaberuretab lagok ndaborok kororok chemakitebit ne makiguitos ole kitaune ak ole tun bekyin. Mutyo lagokyok che mengeny kiy, che biriren kerengani, amu kipkel ne ya ne otuiye eng korikab sogoranik.*

Kis.

Winny, nawahurumia kinamama, woo woi, pole kwa sababu binti wa watu atashangaa akipata baraka ya watoto kisha **kifo**, ambacho mwanzo na mwisho wake hakijulikani, kinamfikia ghafla. Poleni binti zetu, wachanga, msiojua lolote, kwa sababu ya bahati mbaya mnayokutana nayo katika jamii za watu waovu.

Usemi wa Rotich katika mfano 99 ni wa huzuni. Mukstadha wa matumizi unahusiana na kifo na kwa hivyo lugha inayotumiwa ni ya upole mno. Katika jamii nyingi za Kiafrika hasa ya Wakalenjin, kifo si jambo la kawaida na hata hakitajwi kwa jina. Hiyo ndiyo sababu Rotich anatumia neno *chemakitebit* (kisichoulizwa) kama neno mbadala kumaanisha kifo. Wakalenjin wanaamini kuwa kifo ni kitu ambacho hakitakikani kuzungumziwa. Hutapata watu wakiulizana 'kifo kimezuka wapi leo' na ndio sababu ya tasfida hiyo *chemakitebit*.

Tasfida ni mojawapo ya mbinu katika mikakati ya upole. Rotich anaonyesha kuwa mada ya mazungumzo ni muhimu sana kwa sababu msemaji analazimika kufanya uteuzi wa lugha. Kama tulivyotanguliza, mambo mengine hayakimbiliwi kusemwa. Msemaji ana jukumu la kufikiria sana kabla ya kuzungumza kwa sababu lengo kuu la mazungumzo ni kwasiliana bila kuzua hisia hasi kwa wahusika wa mazungumzo.

Kwa ujumla, uteuzi wa mikakati ya upole hutegemea hali ya msikilizaji na msemaji katika miktadha tofautitofauti. Hata hivyo, uteuzi huo huandamana na gharama fulani. Gharama hizo hutokana na sababu kuwa wakati mwingine wahusika wa mazungumzo huwa hawana uwezo juu ya hali zingine. Kwa mfano, kuna wakati msemaji analazimika kutumia mkakati fulani ili ujumbe uwasilishwe utakikanavyo. Aidha msikilizaji naye hulazimika kupokea ujumbe huo ulivyo kwa sababu hana uwezo wa kulazimisha mahitaji yake kwa msemaji. Sehemu inayofuta inaangazia changamoto zinazotokana na matumizi ya mikakati ya upole.

5.2 Changamoto za Matumizi ya Mikakati ya Upole

Kama tulivyotanguliza katika sura ya pili, kila mwanadamu ana aina mbili za uso. Uso chanya na hasi. Waja wanapozungumza, kuna hatari ya kupoteza uso. Ili kutunza uso, hasa wa msikilizaji, wahusika wa mazungumzo hutumia mbinu tofautitofauti katika mawasiliano. Mbinu hizo ndizo tunaziita mikakati ya upole. Hata hivyo, matumizi ya mikakati hiyo hulazimu gharama fulani kwa wahusika wa mazungumzo. Kwamba, matumizi ya kila mkakati yana changamoto zake. Baada ya kuangazia umuhimu wa matumizi ya mikakati ya upole kwa urefu, ni haki kuangazia changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mikakati ya upole.

Kwa kawaida, hakuna kizuri kisicho na waa, hivyo basi matumizi ya mikakati ya upole huibua changamoto kwa wahusika wa mazungumzo. Matumizi ya mikakati ya

upole huwa na gharama kwa msikilizaji na msemaji. Sehemu hii inaangazia changamoto zinazotokana na utekelezaji wa kila mkakati wa upole katika vipindi teule vya *SK*. Mikakati hiyo ni: mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati hasi wa upole, mkakati chanya wa upole, mkakati wa kuwa nje ya rekodi na mkakati wa kutosema kitendo cha kutishia uso.

5.2.1 Changamoto za Mkakati wa Kuwa Kwenye Rekodi

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi ni mbinu ya kusema kitendo kinachotishia uso kama ilivyo na mara nyingi hufanyika wakati kuna dharura au wakati mfaidika ni msikilizaji. Msemaji ana ruhusa ya kusema maneno yalivyo bila kupunguza makali yake. Kusema au kutaja mambo bila kupitia kando huweza kudhuru hisia za msikilizaji na msemaji. Wao hulazimishwa na hali mbalimbali kutumia mkakati huu kwa ajili ya kupitisha ujumbe kwa ukamilifu.

Hata hivyo, mbinu hii ya upole huwa na changamoto zake. Kwanza ni kuwa, licha ya ufanisi wa msemaji kupitisha ujumbe sahihi bila utata, msikilizaji atahisi kudunishwa. Kwa mfano “pita haraka gari linakuja”, usemi huu ni amirifu na ina manufaa kwa msikilizaji lakini yana madhara kwa uso wake. Msikilizaji hata hivyo ataepuka hatari ambayo angeipata kama uso wake haungetishiwa lakini baadaye atahisi kuwa msemaji ametumia uwezo wake kumwamrisha.

Pili, msemaji naye atakuwa amemnufaisha msikilizaji kwa kumwepusha na hatari inayomkumba lakini ataadhirika na jinsi alivyopitisha ujumbe wake kwake. Uhusiano wao utaonekana kuwa mbali kwa sababu ya uwezo wake wa kutoa amri kwa msikilizaji. Hatari ipo kwa msikilizaji na msemaji kwa wakati mmoja, kwamba, urafiki wao unatishiwa na kwa wakati huo, kila mmoja analazimika kuchukua nafasi

yake katika jamii kama vile uwezo wa kiumri au kiuchumi au hata kihadhi. Hii ina maana kuwa uwezo wa kudumisha uhusiano unatishiwa.

5.2.2 Changamoto za Mkakati waUpole Chanya

Mkakati wa upole chanya huelekezwa kwa uso chanya wa msikilizaji na tamanio lake la kutopuuzwa kwa mahitaji yake. Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa mkakati wa upole chanya ni hulka ya kawaida miongoni mwa marafiki au watu walio na uhusiano wa karibu. Wanaendeleza kuwa mkakati huu humtambua na kumshirikisha msemazwa katika shughuli za msemaji kwa kupewa nafasi sawa. Njia hizo ni kama kumsifu, kumheshimu na hata kumshukuru. Mkakati huu unatumia mbinu anuwai kutekeleza mahitaji ya nyuso za wahusika wa mazungumzo.

Wakati wa uteuzi wa maneno ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji, msemaji anagharamika sana. Sababu ya gharama hiyo ni kuwa msemaji anatanika katika hali mbili. Anataka kupitisha ujumbe usiokuwa tata na kwa upande mwingine anataka kutunza uso wa msemazwa ili kudumisha uhusiano wao.

Mfano mzuri ni wakati mwalimu anamwambia mwanafunzi aliyefanya vibaya darasani “Hongera kwa kupata alama hizi, naomba tu utie bidii kidogo”. Kwa kusema hivyo, msemaji anamaanisha kuwa kazi ya mwanafunzi si nzuri. Hata hivyo, anaonyesha kasoro ndogo kwa kutumia maneno yasiyoonyesha kiwango cha kasoro. Maneno ‘bidii kidogo’ hayaonyeshi wazi wazi kiwango cha kuanguka au cha kupita na kuna uwezekano wa mwanafunzi kuchukulia vingine usemi wa mwalimu.

Mkakati huu wa upole pia, unaweza kutekelezwa kupitia mbinu ya kuepuka kutokubaliana na msikilizaji. Hii ni njia inayomhitaji msemaji kufanya kila mbinu ili asitofautiane na msikilizaji. Kwa mfano mtu akiulizwa, “Utakuja kwetu leo jioni?” Kisha anajibu, “Ndio lakini, nina kitabu ninachotaka kukimaliza kusoma kabla ya

kesho”. Kukubali ‘ndio’ kisha kuweka neno ‘lakini’ inampa msikilizaji sababu ya kutotekeleza kitendo. Hii ni njia ya kumtayarisha mtu mapema ili asitegemee kuwa atapata hitaji lake. Hizi ndizo sababu tunasisitiza kuwa licha ya umuhimu wake, utekelezaji wa mkakati wa upole chanya una changamoto zake kimawasiliano.

5.2.3 Changamoto za Mkakati Hasi wa Upole

Baada ya kuangazia changamoto za mkakati wa upole chanya tutajikita katika changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mkakati wa upole hasi. Mkakati wa upole hasi unalenga kutunza uso hasi wa msikilizaji. Tunaposema uso hasi, tunamaanisha uso usiopenda kuingiliwa na wengine. Ni mahitaji ya mtu kutaka uhuru wake wa kutoingiliwa bila mapenzi yake. Kwa mfano kuombwa chochote, kupewa habari isiyopendeza au kutembelewa bila hiari yake.

Aidha, uso hasi hupotezwa wakati mtu anajiingiza katika masuala ya watu wengine bila kukaribishwa. Jambo hilo huleta aibu kwa anayeingiliwa na husababisha hisia hasi. Hivyo basi, uso hasi ni tamanio la kutaka kujiwekea mipaka ya kutoingiliwa. Yaani, msemaji anahisi kuwa mawazo yake, nia yake matakwa yake pamoja na usemi wake unafaa kukubalika kwa wenzake.

Mkakati huu una changamoto zake kwa vile msemaji anahitajika kuwa makini kila wakati. Anatakikana kumpa msikilizaji uhuru wake kwa kuhakikisha kuwa haingilii uhuru wake. Kuna uwezekano wa msemaji kutopitisha ujumbe ipasavyo kwa kutafuta njia mwafaka wa kupitisha ujumbe huo. Aidha, msemaji anajinyima uhuru wake mwenyewe wa kuzungumza atakavyo. Pia, mbinu hii huwaweka wahusika wa mazungumzo katika hali ya kuhofia kuwakosea wenzao. Kwa mfano, “Tuondoke sasa” na “Ukifika unipigie simu”.

Kwa hakika sentensi hizo hazionekani kuwa na shida au hatari yoyote. Lakini kwake msikilizaji, usemi unaonekana kuwa na vitisho kwa uso wake kwa sababu ni amirifu. Asemapo “Tuondoke sasa”, msemaji anamjumuisha msikilizaji katika kitendo, lakini shida ni kuwa anayesikiliza anafasiri kuwa anayetoa amri ana uwezo wa wakati wa kutekelezwa kwa tendo la kuondoka. “Ukifika unipigie simu” ni usemi wa kawaida kwa msemaji lakini unadhihirisha kuwa msikilizaji hana budi ila kutekeleza kitendo kilichotajwa.

Kusema jambo kimzunguko ni mbinu mojawapo ya mkakati wa upole hasi. Kwa mfano msemaji akisema “Samahani, sikutarajia kusema lakini uniruhusu nikuulize tu, waonaje binti Mashaka akiwa mke wako?” Usemi huo, unamchukua msemaji kwa mizunguko kabla ya kutaja lengo lake. Aanzapo kuzungumza msemaji, msikilizaji hatakisia anachotaka kuambiwa. Ni baada ya muda ndipo ataelewa anachomaanisha msemaji. Hii inampotezea muda mzungumzaji hali kadhalika msikilizaji.

Pia, wakati mwingine, msemaji anaweza kutumia ujanja ili asitishie uso hasi wa msikilizaji. Kwa mfano msemaji anaweza kuwa ameona kuwa nguo aliyovalia mwenzake haipendezi. Anaweza kusema “Haki nguo uliyovalia leo inapendeza sana, si hata wewe umeona?” Matatizo ya usemi huo ni kuwa msikilizaji hatajua ukweli wa mambo. Anaweza kuchukulia alivyosema mwenzake na kuendelea kuvaa nguo hiyo mara kwa mara. Mbinu hii inakiuka kaida ya ubora katika kanuni ushirika ya Grice (1975) inayosisitiza kuwa msemaji anafaa kusema tu kile anachojua kuwa kweli.

5.2.4 Changamoto za Mkakati wa Kuwa Nje ya Rekodi

Mkakati wa kuwa nje ya rekodi unasisitiza matumizi ya mafumbo ili kukidhi mahitaji ya uso. Kwa kutumia mkakati huu, msemaji anasema jambo lisilo bayana kwa kudokeza tu, kisha kumwachia msikilizaji ufasiri wa maana. Ni mbinu inayozingatia

sana usemaji wa kitu kimzunguko kuliko mikakati yote ya upole. Mkakati huu kulingana na Brown na Levinson (1987), unabeba utata mwingi. Si rahisi kuhusisha maana moja kwa usemi husika kwa kuwa msikilizaji anaachiwa ufasiri. Ili kutimiza mkakati wa kuwa nje ya rekodi, msemaji anahitajika kukiuka kaida ya namna katika kanuni jumla ya ushirika.

Kwa mujibu wa Grice (1975), kaida ya namna humhitaji msemaji kusema mambo kwa uwazi bila mzunguko ili kuzuia utata wa maana. Mbinu hii ina gharama kwa msikilizaji kwa sababu anaweza kufasiri ujumbe tofauti na kupata maana tofauti na aliyokusudia msemaji. Aidha, msemaji anaweza kukosa kutimiza lengo lake la kupitisha ujumbe kwa kuwa msikilizaji ana uwezo wa kuipa usemi husika maana tofauti. Kwa mfano mtu akitaka apewe chakula, anaweza kumwambia mwenzake “Unaweza kuamini sijala tangu jana?” msikilizaji anaweza kujibu, “Wah! Wewe ni bingwa basi, mimi siwezi, huwa ninahisi njaa haraka”. au, “Pole sana kakangu”. Majibu ya msikilizaji yanaonyesha kuwa hakumwelewa msemaji. Licha ya usalama wa mkakati huu, athari hasi ni kwa msemaji kutotekelezewa jambo muhimu analotaka.

Aidha, mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaweza kutekelezwa kupitia mbinu ya ubadilishaji msimbo. Watu hubadilisha msimbo wakati wa mazungumzo kwa nia moja au nyingine mojawapo ikiwa kukwepa kutaja mambo ya aibu katika lugha zao. Baadhi ya wale wanaotumia ubadilishaji msimbo kama ukwepaji wa kutaja mambo bayana ni wahusika wa mazungumzo ya redio katika vipindi vya *SK* kwenye idhaa ya *KASS FM*.

Wahusika wanapofikiria kuwa usemi katika Kinandi una uwezo wa kuathiri hisia za wahusika wa mazungumzo, wao huamua kubadilisha msimbo. Ubadilishaji msimbo

huwaruhusu kupitisha ujumbe uliolengwa bila mzunguko. Ubadilishaji msimbo una athari zake ifuatavyo.

Kwanza, mwelekezi pamoja na mwasilishaji wa vipindi ni wasomi. Hata hivyo, wao ni wajuzi wa Kinandi. Mashabiki wa vipindi vya *SK* ni mchanganyiko wa wasomi wa kiwango cha juu, kiwango cha wastani na kiwango cha chini. Zaidi ya hayo, kuna baadhi ya mashabiki ambao hawana kisomo kabisa. Kwa kupenyeza maneno ya Kiswahili au Kiingereza ndani ya Kinandi, hao viongizi wa kipindi wanachukulia kuwa wasikilizaji wote wana umilisi wa lugha hizo zote vizuri. Iidhihirika kuwa kuna baadhi ya wasikilizaji ambao hawakuelewa kilichomaanishwa na ndipo ungesikia wakimwuliza mzungumzaji aeleze kidogo kuhusu usemi husika. Hivyo basi, ubadilishaji msimbo haukidhi mahitaji ya wasikilizaji wote wa vipindi vya *SK* kwa sababu hukwamiza mawasiliano.

Pili, ubadilishaji msimbo huwafanya mashabiki kuhisi kuwa watumiaji wa lugha hizo wana maringo. Kwa mfano katika kipindi cha *Amu nee che ipchin muren kotun kwodo age* (sababu za mwamume kuoia mke mwingine), msikilizaji 'P' anadokeza kuwa wanawake waliosoma na kuolewa na wanaume wasio na kisomo, wanawaonyesha waume zao madharau. Anasema:

Kal.

100. *'Pasta', mi kwonyik che amu somanyotin kosir boisiekwak kosasisiei. Ngap kong'alalji boiyot Kingereza ago melen is ile makasei Nandi. Notok amu nee si ngap kotunis chito kogeny.*

Kis.

'Pasta', kuna wanawake ambao iwapo wamesoma kuliko waume zao huonyesha madharau. **Wakati mwingine anaweza kumzungumzia mumewe kwa Kiingereza na sio kwamba haelewi Kinandi.** Hiyo ndiyo sababu mtu anaweza kuamua kuoia tena.

Kutokana na mfano huo, kuna dhihirisho kuwa baadhi ya watu huchukulia kuwa iwapo wazungumzaji wanaelewa lugha ya mama kisha mmoja wao akaamua kuchopeza lugha nyingine, kwao, huko kubadilisha lugha ni kiashiria cha maringo na madharau.

Tatu, matumizi ya ubadilishaji msimbo wakati mwingine huaibisha. Iwapo mtu hakufika kiwango kizuri cha umilisi wa lugha nyingine kando na ya mama, kuna uwezekano wa kujiaibisha kwa kutumia lugha hiyo. Wengine wanaweza kutumia maneno ambayo hayafai kutumiwa katika sehemu fulani ya usemi na kuaibika wanapochekelewa na wenzao. Pia, kutamka neno tofauti na inavyotamkwa au hata kutoweza kutofautisha kati ya maneno mawili. Mfano mzuri ni katika kipindi cha Kalokseet *eng katunisiet* (Mavazi katika ndoa). Msikilizaji ‘Q’ analalama kuwa wanawake wanavaa mavazi yasiyosetiri miili yao kwa kusema:

Kal.

101. ‘Koriryo’, *mochei ngap imwochini kwonyik ak tibiik konai kole makororon ngoroik che nwogen. Ngap ituiye lakwa ne kelach tugun che kikwong’e, ndagerin kogeer olin kou yo mengenin amu aibu. Ang ye kakorusin kwong’et ipkosirto, koweek kabwotutik ibwat ile ngou yo ‘famila’ lakwanotok.*

Kis

‘Koriryo’, wakati mwingine unatakiwa kuwaeleza wana wa kike kuwa mavazi mafupi si mazuri. Kuna wakati unaweza kukutana na binti aliyevaa kiajabu, na akuonapo hujifanya hakuoni na kuangalia kando. Baada ya kupigwa na butwaa, mawazo yako yanarudi na unaanza kujiuliza iwapo sura uliyoona ni ‘**famila**’.

Neno ‘famila’ limetumika vibaya katika mfano huo. Shabiki ‘Q’ anatanika baina ya neno la Kiingereza ‘familiar’ na neno ‘famila’ ambalo ni jina la aina ya unga wa uji unaonunuliwa dukani. Jambo kama hili ni la kuaibisha na huwafanya mashabiki kuogopa kuchangia mjadala iwapo watagundua wamekosea.

Mwisho, wahusika wa mazungumzo wameonekana kutumia mbinu ya ubadilishaji msimbo badala ya tasfida. Matumizi ya tasfida ni mbinu mojawapo ya kutekeleza upole chanya. Mazungumzo baina ya Wasemaji wa Kikalenjin yanadhihirisha matumizi ya ubadilishaji msimbo badala ya tasfida za Kikalenjin. Katika Kipindi cha *Tilyandit eng Katunisiet* (Mahusiano katika Ndoa), ‘Pasta’ Rotich anaeleza kuwa kina mama wanafaa kuwa marafiki na binti zao. Anasema kuwa mama akimkaribia bintiye, kutoa maelekezo kwake kutakuwa rahisi. Anatumia mfano wa wakati msichana akiwa katika hali yake ya hedhi na wazazi wanataka kujua sababu ya kutoenda shuleni. ‘Pasta’ anasema kuwa ni vigumu kwa binti huyo kumweleza babake sababu kamili lakini kwa mamake itakuwa rahisi. ‘Pasta’ anasema hivi:

Kal.

102. *Igere ii Winny, nyamnyum mising eng tie kolenji kamet ‘anyeshani’ kosiir kwan. Ingen ile ma raisi yotok is!*

Kis.

Winny, wajua, ni rahisi kwa msichana kumwambia mamake **nina hedhi** kuliko kumwambia babake. Unajua hilo si rahisi.

Kupitia mfano wa 102, matumizi ya neno *anyeshani* (ninanyesha), yanaonyesha kuwa ubadilishaji msimbo umechukua nafasi ya tasfida za Kikalenjin *ami betusiek* (nina hedhi). Neno *anyeshani* limekopwa kutoka neno la Kiswahili ‘ninanyesha’. Kwa hivyo ubadilishaji msimbo unachangia kupotea kwa tasfida za Kikalenjin kwa sababu kusema katika Kiswahili kunaonekana rahisi kuliko Kikalenjin.

Mifano hiyo imeonyesha jinsi matumizi ya ubadilishaji msimbo unaweza kusababisha matatizo wakati wa mawasiliano. Ni muhimu kwa wahusika wa mazungumzo kuzingatia kiwango cha elimu yao na ya wenzao kabla ya kutumia mbinu ya ubadilishaji msimbo. Kadhalika, mawasiliano yoyote yale licha ya kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji yaweze kupitisha ujumbe uliokusudiwa.

5.2.5 Changamoto za Mkakati wa Kutosema Kabisa Kitendo cha Kutishia Uso

Ni mkakati usiomhitaji msemaji kusema lolote anapoona kuwa usemi una hatari kwa uso wa msikilizaji. Wakati mwingine, wasemaji wanaweza kudondosha maneno mengine au kukatiza usemi kama mbinu ya mkakati wa upole. Si rahisi kujua anachomaanisha msemaji kwa kuwa anaondoa kabisa usemi unaotishia uso. Hii ina maana kuwa msemaji atakuwa amemzingatia sana msikilizaji. Mkakati huu ni salama kuliko mbinu zote za kutekelezea upole.

Hata hivyo mbinu hii humgharimu sana msemaji kwa sababu hawezi kutekelezewa jambo na msikilizaji. Inamaanisha msemaji hatafanikiwa kupitisha ujumbe. Licha ya kuwa ndiyo njia salama zaidi, ni mkakati wenye hasara kubwa zaidi kwa sababu lengo kubwa ya mawasiliano ni kupitisha ujumbe. Bila kuwasiliana, ujumbe hautapitishwa na itakuwa hasara kubwa kwa msemaji. Kwa mfano iwapo mtu anahisi baridi na anaona mwenzake akiwa na fulana mbili, na akose kusema kuwa anahitaji, hatasaidika kwa sababu mwenzake hatakisia mahitaji yake.

Kwa ujumla, mikakati ya upole ina changamoto zake licha ya umuhimu wake. Wahusika wa mazungumzo wanapaswa kuwa tayari kulipia gharama za mkakati wowote ili kufanikisha kupitisha ujumbe wao. Ni kwa msingi huu ndipo wazungumzaji huteua mbinu za kutumia kwa kuzingatia faida na hasara wa kila mkakati na hali au muktadha wa mazungumzo.

5.3 Hitimisho

Sura hii imeangazia kwa undani hali zinazoathiri uteuzi wa mkakati wa upole na changamoto zinazotokana na utumiaji wa mikakati hiyo. Imebainika kuwa wazungumzaji huteua mikakati tofautitofauti kulingana na hali ya mazungumzo. Sababu mbili kuu zinazotumiwa na wanajamii kuteua mkakati fulani ni kuzingatia

faida za mkakati na hali za kijamii. Katika uteuzi kutokana na faida za mkakati, wasemaji hulazimika kutumia mbinu inayowafaidi pamoja na msemzwa. Katika sababu za hali za kijamii, ni dhahiri kuwa vipengele vya muktadha, umri, jinsia, hadhi na mada ya mazungumzo huathiri uteuzi wa mkakati.

Aidha sura hii imeainisha changamoto zinazotokana na utumiaji wa mikakati ya upole. Changamoto hizi huibuliwa na hali za lazima kwa wazungumzaji. Imebainika kuwa mkakati ulio na changamoto kuu ni mkakati wa kutosema kabisa kitendo kinachotishia uso. Licha ya usalama wake, kategoria hii ya upole inamweka msikilizaji katika hali ya kukosa kupitisha ujumbe wake. Hata hivyo, ni nadra sana kwa wazungumzaji kutekeleza aina hii ya upole wakati wa kuwasiliana. Sura hii inahitimisha uchanganuzi wa lengo la tatu katika utafiti wetu. Katika sura inayofuata ambayo ni sura ya mwisho ya tasnifu hii, tunatoa hitimisho la utafiti wetu kwa mujibu wa malengo yote ya utafiti.

SURA YA SITA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.0 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho la tasnifu nzima. Sehemu ya kwanza ni muhtasari wa sura zilizotangulia. Inaangazia yaliyomo katika sura ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne na ya tano. Sehemu ya pili inatathmini ufanisi wa malengo ya utafiti kwa kurejelea sura za tatu, nne na tano. Hatimaye, sura hii inatoa mchango wa utafiti pamoja na mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye.

6.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu umejikita katika uchunguzi na uchanganuzi wa mikakati ya upole inayotumika katika vipindi vya *SK* vya redio ya *KASS FM*. Utafiti wetu umetumia sura tano kufanikisha malengo ya utafiti. Kwa pamoja, sura hizi zimeshughulikia masuala yanayohusiana na mikakati ya upole katika vipindi husika vya *SK*. Sura ya kwanza ambayo ndiyo msingi wa utafiti umejikita katika kuangazia masuala anuwai yanayopambanua vijishehemu kuu kama vile usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mbinu za utafiti.

Sehemu ya usuli wa suala la utafiti imeangazia dhana ya lugha kwa kutoa maelezo ya lugha ya mazungumzo. Kupitia sehemu hii, ilibainika kuwa mazungumzo hayawezi kufanyika bila lugha. Hata hivyo, imebainika kuwa lugha ya mazungumzo ina kanuni zake kama vile kuzungumza kwa sauti, kuwa makini na ubadilishanaji wa zamu. Kanuni hizi zinahusiana na upole kwa sababu zinatumiwa na mtu mmoja kwa wakati mmoja na hivyo kutoa nafasi kwa wahusika wengine.

Pia, katika sehemu ya usuli wa suala la utafiti, upole katika utamaduni wa Wakalenjin umefafanuliwa. Ni bayana kuwa kila jamii ya Wakalenjin ina kanuni zake za mazungumzo. Imedhihirika kuwa kanuni hizo ndizo zinawaongoza Wakalenjin kujua ni kipi kinachukuliwa kuwa upole na kipi kisicho upole. Utafiti huu umethibitisha kuwa Wakalenjin huzingatia sana ustaarabu ambao ni muhimu katika kujiheshimu na kuwaheshimu wengine.

Suala la utafiti limeshughulikiwa pia katika sura ya kwanza ya utafiti ambapo tumeonyesha pengo lililoko na linalohitaji kuzibwa. Tumeonyesha kuwa licha ya kufanywa kwa tafiti nyingi kuhusiana na upole, hakuna utafiti uliofanywa kuhusiana na uchunguzi wa mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wa mazungumzo ya vipindi vya *SK*. Aidha, hakuna uchunguzi wa mikakati ya upole inayohusiana na upole iliyofanywa kwa lugha ya jamii husika. Kwa msingi huo ndipo kazi yetu imechangia kuziba pengo lililoachwa wazi.

Sababu za kuchagua mada na umuhimu wa utafiti ni sehemu zingine ambazo zimeshughulikiwa katika sura ya kwanza. Tumefafanua sababu za uteuzi wa mada yetu kwa msingi wa mapengo yaliyopo katika tafiti zilizotangulia. Tumeonyesha kuwa kazi hii ni ukurasa mpya kwa watafiti wengine wanaonua kufanya tafiti kuhusiana na upole katika vipindi vya redio. Aidha, wasemaji wa Kikalenjin watanufaika kupitia kwa utafiti huu kwa sababu wataboresha mazungumzo yao ya kila siku ili kudumisha uhusiano baina yao. Imedokezwa pia kuwa wanafunzi na walimu wa uamali na isimu-jamii watanufaishwa na utafiti huu.

Upeo na mipaka ya utafiti ni sehemu nyingine ya sura ya kwanza. Tumbaini kuwa utafiti umekusanya data kutoka vipindi vinane vya *SK* na kuweka upeo wake katika uamali kiisimu-jamii.

Sehemu ya mwisho ya sura ya kwanza imeshughulikia mbinu za utafiti. Tumeanza kwa kuonyesha jinsi tumeendesha utafiti mwigo kabla ya utafiti mkuu. Tumetoa sababu za utafiti mwigo huu kuwa ulitupa mwelekeo wa kupata data inayotosha kuchanganuliwa. Pia, utafiti mwigo umetuongoza kukadiria sampuli ya utafiti na ufaafu wa vifaa vya utafiti. Mwisho, sura ya kwanza imeonyesha njia alizotumia mtafiti kuteua sampuli, kukusanya na kusimba data. Mtafiti amechanganua na kuwasilisha data hizo kwa njia ya maelezo kwa sababu data zenyewe ni mazungumzo ya wahusika katika vipindi vya *SK*.

Sura ya pili imejikita katika mapitio ya maandishi ya wataalamu walioshughulikia kazi zinazohusiana na mada yetu. Dhana ya upole imejadiliwa kwa kina kulingana na wataalamu wa jadi hadi wa sasa. Imebainika kuwa suala la upole ni tata na bado linatafitiwa hadi leo. Wanaisimu wengi wanaelekea kukubaliana kuwa licha ya kuwa suala la upole ni tofauti kwa kila jamii-lugha, ubia wake unafaa jamii karibu zote. Kando na hayo, upole ni jambo linalotumika kudumisha amani na tabia njema.

Mazungumzo kwenye vyombo vya habari ni sehemu nyingine ambayo imeangaziwa katika sura ya pili. Ni dhahiri kuwa mazungumzo hayo hukumbwa na changamoto nyingi kwa vile waelekezi wa vipindi na wawasilishaji hawaonani ana kwa ana. Tumesema kuwa wahusika wa mazungumzo kwenye vipindi vya redio wanatakiwa kuwa makini sana wakati wa mazungumzo kwa sababu hawawezi wakapambanua ujumbe kutokana na mkao wa uso wao. Kupitia maandishi ya wataalam wengi, tumeona upana wa pengo tulilotakiwa kuliziba. Maandishi hayo yamekuwa msingi kwetu kwa kutuonyesha njia walizotumia wataalamu waliotangulia katika tafiti zao na kutoa mahitimisho.

Nadharia ya upole imeangaziwa kwa kina katika sura hiyo ya pili. Uasisi na maendeleo wa nadharia hii imejadiliwa kwa kina. Ni dhahiri kuwa nadharia ya upole imepitia mitazamo mingi tangu nyakati za uasisi na bado inakaguliwa hadi sasa. Wataalamu wengi wamejaribu kuboresha nadharia hii lakini mwisho wa tafiti zao wanatoa maoni kuwa mawazo ya Brown na Levinson (1978, 1987) ndiyo yanachukua sehemu kubwa kupima mada zinazohusiana na upole.

Sehemu hii pia imetalii muumano kati ya Nadharia ya Upole na kanuni ushirika kwa kuweka wazi kaida nne za kanuni ushirika ya Grice (1975) ambayo inaonekana kuwa msingi wa Nadharia ya Upole. Imedhihirika kwamba, nadharia ya upole husisitiza kuwa mawasiliano yoyote hufanikiwa iwapo washiriki wa mazungumzo wanazingatia mikakati ya upole kwa makusudi ya kuokoa nyuso zao na za wenzao. Aidha, katika mazungumzo yoyote, kila mshiriki anatakiwa kuhisi kukubalika na wenzake na kwamba mahitaji ya uso wake yanazingatiwa.

Sura ya pili pia imeangazia mitazamo tofautitofauti ya upole na kuhitimisha kwa kujikita zaidi katika mtazamo wa kuokoa uso ambao unaeleza kwa kina jinsi ya kuokoa uso unaokumbwa na vitisho. Hapa ndipo kategoria mbalimbali kuhusiana na uokoaji wa uso zimejadiliwa kwa upana. Kwanza, dhana kuhusu uso na vitendo vinavyotishia uso vimejadiliwa kisha utendakazi wa kategoria hizo umeelezwa. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi, na mkakati wa kuwa nje ya rekodi imejadiliwa kwa kina. Hata hivyo, sehemu hii pia inasema kuhusu mkakati wa kutosema kabisa kitendo kinachotishia uso kuwa mkakati ulio salama kuliko mikakati mingine.

Sura ya tatu ni uchanganuzi wa data zinazohusiana na lengo la kwanza la utafiti huu. Imeangazia kwa utendeti masuala yanayohusiana na mikakati minne ya upole.

Mikakati mine: mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi, mkakati wa kuwa kwenye rekodi na mkakati wa kuwa nje ya rekodi imejadiliwa kwa kina. Data zote za vipindi vya *SK* zinazohusiana na mikakati hiyo minne ya upole imechanganuliwa na kufafanuliwa katika sehemu hii. Tukianza na mkakati chanya wa upole, mkakati huu pamoja na kategoria zake zimeshughulikiwa kwa undani. Kategoria hizo ni kama vile kutafuta makubaliano, kumtambua na kumshughulikia msikilizaji, kuepuka kutokubaliana, kutumia utambulisho wa makundi, kuonyesha urajua na kuwa mcheshi. Imebainika kuwa mkakati hasi wa upole unaweza kutekelezwa kupitia kwa mojawapo ya mbinu hizo.

Mtafiti amefafanua nafasi ya msemaji na msikilizaji kwa kueleza namna msemaji anatakiwa kujitolea kwa kujipa nafasi duni ili msikilizaji afaidike. Mbinu hii humwezesha msemaji kumfanya msikilizaji ahisi vizuri kwa kuonekana kuwa katika nafasi sawa naye. Imedhihirika kuwa wasemaji wanatakiwa kuonyesha uhusiano wa karibu au wa kirafiki kati yao na wasemezwa. Uhusiano huo unatakiwa kudumishwa licha ya hitaji la kupitisha ujumbe uliokusudiwa

Kupitia sehemu hii, ni dhahiri kuwa mkakati wa upole chanya unanua kudumisha uso chanya wa msikilizaji kwa kuepuka kufanya au kusema habari zinazoweza kumuudhi msikilizaji au kuhasiri uso wake chanya. Vile vile, mkakati huu hulenga kuusifu na kuufurahisha uso chanya wa msikilizaji. Jukumu kuu la mzungumzaji huwa ni kumtukua, kumheshimu na kumrai msikilizaji ajihisi kuwa wa maana na thamani kubwa. Kadhalika, kupitia matumizi ya mkakati chanya wa upole, mzungumzaji hulenga kuibua, kukuza na kuyapalilia mazingira ambayo yanadumisha mahusiano baina yake na msemazwa. Mkakati huu hutawaliwa na utoaji mwingi wa miadi chanya kwa msikilizaji.

Sura hiyo ya tatu pia inaangazia mkakati hasi wa upole na kategoria zake. Mkakati wa upole hasi hulenga kupunguza vitisho kwa uso hasi wa msikilizaji. Ni dhahiri kuwa wahusika wa mazungumzo ya *SK* wametumia kategoria mbalimbali za mkakati wa upole hasi. Matumizi hayo ni kwa manufaa ya kuokoa uso hasi wa msikilizaji wanapokabiliwa na kitendo kinachotishia uso.

Aidha, sehemu hii imeonyesha jinsi wahusika wa mazungumzo hutumia mbinu za mkakati wa upole hasi kupunguza ulazimishaji kwa msikilizaji. Mbinu hizo ni; matumizi ya vitangulizi kabla ya kutaja kitendo kinachotishia uso, kutaja kitendo husika kama kanuni ya jumla, kuonyesha staha baina ya msemaji na msikilizaji, kusema jambo kimzunguko na kuepuka matumizi ya viwakilishi vya nafsi.

Sura ya nne ya tasnifu hii imeshughulikia athari zinazotokana na utekelezaji au ukiukaji wa mikakati ya upole katika vipindi vya *SK*. Tumeorodhesha na kufafanua athari za utekelezaji wa mikakati hiyo ya upole. Kutokana na hayo imebainika kuwa utekelezaji wa mikakati ya upole hukuza heshima baina ya wahusika wa mazungumzo ya *SK*. Hali hii hutekelezwa kupitia njia anuwai kama vile; matumizi ya misemo, ubadilishaji msimbo, matumizi ya methali, matumizi ya sifa za kiarudhi, kuzungumza kwa zamu na udondoshaji. Athari nyingine ya utekelezaji wa mikakati ya upole ni kuwafurahisha na kuwavutia wasikilizaji. Ni bayana kuwa katika *SK*, mwasilishaji mkuu wa vipindi na mwelekezi wake hutumia lugha ya utani, yenye kufurahisha, ili kuvutia mashabiki kwa minajili ya kuendeleza vipindi ipasavyo.

Isitoshe, katika utafiti huu, ilidhihirika kuwa wakati mwingine wahusika wa mazungumzo ya *SK* hulazimika kukiuka mahitaji ya utekelezaji wa mikakati ya upole kwa sababu moja au nyingine. Ukiukaji huo hutokea katika hali zifuatazo: matumizi ya lugha mwiko, ukatizaji wa zamu, matumizi ya kauli zinazolenga kundi maalum na

kuzungumzia mada ambazo hutishia uso wa msikilizaji. Athari zote kwa ujumla zimeonekana kuwa chanya au hasi na kuchangia uteuzi wa mikakati ya kutumia katika hali tofautitofauti.

Sura ya tano nayo inapambanua hali zinazoathiri uteuzi wa mkakati na changamoto zinazoibuliwa na utekelezaji wa mikakati ya upole. Tumbaini kuwa uteuzi wa mkakati wa upole wakati wa mazungumzo hutegemea mambo mawili. Kwanza, faida anayopata msemaji au msikilizaji kwa kutumia mkakati husika na pili, ni hali za kijamii ambazo zinawaweka wahusika wa mazungumzo katika nafasi zao katika jamii. Ni wazi kuwa wahusika wa mazungumzo ya *SK* huteua mikakati ya kutumia wakati wa mazungumzo yao. Wao hufanya hivyo kwa kuzingatia faida wanazopata kutokana na matumizi ya mikakati hiyo. Tumepambanua faida hizo kwa kuzingatia kila mkakati.

Pia, hali za kijamii zimejadiliwa kwa misingi ya jinsia, muktadha wa mazungumzo, umri, mada ya mazungumzo na hadhi za wahusika wa mazungumzo. Ni dhahiri kuwa wahusika wa mazungumzo ya *SK* hasa ‘Pasta’ Rotich na Winny ‘Koriryo’ wanatofautiana kiumri na kihadhi. Kutokana na hali hii, wao huteua lugha mwafaka wanapozungumziana. Kadhalika, mashabiki wa vipindi vya *SK* ni wa umri na jinsia tofauti, hali inayowafanya wawe makini sana wanapozungumza ili kukithi mahitaji ya nyuso zao.

Sehemu ya mwisho ya sura ya tano imejadili changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mikakati ya upole. Ni bayana kuwa, kila mkakati una changamoto zake. Hata hivyo, ilibainika kuwa wahusika wa *SK* hulazimishwa na hali fulani kutumia mkakati husika licha ya changamoto zake. Tumbaini kuwa mkakati ulio salama kabisa na usiotishia uso wowote ni wa tano ambao ni wa kutosema kabisa kitendo kinachotishia

uso. Hata hivyo, usalama huo hauna faida kwa sababu changamoto kuu katika mkakati huu ni kuwa msemaji hatafaulu kupitisha ujumbe wake.

6.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kuchanganua mikakati ya upole inayotumika kuwasilisha vipindi vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*. Aidha, mtafiti alinua kuhakiki athari za uzingatiaji na ukiukaji wa kaida za upole kwenye vipindi hivyo vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*. Kadhalika, utafiti huu ulilenga kutathmini hali zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole na changamoto za mikakati hiyo katika vipindi husika vya *SK*.

Lengo la kwanza lililoongoza utafiti huu ni kuchanganua mikakati ya upole inayotumiwa na wahusika wa mazungumzo katika vipindi vya *SK*. Lengo hili limeafikiwa kupitia uchanganuzi wa data katika sura ya tatu. Mikakati yote minne imetumiwa kuchanganua mazungumzo husika. Wahusika katika vipindi husika vya *SK* ni mwasilishaji mkuu 'Pasta' Rotich, mwelekezi wa vipindi Winny 'Koriryo' pamoja na mashabiki kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Wao wametumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole na mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Hata hivyo, mkakati wa mwisho ambao ni mkakati wa kutotekeleza kabisa kitendo kinachotishia uso ulitumiwa lakini kwa uchache mno.

Matumizi ya kategoria mbalimbali za mikakati hiyo yamejadiliwa kwa utendeti ili kuonyesha namna wahusika katika vipindi vya *SK* wametumia mbinu hizo kuokoa nyuso zao. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi, ambao ni wa kusema mambo yalivyo bila mzunguko, umetumiwa na wazungumzaji kuwasiliana na kupitisha jumbe zao bila mkwaruzano. Mkakati chanya wa upole umetumiwa sana hasa kategoria ya udumishaji wa uhusiano kati ya msemaji na msemzwa. Mkakati chanya wa upole umeonekana kutawaliwa sana na utoaji mwingi wa miadi chanya.

Mkakati wa tatu ambao ni mkakati hasi wa upole umedhihirika katika mazungumzo husika. Wazungumzaji wametunza nyuso zao kwa kuzingatia matumizi ya viwakilishi vya kimakundi, kusema jambo kimzunguko na kutumia vitangulizi miongoni mwa mengine. Mkakati wa kuwa nje ya rekodi umetumiwa na wazungumzaji kupitia kategoria zake mbalimbali kwa lengo la kumdokezea msikilizaji kile ambacho msemaji anamaanisha. Mbinu hii haitumii ubayana bali jambo hudokezwa tu na kuachiwa msikilizaji kufasiri ujumbe na kutoa maana kwa usemi husika.

Lengo letu la pili lilihakiki athari za uzingatiaji na ukiukaji wa kaida za upole kwenye vipindi hivyo vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*. Tulifaulu kuafikia lengo hili kwa kushughulikia athari za utekelezaji na ukiukaji wa mikakati ya upole kama ilivyoangaziwa katika sura ya nne. Athari hizo zimebainika kuwa chanya au hasi. Lengo la tatu: kutathmini hali zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya upole na changamoto za mikakati hiyo katika vipindi husika vya *SK* limeafikiwa.

Hali za kuteua mkakati kwa kuzingatia faida inayotokana na mkakati zimejadiliwa kwa kina. Wazungumzaji katika vipindi vya *SK* huteua mikakati ya kutumia kwa kuhakiki na kutathmini faida wanazopata. Aidha, hali mbalimbali za kijamii kama vile jinsia, umri, muktadha wa mazungumzo, hadhi/mamlaka na mada ya mazungumzo zimedhihirika kuathiri uteuzi wa mikakati katika mazungumzo ya *SK*. Kadhalika, lengo la nne ambalo ni kupambanua na kujadili changamoto zinazosawiriwa na wahusika wa mazungumzo ya *SK* wanapotekeleza kanuni za upole limeafikiwa. Hali hizo zimejadiliwa kwa utendeti ili kuonyesha namna wazungumzaji hukumbwa na changamoto nyingi wanapopitisha ujumbe.

6.3 Mchango wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango mkubwa kwa taaluma za lugha na isimu, uamali na isimu-jamii.

- i. Utafiti umedhihirisha matumizi ya lugha ya upole kupitia kategoria mbalimbali katika jamii za Kiafrika hasa lugha ya Kikalenjin. Tafiti za kwanza zinazohusiana na upole, zilifanywa kwa lugha za Kizungu. Utafiti huu ni ushahidi kuwa nadharia ya upole inaweza kutumika katika uchanganuzi wa mazungumzo katika lugha zetu za Kiafrika. Matokeo ya utafiti huu yanashadidia kuwa uteuzi wa mikakati ya upole hutegemea hali tofautitofauti za mazingira. Matokeo hayo yanatoa mchango mkubwa kwa tafiti zijazo kwa kutoa mwongozo wa namna ya kufanya uteuzi wa mkakati wa kutumia katika hali mbalimbali.
- ii. Kupitia utafiti huu, imebainika kuwa utekelezaji na ukiukaji wa mikakati ya upole una athari chanya na hasi. Imedhihirika kuwa wazungumzaji wa mazungumzo yoyote yale wanafaa kuzingatia mikakati hiyo ili kuokoa nyuso zao na za wenzao. Utekelezaji wa mikakati ya upole hukuza heshima kati ya wazungumzaji. Matokeo haya yatawanufaisha wanauamali na wanaisimu-jamii kuwa makini wakati wa mazungumzo ili kukidhi mahitaji ya nyuso zao na za wenzao. Aidha, utafiti huu utawanufaisha wanajamii wa lugha husika kukumbatia upole ili kudumisha uhusiano mwema kati yao.
- iii. Utafiti huu umehakiki hali zinazoathiri uteuzi wa mikakati ya kutumia wakati wa kuwasiliana. Ni bayana kupitia uchunguzi huu kuwa, hali mbalimbali huathiri uteuzi wa mikakati ya upole. Wahusika wa vipindi vya *SK* wamedhihirisha kuwa faida zinazotokana na matumizi ya mkakati fulani na hali za kijamii kama vile umri, jinsia na mamlaka miongoni mwa mengine, ni

vipengele muhimu katika uteuzi wa mkakati. Utafiti huu utawaelekeza wazungumzaji wa mazungumzo yoyote yale kutathmini hali za muktadha husika kabla ya kutumia mkakati wowote.

